**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Kumi na Tisa – Tarehe 11 Julai, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama mtakavyoona kwenye ukumbi wa Mheshimiwa Spika, kuna wageni wa kutoka Vietnam. Yupo Naibu Spika wa Bunge la Vietnam, anaitwa Ndugu Winvan Yu, amefuatana na Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria na Katiba Ndugu Vunde Ken. Pia amefuatana na Mkuu wa Mkoa mmoja wao huko, anaitwa Win Suni Zunne. Pia ujumbe wake yupo pamoja na Balozi ambaye yuko hapa Tanzania na wafanyakazi wa Bunge la Vietnam wamefuatana nao. Tunawakaribisha sana. Ni lengo letu kuanzisha mahusiano na Mabunge ndani ya *East Africa*, Afrika na nje ya nchi tunaanzisha uhusiano wa Mabunge. Kwa hiyo, ni wageni wetu, nafikiri ni *delegation* ya pili, baada ya Rais wa Ireland kuingia katika Bunge letu hili. Karibuni sana. (*Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, waliopo katika *Public Gallery* ni wanafunzi wa Vyuo Vikuu mbalimbali nchini ambao watakuwa na sisi kwa mwezi Julai na mwezi Agosti, 2006 wakijifunza mambo mbalimbali. Mnakaribishwa sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ni kawaida katika Mabunge yote duniani kuwa na wanafunzi wa Vyuo mbalimbali kuanza kujifunza mambo yetu jinsi tunavyofanya kazi. Kusudi tukistaafu ama waweze kutukosoa vizuri ama waweze kuajiriwa humu ndiyo mambo ya kawaida. Kwa hiyo, nadhani tumeanzisha utaratibu huu pia wa kuwa na watu kama hawa. Baada ya hapo Katibu. *(Makofi)*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 176

**Athari za Ugonjwa wa UKIMWI**

**MHE. JUMA SAID OMAR** aliuliza:-

Kwa kuwa, UKIMWI umekuwa ukiathiri sana nguvu kazi ya Taifa hili hasa vijana; na kwa kuwa, dawa za kurefusha maisha zinatolewa bure na Serikali pamoja na kutoa elimu kwa jamii kwa njia ya warsha, makongomano na semina:-

(a) Je, kwa nini hadi sasa idadi ya waathirika inazidi kuongezeka badala ya kupungua?

(b) Je, ni maeneo gani hapa nchini ambayo waathirika ni wengi zaidi na Serikali ina mikakati gani ya kukabiliana na maeneo hayo mbali na elimu ya UKIMWI inayotolewa?

(c) Je, ni yatima na wajane wangapi kwa nchi nzima wameachwa kutokana na vifo vinavyotokana na UKIMWI na Serikali ina mpango gani wa kuwapatia angalau posho yatima na wajane hao ili waweze kukabiliana na maisha?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. LUKA J. SIYAME)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Juma Said Omari, Mbunge wa Mtambwe, naomba kutoa maelezo yafuatavyo:-

UKIMWI ni janga la kijamii kwa maana ya kwamba virusi vya UKIMWI huenea kimya kimya kwa kutegemea mahusiano ya watu, inaweza kuwa kwa njia ya kujamiiana au kwa kutumia vifaa visivyotakaswa (*un-sterilized instruments*) hasa wakati wa kukeketa wanawake na kutoboa au kukata ngozi kwa mfano, utogaji masikio na uchanjaji wa ngozi kwa madhumuni ya tiba au urembo yani *tattooing* na pia kwa maambukizo kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto wakati wa kujifungua ama wakati wa kunyonyesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, si watu wote wenye virusi vya UKIMWI wanaojulikana. Inakisiwa kuwa kiasi kati ya asilimia 15 - 20 tu ya waishio na Virusi vya UKIMWI ndio wanajijua. Wengine hawajitambui kwa sababu ama wako katika kipindi cha mwanzo cha maambukizo tunaita *window period* ambapo virusi hivyo haviwezi kutambuliwa na vipimo vya kitaalamu au wahusika hawajajipima kutokana na sababu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, yatima na wajane watokanao na vifo vinavyohusiana na UKIMWI wanaojulikana ni sehemu tu ya jumla ya wahanga hao kutokana na baadhi ya vifo vitokanavyo na ugonjwa wa UKIMWI kutotambuliwa au kuwekwa siri na ndugu na jamaa za waathirika kwa kuogopa unyanyapaa katika jamii. Hali hii inafanya takwimu sahihi za idadi kamili kitaifa kutopatikana na kama zikipatikana kuwa nyuma ya hali halisi, hasa ikizingatiwa kuwa maambukizo na vifo hutokea kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Juma Said Omar, Mbunge wa Mtambwe, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti wa viashiria vya UKIMWI Tanzania uliofanywa mwaka 2003/2004 ulionyesha wastani wa maambukizo kuwa ni asilimia 7, wanawake ilikuwa ni asilimia 7.7 na wananume ni asilimia 6.3. Jitihada za kujua kama waathirika wameongezeka au wamepungua, zinafanyika kupitia utafiti mwingine uliopangwa kuanzia mwezi Julai, 2007 hadi Machi, 2008.

Utafiti huo utafanywa kwa ushirikiano na Tume ya Kudhibiti UKIMWI yaani *TACAIDS,* Wizara ya Afya, Taasisi ya Takwimu (*Bureau of Statistics*) ambayo iko chini ya Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Marekani *(USAID). (Makofi)*

Kwa kuwa harakati za udhibiti wa maambukizo ya UKIMWI zinaendelea, tunaamini kwamba maambukizo hayo mapya yanapungua. Kwa mfano, tu tukiangalia katika Wiki ya Maonyesho ya Kimataifa ya Dar es Salaam walijitokeza watu 516 kupima UKIMWI na kati yao ni watu 35 waliogundulika kwamba wana UKIMWI ambayo ilikuwa ni karibu asilimia 7 ile ile. Wanawake wakiwa 25 sawasawa na asilimia 69 na wanaume wakiwa 11 sawasawa na asilimia 31.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti kuhusu maeneo na kiwango cha maambukizi ulionyesha kwamba Mikoa inayoongoza kwa maambukizi ni Mbeya ambayo ilikuwa na asilimia 13.5, Iringa asilimia 13.4 na Dar es Salaam asilimia 10.9 kwa wastani tu. Katika Mikoa yote hata ile yenye asilimia ndogo, kama Kigoma na Manyara yenye asilimia 2, kuna maeneo ambayo yameathirika zaidi kuliko mengine. Hivyo basi, maeneo yote yanalazimika kutolegeza msimamo juu ya udhibiti wa UKIMWI.

Maeneo yenye wagonjwa wengi zaidi yanaongezewa vituo vya kupimia virusi na kupewa mgao zaidi kuliko yale ambayo hayajaathirika sana. Kwa maana ya kupewa dawa za kupunguza makali ya UKIMWI. *(Makofi)*

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya yatima na wajane ni kubwa ingawa kama nilivyoeleza hapo awali, idadi kamili hatuijui, na jitihada zinaendelea kupitia Serikali za Vijiji kupata takwimu sahihi. Yatima peke yao wanakadiriwa kuwa 2,500,000. Mamlaka za Serikali za Mitaa wametakiwa kuwahesabu yatima na watoto wote walio katika mazingira magumu bila kujali chanzo cha hali yao na kuwafanyia mipango ya kuwahudumia ili Serikali iweze kuwasaidia kwa ufanisi zaidi.

Wapo wanaopatiwa huduma, hasa Mijini, kutoka vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na Serikali, lakini hawajafikiwa wote kwa wastani tu ni asilimia 6 ya watoto wanaoishi kwenye kaya zenye hatima ambao wameweza kuhudumiwa. Wepesi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wa kuwatambua utaharakisha mchakato huo. *(Makofi)*

Na. 177

**Wakulima Wadogo Wadogo wa Miwa Kilombero**

**MHE. HALIMA J. MDEE** aliuliza:-

Kwa kuwa, kilimo ndio uti wa mgongo wa uchumi wa Taifa letu; na kwa kuwa, wakazi wa Wilaya ya Kilombero katika Kata za Kidatu, Mkula, Sanje, Mang'ula; Kisawasawa na Kiberege wanategemea kilimo hususan kilimo cha miwa kuendesha maisha yao ya kila siku.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba, wakulima wadogo wadogo wa miwa wanaokizunguka Kiwanda cha Sukari cha Kilombero wanafaidika na kuwepo kwa Kiwanda husika kwa kuuza mazao yao kwenye kiwanda hicho?

(b) Je, kwa nini baada ya msimu wa mavuno kufika, Miwa ya wakulima hao wadogo wadogo hainunuliwi mpaka ipite miaka mitatu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Sukari Kilombero ni mojawapo ya viwanda vinavyotoa mchango mkubwa katika utekelezaji wa Mpango wa Kuendeleza Uzalishaji wa Sukari Nchini ambao lengo lake ni kuliwezesha Taifa kujitosheleza kwa mahitaji yake ya sukari ifikapo mwaka 2010. Kiwanda hicho hupata takriban asilimia 97 ya mahitaji yake ya miwa kutokana na miwa inayozalishwa na wakulima wa nje ya Kampuni yaani *out growers*.

Kwa hiyo, ni dhahiri kuwa wakulima wa nje ya Kampuni wanatoa mchango mkubwa katika uzalishaji wa miwa katika kiwanda hicho. Kwa mfano, ununuzi wa miwa iliyozalishwa na wakulima hao uliongezeka kutoka tani 95,765 mwaka 1997/1998 hadi tani 696,253 mwaka 2005/2006 na idadi ya wakulima wa nje ya Kampuni walioshiriki katika uzalishaji wa miwa hiyo katika kipindi hicho iliongezeka kutoka wakulima 2,460 hadi wakulima 6,091 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 42.

Ongezeko hilo linaonyesha wazi kwamba wakulima hao wanafaidika na mpango uliopo wa kuuza miwa kwenye kiwanda hicho.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Sukari cha Kilombero kimekuwa kikinunua wastani wa trakiban asilimia 95 ya miwa yote iliyozalishwa na wakulima wa nje ya kiwanda kila msimu wa mavuno unapofika. Wastani wa asilimia tano inayobakia imekuwa hainunuliwi kutokana na matatizo mbalimbali yakiwemo ya ubovu wa miundombinu, uwezo usio tosha wa kiwanda, na ubovu wa barabara katika maeneo ilikozalishwa miwa ya wakulima hao.

Hata hivyo, tatizo la barabara mbovu linatafutiwa ufumbuzi kwa kutumia mfuko maalum wa kutengeneza barabara (*Road Fund*) waliojiwekea wakulima wenyewe wakisaidiwa na Mfuko wa Kilombero *Trust Fund.* Aidha, ufumbuzi wa kuaminika ni kwa njia ya maelewano kupitia Kilimo cha Mkataba *Contract Growing* wenye wajibu unaoeleweka na wa kuamini wa pande zote mbili. Hatua ambayo nimetaarifiwa imefikiwa hivi karibuni na nawapongeza sana kwa kufikia hatua hiyo.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Na Vilevile namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

La kwanza, taarifa ambazo zipo za hivi karibuni ni kwamba katika Kata ya Sanje ekari zaidi 300,000 za miwa hazijavunwa. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba mavuno yanafanyika na wakulima wanapata fedha zao ili waweze kuendelea na kilimo?

La pili, kwa mujibu wa maelezo ya wakulima wa miwa tatizo la kusafirisha miwa ndilo linalosababisha ukwamishaji wa zoezi husika.

Je, Serikali ikiwa mmoja wa wamiliki wa *share* katika hicho kiwanda ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba usafiri wa maana unapatikana ili mazao husika yaweze kuvunwa na hatimaye kusafirishwa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokuwa najibu swali la msingi nilieleza kiasi ambacho kinanunuliwa na kiwanda kutoka wakulima hao wanaozunguka kiwanda. Na nikasema kwamba ni asilimia 5 tu ndiyo inayobaki kwa matatizo mbalimbali ambayo nimeyataja, mojawapo likiwa hilo la miundombinu mibovu ya barabara na kadhalika. Kwa hiyo, inawezekana kabisa kwamba pengine miwa hiyo ambayo itakuwa bado haijavunwa ni katika hiyo asilimia 5 ambayo nilikuwa nimeizungumzia. Lakini nikasema pia kwamba njia za kutatua matatizo hayo zinaandaliwa kama nilivyoeleza katika jibu la msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusu suala la usafiri ambalo ni swali la pili, ambalo amelisema Mheshimiwa Mbunge. Nimekwisha kueleza hapa kwamba kuna

utaratibu wa kutumia Mfuko Maalum ulioandaliwa na wakulima wenyewe pamoja na ile *Trust Fund* ya barabara itakuwa ndiyo suluhisho la mwisho katika tatizo hili.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri aliyotoa mwenzangu Mheshimiwa Naibu Waziri. Ningependa kutoa maelezo ya ziada kwenye swali la nyongeza alililoliuliza Mheshimiwa Halima Mdee. Ni kwamba kama bado lipo tatizo la kusafirisha miwa.

Pamoja na zile juhudi ambazo zinafanywa na *Trust* tuliyoeleza katika swali. Bado katika Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo wakati wa kuibua ule Mpango wa Maendeleo ya Kilimo wa Wilaya ambao unaibuliwa kutoka miongoni mwa wakulima wenyewe kule Kijijini bado wakulima wa Kata ile anayoizungumzia wanaweza wakaibua kwamba barabara au daraja ni tatizo lao. Na kama wataibua hivyo ikaingizwa katika Mpango wa Maendeleo ya Kilimo wa Wilaya basi fedha za kutengenezea hiyo barabara zinaweza zikachukuliwa kutoka kwenye lile kapu la Kitaifa nililolieleza katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, pale ambapo kuna matatizo ya aina hiyo tuhakikishe kwamba vikwazo hivyo kwa wakulima vinaibuliwa na kuingizwa katika Mpango wa Maendeleo wa Kilimo ya Wilaya ili tuweze kuviondoa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Waziri juu ya uendelezaji wa miundombinu. Lakini linalojitokeza pale kama ni tatizo kubwa ni kiwanda kutokumudu kununua miwa yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimwulize Waziri, katika hotuba yake alizungumzia kwamba Irovo itaendelea na *capacity expansion*. Kutokana na kauli yake hiyo anaweza kuwahakikisha Wakulima wa Miwa wa Kilombero kwamba kiwanda kingine kitajengwa katika maeneo ya Kiberege na Mang'ula ili kukidhi ununuaji wa miwa yote?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeshafanya mazungumzo na wenye kiwanda na maelezo yao ni kwamba walikuwa hawawekezi kuongeza nafasi ya kile kiwanda cha Kilombero kwa sababu bado walikuwa hawajawa na Mkataba na wale wakulima wa nje ya kiwanda. Lakini kwa sababu sasa wamekwishaafikiana na wana Mkataba na Mkataba huu kama utaimarishwa. Maana yake sasa wana Mkataba ule wa kiujumla kama utaimarishwa na ile Mikataba ya kila mkulima na kiwanda wataweza kuongeza nafasi ya kiwanda cha Kilombero kuhakikisha kinafikia ile *capacity* inayoweza kuchukua miwa yote. Na tayari tuna waombaji wengine ambao wanataka kuongeza uwekezaji wa kiwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda kuchukua nafasi hii kusisitiza kwamba pande mbili ziimarishe kilimo cha Mkataba ili kikiwa kimeimarika kabisa tatizo

hili litaondoka. Kwa sababu kwa uhakika wa miwa inayolimwa wenye kiwanda watakipanua kile kiwanda. Pamoja na fikra ambazo zipo za kufungua kiwanda kingine katika eneo la Lwipa.

Na. 178

**Kutengeneza Mazingira ya Kuwawezesha Vijana Kujitegemea**

**MHE. FELISTER A. BURA** aliuliza:-

Kwa kuwa, vijana wengi kwa sasa wanakimbilia Mijini wakidhani kuwa ndiko kwenye maisha mazuri lakini badala yake wamebaki kuwa vibaka, wavuta bangi na wengine kuwa makahaba:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kutengeneza mazingira mazuri ya kuwawezesha vijana kujitegemea huko huko Vijijini badala ya kukimbilia Mijini?

(b) Je, Serikali haioni kuwa, isipoikomesha tabia hiyo ya vijana kuzurura Mijini watawaoa wazururaji wenzao na kuzaa watoto wazururaji wasiopenda kazi na kwa msingi huo nguvu kazi ya Taifa itapotea na uchumi imara tunaozungumzia na kukusudia kuujenga hautajengeka?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Felister Aloyce Bura, Mbunge wa Viti Maalum, napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa vijana wengi hivi sasa wanakimbilia Mijini kwa kudhani ndiko kwenye maisha mazuri, aidha matarajio yao ni kutafuta na kuboresha maisha yao. Kinyume chake vijana hawa hujikuta katika dhiki na shida nyingi ikiwa ni pamoja na kujihusisha na vitendo vya uhalifu kama vile wizi, ubakaji ukahaba na madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo mafupi sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Felister Aloyce Bura, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inayo mikakati madhubuti yenye mwelekeo wa kuweka mazingira mazuri sehemu za vijijini ili vijana waweze kubakia vijijini wakizalisha mali na kujipatia kipato.

Mikakati hiyo ni pamoja na kuwahamasisha vijana kujiunga na vikundi vya uzalishaji mali na vikundi vya kuweka akiba na mikopo *(SACCOS)* katika sehemu za Vijijini na Mijini, ili Serikali na vyombo vingine vya fedha viweze kuwawezesha vijana kimtaji, mafunzo na vitendea kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya hivyo, vijana wengi na hasa wa vijijini watapata motisha ya kubaki vijijini wakiendesha maisha yao badala ya kukimbilia Mijini. Aidha, huduma muhimu kama vile hospitali, umeme, shule, masoko ya kisasa, sehemu za burudani na miundombinu zitaendelea kuboreshwa na Serikali hatua kwa hatua ili kuhakikisha huduma ambazo vijana wengi wanazifuata mijini zinapatikana katika maeneo ya vijijini. Suala zima la vijana kukimbilia mijini ni changamoto pia kwa Waheshimiwa Wabunge natoa wito tushirikiane kwa karibu na Serikali za Mitaa na Serikali Kuu ili kuendelea kujenga mazingira mazuri vijijini ili kupunguza tatizo la vijana kukimbilia mijini. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, suala la vijana kuzurura Mijini na tatizo la kuoana wao kwa wao na hatimaye kuzaa watoto wazururaji na wasiopenda kazi ni changamoto yetu pia ikiwa ni pamoja na wajibu mzima wa malezi katika ngazi ya familia. Hata hivyo kama nilivyoeleza hapo awali mikakati inayoandaliwa hivi sasa ni pamoja na mkakati wa Taifa wa ajira na uhamasishaji wa vikundi vya vijana vya uzalishaji mali. Mkakati huu utaweza kuleta sura mpya ya ufumbuzi wa tatizo hili na kuhakikisha kuwepo kwa matumizi mazuri ya nguvu kazi ya vijana ambayo ni takriban asilimia 68 nguvu kazi yote ya Taifa ili nguvu kazi hii itumike vizuri kwa manufaa ya vijana na kwa manufaa ya Taifa. *(Makofi)*

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

(a) Kwa kuwa mikakati ya Serikali ni kuwawezesha vijana huko waliko Vijijini. Je, vijana hao watapata mafunzo ya ujasiriamali kabla ya mkakati huo kuanza?

(b) Kwa kuwa Serikali ina lengo la kuwapa mikopo vijana hawa kupitia mabenki ambayo yatapewa kazi hiyo ya kuwakopesha vijana. Je, Serikali imeandaaje udhamini kwa vijana hao?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kwamba Serikali na vyombo vya fedha tunaandaa mkakati wa kuwawezesha vijana kupata mitaji na mafunzo ikiwa ni pamoja na vitendea kazi. Lakini yote haya yatabainishwa rasmi katika hotuba ya Mheshimiwa wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana atakapoisoma hapo tarehe 4 Agosti, 2006. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge avute subira kidogo ili nisimalize uhondo wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, kuhusu udhamini. Hali kadhalika hilo tumelitazama sana kwamba vijana wengi hawana mali na mkakati huo unaandaliwa.

Lakini nipende kusema kwamba yote haya yatajibainisha kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ajira, na Maendeleo ya Vijana hapo 4 Agosti, 2006. *(Makofi)*

Na. 179

**Jitihada za Kubadili Tabia Mbaya kwa Vijana**

**MHE. AMINA C. MPAKANJIA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Nchi ya Kenya ni mfano mzuri wa kuigwa kwa suala la kubadilisha mwelekeo wa tabia za vijana waliojiingiza katika vitendo viovu kama vile uvutaji bangi, madawa ya kulevya, wizi, ujambazi na kujiingiza katika biashara za ngono; na kwa kuwa, nchi hiyo ina vivutio maalum vya Serikali ambapo pindi vijana wanapomaliza kutumikia kifungo na adhabu hupelekwa katika vituo hivyo ili kuwasaidia kubadilli mienendo yao; na kwa kuwa, katika nchi yetu vijana wetu wanapomaliza vifungo na adhabu zao huachwa huru na matokeo yake wanarudia vitendo vilevile viouvu:-

(a) Je, Serikali inafikiriaje kufungua vituo kama hivyo kwa lengo la kuwasaidia vijana wetu?

(b) Je, Serikali haioni kwamba, ikifungua vituo kama wenzetu wa Kenya wanavyofanya vitasaidia sana kupunguza uhalifu unaofanywa na vijana wetu na kuyaingiza maisha yao hatarini?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Mpakanjia, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango unaozungumziwa na Mheshimiwa Mbunge wa vituo kwa ajili ya kubadili tabia za vijana waliojiingiza katika vitendo viovu kama biashara ya ngono na kama unavyotumika Nchini Kenya kwa hakika ni mpango mzuri. Lakini kwa wakati huu Serikali yetu haina utaratibu kama huo. Hata hivyo, Wizara yangu inaendelea kukamilisha mpango wa kuanzisha Makambi Kazi ya Vijana ambayo tunatarajia kushirikiana kwa karibu na Jeshi la Kujenga Taifa ili kujenga mfumo ambao utasaidia vijana kubadili tabia na kupenda kazi.Tunatarajia pia katika mpango huu, Wizara yangu itashirikiana na Taasisi na Wadau mbalimbali kama vile Tume ya Taifa ya Kudhibiti dawa za kulevya, *TACAIDS,* Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Jeshi la Magereza ili kufikia kwa kiasi kikubwa mkakati wa kubadili tabia za vijana ikiwa ni pamoja na wale wanaomaliza adhabu walizohumiwa kuzitumikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, chini ya mpango huu tunatarajia kuwa vijana watajiunga na kupata mafunzo ya Stadi za maisha ili waweze kumudu maisha yao kwa hali iliyo endelevu na wakati huo huo kupata stadi za kazi ili waweze kuwa na uwezo wa kumudu maisha yao kwa kufanya kazi za uzalishaji mali na kujiongezea kipato.Tuna matumaini kuwa chini ya mpango huu tutaweza kuwajumuisha vijana wengi zaidi katika kazi za kujishughulisha kiakili, kimwili na kimaadili na mpango huu utasaidia kupunguza tatizo hili kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

**MHE. AMINA C. MPAKANJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwanza, ningependa kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kusema wanao mpango wa kuanzisha vituo ambavyo vitakuwa vinawakusanya vijana hawa.

La kwanza, ni kwamba kwa wale ambao tayari wamekwishaathirika na madawa haya ya kulevya sawa watapelekwa watu kufanya kazi. Lakini wale ambao tayari wamekwishaathirika Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuanzisha vituo maalum vya kuwakusanya vijana hao kwa sababu wako ambao tayari wameshaathirika. Lakini wanataka kurudia hali yao ya kawaida kama zamani ili waweze kupewa matibabu maalum na kurudia hali ya kawaida? Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa wanaotumia madawa ya kulevya ndio chanzo kuwajua wale ambao wanauza madawa ya kulevya. Na yapo maeneo kabisa maalum ambayo yanajulikana kwa ajili ya kuuza madawa ya kulevya kwa mfano eneo la Kinondoni kuna Mtaa fulani mimi nadhani hata Serikali mnafahamu kama hamjui basi mimi nitaomba mje mnione ili niwaelezee na ni waelekeze mpaka muende katika hiyo sehemu. Sasa kama maeneo kama haya yako wazi kwa nini Serikali haiendi kuwakamata au kuwafuata wale vijana wanaotumia madawa ili wawaonyeshe wale ambao huwa wanawauzia na muweze kuwakamata na kuzuia kabisa vitendo hivi vya kuuza madawa ya kulevya ovyo ovyo kwa sababu vijana wetu wanaathirika sana? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wale ambao wameathirika Serikali haioni umuhimu. Kama nilivyosema tangu Awamu ya Tatu mkakati huu umezungumzwa na tuko katika hatua za mwisho sisi na wenzetu wa JKT kuanzisha vituo maalum kwa ajili ya kukabili tatizo hili. Pia nimezungumza kwamba tunafanya mazungumzo na Jeshi la Magereza kuhakikisha kwamba mpango huu tunauanzisha hivi karibuni. Lakini kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi vituo kama hivi hapa kwetu havipo. Nasema Kenya wanavyo ni jambo jema lakini sisi kwa sasa hatuna lakini Mheshimiwa Mbunge avute subira na Taasisi na wadau wenzetu hawa tutalifanyia kazi kwa haraka sana.

La pili, ambalo ni gumu kidogo madawa ya kulevya. Kwamba eneo la Kinondoni maeneo yanafahamika, wauza unga wale wanafahamika kwa nini hawakamati. Labda nisisitize kwa sababu swali linahitaji takwimu na ni suala la undani kidogo nashauri Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine wa Dar es Salaam wangetusaidia kutupa

dondoo hizo ili sisi na wenzetu wa Wizara ya Usalama wa Raia tuweze kuangalia mkakati wa kuwatia mbaroni watuhumiwa hawa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mnapojibu msogee kwenye *mike* kuna watu hawasikii.

Wakati nawatambulisha wageni wale wa kutoka nje nimefanya vizuri kumtambulisha kwa sababu yuko peke yake yupo *Honorary Chancellor* wa Tanzania katika *State* ya Israel ambaye ni Bi Eric Shevic ambaye yuko pamoja na sisi ni kwamba yeye ni Muisrael lakini anawakilisha hapa ameletwa na Mheshimiwa Nyalandu. (*Makofi)*

Halafu tutakuwa na mashindano ya mbio za *VIP* kilomita 5 tarehe 22 Julai inadhaminiwa na *Cargo Star*. Sasa waandalizi wa shughuli hiyo wamekuwepo hapa naomba wasimame wote kwa pamoja. (*Makofi)*

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mwongozo wa Spika. Naona swali namba 180 halikutamkwa limerukwa.

**NAIBU SPIKA:** *I beg your pardon* kweli.

Na. 180

**Fedha Kwa Mikopo ya Wanawake Katika Halmashauri**

**MHE. MARIAM S. MFAKI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imeweka utaratibu wa kupeleka fedha kwa kila Halmashauri kwa ajili ya kuwakopesha Wanawake na Vijana; na kwa kuwa, Wanawake wameonyesha jitihada na uaminifu wa kurudisha mikopo hiyo, na kwa kuwa, fedha hizo wanazokopeshwa ni ndogo kiasi kwamba, haziwezi kuendesha mradi unaoweza kuleta faida na kuhimili gharama za uendeshaji pamoja na kupata faida ya kujikimu:-

(a) Je, mpaka sasa Serikali inatoa fedha kiasi gani kwa kila Halmashauri?

(b) Je, ni lini Serikali itaongeza kiasi hicho?

(c) Je, fedha hizo ndizo zinategemewa kuanzisha Benki ya Wanawake?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mariamu Mfaki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kupeleka Shs. 4,000,000.00 za Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake kwa Halmashauri ambazo tayari zimeshakamilisha marejesho ya fedha walizopatiwa na kumaliza taratibu za kusaini Mikataba mipya.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kuwa kwa hivi sasa Serikali haijaongeza kiasi hicho cha fedha. Hata hivyo Mfuko huu unaendelea kuchangiwa na Halmashauri husika kwa kutenga asilimia 5 ya mapato yao kwa Mfuko huu.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake hazikusudiwi kwa sasa kutumika kuanzisha Benki ya Wanawake. Aidha, Serikali itaweka miundombinu ya awali ya kuanzisha Benki hii ikiwa ni pamoja na kuwahamasisha wanawake pamoja na wananchi (mmoja mmoja na katika vikundi) ili waweze kununua hisa.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kama alivyojibu Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu suala la Halmashauri kuchangia Mfuko huu. Lakini naamini kwamba Halmashauri nyingi hazichangii mifuko hii. Je, Mheshimiwa Naibu Spika, Naibu Waziri yuko tayari kuziagiza na kusisitiza na kufuatilia juu ya Halmashauri kuchangia mfuko huu? Swali la kwanza.

La pili, ningeomba nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba nashukuru amenipatia orodha ya wale waliolipa na wasiolipa. Je, wamejiandaa au wameweka mkakati gani ili kuhakikisha kwamba wanawakopesha au wanakopeshwa fedha wale ambao hawajalipa ili waweze kulipa mikopo hiyo na ikiwezekana wasipopewa hizo fedha basi wafanye utaratibu wa kuwasamehe?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kutumia Bunge letu hili Tukufu kuhamasisha na kuzitaka Halmashauri kuchangia fedha ile asilimia 5 kama ilivyokubalika katika Bunge hili Tukufu. Kwa hivyo Waheshimiwa Wabunge tushirikiane pamoja sisi kama Madiwani kule na sisi bado tunaongea na Wizara husika (TAMISEMI) ili kuweza kuhakikisha kwamba Halmashauri zote zinachangia asilimia 5 kama ilivyokubalika.

Kuhusu suala la pili, kweli Wizara tumeshatoa orodha ya Halmashauri zote ambazo tayari zimesharejesha mikopo na zile ambazo zinadaiwa. Kwa ruhusa yako naomba tu niseme kuna Halmashauri ambazo tayari zimesharejesha mfano Halmashauri ya Sumbawanga kwa Mkoa wa Rukwa, Tunduru, Songea, Namtumbo, Shinyanga, Bukombe, Igunga, Urambo, Kibondo, Kigoma, Biharamulo na kadhalika. Hizi ni baadhi ya Halmashauri 31 ambazo tayari zimerejesha marejesho yao ya shilingi 4,000,000.00. Sisi katika kuhamasisha tulisema kwamba Halmashauri zitakazofanya vizuri

tutawaongezea tena shilingi 4,000,000.00 na tayari tumeshawaongezea kwa zile ambazo zimeshasaini mkataba tumeshawaongezea tena shilingi 4,000,000.00 kwa hiyo wamekuwa na shilingi 8,000,000.00. Kwa hivyo tunahamasisha wale ambao watafanya vizuri tutawaongezea shilingi 4,000,000.00 ziwe shilingi 8,000,000.00 ili waweze kukopesha wanawake wengi zaidi. Lakini kwa zile ambazo hazijarudisha tunazitaka zirudishe na tutawafuatilia na wahakikishe kwamba wanarudisha kwa sababu hii ni mikopo na sio hisani wala sio zawadi.

Na. 181

**Vyuo vya Maendeleo ya Jamii**

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE** aliuliza:-

Kwa kuwa, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi havijiendeshi vizuri na mara nyingi sana vyuo hivyo vinakuwa na uhaba wa wanafunzi na fedha ya uendeshaji:-

(a) Je, isingekuwa vema kwa vyuo vinavyoshindwa kujiendesha vikageuzwa kuwa Sekondari chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi?

(b) Je, ni mitaala ipi hasa inayotumika katika Vyuo vya Maendeleo?

(c) Je, kwa nini vyuo vingi hufanya vibaya na matunda yake hayaonekani kwa wanaomaliza vyuo hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, (Kigoma) napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilianzisha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi *(Folk Development Colleges (FDCs)* nchini mwaka 1975 kwa madhumuni ya kuwapatia wananchi hususan wale wa vijijini elimu na stadi mbalimbali za maisha ili kuwawezesha kupambana na mazingira yanayowazunguka katika kuondokana na ujinga, maradhi na umaskini na hatimaye kujiletea maendeleo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya mafupi sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Genzabuke lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kweli nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kwamba vipo vyuo vyetu vichache ambavyo bado vinajiendesha chini ya kiwango kinachohitajika. Lakini pia vipo vyuo vingi vinavyofanya vizuri hasa ikizingatiwa Kasma ndogo ambazo vyuo hivi vimekuwa vikipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ni miongoni mwa vyuo vichache sana hapa nchini ambavyo vinatoa mchango mkubwa sana wa kutoa mafunzo kwa wananchi vijijini. Aidha, vyuo hivi vinatoa mafunzo mbalimbali kama vile ya ufundi, stadi za maisha na ujasiriamali kwa vijana wengi hususan wale wanaomaliza Elimu ya Msingi na ambao hawakupata nafasi ya kuendelea na Elimu ya Sekondari. Wananchi wanaoishi kwenye maeneo ya vyuo hivyo ndio mashahidi wa manufaa wanayopata kutoka kwenye vyuo hivyo. Hivyo ni vyema vikaimarishwa ili viendelee kutoa elimu hii ya stadi za kazi kwa jamii zilizoko vijijini. Wizara yangu inaendelea na jitihada za kuviwezesha vyuo hivi, kwa mfano mwaka 2005/2006 Wizara ilituma fedha za kufanya ukarabati wa majengo ya baadhi ya vyuo na kadri Serikali inavyoendelea kuongeza fedha kwenye Bajeti ya Wizara, nina hakika vyuo vingi vitaendelea kutoa mafunzo bora zaidi kwa wananchi vijijini.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, mtaala unaotumiwa na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi umeandaliwa kijumla kwa kushirikisha wadau mbalimbali wakiwemo wakufunzi wa mitaala wa kitaifa kutoka Taasisi ya Elimu, Wataalamu wa masomo na fani mbalimbali zinazofundishwa Vyuoni na Wakufunzi wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Mtaala huu ulidurusiwa mwaka 2002 ambapo modula kumi (10) ziliongezwa kukidhi mahitaji yaliyojitokeza kutoka kwa watumiaji wa Vyuo hivi. Aidha, Vyuo hivi vinatumia mtaala huu kwa kuzingatia pia mahitaji halisi ya wananchi wanaoishi kwenye maeneo ya Vyuo na raslimali walizonazo.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulithibitishia Bunge lako Tukufu kuwa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vingi vinafanya vizuri na matunda yake yanaonekana wazi kwa wananchi walioko vijijini kutokana na wale waliohitimu mafunzo na kuyatumia katika kujiletea maendeleo yao huko vijijini.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri napenda kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa watoto zaidi ya asilimia 70 wanaomaliza darasa la saba huwa hawafaulu mitihani yao ya kumaliza darasa la saba. Na kwa kuwa vyuo vingi vinavyotoa mafunzo ya stadi za kazi kama vile *VETA* inabidi vichukue mtoto aliyefaulu mitihani ya vyuo hivyo. Je, Serikali ina mpango gani wa dhati wa kuvisaidia Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ili viweze kuboreshwa na kuweza kusaidia na kutoa huduma kwa vijana wengi ambao hawakupitia *VETA?*

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba tu nieleze kwamba mfano wanafunzi waliomaliza Shule ya Msingi kwa kipindi kilichopita waliofaulu walikuwa asilimia 62. Kwa hivyo wale waliokuwa hawakufaulu ni asilimia 38. Lakini waliochukuliwa katika hao 62 walichukuliwa asilimia 49 kwa ujumla wake maeneo mengine walikwenda mpaka asilimia 70 lakini waliochukuliwa walikuwa pungufu ya asilimia 30. Kwa hivyo ni kweli kabisa kama alivyosema mbunge kwamba asilimia 38 wale ambao hawafaulu na asilimia

40 na zaidi ya wale ambao hawapati nafasi kutokana na ufinyu wa shule zetu za Sekondari wanakosa fursa ya kuweza kujiendeleza na kuwa na mchango katika jamii hii.

Kwa hivyo, Wizara kwa kutambua hili tuna mikakati madhubuti kabisa kuviimarisha vyuo vyetu ili viweze vikawa na mchango mkubwa zaidi wa kuweza kuwasaidia hao watoto ambao wengi wanakuwa hawapati nafasi.

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa ni dhamira ya Serikali sasa kujenga angalau chuo kimoja kwa kila Wilaya kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005 ukurasa wa 79 ibara ya 64 (b). Kwa kuwa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na Vyuo vya *VETA* vyote ni mali ya Serikali ambayo ni moja. Je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba sasa ni wakati muafaka kuunganisha vyuo hivi vya Maendeleo ya Wananchi na Vyuo vya *VETA* ili tuweze kupata matarajio mazuri zaidi kuliko yale tunayoyaona sasa katika Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Chilala kule Mtama?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba katika Ilani yetu ya Uchaguzi tumekusudia kujenga vyuo vya Stadi za Maisha yaani kama vile Masuala ya *VETA* na hizi za kwetu za Maendeleo ya Wananchi katika Wilaya zote za hapa nchini.

Lakini labda niseme tu kwamba Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vinatoa mafunzo tofauti na vile vyuo vya *VETA*. Vyuo vyetu havina mtihani wa kuingia kwa hivyo wale wanafunzi ambao hawajaanza shule kabisa ama kutokana na sababu mbalimbali wanaweza wakajiunga na vyuo vyetu. Wale waliofika darasa la saba wanaweza kujiunga na Vyuo vyetu. Kwa hivyo Vyuo vya *VETA* inabidi ufaulu mtihani wa kuingia kuanza Chuo cha *VETA.*

Kwa hivyo kwa kuunganisha itakuwa vigumu lakini kushirikiana kupo na bado tunaendelea. Wale wanaomaliza Vyuo vyetu wanafanya mitihani wanaopenda wakifaulu wanaingia katika vyuo vile vya *VETA.* Lakini vyuo hivi vinapendwa na ndio maana ongezeko limekuwa kubwa tuchukulie mwaka 2000/2001 kulikuwa kuna wanachuo 4,130, lakini mwaka 2004/2005 imeongezeka kwa mara mia tano wamefika wanafunzi 4,708 ni ongezeko kubwa sana. Kwa hivyo wananchi wanavipenda vyuo hivi kwa sababu vinamchango mkubwa.

Na. 182

**Mafanikio Yatokanayo na Utalii**

**MHE. PONSIANO D. NYAMI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ya Awamu ya Tatu na ya Nne kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii imefanya vizuri na kuongeza watalii wanaoingia nchini na kuliingizia Taifa fedha nyingi:-

(a) Je, Mheshimiwa Waziri mhusika pamoja na wataalam wake anaweza kulieleza Bunge amefanyaje hadi kuleta mafanikio yaliyopo?

(b) Je, ni mipango gani mizuri ambayo Wizara imeandaa ili kukuza na kuendeleza zaidi Utalii nchini?

(c) Je, ni vigezo gani vilivyosababisha hata tukaweza kupewa vyeti vya ushindi kwenye maonyesho ya Kimataifa ya Utalii yaliyofanyika huko Ulaya?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kumpongeza Mheshimiwa Nyami, Mbunge wa Nkasi, kwa kufuatilia kwa makini na kwa karibu maendeleo ya sekta ya utalii. Baada ya maelezo hayo naomba kujibu swali lake lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Baada ya kubaini umuhimu wa sekta ya Utalii katika kuchangia pato la Taifa, mwishoni mwa awamu ya pili Serikali ilivunja lililokuwa Shirika la Utalii *(TTC)* na kuunda Bodi ya Utalii *(TTB)* yenye jukumu la kutangaza Tanzania kama Kituo cha Utalii (*Tourist Destination*) Serikali iliandaa mpango kamambe wa uendelezaji utalii na kuanza utekelezaji wake, hivyo kuhamasisha ukuaji wa sekta.

- Aidha, Wizara kupitia Bodi ya Utalii inatengeneza vielelezo vya Utalii vyenye hadhi ya Kimataifa kwa lugha mbalimbali za Kimataifa ambazo ni: Kiswahili, Kiingereza, Kifaransa, Kijerumani, Kirusi, Kihispaniola, Kitaliano, Kijapan, Kichina na Kiarabu.
- Wizara kupitia Bodi ya Utalii inashiriki maonyesho mbalimbali ya Utalii.
- Kuwa na wakala (wawakilishi) katika masoko makuu.

- Kushirikiana na Balozi zetu katika kutoa taarifa na kusambaza vielelezo vya Utalii na kuwa wenyeji wa mikutano.

Hatua hizi zimefanya nchi yetu ijulikane zaidi, watalii kuongezeka, mapato yanayotokana na watalii kuongezeka na hivyo kuleta mafanikio kwa nchi.

(b) Ili kuendeleza zaidi sekta ya utalii, Wizara inaendelea kushirikiana na wadau wake katika kutekeleza Mpango Kamambe wa Utalii. Mipango mingine ni:-

- Kuandaa Programu ya Uendelezaji utalii.

- Kukamilisha na kutekeleza Mpango Mkakati wa miaka mitano wa kukuza na kutangaza utalii.

• Kuhamasisha utalii wa ndani kwa kuimarisha maonyesho ya *Karibu Travel Fair* inayoonyeshwa na Wizara kwa Ushirikiano na sekta binafsi. Maonyesho hayo hufanyika Arusha na Dar es Salaam.

• Kufungua ofisi za Wakala (wawakilishi) kwenye masoko mapya muhimu.

• Kuendeleza jitihada za kutafuta na kuimarisha masoko mapya ya utalii.

• Kuendelea na kuainisha vivutio vya utalii nchini kwa lengo la kuviendeleza kwa ushirikiano wa wadau na kuvitangaza ili kupanua wigo wa vivutio vyetu.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, vigezo vilivyotumika hata tukaweza kupewa ushindi kwenye Maonyesho ya Kimataifa ni kama vifuatavyo:-

(i) Jitihada za kuendeleza utalii unaomjali mwananchi.Ilikuwa ni kigezo kimoja na tukapata (Tuzo ya *TODO 1999 – German)*
(ii) Ubora wa filamu ya kutangaza Utalii. Tuliingia katika mashindano hayo tukapata tuzo *(Grant Prix 2004 Australia)*

(iii) Utalii unaojali kizazi kipya. Tuliingia katika mashindano hayo tukapata tuzo *(British Airways 2001* – Uingereza)

(iv) Nchi yenye vivutio bora kwa nchi za Kusini mwa Afrika. Tulikuwa na mashindano hayo tukaingia tukapata tuzo *(SADC* Afrika ya Kusini 2001 – 2003)

(v) Ubora wa vivutio kimataifa. (Tulikuwa na mashindano ambayo yalikuwa yanaangalia ubora Marekani 2003)

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Nami nitajitahidi niulize maswali mawili madogo mafupi na kwa majibu mafupi.

Kwa kuwa mafanikio haya yanapaswa kuendelezwa kwa nguvu zote kwa lengo la kuongeza mapato zaidi ya Taifa letu kupitia utalii. Je isingekuwa ni vizuri kila Ubalozi wetu akawepo Afisa maalum anayeshughulikia masuala ya utalii kuliko ilivyo hivi leo ambapo hata Mabalozi wengi hawajali? Pili, kwa kuwa hivi sasa nchi nyingi duniani zinajitahidi na zinajizatiti kuhakikisha kwamba zinakuza utalii kwa kuweka wana taaluma wao. Je, Serikali ina mpango gani mahsusi wa kuhamasisha wasomi walio wengi waingie katika fani hii na hata kuanzisha Vyuo vya Utalii hapa nchini ukitilia maanani kwamba hatuna hata Chuo Kikuu kimoja kinachotoa digrii ya utalii?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali kabla ya miaka ya 1980 tulikuwa na wawakilishi katika Balozi zetu ambao walikuwa wanahusika na kutangaza utalii wa nchi yetu. Lakini ilipofika mwaka 1985 utaratibu huo ulisitishwa kutokana na hali ngumu ya kifedha ya nchi yetu. Lakini hata hivyo tunao Mawakala katika nchi mbalimbali ambazo zenye masoko makuu, tumeweka

Mawakala wetu ambao nao pia wanasaidia kufanya kazi hiyo. Hali ya nchi ikiwa nzuri tutaangalia uwezekano wa kuwarudisha tena hao wawakilishi wa utalii katika Balozi zetu. Kuhusu kuhamasisha wananchi kujiunga na sekta ya utalii na pia kwa na Chuo. Sekta ya Utalii kwanza inahamasisha wanafunzi kutokea Shule za Msingi hata Shule za Awali wanapotembelea hifadhi zetu huwa hawalipi ada wanaingia bure hiyo nayo tunaona ni njia mojawapo ya kuwapatia kivutio cha aina fulani. Lakini vile vile huwa kuna *projects* zinazoandikiwa na wanafunzi wetu wa Shule za Sekondari wengi wanaonekana siku hizi miaka hivi karibuni kuvutiwa na kuandika *projects* zinazohusu masuala ya utalii na idadi inazidi kuongezeka. Lakini vile vile Chuo chetu cha Utalii ambacho tunacho sasa hivi kimeanza nacho kutoa mafunzo ya ngazi ya diploma na Serikali yetu kwa kushirikiana na Serikali ya Ufaransa tuna mpango wa kujenga Chuo cha Utalii mjini Dar es Salaam. Kiwanja kimeshapatikana

**NAIBU SPIKA:** Nadhani majibu yametosha. (*Makofi)*

Na. 183

**Ubora wa Hoteli Nchini**

**MHE. CAPT GEORGE H. MKUCHIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika nchi nyingi duniani watu hutambua ubora wa hoteli kwa kuzingatia daraja la hoteli husika (yaani *one star hotel, two star hotel* au *five star hote*l na kadhalika) na kwa kuwa, katika nchi yetu hoteli hazijapangwa katika madaraja hayo na hivyo kuwapa shida wageni wanapohitaji kujua ubora wa hoteli zetu:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa, ni wakati muafaka sasa wa kuzipanga hoteli zetu katika madaraja hayo?

(b) Kwa kuwa, bei ya malazi katika hoteli zetu ni kubwa sana hivyo kusababisha wageni wengi hasa watalii kufikia *guest house*s; Je, Serikali ina mpango gani wa kukutana na wamiliki wa hoteli hizo ili kuangalia upya gharama za hoteli zao?

(c) Kwa kuwa, wafanyakazi wa hoteli nyingi wengi wao wakiwa ni wasichana hulipwa mishahara midogo hata kama wahusika wamepitia katika vyuo vya Utalii au kuwa na diploma au shahada ya uongozi wa hoteli?

Je, Serikali haioni kuwa, kuna umuhimu wa kuzungumza na wamiliki wa hoteli hizo ili waweze kuongeza mishahara ya wafanyakazi hao?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Capt. Mkuchika, Mbunge wa Newala, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kazi ya kupanga hoteli katika madaraja ni jukumu ambalo linafanywa kwa pamoja kwa nchi zote tatu za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa kuzingatia ibara ya 115(2) ya Mkataba wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, nchi wanachama ziliunda Kamati ya Wataalamu 15; wataalamu watano toka kila nchi. Kazi kubwa ya wataalamu hao ilikuwa ni kuhuisha vigezo vya nchi hizi tatu ili kuwa na aina moja ya vigezo vitakavyotumika katika nchi za Jumuiya. Kazi hiyo ilianza Novemba, 2000 na hivi sasa imeshakamilishwa. Wizara yangu kwa hivi sasa; imeanza kazi ya kubaini hoteli (*hotel inventory*) katika mikoa mbalimbali ikiwa ni hatua mojawapo ya matayarisho ya kazi ya upangaji hoteli katika madaraja. Kazi hii inaenda sambamba na ushauri/ukaguzi wa kubaini kwa kiasi gani hoteli zimezingatia sifa za msingi za kusajiliwa na hivyo kuweza kupangwa katika madaraja. Lengo letu ni kuwa na taarifa za hoteli za nchi nzima. Wizara imefanya *Inventory* katika mikoa 10 hadi sasa. Hatua hii itafuatiwa na *a Pilot Hotel Classification* ambapo tumejiwekea lengo la kuwa katika madaraja hoteli za angalau mikoa 3 ifikapo mwisho wa mwezi Juni, 2007.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, bei za hoteli hazipangwi na Serikali bali soko la eneo hilo ndilo linaloelekeza bei za huduma hiyo. Wizara itaendelea na kusimamia uboreshaji wa huduma zinazotolewa na hoteli katika maeneo mbalimbali.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu swali Na. 82 la Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mbunge wa Mkoani, la tarehe 26 Juni, 2006. Kisheria waajiri wote nchini wana uhuru wa kujipangia viwango vya mishahara ili mradi viwango hivi hawalipwi chini ya kima cha chini kinachopangwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha hali ya kipato cha wafanyakazi, Wizara kwa kushirikiana na wadau kama *Tourism Conferation of Tanzania (TCT), Hotel Association of Tanzania (HAT),* Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana na *CHODAWU* itaandaa mkutano wa pamoja ili kuyachambua kwa umakini matatizo haya na kuyatafutia ufumbuzi. *(Makofi)*

**MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwanza nataka niwapongeze Watanzania wenzangu na wawekezaji katika kusimamia shughuli za watalii kwa mafanikio mazuri tuliyokwishapata mpaka sasa. Swali langu nilitaka kujua kwamba je, Serikali inakubali kwamba watumishi wanaofanya kazi katika hoteli za kitalii hawalipwi vizuri na nikasema hapa ndani hasa wasichana ambao wamesoma mpaka *form four* wana *Diploma* wanapata mshahara wa shilingi 40,000 Dar es Salaam, hawana nauli ya kwenda kazini?

Nataka kujua je, Serikali inawasaidiaje watu hawa? Majibu ya maswali haya Mheshimiwa Waziri ninaomba niyapate.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu katika swali langu la msingi nimeeleza kwamba wenye hoteli wote wanatakiwa walipe mishahara ya wafanyakazi wao ambayo haitakuwa chini ya kima kilichowekwa na Serikali, na nimeeleza kwamba ili kuboresha kipato cha wafanyakazi

Wizara ya Maliasili na Utalii itakuwa na Mkutano wa pamoja na wadau kama nilivyotaja *Tourism Confederation of Tanzania, Hotel Association of Tanzania* na Wizara ya Kazi, Ajira na Mendeleo ya Vijana tutakuwa na kikao cha pamoja kuangalia maswala hayo. *(Makofi)*

Lakini kama Mheshimiwa Mkuchika kuna hoteli ambazo unazifahamu kwamba kuna tatizo hilo, tafadhali tuonane twende tukafanye uchunguzi zaidi katika hoteli hizo.

Na.184

**Ufundishaji wa Masomo ya Taaluma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam**

**MHE. GODFREY W. ZAMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa, baadhi ya kozi zinazofundishwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kama vile Sayansi ya Siasa, Biashara, Ualimu, Uhandisi, na taaluma za maendeleo *(Development Studies)* zinakuwa na wanafunzi zaidi ya 500 kwa kozi moja na hivyo kuwafanya Wahadhiri kufundisha kama vile wanahutubia mikutano ya hadhara:-

(a) Katika mazingira ya namna hiyo, je, Serikali haioni kwamba anachopata mwanafunzi si elimu bora bali ni bora elimu?

(b) Je, Serikali ina mipango gani ya kurekebisha hali hiyo ili wahadhiri wafundishe idadi ya wanafunzi wanayoweza kuimudu na kufuatilia maendeleo ya mwanafunzi mmoja mmoja kwa urahisi zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia naomba kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, wanataaluma wanaofundisha Vyuo Vikuu wanaitwa Wahadhiri na njia inayotumika kufundisha huitwa mihadhara. Kufundisha kwa njia ya mhadhara/kuhutubia ni moja ya njia rasmi zinazotumika kufundishia wanafunzi katika Vyuo Vikuu.

Hivyo Mhadhiri kutoa mhadhara kwa wanafunzi wengi haimaanishi kwamba ni kufanya elimu itolewayo kuwa hafifu. Aidha idadi kubwa ya wanafunzi wanaohudhuria mhadhara kwa wakati mmoja, sio kigezo cha kupima ubora wa utoaji elimu katika vyuo vikuu. Kwa kutumia teknolojia ya kisasa wakati wa mihadhara, Mhadhiri anaweza kuwafikia wanafunzi hata zaidi ya 1000, kwa wakati mmoja bila kuathiri ubora wa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ubora wa elimu katika taasisi za elimu ya juu, hupimwa kwa vigezo vingi. Miongoni mwa hivyo ni udhibiti wa programu

zinazofundisha katika vyuo vyetu vya elimu ya juu ambao hufanywa na tume ya vyuo vikuu Tanzania yaani *Tanzania Commission for Universities* na kigezo kingine ni ripoti na maoni yatolewayo na watahini wa nje yaani *external examiners* kwa mujibu wa utaratibu hawa huitwa kuratibu viwango vya elimu inayotolewa. Aidha ukaguzi maalum wa shughuli za kitaaluma, katika vyuo vikuu *Academic Audit* hufanyika kila baada ya miaka minne hadi mitano ili kufahamu ubora wa taaluma chuoni. Kwa hali hiyo napenda kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge kuwa elimu itolewayo katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ni elimu bora na si bora elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo tuna ushahidi wa wanafunzi wanaotoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwenda vyuo vikuu vya nje kusoma Shahada za Uzamili yaani *Masters* Hawa wana rekodi ya kufanya vizuri, hii kuthibitisha kwamba elimu waliyoipata kwenye msingi wao Shahada ya Kwanza ilikuwa elimu bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kumwambia Mheshimiwa Mbunge, kwamba tunao uthibitisho mwingine kupitia ripoti ya *Webo Matrix*" Shirika la Kimarekani, ambao walikipatia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam nafasi ya Kwanza kitaaluma kwa vyuo vikuu vya Kusini mwa Jangwa la Sahara na Kaskazini mwa mto Limpopo. *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Moja ninataka kujua kuna habari zinazosema kwamba kwa sababu ya idadi ya wingi wa wanafunzi madarasani Wahadhiri wanalazimika kuwatungia wanafunzi mitihani ya kuchagua yaani *multiple choices* kama ni kweli je, maswali kama hayo yanamsaidia mwanafunzi katika ngazi ya Chuo Kikuu kweli kuweza kupata Tuzo *of analysis au reasoning?*

Swali la pili, sasa hivi *rate* ya kufeli hasa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na hili nalisema ninaushahidi kwamba kwa mwaka mmoja uliopita zaidi ya nusu ya wanafunzi wa *faculty of law* walifeli mitihani yao. Je, hii si kutokana na wingi wa wanafunzi ambao walimu wanashindwa kumudu kufundisha sawasawa?

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri yaliyotolewa na Naibu Waziri napenda kujibu maswali mawili madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Zambi kama ifuatavyo:-

Kuhusu mitihani ya aina ya *multiple choices* amelitamka Mheshimiwa Mbunge lakini kuna taratibu za vyuo ambapo tulikubaliana kwamba ili kuongeza ufikiri wa watahiniwa maswali ya *multiple choices* kwa kadri inavyowezekana yasitumike. Sasa kama Mheshimiwa Mbunge anaushahidi wa kutosha juu ya hili tunasema tutalifuatilia ili kusudi tuweze kubaini hili alilolisema.

Kuhusu kufeli kwa wanafunzi wa sheria, nafikiri hii ilikuwa ni miaka mitatu iliyopita. Baada ya tukio hilo tume iliundwa palepale Chuoni ikijumuisha wajumbe ambao walikuwa wametoka nje ya Chuo wamelifanyia kazi na wamefanya marekebisho

ambayo yanahitajika na sitegemei tena kwamba jambo hilo litajitokeza na sidhani kama hili lilitokana kwa sababu ya wingi wa wanafunzi.

Kuna namna mbalimbali za kutoa hii mihadhara kama alivyoeleza Naibu Waziri. Kuna *facilities*, siku hizi si lazima mwanafunzi aonane uso kwa uso na mwalimu. Kuna e-*learning* hapa tunaweza tukakaa katika lile Jengo la Bunge la zamani, wengine wakakaa hapa na wengine wakaa mahali pengine lakini Mhadhiri anakuwa mmoja, ninyi mnamwona tu na mnaweza mkauliza hata maswali. Wengi mnafahamu juu ya *Conference Facilities* na vyuo vyetu sasa vinajitahidi kuweka taratibu za namna hiyo ahsante sana

**NAIBU SPIKA:** Swali la mwisho, natumia muda huu kwa sababu nilifanyakazi ya kutambulisha baadhi ya wageni na niliwatambulisha wote ni orodha hii yote. Kwa hiyo, wote mliyoniandikia kuhusu wageni wenu. Wageni wote nawakaribisheni na hii ni *Public Gallery* mnaweza kushinda humu au mkaenda mkarudi.

Na. 185

**Udhibiti wa Mitaala katika Vyuo Vikuu**

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR** aliuliza:-

Kwa kuwa moja ya changamoto inayovikabili Vyuo Vikuu pamoja na taasisi zingine ni kubadili mitaala yao kwa lengo la kutoa wahitimu wenye kukidhi haja ya soko la ajira *(Labour Market):*-

(a) Je, tayari vyuo vyetu vimeshafanya hivyo?

(b) Kama bado. Je, Serikali haioni kuwa hatuendi sambamba na mabadiliko ya dunia?

(c) Je, soko la ajira linachukua Watanzania kiasi gani kwa mwaka?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu Mzee Ngwali Zubeir, Mbunge wa Mkwajuni Zanzibar, swali lake namba 185 kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Vyuo Vikuu kupitia mitaala na kuiboresha ili iweze kukidhi mahitaji ya soko la ajira ni la kudumu, kwani vyuo vyetu hupitia mitaala yake mara kwa mara. Kama tunavyofahamu ya kuwa hapo awali wahitimu wa vyuo vikuu walikuwa na uhakika wa kupata ajira baada ya kuhitimu masomo yao. Hali hiyo imebadilika kutokana na utandawazi na hivyo kusababisha vyuo vikuu kubadilisha mitaala yake mara kwa mara ili kuwawezesha wahitimu kukidhi mahitaji ya soko la ajira ikiwa ni pamoja na kujiari wenyewe.

Aidha, kuwepo kwa umoja wa Afrika Mashariki na Kati kumeongeza ushindani katika soko la ajira na hivyo kuvilazimu vyuo vikuu nchini kubadili mitaala yake ili kukidhi mahitaji ya soko la ajira katika nchi hizo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, majibu ya sehemu (a) hapo juu inafuta umuhimu wa kujibu sehemu (b).

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, swali la sehemu (c) linahusu zaidi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Lakini hata hivyo naomba kujibu kuwa utafiti uliofanywa na Ofisi ya Rais Mipango, kupitia kitengo cha Takwimu cha Taifa, katika kitabu chao cha *Economic Survey* cha 2004 kuna taarifa zifuatazo:

Katika mwaka 2000/2001 watu waliokua na uwezo wa kufanya kazi *active labour force* walikuwa 17.8 milioni, kati ya hao 650,000 – 750,000 huwa wanapata ajira kila mwaka katika maeneo yafuatayo, kilimo huchukua asilimia 84, asilimia 6.0 huingia katika sekta isiyo rasmi. asilimia 4 huingia katika sekta binfsi asilimia, 3.5 huajiriwa katika kazi za nyumbani *domestic work* asilimia 2.0 huajiriwa Serikalini na asilimia 0.5 huajiriwa katika mashirika ya umma.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali yamekwisha na muda wake umekwisha, matangazo. Kwanza kabisa Mwenyekiti wa Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa Lindi Mheshimiwa Mudhihir anaomba Wabunge wa Mkoa huo wakutane *Canteen* mara baada ya Maswali.

Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, Mheshimiwa William Shellukindo, anawatangazia wajumbe wake kwamba wakutane kwenye chumba Namba 219, W*ing B* ghorofa ya pili kuanzia saa tano asubuhi hii.

Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje Mheshimiwa Anna Abdallah anawatangazia wajumbe wake wakutane chumba namba 231, ghorofa ya pili, saa nne na nusu asubuhi hii.

Mwenyekiti wa Kamati ndogo ya Ulinzi na Usalama Mheshimiwa Kanali Feteh Saad Mgeni, anawatangazia wajumbe wa Kamati hiyo wakutane kwenye ukumbi namba 133, saa tano asubuhi. Baada ya kusema hayo naomba nieleze yafuatayo:

Tarehe 6 Julai, 2006, wakati Bunge likikaa kama Kamati ya Matumizi kupitisha vifungu vya Makadirio ya Waziri wa Kilimo Chakula na Ushirika, Mheshimiwa John Momose Cheyo, Mbunge wa Bariadi Mashariki, alitamka kuwa: “Mfuko wa Wakulima wa Pamba unaliwa na wajanja wakati Serikali inajua.” Mheshimiwa Spika, alimtaka Mheshimiwa John Cheyo athibitishe usemi huo na alipewa muda hadi tarehe ya leo tarehe 11 Julai, 2006. Mheshimiwa Cheyo ameandika barua ya maandishi akiomba apewe muda zaidi wa kutafuta ushahidi huo.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Spika, ameniagiza kuwa Mheshimiwa John Cheyo ameongezewa muda wa kutafuta ushahidi huo hadi tarehe 13 Julai, 2006 saa tano asubuhi ampelekee Spika, *document* hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Zambi nakushukuru kwa kukumbushia jambo hilo. Kwa hiyo, inaonekana Waheshimiwa Wabunge mko makini. Baada ya hapo Katibu, endelea na *Order Paper. (Makofi)*

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

*Kusomwa Mara ya Kwanza.*

Muswada wa Sheria kwa ajili ya kufanya mabadiliko katika Sheria mbalimbali za Fedha na Kodi kwa madhumuni ya kutoza au kubadili viwango vya Kodi na Ushuru wa Mwaka 2006. *(A Bill for an Act to Impose and alter certain Taxes and to amend certain written Law Relating to the Collection and Management of Public Revenues Bill for the Year 2006.)*

*(Muswada uliotajwa hapo juu ulisomwa kwa Mara ya Kwanza Bungeni)*

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2006/2007 Wizara ya Maji.**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. LAUS O. MHINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote nataka nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa hii ya kuwa hapa. Kabla ya yote napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Maji kwa hotuba yake nzuri na si hotuba tu bali kwa ufuatiliaji wake wa karibu kuhusu masuala ya maji. Vilevile sitasahau kumpongeza Naibu Waziri wa Maji pamoja na Wizara nzima kwa ujumla kwa maandalizi mazuri ya huduma za maji kwa ajili ya mijini na vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda niipongeze Serikali ya awamu ya nne kwa makusudio yake ya dhati ya kukabiliana na tatizo la maji safi kwa Ari mpya, Nguvu mpya na Kasi Mpya. Baada ya pongezi zote hizo pamoja na shukrani napenda sasa nianze kuchangia masuala ya sekta ya maji japo itakuwa mchango mfupi tu.(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda mchango wangu uzingatie sana utekelezaji na malengo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM na ahadi alizotoa Mheshimiwa Rais wetu wakati wa kampeni hususan alipotembelea Jimbo langu la Korogwe Vijijini. Kutokana na maandalizi ya kitabu hiki ambacho amekitoa Waziri wa Maji, nimepata kidogo wasiwasi kama kweli ongezeko kufikia asilimia 65.0 ifikapo mwaka 2010 tutalifikia. Nasema

hivyo maksudi kwa sababu kutokana na takwimu zilizopo humu zinasema kwamba ongezeko ukichukulia la mwaka 2004/2005 ni asilimia 0.2 tu. Kama tutachukulia ongezeko hilo inamaana kufikia lengo letu la asilimia 65.0 itatuchukua si chini ya miaka 50. ina maana mpaka mwaka 2055 ndiyo tutafikia lengo la wananchi wa vijijini kupata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii kidogo inanipa wasiwasi, na elewa wazi kabisa kwamba ameweka kigezo kikubwa kwamba lengo hilo lilikuwa pungufu kutokana na ukame. Lakini suala la ukame ni suala ambalo kwa kweli kwa maoni yangu tusiliweke maanani sana kwa sababu hali ya joto duniani inazidi kuongezeka.

Kwa hiyo ni suala ambalo litakuwepo kwa hiyo mimi najaribu kuzungumzia hilo ili kujaribu kutafuta sababu nyingine au vyanzo vingine vya kuikuza hii asilimia 0.2 tufikie lengo letu lile la asilimia 2.0 ambalo ndilo linaloweza likatufikisha mwaka 2010 kufikia *target* yetu ya asilimia 65.0 ya wananchi wa vijijini wapate maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nizungumzie suala la maji hususan katika Wilaya ya Korogwe ambako ndiko nitokako. Korogwe tunabahati moja tumezungukwa na milima. Kwa hiyo, Korogwe tunaishi mabondeni. Kwa kweli suala la ukosefu wa maji isingepaswa tuwenalo, nasema hilo maksudi kwa sababu chemchem tulizonazo zingeweza kabisa zikatosheleza kama zingekingwa na kutumika kikamilifu. Uhaba wa maji wa Wilaya ya Korogwe hususan Korogwe Vijijini.

Kwa kweli haupaswi uwepo, na hii ninaidhihirisha kabisa usemi wangu tukichukulia hivi sasa kwa mfano Wilaya ya Handeni au Mji wa Handeni, maji ya Mji wa Handeni yanatokea Korogwe. Kitu kibaya ambacho kidogo kinashangaza sielewi hizi *policy* au hii *policy* ya maji inakuaje. Utakuta Korogwe yenyewe inashida ya maji hatuwezi kukayatumia maji yale ambayo yanatoka katika kijiji ch Tabora. Kijiji cha Tabora kipo katika Wilaya ya Korogwe Jimbo la Korogwe Vijijini, tuna shida ya maji watu wanaugua kipindupindu kila mara lakini maji yale hatuwezi tukayatumia sisi watu wa korogwe bali wanatumia watu wa Handeni. (*Makofi*)

Kama yangekuwa ni ya uchache tu tungesema labda kuna sababu lakini ninaimani kabisa maji yale ni mengi yanaweza yakatosheleza kwa Korogwe na huko Handeni wakapata bila matatizo yoyote. Kwa hiyo, hapo labda kidogo tunge badilisha hizi *policy* zetu za maji huenda ingekidhi suala la maji kwa wananchi wa Korogwe. Hii ni sawasawa na mtu Mwaza leo tunatoa maji ya Ziwa Victoria kuwapelekea watu wa Shinyanga na hali ya watu wa Mwanza wanashida. (*Makofi*)

Watu wa Korogwe kwa kweli tunahitaji maji na ninaweza nikasema kabisa kwa dhati kwamba tunahitaji maji yetu wala si maji ya mtu mwingeni, ni yaleyale yanayotokea Korogwe ili tupate kuokoa maisha ya wananchi wa Korogwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda kama nilivyotangulia kusema kwamba mchango wangu hauta chukua muda mrefu, naomba tu nijaribu kueleza machache ambayo watu wa Korogwe watu wa Jimbo la Korogwe Vijijini, wamenituma wameniomba niyalete.

Wananchi wa Jimbo la Korogwe Vijijini, wameiomba Serikali yao ya awamu ya nne yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza idadi ya visima virefu kama ilivyokatika mradi wa maji na usafi wa mazingira vijijini iongezwe kwa kuzingatia ukubwa wa Jimbo letu la Korogwe Vijiji. Korogwe Vijijini linaukubwa wa eneo za kilomita za mraba zisizopungua 3,350. Kwa kweli ni Jimbo kubwa sana.

Leo tukipatiwa katika mradi huu vijiji vitano tu, kwa kweli kidogo hapa panatia namna ya sijui niseme mashaka au sijui nitumie neno gani. Korogwe Vijijini ina vijiji visivyopungua 122, na ina wakazi wasiopungua 210,000 hebu imefika wakati tuifikirie hii Korogwe Vijijini, kuwapatia maji ili lengo letu ifikapo 2010 wananchi asilimia 65.0 wapate maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nimeagizwa na wananchi wa Korogwe Vijijini, ni kuhusu Mji wa Mombo, Hale na Mji wa Magoma. Miji hii inakuwa kwa kasi kubwa sana, hebu suala la maji litizamwe kwa mapana na marefu katika miji hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu ni kuhusu visima ambavyo tayari tunavyo bahati nzuri Mkoa wa Tanga tulipata mradi mmoja unaitwa *TIRDEP.* Tulichimbiwa visima vingi na Wajerumani. Katika Wilaya ya Korogwe katika Jimbo langu la Korogwe Vijijini tulifaidika sana na mradi huu.

Lakini kibaya zaidi ni kwamba visima vingi katika mradi huu vimekufa. Kwa hiyo, nadhani wakati tunasubiri ule mradi wa *Wold Bank* ni vizuri visima hivi tungevifufua tujaribu kuokoa kuwasaidia mama zetu, dada zetu, wanaoishi karibu na maeneo haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jingine linalofuatia Wilaya au Jimbo langu la Korogwe ni Jimbo ambalo linamchanganyiko wa wakulima na wafugaji. Nimeombwa na wenzangu wafugaji nifikishe ombi hili mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba tunahitaji malambo katika maeneo ya wafugaji ili nao wafaidike na matunda ya awamu hii ya nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi la mwisho kabisa ambalo kwa upande wangu naona ni la msingi. Kidogo nadhani katika utamaduni wetu tumesahau utamaduni wa kufanyia matengenezo mali tulizonazo. Ninaiomba Wizara yetu ya Maji ijaribu, tuwe na kitu tunakiita *Culture of Maintenance. (Makofi)*

Nimeongelea hapa visima vidogo ambavyo tunavyo kwa kweli matengenezo yanayohitajika pale ni madogo madogo. Matengenezo labda yanayohitaji kiasi cha shilingi 200,000/- mpaka 300,000/- kwa kisima kimoja. Lakini kwa sababu zisizofahamika matengenezo haya yamesahaulika kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kupenda kutoa shukrani zangu labda na kutoa sifa kwa Idara ya Maji katika Wilaya ya Korogwe, juu ya mambo yote haya magumu lakini naweza nikasema kwa kweli wanajitahidi kwa nguvu zao zote za kuondoa tatizo la maji katika Wilaya ya Korogwe hususan nazungumzia Jimbo la Korogwe Vijijini. Baada ya hapo naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia, ahsante. (*Makofi*)

**MHE. DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninapenda nitoe machache kuhusu mjadala huu. Kwanza kabisa na mimi naomba niwapongeze na niwape pole wale wanaoshughulikia maji, Mhshimiwa Waziri Stephen M. Wasira, Mheshimiwa Naibu Waziri, Shamsa S. Mwangunga - Manafunzi wangu na Katibu Mkuu, Rutabanzibwa.

Hii kazi wanayoifanya, *I don't envy them*. Baada ya kusema hayo, ninapenda tu niseme kwamba kwa kweli maji nchini yanatizamwa kwa sura ya vipande vipande. Na kama kweli tunataka kuiondoa Tanzania kutoka katika nchi ambayo haikuendelea, kuifikisha mahali ambapo nchi zingine zimefika, hatuwezi tukaendelea kufanya *budgeting* ya namna hii katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya maji mimi ningewaomba wanaohusika waanze kuyaangalia kwa makini zaidi na kupeleka rasilimali kubwa huko kwa sababu nchi zilizoendelea, zimeendelea kwa sababu ya maji, nishati na watu wake katika kuwafundisha na kuwapa uwezo wa kukabiliana na mambo kisayansi na teknolojia. Katika Wizara hii, maji yanabebwa na wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumza kutekeleza *MDGs* na mambo mengine ambayo mataifa mengine yanazungumzia, huwezi kui-*Industrialize* na maji ya ndoo! Ati unafanya *Industrialization* na ndoo kichwani! Dar es salaam ambalo ni Jiji kubwa, unaona watu wamebeba maji kichwani. *Industrialization* itatoka wapi! Tunazungumza visima vifupi vya watu binafsi navyo ni ndoo tupu. Una-*Industrialize* nchi! Hili suala siyo hata la Waziri Stephen M. Wasira, ni suala la *Government* nzima kulitizama kwa makini kama kweli tunataka kupiga hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia katika magonjwa yetu, mengi ni *waterborne diseases*. Ni kichocho, ni kuharisha, kuhara damu, minyoo, ndiyo inayochukua Bajeti ya Wizara ya Afya! Haya magonjwa mengine ambayo ni ya kimaendeleo ni machache. Lakini bado tuna mambo ya kipindupindu, yote hayo ni magonjwa ya kutoendelea, ya kutokuwa na maji. Kwa hiyo, kama tunataka kuyaangalia hatuwezi tukapiga hatua, tukasema tunaondoa umaskini, bila maji! Bila nishati! Unaondoa umaskini gani! Tunapoteza pesa bure, afadhali vyote hivyo vipengele vya kuondoa umaskini, vingepelekwa kwanza kwenye maji, watu tupate maji, tuzungumze namna ya kupiga hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia nizungumzie juu ya tatizo la watumishi. Jamani, Wilaya ya Ukerewe eti ina Fundi Bomba ndiye *Engineer*! Sasa, unamtegemea asambaze maji Fundi Bomba Kuna siku nilimzungumza, akaniambia mama mimi sina ujuzi. “Sasa, uliletwaje hapa” “Ndiye niko sasa nitumie mimi” Hajui

cha kufanya. Sasa mimi nataka kusema Wilaya kama ya Ukerewe ingekuwa haina tatizo la maji, Mkoa wa Mwanza ungekuwa hauna tatizo la maji, Mkoa wa Ruvuma ungekuwa hauna tatizo la maji, Mkoa wa Mara ungekuwa hauna tatizo la maji, Mkoa wa Kagera ungekuwa hauna tatizo la maji, Tanga, Kigoma kwa sababu ya Jiografia yake. Una Mto Malagarasi, unashindwaje kuwapa watu wa Kigoma maji! Una Ziwa Victoria, unashindwaje kuwapa watu wa Mara, Mwanza, Kagera maji! Na ndiko kuliko na wanadamu wengi kuliko mikoa mingine yote. Sasa, tukipanga hivi vipande vipande, tutafika mahali nchi hii hatutaondoka na wote tunajua waliomo humu na wataalam mnaonisikiliza, hakuna *revolution* ya maendeleo bila maji, bila nishati, vitu viwili hivi na bila watu.

Unaniletea Fundi Bomba Ukerewe, naomba Waziri aniletee *Engineer*. Fundi Bomba peleka mahali kwingine, mimi namwomba *Engineer* wa maji kwa sababu kazi iliyopo Ukerewe siyo ya kutafuta maji, ni kazi ya kusambaza maji. Tuletee kwenye Mikoa yenye *potential*, tuanzie huko, tumalize na twende hatua kwa hatu mwaka mmoja mmoja tunasema Mikoa mitatu tumemaliza tatizo la maji, mikoa mitano tunamaliza. Ikifika miaka mitano, Mikoa 21 ya Tanzania Bara yote ina maji. Ama sivyo tukifanya huu mchezo, sasa tunaanza kuoneana wivu. Wengi tunasema mbona mahali fulani yamepelekwa, eeh sasa kama nagawa kitoweo, nisijigawie nina wazimu! Mimi hili wala halinisumbui kwa sababu halinipeleki popote. Leo nitamwonea wivu fulani, kesho nitamwonea wivu. Mimi nasema, hatuwezi kusonga mbele bila kuhakikisha tuna maji, tuna nishati na tuna watu walisomeshwa vizuri katika dhana hiyo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikumbushe Wizara hii. Mpango mahususi wa maji ulikuwepo na wa kufundisha watu. Nilikuwa Balozi India, kulikuwa na Chuo Maalum ambapo mpaka Tanzania nadhani tulijenga *Hostel* kwa kupeleka vijana wetu wafundishwe waje wafanye shughuli ya maji. Nataka nijue, ni mpango upi sasa wa *training* uliopo wa kuweza kuwa na watu. Hizi pesa tunaenda kuzipoteza. Kama unampelekea Fundi Bomba *OC*, akafanye nayo nini! Si anazurura tu kwenye gari! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, lazima tuwe na mpango mahususi wa ku-*train* watu ambao wataweza kuifanya kazi kweli ya kutuletea maji. Kule kuliko na maji, maji yasambazwe. Ndiyo teknolojia tunayoihitaji. Kule kusikokuwa na maji, maji yatafutwe. *Underground wells* zichimbwe, ndiyo visima virefu huko vinako hitajika. *(Makofi)*

Lakini pia ifanywe kwa utaratibu. Mimi nimeenda Libya, Libya hawana maji, wamechukua mafuta yale ndiyo wanayabadilisha maji. Pesa za mafuta kwa sababu hawana maji wanazifanya ndiyo pesa za kuleta maji. Wakachimba chini ardhini visima kadhaa sehemu mbali mbali, wakatengeneza ziwa *artificial*, wakatengeneza na mto *artificial* wa kusambaza maji katika Libya nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nauliza, hivi ukichukua pesa za dhahabu, ukazitafsiri zikawa ni pesa zinazoweza kuwa na mradi mkubwa kama ule wa Chalinze, mradi mzuri tu, kama ule wa kupeleka maji Shinyanga ukaupeleka Ruvuma, ukaupeleka Mwanza, ukapeleka kila mahali, kuna kosa gani, kwa sababu mali uliyonayo

unaibadilisha ili ikusaidie. Sasa isipokusaidia kama dhahabu isipomsaidia huyu Msukuma kupata maji, inamfaa nini! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hayo ndiyo mambo ambayo mimi nataka niyachangie. Lakini, lingine linaloudhi, katika Mkoa wa Mwanza kuna miradi iliandaliwa chini ya *REDEP* mwaka 1976. Leo kuna Wabunge humu walizaliwa wakati huo, wamesimama hapa wanatoa hoja.*(Makofi)*

Miradi hiyo ipo na kama Wilaya ya Ukerewe huo mradi wa Kazilankanda ambao ungeweza ku-*cover* zaidi ya vijiji 13, mpaka na matenki yamejengwa makubwa, mabomba yaliwekwa ndani mpaka na vile vichwa vya maji vilikuwa vimewekwa, ilibaki tu kukamilisha. Yako pale siku hizi wakina mama wanaanika unga juu ya matenki, ni aibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wakamalize yale madudu yanayotuonyesha aibu katika Wilaya ya Ukerewe hatutaki kuyaona. Wakitaka waje wayang'oe, tujue moja. Lakini, *that's a waste of resourses*. Kwa hiyo, hilo naliomba na iko pia katika Wilaya ya Geita. Wilaya ya Geita, Kasana, Nsela, Namtukuza yote nayo yamesimama hivyo hivyo ni magofu. Kwimba, yapo ni magofu vile vile. *(Makofi)*

Kwa hiyo mimi ningeomba, miradi yote, nimeitaja hiyo kwa sababu naijua, lakini nadhani kuna magofu mengi katika nchi nzima. Kwa sababu kama ninavyosema sisemei eneo moja, hatuwezi wa Mwanza tukaondoka kabla ya wenzetu nao hawajaondoka, itakuwa *liability* hawa watu wanaobaki nyuma. Kigoma haiwezi ikabaki nyuma, halafu mimi nikajitapa, Mheshimiwa Felix N. Kijiko kaa hapa hajafua nguo tangu alipoingia Jimboni, ati mimi nasema kwa sababu mimi natoka UK, basi mambo ni safi. UK ni Ukerewe kwa wale wasioijua. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, napenda pia niseme kwamba upangaji wa maji na mkakati wa kufanya maji yawepo hapa nchini hauwezi kuwa huu. Tunayasema hayo kwa kulia lia tu kwa shida. Haiwezi kuwa, ooh na mimi Ukerewe, na mimi sijui wapi, na mimi wapi. Tunayasema kwa sababu upangaji wenyewe ndivyo ulivyo. Lakini mimi nasema chukua mradi mkubwa kama tulivyofanya wa Mwanza, wa Chalinze, na uchukue uweke kwenye Mto Ruvuma, chukua uweke katika Mto Malagarasi, chukua weka katika Ziwa Vioctoria katika hii mikoa ambayo inazunguka na Ziwa. Fanya hivyo katika *Lake* Nyasa, Fanya hivyo katika Tanganyika, utakuwa umemaliza. Na kwa nini tunahangaika na vimiradi vidogo vidogo hivi! Tukubaliane tuje tuzungumze hapa Wabunge tupitishe, tupewe ratiba, au sivyo hii ni upotezaji wa pesa tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini, ningeomba kitu kimoja, kama tunaendelea hivyo kugawa kidogo kidogo, hakikisheni kama ilivyofanywa Wizara ya Nishati. Walisema kufika tarehe fulani, tunafikisha kila Makao Makuu ya Wilaya. Basi tuweke utaratibu, ikifika tarehe fulani, tufikishe kila Makao Makuu ya Wilaya, maji. Ikifika tarehe fulani, tufikishe kila Sekondari, maji. Ikifika tarehe fulani tufikishe kila Hospitali, maji. Mimi nadhani tutakuwa tuna lengo, angalau *it's measurable*, unaweza kupima ukasema sasa tuko wapi. Kwa mfano, nishati, sasa tunapima. Nawashukuru waliotuletea

na umeme Ukerewe na mwaka huu natumaini wanasambaza. Kwa hiyo ni kwa sababu ya vigezo hivyo na sisi tulikuwa na sauti ya kusema. Lakini, sasa Hospitali ya Ukerewe, mtu unajifungua, unamaliza kujifungua, unaenda Ziwani kufua nguo, ndiyo umalize ukabidhi mashuka ya watu na katoto kako uanze kutembea kurudi kijijini, kweli! Na hivyo hivyo hata katika Wilaya ya Bunda anakotoka Mheshimiwa Stephen M. Wasira, kukavu afadhali hata kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi ningependa niseme hivi, kopeni pesa nyingi katika hili la maji kuliko kukopea kitu chochote ndani ya nchi hii, kopeeni maji tukamilishe hii kazi kama ni miaka mitano tuikamilishe tujue tumeimaliza tunalipia maji ambayo tunayanywa. Kwa sababu Bajeti kama tutacheza nayo tusipokopa pesa za kutosha *World Bank*, katika Ma-Benki yanayojulikana. Dunia inajengwa kwa mikopo, ndiyo maana watu walioendelea hawatembei na pesa, wanatembea na kikaratasi. Kwa hiyo, mikopo tusiogope. China wana pesa, tukope China. Wana pesa! Nchi ambazo zimeweka mafuta, zimebaki na pesa. Norway wana pesa, tukakope pesa kwa sababu mafuta yalipokwenda juu, na wana mafuta mengi, wana pesa. Na sisi dhahabu yetu ime-*appreciate*. Tuchukue pesa zile tupeleke katika Mkoa wa Mwanza tumalize matatizo. Ile *advantage*, wale wanaochimba dhahabu watuambie, kwa sababu imeruka karibu mara mbili. Iko wapi ile faida, iende ikatatue matatizo ya maji katika Mkoa wa Mwanzaa.

Ninataka kusema kwa kweli nawapa pole wa Wizara hii. Nawapa pole, tunahitaji maji. Lakini, kitu ambacho mimi sikukipenda, ni juu ya wanawake. Wanawake tunadanganywa, tunapewa *lips service*, ikitokea mahali ambapo tutapata kura, “wakina mama ni muhimu” Imekuja maji, “wakina mama ni muhimu” Wakina mama ni muhimu, wanalala kwenye visima, wanaong’atwa na nyoka wakienda visimani na tumeendelea kusema katika *statement paragraph* 95, imesema hivyo hivyo.

Mimi naomba tunyamaze mpaka tutakapo waita wakina mama Watanzania tunawaambia sasa maji haya hapa. Lakini haya mambo ya kukaa tunaabiwa tuko muhimu, tunajua tuko muhimu. Tuko muhimu katika mambo yote, mpaka na kupiga kura, wote tumo humu kwa sababu ya Wanawake wa Tanzania. Hakuna Mbunge ambaye anaweza kusema hapa kwamba kama siyo wanawake wa Tanzania asingefika humu ndani ya Bunge! Kuna Mbunge hapa anayeweza kusema wanawake siyo muhimu?

Lakini, *lips service*, ni kuwadanganya wanawake wa Tanzania, wanateseka na ndoo, si vijijini, zamani tulikuwa tunasema vijijini. Afadhali sasa hata vijijini, kijijini unaweza kuwa karibu na kisima. Tizama Dar es salaam, miji mikubwa yote hii unakuta haina maji. Wakina mama wanahangaika katikati ya barabara. Kama siyo mwanamke aliyeolewa, itakuwa ni *house girl*, naye ni mwanamke. Kwa hiyo, matatizo ya wanawake na maji ukiyapambanua ni makubwa. Nashukuru ya kwamba mmeweka *desk* la wanawake, na mimi kwa sababu ni *Jender Activist*, ninaomba mnikaribishe niweze kuwasaidia kufanya uchanganuzi wa maji na jinsi unavyo-*affect* maendeleo ya wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nataka kuwapa hizi pesa kama jaribio. Kwa hiyo, naunga mkono hoja. Mwaka kesho kama Ukerewe hayo niliyoyataja hayakuwekwa kwenye makisio, hapo tutazungumza. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Waziri Mkuu amekwenda Makumira, Arusha kufungua Chuo Kikuu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mohamed Seif Khatib, Waziri wa Nchi Habari, Utamaduni na Michezo, ndiye Kaimu Kiongozi Mkuu wa Shughuli za Serikali hapa Bungeni. Kwa nini Mohamed Seif Khatib, yeye ni katika *rules* zetu tunasema, *Senior Ministers*. Kwa hiyo, ndiyo hivyo.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kutoa pole na kutuma salaam zangu za rambirambi na saalam za Wabunge, nikiamini kila mtu ameguswa na Msiba ambao Taifa limepata kutokana na kufariki kwa Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Dar es salaam, Profesa Chachage.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, napenda kuchukua fursa hii kabla sijaanza kutoa mchango wangu, kutoa pongezi kwa hatua ambazo zimeanza kuchukuliwa kutengeneza barabara ya Makoka ambayo katika hoja yangu niliyokuwa nikichangia katika hotuba ya Waziri Mkuu, nilieleza kwamba imepasuka. Kwa sasa hivi tumeambiwa kwamba hatua zimeanza kuchukuliwa. Kwa hiyo, napenda kutoa pongezi za dhati.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nianze moja kwa moja katika kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Maji. Kwanza, nipongeze pia hotuba iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri ambaye ni Mwalimu wangu kwa kiasi fulani. Nashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze moja kwa moja kuchangia kwamba hotuba hii kama vile hotuba zingine imejaa maelezo mengi, maelezo ambayo naamini kama yakitekelezeka, yatanufaisha au yatasaidia kwa kiasi kikubwa sana katika ongezeko la huduma ya maji nchini Tanzania. Lakini, ninakuwa na wasi wasi katika utekelezaji mzima wa mkakati huu kufuatana na maelezo yafuatayo ambayo nitayatoa:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya maji ya miaka ya 1990 ambayo Serikali iliitumia katika kujinadi katika Uchaguzi wa Mwaka 1995, 2000 hadi 2005 ilionyesha kwamba ifikapo mwaka 2005, watu watakuwa wanaweza kupata maji katika umbali ambao hauzidi mita 400.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi hapa tunaambiwa Sera husika ili-*fail* ndiyo maana ikaundwa sera nyingine tena. Lakini, vile vile katika Ripoti ya MKUKUTA mwaka 2005, tunaambiwa mpaka sasa asilimia 53 ya vijiji vyote vina maji na vile vile asilimia 73 ya miji imepata maji ambayo nia ni kwamba ifikapo mwaka 2010 asilimia 90 iwe imepata maji.

Lakini, cha kushangaza ni kwamba michango yote ya Wabunge wanayoitoa inaonyesha kwamba maeneo wanayotoka hakuna maji. Sasa, nakuwa nashindwa kuelewa, hivi kweli hivyo vitu tunvyoambiwa au hizo ripoti ambazo tunapewa ni za kweli au siyo za kweli!

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema hivi vile vile kwa sababu nimefanikiwa kuangalia ripoti ya utafiti ya Tume ya Utafiti wa Uchumi wa Afrika kuhusiana na Malengo ya Milenia. Ninaamini ripoti hii iko huru zaidi kuliko ripoti ambazo zinatolewa na wataalam wetu wa ndani. Ripoti hii inasema kwamba Tanzania hadi ikifika mwaka 2015 ndipo itakapoweza kutatua nusu ya tatizo la maji vijijini. Ripoti ya Tume ya Uchumi wa Afrika ambayo imejaa wataalam ambao wana uwezo wa hali ya juu na ni wataalam ambao wako huru, wanatuambia hivyo. *(Makofi)*

Leo hii tunaambiwa kwamba tayari tushavuka hiyo asilimia 50, ambayo matunda yake hatuyaoni kwa vile kila Mbunge hapa wote ambao wamechangia wanalalamika, mwingine anafikia hatua hadi ya kusema kwamba katika vijiji vyake vyote 60, hakuna maji hata kidogo. Sasa, inabidi tujiulize hizi takwimu ambazo tunaletewa, kweli zina ukweli, au unakuta kwamba kweli visima vimejengwa au kweli mabomba yamepitishwa lakini hakuna maji yoyote ambayo yanatoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, nategemea Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wakati wakinipa majibu, watanipa ufafanuzi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nataka kuzungumzia kuhusu Idadi ya miradi. Hotuba ya Waziri inaonekana ina miradi mingi sana. Sasa ningependa tufafanuliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo miradi ambayo inasemekana kwamba labda kiasi fulani kitapelekwa Mkoa fulani au Kata fulani au Kijiji fulani, hizo pesa tunazo mkononi au ni pesa ambazo tuna- *negotiate* ili tuweze kupata. Kwa sababu Mheshimiwa mmoja jana alikuwa anachangia, akasema kwamba kulikuwa na mradi wa Japan miaka mitatu iliyopita, ambao ulikuwa uanze, wakaambiwa kwamba utaanza lakini hadi leo imebakia historia. *(Makofi)*

Sasa, ni vizuri mtueleze tujue kwamba katika hili fungu, shilingi milioni kadhaa, kiasi fulani tunazo mkononi ambazo kweli zitaenda zitapelekwa katika maeneo husika kama ambavyo yanatakiwa na kiasi fulani tunategemea kuomba ambako tusitegemee sana kama tutapata ili kuondoa ile dhana kwamba mtu anakuwa na mategemeo fulani au Watanzania wanaambiwa kwamba *by* 2010, asilimia 90 ya Dar es salaam itakuwa na maji, hali ambayo sivyo! Tunaambiwa leo asilimia 73 itakuwa na maji, leo tunajua kabisa karibia kila eneo la Dar es salaam, sasa hivi hali ni mbaya kuliko ambavyo ilivyokuwa miaka 10 iliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo asubuhi Mheshimiwa Mussa Azan Zungu ameonyeshwa kwenye Televisheni akiwa anazungumza na watu wake wa Ilala. Anasema kweli mabomba yamewekwa pale lakini hayatoi maji. Wakifuatilia kwa ajili ya huduma, wanazungushwa. Kwa hiyo, unakuta vitu vinakuwa viko kwenye maandishi zaidi kuliko hali halisi.

Kwa hiyo, mimi natarajia kwamba Mheshimiwa Waziri na Naibu wake watatoa kitu ambacho kiko *concrete*, siyo tunakuwa tunaleta vitu tu maandishi tu maneno mengi, yanachanganya watu hadi wanashindwa kugundua tumetoka wapi, tunaelekea wapi na nini kilichopo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia hapo, nadhani sitakuwa na la ziada la kuongea. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nishukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Bajeti hii ya Wizara ya Maji. Lakini, pia nadhani itakuwa sijatenda haki kama kwa kweli sitaanza kwa kumpongeza kwanza Waziri wa Wizara hii Mheshimiwa Stephen M. Wassira, lakini pia Naibu wake, Mheshimiwa Shamsa S. Mwangunga kwa namna ambavyo kwa kipindi cha kwanza tu cha miezi kama sita tu wameweza kufanya kazi yao. Kuna dalili njema inaanza kuonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi zangu hizo, nadhani ziendelee tu moja kwa moja hasa kwa sababu hivi ninavyozungumza kwa kuwasiliana na Wizara hii, wamenipa taarifa kwamba katika Jimbo langu la Kibakwe lipo katika mpango wa miradi mitano ambayo ni miradi inayotokana na ile Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Labda tu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kibakwe na hasa wa Vijiji hivi ambavyo vimepata miradi hii, mimi ningependa nitoe shukrani za dhati kwa utaratibu huu mzuri wa namna ya kugawana miradi na ningependa nivitaje vijini hivyo:- Kijiji cha Kisima, Kijiji cha Uyenzele, Kijiji cha Chinyanhuku, Kijiji cha Makose na Kijiji cha Kidenge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Vijiji hivi, vimepata miradi ya maji ambayo itaanza kutekelezwa kuanzia wakati wowote kuanzia sasa. Kwa kweli hii ni hatua nzuri kama itatokea hivyo tena na mwaka mwingine na mwaka mwingine, ninaamini mpaka inapofika mwaka 2010, mimi katika Jimbo langu nitakuwa ninaongea lugha nzuri sana na wapiga kura wangu juu ya suala zima la maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini pia, katika mipango inayoendelea, vijiji vingine vyenye shida sana ya maji kama cha Mingui, Singonali, Ludewa na hata Kibakwe Makao Makuu ya Jimbo ambako maji yale hayatoshi japo ni maji ya mtiririko na kuna visima vilivyokuwepo na vimeharibika. Basi vinaweza vikaingia katika mpango wowote utakaokuja maana huu mwanzo kwa hakika ninauona una utaratibu ambao ni mzuri sana wa kugawana kutokana na Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizi, lakini bado Wizara hii ina kazi kubwa. Nimekipitia hiki kitabu chote kwa umakini mkubwa karibu mara mbili mara tatu, dalili njema zinaonekana, lakini kazi bado ni kubwa. Ni kubwa hasa kwa sababu kwa kweli si watu wote katika nchi, hata wale ambao wanasema wana maji, kama kwa mfano wanaoishi milimani kule, ni kwamba wana vijito vile vya maji mtiririko. Vile si maji ambayo ni maji safi ya kuweza kutumika na wanandamu. Kwa hiyo, bado tuna kazi kubwa na mimi naamini kwa utaratibu huu, basi baada ya muda si mrefu tunaweza tukafikia lengo lile la asilimia 65 la watu wote kupata maji katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi leo sina mengi sana ya kusema juu ya suala la maji. Lakini pia kwa sababu nafahamu kwamba Wizara hii ya Maji ndiyo *custodian* wa maji yote katika nchi hii na wote tunaotumia maji kama ni kuzalisha umeme au kwa jambo lolote lile, nadhani wao ndio wenye maji hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nichukue nafasi hii kuzungumzia suala la Wafugaji na hasa wafugaji ninao wazungumzia hapa ni wale wanaozunguka Bwawa la Mtera.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafugaji wale nimesoma hapa katika hatua ambazo zimechukuliwa na Wizara hii kuhakikisha kwamba wanatunza mazingira ili kutunza vyanzo vya maji na mambo mbali mbali ukurasa wa 10 hapa. Ni kweli tunakubaliana na hatua hizi.

Lakini hizi hatua za kutunza mazingira haya ili tuweze kupata maji ni lazima tutambue kwamba tunazichukua wakati huu wa sasa ambapo tayari kuna ukame na kuna *Conflict of Interest*. Tunasema tunataka kuzalisha umeme na watu wa umeme wanahitaji maji, lakini pia tujue kwamba kuna watumiaji wengine na kuna wanyama wengine ambao wanategemea maji hayo hayo. Sasa hapa refarii wa *Conflict of Interest* anatakiwa kuwa makini sana kuhakikisha kwamba anazingatia kwamba watumiaji wa maji haya ni watu wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika lile Bwawa la Mtera viko vijii vingi vinavyozunguka, vijiji vinavyozunguka Bwawa la Mtera vilivyoko Wilaya ya Mpwapwa kwenye Jimbo la Kibakwe na vilivyoko kwenye Jimbo la Mtera, Dodoma Vijiji. Vijiji hivi, maanake Bwawa lile la Mtera ni karibu lina umri tu wa miaka kadhaa, limekamilika kabisa miaka ya 1984. Liliwakuta hawa watu wanaishi pale, na watu hawa walikuwa wanalitegemea hili Bwawa na lile eneo lilikuwa ni *grazing area*, lilikuwa ni kwa ajili ya wafugaji na ndio maana kule kuna ng’ombe wengi sana. *(Makofi)*

Pale kuna ng’ombe kuzunguka Mtera, karibu ng’ombe 30,000 wa wenyeji ukiondoa hawa wa wageni waliokuwa wanavamia kwa ajili ya kutafuta malisho. Sasa, hapa ndipo ninaposema *there’s a Conflict of Interest* na Serikali ni lazima iwatambue hawa wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuga si laana, ni baraka. Kwa namna ambavyo tunawa-*treat* hawa ni kama vile hatuwatambui, ile si laana.

Mheshimiwa Naibu Spika, viko vijiji vinavyozunguka pale, cha Msisiri, Mdumbwi, Chungu, Chipogolo, Chinyanhuku, Uyenzele, Seluka, Kisima na Mtera yenyewe. Lakini viko vijiji vingine kama Chiboli ambako kuna ng’ombe wengi sana wanazunguka pale na wenyewe ng’ombe wale wanategemea Bwawa lile lile la Mtera na kwa sasa katika hali ya ukame huu yale makorongo ambayo huwa yana-*restore* maji na wale wanachimba chimba mle ili kunywesha mifugo yao, sasa hayakuweza ku-*retain* maji kwa sababu ya ukame na mvua zilikuwa kidogo. Lakini pia, wale watu hawana *alternative*, maana hakuna mabwawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninashauri kwamba pamoja na maagizo ambayo yametolewa na Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, kupitia Wizara ya Maji, kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu. Lakini, Waziri Mkuu alionekana kutambua umuhimu wa

kuwaangalia hawa hata tunapowaambia waondoke katika maeneo yale, alionyesha kutambua kwamba tuwaonyeshe hata njia. Lakini, mimi nasema katika hatua za sasa ambapo hatujawatafutia *alternative*, katika hatua ya sasa ambapo hatuna mahala ambapo tunaweza tukawaambia kwamba hapa mtanywesha mifugo yenu na wale watu hawawezi wakakubali wakatoka pale maanake wana asili ya pale, wamezaliwa pale, lile Bwawa la Mtera limetengenezwa limewakuta pale, hawana pa kwenda. Pamoja na umuhimu wa kutunza mazingira yale, nadhani tuwatafutie utaratibu ili na wao waweze kuyatumia maji yale. Utaratibu ambao hautaharibu mazingira yale lakini pia utawahakikishia na wenyewe kama Watanzania haki yao na ku-*enjoy* na kufurahia uhuru wa nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali ilivyo sasa, nimepata taarifa kutoka kule, wananipigia simu kwamba hawafahamu sasa wafanye nini. Wameambiwa wasogee mita 100 kutoka kwenye lile Bwawa na kwa sababu tabia ya kule kuna wavuvi pia walikuwa wamejenga nyumba zao tena za kudumu kabisa maeneo ya karibu na ndio wavuvi wengi wanapenda kushi hivyo karibu na Bwawa.

Mimi hili nakubaliana kabisa na Serikali, lakini lifanyike pia kwa uaminifu na utaratibu mzuri, kwa sababu wale watu wamejenga shule za msingi ziko kule na zimejengwa katika mazingira hayo. Kwa hiyo, wanaosimamia hili, wasimamie kwa uangalifu mkubwa. *(Makofi)*

Lakini kikubwa hapa nilichokuwa naomba, Waziri wa Maji atakapokuwa ana-*windup* mjadala huu, aseme wale watu watumieje yale maji kwa sababu hawana njia mbadala? Watumieje yale maji hata kwa kunywesha mifugo tu, wapewe *a special corridor* fulani kwamba, hapa ni kwa sababu ya kunyweshea na kuondoka. Maana yale maji ya Mtera siyo kwamba, yanatoka Mtera pale pale, yale maji huwa ni matokeo ya mikondo mbalimbali ambayo inatoka Mbeya, Iringa, Milima ya *Walter*, Singida, yanakuja tu pale. *(Makofi)*

Sasa anayetumia kama ni ng'ombe tu wanakwenda kunywa, nadhani si tatizo sana na labda niiombe Wizara ilione hilo na wao wanaomba kibali watumie maji tu kama wanavyoomba *TANESCO* kutumia yale maji. Ningeomba sana Serikali ione kwamba, ufugaji kwa kweli si laana ni baraka na neema, ambayo si wote tunaoweza kuwa na mifugo kwa sababu ni wachache wanaoweza kuwa nayo. Ni kama karama au zawadi kutoka kwa Mungu. Kwa hiyo, tuwawekee mazingira mazuri wafugaji, tuwatambue uwepo wao, lakini hata *effect* yao kwa uchumi wa nchi yetu. Ninaamini kwa jinsi Serikali hii ilivyo makini na inavyopenda watu na hasa watu hawa wa kawaida, itatoa majibu mazuri katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie na jambo la mwisho, ambalo ni maji kwa *secondary schools*. Hizi *secondary schools* tulizojenga za Kata, hazina utaratibu wala mfumo wowote na hakuna anayefahamu mpaka sasa utaratibu gani utatumika kuwapatia maji. Mimi nasema kwa hali ilivyo sasa, basi angalau tungetoa utaratibu wowote ule, kama ni kuziagiza Halmashauri au vyovyote vile, zikaweka utaratibu maalum wa kuzipatia *secondary schools* za Kata maji angalau watoto waweze kunawa hata uso tu. Shule nyingi ambazo zipo nikichukulia za Wilaya tuseme za Mpwapwa, hazina maji. Hali

hiyo inapotokea katika eneo ambalo ni *public* na ni eneo *registered* la Serikali, kwa kweli si jambo zuri sana, lakini naamini kwa sababu tunakwenda taratibu na hatimaye mwisho, tutafika kuwapatia karibu sekta zote kama inavyohitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, kwa kunipa nafasi hii na mimi kwa kuona hii mipango mizuri iliyoandikwa hapa, ambayo kwa kweli inaonekana ni ujumla wa Mpango Maalum, ambao unataka kuondoa kero ya maji nchini, ninaona sina sababu ya kutokuunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja, kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kwanza, nakushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia mjadala wa Wizara ya Maji.

Naomba nianze kwa kumpongeza sana Waziri wa Maji, Mheshimiwa Stephen Wasira, Naibu Waziri na Watalaam wa Wizara, kwa kuandaa Mpango mzuri wa Maji. Wengi tunasema kwamba, hizi bajeti zinakuwa nzuri sana, tatizo linabaki kwenye utekelezaji. Mimi naomba niamini, kama Wizara itasimamia vizuri haya ambayo yameandikwa, nadhani tutakuwa tunapiga hatua moja kubwa sana huko mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, imeanza na *preamble,* ambayo iko kwenye ukurasa wa kwanza, ni *quotation* kutoka kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Rais, aliyoitoa wakati akilizindua Bunge lako Tukufu tarehe 30 Desemba, 2005. Hii ni *commitment* kubwa sana na kama Wizara haiwezi ikajielekeza, kwa sababu hakuna aliyewaambia wachukue *quotation* hiyo, wao wenyewe wameichukua na wameona ina umuhimu, kwa maana hiyo, tunaomba waendane nayo. Kama tukiendana nayo, ndipo tutakapokuwa tunatekeleza Mpango wetu wa Maji, vinginevyo kwenye bajeti ijayo ya 2007/2008, kama walivyosema wenzangu, tutakuja tuulizane mlituletea hotuba nzuri, lakini hakuna utekelezaji.

Kuna mambo mengi sana ya msingi au sekta muhimu sana, ambazo mimi nilikuwa naomba pengine niishauri Serikali ichukulie hizi kama *priority sectors*. Maji ni muhimu sana, tunasema maji ni uhai kwa maisha ya binadamu. Kwa hiyo, ni Sekta muhimu sana. Kama zilivyo barabara na mawasiliano, kilimo, elimu, afya, nishati na maji ni muhimu sana. Kwa hiyo, nilikuwa naomba niishauri sana Wizara ya Maji, pengine inakuja na Mpango wake kama Wizara ya Elimu ilivyokuja na Mipango ya MMEM na MMES, ambayo wengi tunaona kwamba, kumekuwa na mafanikio makubwa na sasa hivi elimu yetu inapiga hatua kubwa sana. Kama Wizara inaweza ikaja na Mpango wa namna hii, nadhani inaweza ikasaidia sana katika kutatua tatizo la maji kwa wananchi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona kwenye hotuba hii pia Wilaya ya Mbozi, kuna maeneo yale ambayo wanasema maji yalipimwa yakaonekana yako maeneo 48. Lakini maeneo 48 hayo wanayosema, yako katika Kata nne tu, kwa maana ya Kata ya Kamsamba na Kata ya Tunduma, kwa Jimbo la Mbozi Magharibi, lakini pia kuna Kata ya

Vwawa na Kata ya Mlowo kwa Jimbo la Mbozi Mashariki. Sasa unasema umepima maeneo 48, lakini yako kwenye Kata nne tu na katika Kata hizo nne, inawezekana ni vijiji visivyozidi kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hii inatueleza nini, maana yake mtu anaweza kuwa *convinced* na *figure* iliyoko pale, lakini maeneo yaliyopimwa kwa kweli ni machache sana. Mimi naomba niseme kwamba, Wilaya ya Mbozi ni moja ya Wilaya ambazo ziko nyuma sana katika suala zima la maji. Hakuna Mpango wowote Kabambe wa maji katika Wilaya ya Mbozi. Hapa naomba niseme tu kwa kuanza kwamba, tarehe 31 Agosti, 2005 alipopita Mlowo na Mji wa Tunduma, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, aliyekuwa mgombea Urais kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi na ambaye sasa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliahidi kuipatia miji hiyo maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wale ambao wamefika kule au wale ambao hawajafika kule, miji hii ni miji ambayo inakua kwa kasi sana. Mji wa Tunduma unapakana na nchi yetu ya Zambia na pana biashara kubwa sana na idadi ya watu inaongezeka kwa kasi kubwa sana. Mji wa Mlowo uko Jimbo la Mbozi Mashariki, ni mji mdogo lakini unakua kwa kasi sana na biashara kubwa sana inafanyika mahali pale. Miji hii imekuwa na matatizo ya maji kwa muda mrefu sana na bado hakujawa na Mkakati Maalum wa maji katika miji hiyo na ndio sababu naamini, mgombea wetu alipopita pale alilazimika kutoa ahadi ya kutatua tatizo la maji katika miji hiyo. Lakini nasikitika sana, niliposoma kitabu kile ambacho Wabunge ambao ni Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM wote, tulipoenda Chimwaga tulipewa kitabu ambacho kilikuwa na ahadi za Mheshimiwa Rais, zile alizoahidi wakati akipita kwenye kampeni, bahati mbaya sana, ahadi ya Mheshimiwa Rais kuipatia maji Miji ya Tunduma na Mlowo haipo.

Nilimfuata Mheshimiwa Waziri wa Maji, nikazungumza naye, kwanza naye akashangaa sana kwamba, eti Tunduma haina maji. Mimi pia nilimshangaa kwamba, Mheshimiwa Waziri, anashangaa mji hauna maji na yeye amesema kwamba, ameunda Bodi sasa ameunda Bodi ya Maji kama hakuna maji! Mimi nafikiri alipaswa ajue kwamba, Tunduma haina maji na kama aliunda Bodi, basi aliunda bodi ambayo inaweka Mikakati ya kuupatia mji ule maji, lakini sio Bodi ya kuendeleza maji ambayo hayako Tunduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilimpa Mheshimiwa Waziri, nakala ambayo Mkurugenzi wa Maendeleo wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, alimwandikia kwamba, hii ilikuwa kwenye ahadi ya Mheshimiwa Rais. Tunaomba waiweke kwenye Mpango wao. Mimi nasema hatuna ugomvi, tunajua ahadi hizi ni za miaka mitano, kwa hiyo, tunaomba ikiwezekana labda mwaka ujao au mwaka mwingine wa fedha, lakini kabla ya mwaka 2010, basi tujue kuna maendeleo ya maji katika Miji ya Tunduma, pamoja na Mlowo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Mbozi, wakati wote nikapata nafasi ya kuzungumza kwenye Bunge lako Tukufu, huwa nasema ni Wilaya ya Kilimo. Tunazalisha kahawa kwa wingi sana. Tunapozalisha kahawa, inatumia maji mengi sana kuanzia ukoboaji wake mpaka hatua ya mwisho. Kama hakuna maji, itakuwa ni vigumu

sana kuweka kahawa hii katika mazingira ya ubora. Wilaya ya Mbozi tumekuwa na tatizo, kama nilivyosema, tunalima kahawa lakini tuna tatizo la maji kwa ajili ya kuoshea kahawa hii. Kahawa yetu imekuwa inakosa ubora kwenye soko la dunia, kwa sababu maji tunayotumia yamechanganyika na udongo. Kwa hiyo, wataalam wanapo-*taste* kahawa, inakuwa na *taste* ya udongo, kwa hiyo, inapata *grade* ya chini zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri nimeshawahi kuzungumza naye juu ya suala hili, analijua na mimi kwa kweli naomba nichukue sasa fursa hii, kumwomba Waziri atembelee Mbozi, aje aone mazingira ya wananchi wale wanaolima kahawa na mazingira ya visima wanavyotumia kwa ajili ya kusafishia kahawa yao. Kwa kweli napaswa nisisitize kwamba, Wilaya yote ya Mbozi kama ilivyo, ambayo ina vijiji 175, ina tatizo kubwa sana la maji. Najua pia tatizo la maji ni la Watanzania wote, kama wenzangu walivyosema, lakini ndio sababu pia nikasema ni vizuri Wizara ikaja na Mipango Madhubuti kabisa, kama ilivyokuwa kwa Wizara ya Elimu ili tuhakikishe kwamba, tatizo hili tunalitatua kwa nchi nzima.

Lakini kama tukiwa na matatizo haya, tunapeleka leo shilingi milioni kumi kwa Wilaya, shilingi milioni 100 kwa Wilaya, tutakuwa hatufanyi kazi yoyote ya maana, tunaweza tukafika miaka kumi tukashindwa kuwaeleza Watanzania kuna kitu gani juu ya tatizo la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi, tunasema kwamba, azma ni asilimia 65 ya watu wa vijijini ni lazima wapate maji safi na salama na asilimia 90 ya Watanzania maji safi na salama. Tusipokuwa makini sana, tutashindwa kuja kuwaeleza Watanzania wetu, ambao walituamini kwa sababu sina hakika kama tunaweza tukafikia hiyo azma ambayo tumejiwekea sisi.

Bahati mbaya sana katika Wilaya yetu ya Mbozi, upatikanaji wa maji kwa Watanzania waishio vijijini ni asilimia 38 tu, kama Mheshimiwa Waziri, alivyoonyesha kwenye hotuba yake kwamba, Kitaifa ni karibu asilimia 53 hivi, lakini kwetu bado ni asilimia 38. Kwa hiyo, naomba Wizara hii, ifuatilie sana. Naomba nitaje vijiji vichache ambavyo pamoja na kwamba, sehemu zote zina matatizo ya maji, labda kwa sababu ya muda nitaje tu Kata fulani fulani; Kata ya Nambizo ina tatizo kubwa sana la maji katika Jimbo la Mbozi Mashariki, lakini pia Kata ya Ivuna kwa Jimbo la Mbozi Magharibi, ina tatizo kubwa sana la maji.

Mimi nasema kwa sababu nimekwenda huko, kama wenzangu walivyosema, maji wanayokunywa kwa kweli kama hujabeba maji yako, wakati mwingine huwezi ukanywa. Lakini kwa mazingira yetu, ukibeba maji yako, ndio wanapoanza kusema huyu anataka tumpe Ubunge, anakuja na maji yake, kwa hiyo, tayari wewe wameshakufanya kwamba una kiburi. Kata nyingine ni Kata za Itaka hususan Kijiji cha Maninga, kina tatizo kubwa sana la maji; Kata ya Isansa ina tatizo kubwa la maji, lakini pia Kata ya Ruanda ina tatizo kubwa sana la maji na kuna sekondari mahali zimejengwa, hazina maji kabisa, wanafunzi wanalazimika kusafiri kwenda sehemu za mbali kutafuta maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunapozungumza hapa, tunazungumza mawazo ya wananchi ambao wametutuma. Ndiyo sababu mimi naomba niseme kwamba, tunaomba tumwalike Mheshimiwa Waziri na huu uwe mwaliko rasmi, bila shaka atakapokuwa ana-*wind up speech* yake, atatueleza kama anapanga kuja lini. Mimi ningemshauri aje wakati wa kiangazi, kwa sababu akija wakati wa masika, hii inaweza ikamdanganya kwamba, wananchi wa kule pengine wana maji ya kutosha wakati yale ni maji ya kupita tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza hilo, naomba pia nizungumze sehemu nyingine ya kuvipatia maji baadhi ya vijiji. Kule Mbozi kulikuwa na mpango mmoja wa maji, ulioitwa mpango wa kuvipatia maji vijiji vinane *(Group 8),* vijiji hivyo vipo sanasana katika Kata ya Iyura na Kata ya Ruanda. Mpaka leo, hakuna hatua yoyote iliyofikiwa. Kanisa la KKKT lilikuwa na mpango wa kuvipatia vijiji hivi maji. Lakini inaonekana kwamba, hakuna hata mtu anayefuatilia mpango huo. Lakini wenyeji wa kule, wakifuatilia kanisani wanasema kwamba, tunatafuta mwekezaji. Kwa hiyo, mimi naishauri Serikali, ichukue hatua madhubuti za kuongea na kanisa kwa sababu lilishaonyesha *interest* ya kuleta maji kule. Wizara izungumze na kanisa, tuone kama mpango huo upo au haupo, kuliko kuwaacha wananchi wakiwa na matumaini kwamba, watapatiwa maji safi wakati hawatapata hayo maji. Lakini pia kulikuwa na mpango wa kuvipatia vijiji vingine maji na pia Mradi huu ungenufaisha hata Kata ya Mlowo, ambayo ina tatizo kubwa sana. Kuna mto ambao unatoa maji muda wote, unaitwa Mto Lukululu. Mto huo ungevipatia maji vijiji 12, pamoja na Kata ya Mlowo. Lakini tatizo letu kama nilivyosema, bado Wizara haijafanya lolote. Wizara haijawasaidia wananchi wale, pamoja na Idara ya Maji kule Mbozi na kwa maana hiyo, bado tuko nyuma sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishukuru kwamba, sisi tuna mhandisi tofauti na wenzetu, ambao pengine hawana wahandisi kwa sababu ya shida. Tuna mhandisi ambaye huwa anajitahidi kadri anavyoweza, lakini kama hakuna fedha, inakuwa ngumu sana kutekeleza miradi katika Wilaya kubwa kama vile ya Mbozi. Ni kweli tuna majimbo mawili ya uchaguzi; Mbozi Mashariki na Mbozi Magharibi, lakini kwa sababu ile ni Halmashauri moja, watendaji wao wanatembea Wilaya zote. Sasa kama huna *funds* za kutosha, inakuwa vigumu sana kwa hawa wenzetu kuweza kutembelea maeneo yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza hayo, naomba tena niseme kwa kweli na napenda nichukue nafasi hii, kuishukuru sana Wizara, kwa hotuba yao nzuri na kwamba, Wilaya ya Mbozi imepewa shilingi milioni 153 katika usimamizi wa maji, siyo haba kwa sababu ya kiwango chenyewe cha fedha ambacho kiko kwenye bajeti. Lakini naomba nimalizie kwa kuisisitiza Wizara yenyewe ichukulie suala la maji katika nchi hii kama suala la kufa na kupona, lakini pia ilichukulie suala la maji kwa wananchi wa Mbozi ambao ni wakulima mahiri sana katika nchi hii kwamba, basi nawatatulia tatizo kubwa sana la maji ili wasipate tabu sana. *(Makofi)*

La mwisho kabisa, ninaomba suala la uvunaji ya maji ya mvua, Mbozi ni mojawapo ya maeneo ambayo mvua inanyesha sana katika nchi hii, lakini suala la uvunaji wa maji halipo hata kidogo. Mimi nashangaa kwamba, Wizara inasema itaanza na teknolojia hii ya uvunaji maji, kwa kuwafundisha wananchi katika maeneo machache

sana, hatuoni kwa nini iwe na maeneo machache sana. Mimi nadhani tungeanza na maeneo mengi, hususan yale ambayo kwanza, yana ukame, yanapopata mvua basi yale maji yatumike kuyatunza sawa sawa na maeneo ambayo yana mvua, lakini yana kipindi kirefu cha kiangazi kama Mbozi ilivyo, basi wananchi wafundishwe teknolojia ya kuvuna maji ili maji yale ambayo tunayavuna yasipotee. Hii kama wenzangu walivyosema, inaweza ikatusaidia sana katika kutuokoa pengine na ukame utakaotukabili siku sijazo, kama hatutakuwa makini sana katika masuala yote ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza hayo, naomba tena niseme kwamba, naunga mkono hoja kwa asilimia zote, naomba niseme hivyo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii, vile vile nakupa pole kwa matatizo ya kifamilia uliyokuwa umeyapata, naomba upate nguvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na nina sababu za kuunga kwanza, ninahitaji fedha kwa sababu bila kupata hizi fedha, Miradi katika Wilaya ya Kwimba haitafanyika. Kwa hiyo, naunga mkono hoja hii. Lakini vile vile Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watalaam wao, tukiwapatia hizi fedha, watafanikiwa na wataweza kusimamia mipango ambayo wamesema wataweza kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri na timu yake, wafahamu kwamba, bingwa hawi bingwa kwa kufanya mambo tofauti, ila anakuwa bingwa kwa kufanya mambo kitofauti. Namwomba Mheshimiwa Waziri na timu yake, wajaribu kufanya haya kitofauti. Nitajaribu kutoa mifano iliyotokea katika Jimbo la Kwimba na Wilaya ya Kwimba. Tunazishukuru Serikali zote tatu zilizotangulia na hii ya nne, kwa jinsi inavyoshughulikia mambo ya maji katika Wilaya ya Kwimba. Mwaka 1974, 1975, 1976, tulikuwa na Mradi wa kupeleka maji Tarafa ya Mwamashimba, haukufanikiwa. Chanzo ilikuwa maji ya chini ya ardhi. Ukaja Mradi wa *HESAWA,* haukufanikiwa sana lakini haukumaliza tatizo la ukame katika Wilaya ya Kwimba. Mheshimiwa Waziri, ameongelea juu ya maji ya chini ya ardhi, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, aone maji ya chini ya ardhi kama akiba yetu na aweke uzito zaidi katika kulinda mazingira ya vyanzo vya maji hayo. *(Makofi)*

Kama nilivyosema, Jimbo la Kwimba sehemu yote ni kame. Tunashukuru sana Serikali sasa hivi imekubali kutuletea maji kutoka Mradi unaopeleka maji Shinyanga na Kahama kutoka Ziwa Victoria. Kwa hiyo, tunaamini kwamba, kwa muda mrefu sana utakuwa endelevu, tofauti na vyanzo vya maji chini ya ardhi. Hata hivyo, nilitaka kumwuliza Mheshimiwa Waziri, baadaye ajaribu kunisaidia kutoa maelezo fulani, Mradi huu kwa Jimbo la Kwimba, unaleta maji mpaka kwenye tangi la Mradi wa zamani ambalo liko Mhalo. Tangi hilo lilijengwa kati ya mwaka 1975 – 1976, lilikuwa limelenga watu 39,475. Hivi sasa kuna watu 74,777 kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2002. Tangi hilo lililenga kuhudumia ng'ombe 51,255, leo kutokana na sensa ya mwaka 2002 kuna ng'ombe 1,031,864, mbuzi walikuwa 18,517, sasa hivi wako 39,069. Kipindi kile vijiji vilikuwa 17 hivi sasa tuna vijiji 18. Ukiangalia takwimu hizo utaona kwamba, tangi hilo ni dogo sana. Inawezekana katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri, atatueleza kwamba,

linategemewa kutumika kwa utaratibu gani ili liweze kutosheleza idadi ya watu walioongezeka, ng'ombe walioongezeka na vijiji vilivyoongezeka. *(Makofi)*

Suala la pili ninalotaka kufahamu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, ni ipi nafasi ya Halmashauri katika Mradi; je, mawasiliano yameshafanywa na Wilaya ya Kwimba na je, imejiandaaje kushiriki katika Mradi huu, ili Mradi huu uweze kukamilika haraka sana?

Vile vile nilipenda kufahamu, wananchi wana nafasi gani katika Mradi huo, kwa sababu hatungependa baadaye Mradi huu usifanikiwe, tunahitaji sana maji hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na maombi kadhaa kwa Mheshimiwa Waziri. Ombi la kwanza, Mradi nilioutaja unaelekezwa kwenye Tarafa moja ya Mwamashimba, ambayo ni kame. Kuna Tarafa ya Nyamilami ni kame, Makao Makuu ya Wilaya Ngudu ni pakame. Ombi langu, nafahamu kwamba, kuna Mradi ambao umeelekezwa kupeleka maji Ngudu na Hungumalwa, lakini Miradi hiyo inatarajia kutumia maji ya kutoka ardhini. Miradi ambayo nimesema kwangu mimi sioni, kwa sasa hivi ni muafaka sana kwa sababu tumeona katika Wilaya ya Kwimba, katika Tarafa ya Mwamashimba, tulitegemea kuwa na visima 37 vya *HESAWA,* hivi sasa ni kati ya visima vinne au vitano, ambavyo vinafanya kazi. Maji hayaaminiki sana chini ya ardhi. Ombi langu ni kupanua Mradi huu, ufike katika Makao Makuu ya Wilaya, Ngudu, ufike Hungumalwa, Lunele na Ilula, tutakuwa tumesaidia sana watu wa Tarafa hizo zote tatu. *(Makofi)*

Lakini ombi la pili ambalo ni ushauri tu kama nilivyoanza kusema, kwa kweli maji ya chini ya ardhi, tuyaone kama ni ya akiba. Tuweke uzito katika kutunza mazingira kwa kuhifadhi vyanzo hivyo, lakini tujielekeze kwenye Malambo. Mimi nafahamu kwamba, kila sehemu hapa nchini, tuna mito, vijito na makorongo, ambayo ni ishara kwamba, kuna maji katika maeneo hayo. Tutumie nguvu nyingi sana kukinga maji, tuzuie maji yasiende baharini na ziwani, ambako hatuwezi kuyapata kwa urahisi sana. Naomba sana Wizara kwa kushauriana na Wizara nyingine, waje na mipango hiyo. Mheshimiwa Rais sijui alikuwa anaekelea wapi, upandaji wa miti kwamba, tupande kama wendawazimu. Naomba Wizara hii nayo ishambulie mito, makorongo, kuzuia maji yasipotee na ichimbe malambo. Naamini kwamba, wananchi wetu hawaongelei juu ya maji safi na salama, tunachohitaji kwanza kabisa ni maji. Kama Serikali itakuwa na uwezo, basi ilete maji safi, kama itakuwa na uwezo zaidi ilete maji safi na salama. *(Makofi)*

Naamini watu wanao uwezo wa kuchemsha maji, kuna *water guard* na wanachohitaji ni maji. Watu wa Kwimba, wanaipenda sana Wilaya yao, hata wafugaji wanaipenda sana Wilaya yao, hawapendi kutoka nje ya Wilaya hiyo, kinachowatoa pale ni shida tu na shida kubwa ni ya maji. Naomba sana malambo yaongezwe, tunazo sehemu kama Tarafa ya Kikubiji kwa mfano, Tarafa ya Mwamalu, kuna maji ambayo yanatoka katika sehemu hizo yanaingia Itongitale yanakwenda Ziwa Victoria. Lakini kama tukiwekewa malambo au yakakingwa, tukapata maji ya kutosha, tunaamini kwamba, watu wa Kwimba hawatahama sana. Baadaye waambie kwamba, wanahitaji mazingira katika maeneo mengine.

Naomba sana Wizara ije na Mpango wa kuongeza malambo zaidi, ikinge mito na makorongo. Naamini kwamba, baada ya kupata vitu hivyo, hata Wizara ya Kilimo tunapoongelea juu ya *green revolution,* watu watalima kwa kumwagilia, hakutakuwa na matatizo yoyote ya kuwaambia mpande mboga mboga kwa sababu watakuwa karibu na maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kutakuwa na malambo na mito ambayo itakuwa imezuiwa, hata mazingira yatabadilika sana. Naomba sana ushauri huu, uzingatiwe ili tuwapatie watu wetu maji ambayo wanayahitaji, maji safi na ikiwezekana baadaye tupate maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, naunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SIRAJU JUMA KABOYONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena kuchukua fursa ya kuchangia mada iliyo mbele yetu, nayo ni bajeti ya Wizara ya Maji. Napenda nitumie nafasi ya awali, kumpa pongezi Waziri, Naibu wake na Watendaji wao, kwa kazi nzuri waliyoifanya katika utayarishaji wa bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni nyenzo muhimu sana katika maendeleo ya binadamu na nchi kwa ujumla. Upatikanaji wa maji, unafanana umuhimu wake kama vile zilivyo Sekta za Nishati, Miundombinu na kadhalika. Kwa bahati nzuri, Tanzania imejaliwa kuwa na neema kubwa ya maji. Nchi hii imezungukwa na maziwa makubwa, ina mito mingi, lakini cha kushangaza leo hii moja ya mada kubwa iliyo mbele yetu ni kwamba, nchi yetu au watu wake, hawana maji safi na salama. Tatizo ni nini? *(Makofi)*

Tatizo ni kwamba, tunachukulia upatikanaji wa maji ya salama kwa wananchi wa Tanzania katika vipande vipande. Msemaji aliyenitangulia, wakati fulani alilizungumza hili na mimi nalisisitiza. Tuna haja kama nchi sasa, kuliangalia tatizo hili kwa ujumla wake. Kwa kweli ni aibu, tuna Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa, mito mingi katikati, tunazungumzia juu ya matatizo ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri tuwe na Mipango au Mpango Kabambe wa kushughulikia tatizo la maji kinchi, siyo kiwilaya au kimkoa. Katika bajeti hii ukiiangalia kwa ujumla wake, bajeti nzima ni shilingi bilioni 170. Katika bajeti hiyo shilingi 147 ni za maendeleo. Hii peke yake inadhihirisha jinsi ambavyo eneo na tatizo hili la maji linavyohitaji kuwa na bajeti kubwa ya maendeleo. Naipongeza Wizara kwa kulielewa hilo na kupanga sehemu kubwa ya bajeti ikawa ni bajeti ya maendeleo. Lakini sasa tatizo ni kwamba, ukiiangalia bajeti hii kubwa ya maendeleo kama ilivyo, sehemu kubwa ya bajeti hii ya maendeleo inakwenda kwenye miradi michache, hususan miwili kama siyo mitatu.

Moja ni Ziwa Victoria, mwingine ni *DAWASA* na mingine ni midogo midogo tu, lakini *impact* sasa kinchi haipatikani. Kwa sababu ya upungufu wa fedha na hasa nilipokuwa naitazama bajeti yenyewe ya maendeleo, nikakuta kwamba, sehemu kubwa

ya bajeti ya maendeleo inatoka ndani. *In relative terms* kwamba, bajeti ya maendeleo ya Wizara hii shilingi 77 bilioni zinatoka ndani na shilingi 69 bilioni ndiyo zinatoka nje. Sasa kwa maana ya kuleta maendeleo, nilikuwa napendekeza tubadilishe mfumo huu. Tupate nyingi zaidi kutoka nje, tena kwa mikopo ya muda mrefu. Kuna *World Bank, African Development Bank* na sasa hivi kuna *BADEA.*

Lakini vile vile kuna *KUWAIT Fund,* wanaweza kutoa mikopo ya muda mrefu, kwa ajili ya shughuli za kijamii na hasa katika kushughulikia Sekta ya Maji. Tabora, katika s*peech* ya bajeti, Waziri ametamka bayana kwamba, Bwawa la Igombe, ambalo ndilo linalotoa maji ya Mji wa Tabora, limepungua kutoka kina cha mita tano mpaka kina cha mita moja. Katika hali ya namna hii, nilifikiria bajeti hii ingechukulia jambo hili kama jambo la dharura. Mahali pekee panapotoa maji ya Tabora, pamepungua kwa mita kutoka tano mpaka moja, lakini bado tunadhani au tunalichukulia kama jambo hili ni la kawaida.

Namshukuru Waziri na Serikali kwa ujumla kwamba, kuna Mpango utakaojumuisha Serikali ya Uswisi kulishughulikia tatizo la maji Tabora. Lakini huu bado ni Mpango, hatujui utakamilika au vipi. Sasa nilikuwa naomba kwamba, kweli Serikali itilie mkazo katika kuhakikisha tatizo hili la maji katika Mji wa Tabora, linapata ufumbuzi ukizingatia kwamba, sasa hivi maji ya Tabora yananuka, tena ya bomba lakini yananuka, maji ya bomba yana tope na hayapatikani kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, isitoshe Tabora ina Kata 21, kati ya Kata hizo zipo Kata zifuatazo: Misha, Ndevelwa, Itetemwa, Tumbi, Kalunde, Kakola, Itonjanda na Uyui. Kata hizi ziko nje ya Mji wa Tabora na kwa maana hiyo, hata huu Mradi ambao utafadhiliwa na Serikali ya Uswisi, hautozigusa hizi Kata nane. Sasa tunafanya nini, ukiangalia katika orodha ya vijiji au kama ilivyotolewa katika bajeti hii ni kwamba, kuna visima vinne vitachimbwa na pesa za msaada kwa ajili hiyo, Tabora Mjini imepewa shilingi milioni 16. Unazifanyia nini shilingi milioni 16 kwa Kata nane ambazo haziko katika mfumo wa maji ya mjini Tabora? Naiomba Wizara, ilitazame jambo hili, kwa dhamira ya kulitafutia ufumbuzi ambao utawapatia maji ya uhakika wananchi wa Kata hizi nane zinazozunguka Mji wa Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna *allocation* ya shilingi 500 milioni kwa ajili ya kuangalia mfumo wa maji ya Mji wa Tabora, Sumbawanga, Lindi, Kigoma na Musoma, imezungumzwa katika ukurasa wa 36 kipengele cha 74. Katika kipengele cha 75 kinachozungumzia ufadhili wa mambo kama hayo hayo, Tabora haimo. Lakini Dodoma ambayo imechanganywa pamoja na Tabora katika kipengele cha 74 imo. Sasa *BADEA* wataifadhili Dodoma, Uswisi wataifadhili Dodoma, lakini inapokuja Tabora ikitafutwa Tabora kwenye mikopo ya *BADEA* haimo. Vyanzo mbadala, Tabora ina matatizo ya maji, *Igombe Dam* inakauka na wala haina ukahika. Lakini Tabora iko karibu sana na Mradi mkubwa kabambe wa kuchukua maji kutoka Ziwa Victoria, yatafika Kahama, Shinyanga na yanatarajiwa kwenda Nzega, swali kwa nini yasije Tabora?

Kama haiwezekani, basi Tabora iko karibu na Mto Malagarasi. Ndiyo yale tunayoyasema, tuangalie tuanzishe Miradi Kamambe, ambayo itatuwezesha kupata maji

kutoka vyanzo ambavyo ni vya uhakika. Hata hivyo, Tabora iko karibu na Ziwa Tanganyika, nalo pia liangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma ya *drilling and consultancy services,* katika bajeti hii, huduma hii imetengewa shilingi bilioni 1.5. Mimi kimtazamo, naiona huduma hii ni muhimu sana, hasa ukizingatia kwamba, tunataka kuchimba visima vingi sana nchi nzima. Sasa kama hiyo ndiyo dhamira, shilingi bilioni 1.5 kwa kazi ambayo tunataka ifanywe nchi nzima, kwa kweli haitoshi. Napendekeza, tuangalie uwezekano wa kuongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mjini Tabora kuna sehemu ndogo sana ya wananchi ambao wanapata huduma ya maji taka. Utaratibu wa maendeleo unatutaka pamoja na mambo mengine, tuondokane na vyoo vifupi vifupi vya mashimo. Tuwe na utaratibu wa maji taka, unaoyakusanya maji na kuyapeleka mahali pengine, kisha kule yakafanyiwa utaratibu mwingine, ikiwa ni pamoja na kuyarudisha katika mzunguko. Kwa maana hiyo, napendekeza Serikali iliangalie suala hili la mfumo wa majitaka Mjini Tabora kwamba, ni ndogo sana. Ikiwezekana tuangalie ni namna gani tunaweza tukapanua huduma hii ya majitaka kwa Mji wa Tabora, ili kuwapata na watu wengine zaidi kuliko wale wanaofaidika na huduma hii. Kwa kweli ni *percent* ndogo sana ya wananchi wa Tabora, wanaopata huduma hii.

Mheshimimiwa Naibu Spika, Kata nane zinazozunguka Mji wa Tabora, kama nilivyozitaja, zina matatizo makubwa sana ya maji. Tulipokuwa tunapita katika kampeni, tuliwaeleza wananchi ni jinsi gani jambo hili na tatizo hili la maji, linavyotukera na kwamba, Serikali itakayoingia madarakani, itatilia mkazo suala hili la maji. Nahitimisha kwa kuiomba Serikali, kwa kupitia Wizara husika, ilitazame tatizo hili, kwa uzito unaostahili na ikiwezekana, zipatikane fedha, ikiwezekana vile vile katika orodha ya visima vitakavyochimbwa vilivyomo katika bajeti hii, hakuna hata Kata moja ya Tabora, ambayo imepangiwa kuchimbiwa kisima, nayo iwekwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine tena, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia katika mada hii muhimu kwa uhai wa binadamu. Nasema ahsante sana na naunga mkono bajeti ya Wizara ya Maji. *(Makofi)*

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote na mimi nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, hasa kwa kuweza kuchangia mjadala ulio mbele yetu. Mjadala muhimu wa Wizara hii ya Maji, Wizara nyeti kabisa kati ya Wizara ndani ya Serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami niungane na wazungumzaji waliotangulia, nampongeza Waziri wa Wizara hii, Mheshimiwa Stephen Wasira, Naibu Waziri, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Katibu Mkuu wa Wizara, Ndugu Patrick Rutabanzibwa na Watendaji wote wa Wizara, kwa kazi nzuri ya kuandaa Bajeti hii ya mwaka 2006/2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda kabla sijaingia katika kuchangia zaidi, niseme machache kuhusiana na Wizara hii. Wizara hii ni Wizara nyeti sana na ni Wizara ambayo sisi Wabunge katika kuomba kura wakati ule wa kampeni, moja ya jambo kubwa ambalo tulikuwa tunakutana nalo na ambalo lilikuwa ni *agenda* ya wapiga kura, ilikuwa ni suala la maji. Suala la maji, wapiga kura walihitaji hasa ukishachaguliwa kuwa Mbunge, walihitaji namna utakavyoweza kulishughulikia. Kwa mantiki hiyo na mimi nasema pengine katika kauli hiyo na hasa aliyekuwa mgombea Urais, ambaye sasa hivi ni Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, aliwahi kutoa hotuba ambayo naamini hotuba hiyo aliitoa tarehe 30 Desemba, 2005 na humu kwenye kitabu hiki cha Bajeti, Wizara imeifanya kama *mission statement*. "Ninaomba ninukuu, inasema: Tatizo la maji ndicho kilio kikubwa cha Watanzania, mijini na vijijini, ndiyo kero namba moja, Serikali za Awamu zote, zimefanya jitihada kubwa kukabiliana na tatizo hilo. Serikali ya Awamu ya Nne imekusudia kukabiliana na tatizo hili kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya." Ni sahihi kabisa kwamba, kero ya maji kwa kweli ni tatizo kubwa sana nchini mwetu na hili haliwezi kupingika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie tatizo la maji hasa katika jimbo langu la Iramba Magharibi. Wilaya ya Iramba na Mkoa mzima wa Singida, tunapozungumza basi kama kuna tatizo linalohusiana na maji nchini, ukiuweka kando Mji wa Singida, utakuwa hutendi haki. Mkoa wa Singida una hali mbaya sana, kwa sababu ya ukame na hali ya maji ina matatizo makubwa na si tatizo la leo au la mwaka 2005, ni tatizo la muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipindi cha miaka ya 1980, kwa kuona tatizo hili, walitokea wahisani walikuja na *morale* ambayo iliitwa *Tanzania Austrialian Water Project.* Hawa walikwenda wakaanzisha Mradi wa uchimbaji wa visima virefu ndani ya Mkoa wa Singida na walileta magari mawili ya kuchimba visima virefu na kwa uhakika kwa kiwango fulani, Mradi ule uliweza kukidhi haja na angalau Singida ingeweza kupata maji kwa kupitia zile mashine zilizokuwa zinaitwa *wind mill,* ambazo zimebakia chache nazo katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyozungumza hadi hivi sasa, hatujui Mradi ule ulivyokwenda na wala yale magari yaliyoondolewa Singida hatujui yamepelekwa wapi. Kwa hiyo, nitaomba atakapojibu Mheshimiwa Waziri, atueleze ule Mradi ambao ulionekana kwamba, ni mkombozi kwa Mkoa wa Singida, ulipelekwa wapi na yale magari yalikwenda wapi? Hili ni swali ambalo mimi naomba sana tusaidiwe, kwa sababu watu wa Singida wanaulizia na wanaona kwamba, ilikuwa ni afadhali hata ungekuwepo ule Mradi ambao uliwasaidia basi ungeweza ukawaendeleza kwa sababu walishaanzisha Miradi fulani, ambayo baada ya kufa, ilikosa mtu wa kuweza kuiendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli wenzangu waliopita wamesifia ubora wa bajeti, wameeleza bajeti imelenga mambo muhimu, lakini nimekipitia kitabu hiki kwa umakini na nimeangalia sehemu mbalimbali. Katika miradi iliyotajwa si ya 2005/2006 na 2006/2007, ukweli ni kwamba, Wizara imeonyesha kuiweka pembezoni kabisa si Mkoa wa Singida pekee, hasa Jimbo la Iramba Magharibi, wametuweka pembezoni kabisa kabisa. Sioni mahali panapozungumziwa kwamba, sasa kuna Miradi, Wabunge wenzangu wakisimama hapa wanasema kwamba, nashukuru tuna Miradi mitano

tumeletewa ya uchimbaji wa visima, tunashukuru Wizara imetuletea pesa za kutosha, tutaendelea na ukarabati na miundombinu yetu. Lakini kwa pale kwetu, nataka niseme kwamba, kwa ukweli kabisa hakuna pesa mbali ya hizi ambazo nimeziona. Hakuna pesa mbali ya hizi ambazo nimeziona wanasema upanuzi wa miundombinu, maji safi na utendaji, majitaka. Wanasema wametenga shilingi bilioni 8.73 kwa ajili ya Babati na Singida. Lakini sasa hizi hela zimetengwa hazijaelezwa, mchanganuo haujatolewa kwamba, hizi pesa ni kwa ajili ya nini au mbinu gani zinatengenezwa.

Kwa sababu hata ukizungumza ukisema unakarabati miundombinu, sasa hiyo miundombinu ni ipi? Ni lazima wangeainisha kama sehemu nyingine zilivyoainishwa, hivi sasa hata wananchi unapokwenda kuwaeleza nao wapate matumaini waamini kwamba, katika kipindi hiki cha bajeti ya mwaka 2006/2007 kwamba, watapata ahueni na wanaweza kupata maji katika baadhi ya sehemu. Kwa hiyo, hili naliona kwamba, bado Singida kwa ujumla tumewekwa pembezoni sana kuhusiana na suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya Jimbo langu la Iramba Magharibi, nina Kata 15 na vijiji visivyopungua 67. Katika Kata hizi 15, hakuna hata moja pamoja na kwamba kupitia Halmashauri, wananchi wamehamasishwa, wakaambiwa waunde vikundi na badala yake waanzishe akaunti za maji. Wameanzisha, lakini katika Kata hizi 15 hakuna Mradi ambao unaonekana kwamba, huu Mradi sasa unatekelezwa na unafanya kazi. Mradi mmoja ambao tumeupata na bado unaendelea, lakini hata hivyo, unaendelea kwa kusuasua. Huu Mradi upo Kata ya Shelui, lakini Kata ya Ndago sasa hapa ndiyo nataka kusema kwamba, ndiyo kuna kiama kikubwa cha maji. Haya mliyokuwa mnayazungumzia Waheshimiwa Wabunge kwamba, tunasema kwamba mwanamke anatoka alfajiri kwenda kutafuta maji, kule Kata ya Ndago unajua shughuli. Asubuhi kukikucha ni kwamba, lazima asafiri si chini ya kilomita 15, anasafiri na ng'ombe, kwa hiyo, akishakwenda kule anakwenda kubahatisha maji. Atakapopata ng'ombe wale, atawafungua waanze kutafuta majani, baadaye atawafunga na atarudi saa tatu au nne usiku. Kwa hiyo, anapofika saa sita usiku, anaamka tena anaondoka kwenda kutafuta maji kwa siku ya kesho. Kwa hiyo, hili tatizo ni kubwa sana.

Nilishawahi kuongea na Mheshimiwa Waziri mwenyewe na nikamwambia nakuomba Mheshimiwa Stephen Wasira, twende ili ukaone tatizo la maji katika Kata hii ya Ndago. Kata ambayo ina matatizo makubwa. Tuna Kata ya Mtoa nayo ina matatizo makubwa, kuna Mbunge amesema hapa, watu wanakunywa maji, unayaangalia huna sababu ya kutafuta maziwa. Sasa kule ndiyo maji ya aina hiyo yapo, maji yanayotumika kwa mifugo ni hayo hayo, maji yanayotumika kwa binadamu ni hayo hayo. Kwa hiyo, tunaposema kwamba, tunapiga vita sijui magonjwa ya kuharisha, sijui huyo binadamu wa aina hiyo ataishi kwa hali ya namna gani, naomba sana Wizara hasa kupitia mipango yake hii niliyoiona ndani ya Wizara, wamefanya katika mgawanyo huo, wanasema fedha zimetengwa kwa ajili ya kuendesha na kusimamia huduma za maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona Singida tumetengewa shilingi milioni 248, Mkoa wa Singida ambao una watu karibu laki nne, lakini tukienda kwa upande mwingine, naona Wilaya ya Bunda, imetengewa milioni 278, hii ni wilaya moja, unalinganisha na wilaya ya Iramba ambayo imetengewa milioni 52, unalinganisha na Wilaya ya Namtumbo shilingi milioni tano. Hivi jamani hii *criteria* ya kugawa hizi fedha tunagawaje! Tunagawaje hizi fedha kwamba, leo wilaya nyingine inapata sana,

nyingine inakosa. Sasa unajua wakati mwingine, nilianza kuamini hata maneno ya Spika Kaparo, alipokuja alisema, *back benchers,* wanaanza kusema pale wanapoona kuna matatizo. Wanaona jimbo unalotoka wewe Waziri linapata kiwango kikubwa zaidi, lakini jimbo la *back bencher* halipati chochote. Kwa hiyo, hili linatugusa sana. *(Makofi)*

Lazima tuseme maana tusiposema humu, sisi ndiyo tutakwenda kuadhibiwa na wananchi. Iramba mimi nasema hakuna Mradi wowote, Waziri anayaona haya, leo nimeangalia humu mmesema kwamba, visima ambavyo vinamilikiwa na watu, nimeona visima vitatu tu kwa Singida nzima. Kampuni hiyo hiyo moja, inayojenga barabara, ina maana ikiondoka na visima vile vimekwenda, ni Kampuni ya Chiko. Sasa mimi ndiyo natoka Jimbo la Iramba Magharibi, ni sehemu gani hapa inamiliki hicho kisima, mbona sijawahi kukiona hicho kisima; kiko wapi? Tusije tukawa tunaridhishana, lakini nasema inauma sana. Ndiyo maana unaona tunasema kwa uchungu kwa sababu hali ya wananchi wetu, wanapata tabu, tunapozungumzia suala la maji, napata uchungu sana. Hii ni Karne ya 21, lakini leo watu wa Iramba bado wanachanga maji na mifugo. Ni tatizo kubwa sana.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri utakapojibu, uzingatie na utilie kipaumbele katika Kata zangu za Ndago, Mtoa, Urugu, Tulia, Kidaru, Twike, Kinampanda na Kengege, uzipe kipaumbele. Uniambie ni lini, kwa sababu gani na nitarudi huko watakwenda kuniuliza. Nimesema sana, nakuomba sana kwa sababu tunapozungumza, tunazungumza kwa uchungu. Wananchi tunapofikia mahali katika hili suala zito na limetajwa na wao wamesema kwamba, kama kuna kero, basi hii ndiyo kero namba moja. Kama tunakubali ndiyo kero namba moja, basi tunapofanya huu mgao, ulingane na hali halisi kwa kila wilaya na tusifanye mgao unaobeba wilaya fulani na wilaya fulani inaachwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri labda nimalizie kwa kusema kwamba, tuna Miradi mikubwa ya maji. Mradi kama huu wa Ziwa Victoria ni mkubwa na pengine kwa kujenga mipango ya baadaye na mipango endelevu. Nilikuwa naomba basi haya maji yanakwenda Kahama, nilikuwa nafikiri Wizara ingeweka mipango ya kuendeleza haya maji yafike mpaka hapa Dodoma. Ili kama yakifika hapa Dodoma, najua kwamba Nzega watafaidika, Igunga watafaidika, Jimbo langu la Iramba Magharibi watafaidika, kadhalika yatakuja mpaka Singida, Manyoni itafaidika, sasa yatafika mpaka Dodoma. Hivyo, tutaweza kusema sasa tumeshakuwa na mkakati wa kudumu wa kuweza kuondoa tatizo la maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu ya Maji.

Mimi natoka Kigoma. Kigoma tunayo bahati kubwa sana, tunalo Ziwa Tanganyikia, tunayo mito mikubwa kama Malagarasi na Mto Lwiche. Lakini sio kama wenzetu, angalau bado tuna uwezo tutaenda kuchota maji mtoni, tutaenda kuchota maji

*Lake Tanganyika*. Maji tunapata kwa sababu tunakwenda kuchota *Lake Tanganyika,* lakini dunia ya leo, Karne ya 21 bado mama zetu, wanabeba ndoo kwenda mtoni na ziwani. Usalama wa maji yale haupo na ndiyo maana kama mnafahamu, haipiti miaka miwili, mitatu, Kigoma haijapata tatizo la kipindupindu, ni kwa sababu tunakunywa maji ambayo siyo salama. Leo mji ule wa Kigoma, miundombinu iliyowekwa toka wakati huo mpaka leo ni hiyo hiyo mpaka kesho. Lakini idadi ya watu inaongezeka, Kata ya Kagera hakuna maji, Kata ya Kiwandabusinde hakuna maji, Kata ya Kibirizi ambapo ni karibu na Ziwa, hakuna maji, kule Gungu hakuna maji na Mlole hakuna maji.

Sasa nilichokuwa najiuliza, watu hawa tunawafanyaje, ukitaka kusema tatizo la maji Mji wa Kigoma ni kubwa, lakini tatizo la maji kwa Kigoma yote kama Mkoa ni kubwa zaidi. Ukienda kule Kasulu, wanayo mito mikubwa inapita lakini hakuna maji, Kasulu Mashariki wako karibu kabisa na Mto wa Malagarasi, ungetumia ule mto kuwapa maji wa Kasulu Mashariki karibu vijiji 20 vingepata maji, lakini mpango hapa siuoni. Ukienda vijijini mambo ni hayo hayo, ukienda Kibondo mambo ni hayo hayo, sasa nikawa naiangalia Kigoma, naona tatizo lilivyo kubwa ingawa maji yapo, kwa maana tunakwenda kuchoka ziwani au mtoni, lakini tatizo bado ni kubwa.

Tunafanyaje kama nchi, nilidhani umefika wakati sasa, Waziri mwenye dhamana ya maji, nilidhani kazi ya kwanza tujue mahitaji ya maji ya watu wa nchi hii, tufanye *inventory,* tujue tatizo ni kubwa kiasi gani kutoka mkoa mmoja kwenda mkoa mwingine. Tukimaliza hapo, tukilijua tatizo vizuri, twende sasa kutengeneza vipaumbele, tujue tunaanza na watu gani, tunaishia na watu gani.

Nasema bajeti hii kilichofanyika humu ndani, ni angalau kila mtu amepata kidogo kidogo, matokeo yake tutamaliza miaka hii kumi, atakuja mwingine tutakuwa tunaongea tatizo la maji kila siku. Kwa sababu tulichonacho kidogo tunakigawa, wewe kisima kimoja, wewe visima viwili, wewe hiki na kweli kila mtu humu ukisoma hii bajeti ameguswa. Lakini hakuna ambaye hana tatizo la maji, hayupo. Kwa hiyo, nasema tukishatengeneza *inventory* ya kujua tatizo la maji, *stage* ya pili tutengeneze vipaumbele, tuje Bungeni hapa tukubaliane kwamba, kidogo tulichonacho hiki tunaanza na hawa, tunamalizia na hawa na hakuna atakaye mlaumu Waziri na hata hizi lugha kwamba, kwangu umeweka kidogo, huku umepeleka nyingi, hazitokuwepo kwa sababu tutakuwa tumepitisha vipaumbele sisi wote pamoja. *(Makofi)*

Lakini kama suala ni kugawa kidogo kidogo, ni kweli tutapiga kelele, Kigoma mimi nimepangiwa shilingi milioni 10, nikawa najiuliza hizo shilingi milioni 10 ni za vikao ama ni za kuendeleza maji; sijaelewa mpaka hivi sasa? Ambacho sielewi, huyo aliyegawa pesa hizi, ningetamani sana aniambie, ametumia vigezo gani kugawa pesa hizi; je, ameangalia upatikanaji wa maji; na je, ameangalia shida walizonazo watu? Kwa sababu ukiangalia zilivyogawiwa, sitaki kuamini kama ni Mheshimiwa Stepehn Wasira ninayemjua, naamini si yeye aliyegawa pesa hizi, lakini huyo aliyegawa, atupe sababu tuelewe ni kwa nini amefanya hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuondoke kwenye haya maneno, twende kwenye kutengeneza vipaumbele, ni kweli keki ya nchi ni ndogo, bajeti ya maji ni ndogo,

haitoshi. Sasa kama bajeti ya maji haitoshi, tunafanyaje, ukiangalia bajeti hii nilikuwa nasoma hapa, tumetenga shilingi bilioni, 92 kwa ajili ya *Urban Water Supply and Sewerage*. Hizi shilingi bilioni 92 zina kazi tano, kazi ya kwanza ni *Urban Water Supply Rehabilitation,* sasa najiuliza *urban* ipi tunayoiongelea hapa, maana kwenye kitabu humu huoni hizi pesa zimegawanywa kwenda mkoa upi? Ukitoka hapo kuna *expansion* ya *urban water supply,* nayo imewekewa bajeti, ningependa Waziri atuambie ni *urban* zipi ambazo tunafanyia *expansion* kwa sababu kwenye kitabu hakuna, imewekwa *figure* tu basi? Ukitoka hapo kuna *Construction and Rehabilitation of Sewerage Facilities*, tuna *construct* wapi na tuna *construct urban* ipi, tuambiwe? *(Makofi)*

Ukitoka hapo kuna *Lake Victoria Project,* ambayo inafahamika, ime-*consider about 52 billion* kwenye hizi pesa, sina tatizo nalo. Kuna *improvement* ya *DAWASA* shilingi bilioni 18, sina tatizo nayo, lakini nauliza hizi *element* tatu ni kwenye mikoa ipi tuelewe? Inawezekana Wabunge tunapiga kelele kumbe humu ndani kuna hela zimepelekwa kwenye Wilaya yako, kwa hiyo, ni vizuri tuambiwe watu walielewe hili jambo. Ukienda *Rural Water Supply*, tumeweka shilingi bilioni 46, kazi zake ni nne, *expansion* ya *rural water supply…*

**MBUNGE FULANI**: *Where*?

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** *Where! In this country.* Kuna *borehole drilling and dams construction,* tuna *construct* hizi *dam*s wapi, kwenye kitabu humu sijaziona? Kazi nyingine kuna *rehabilitation* ya *rural water supply* tuna *rehabilitate* wapi *in this country;* kuna *rural water supply and sanitation* wapi? Kwa hiyo, nachotaka kusema, hizi shilingi bilioni karibu 92 na shilingi bilioni 46, hivi tukiamua kwamba, hatuongezi hela nyingine kwa miaka mitano ijayo, lakini tuamue, alisema mtu mmoja hapa kwamba, pesa hizi mwaka huu tuna-*concentrate* kutatua matatizo ya maji kwenye mikoa, *let say* mitaani na wengine watasubiri hawana tatizo, tutaambiana tutakubaliana hapa, lakini tuna hakika baada ya miaka mitano, tumeenda mikoa 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana tuondoke kwenye *traditional way of making our budget*. Kama miaka yote tutaendelea hivi, sungura mdogo tumgawanye kila mtu apate, tutapigiana kelele kila siku. Hata ningekuwa mimi ni Waziri wa Maji, nisingepeleka Kigoma shilingi milioni kumi, ningepeleka nyingi, maana ndio mazingira yenyewe, ni ubinadamu huu. Huyo anayegawa au anayesimamia Sekta hii, ameomba kura kwa watu, naye ataulizwa inawezekana tena alipita bila kupingwa, tatizo la Bunda ni maji, ataulizwa. Kwa hiyo, naye ni binadamu, ili tuondoke huko, tutengeneze *priority list*s za nchi yetu, lakini bila kutengeneza hivyo, maana tumeambiwa tunapofika 2010, asilimia 90 tutakuwa tumemaliza matatizo ya maji miji, asilimia 65 matatizo ya maji ya vijijini. Lakini ndugu zangu, tukiliangalia vizuri, Mungu anisaidie, mwaka huu tu vijijini kwa mwaka mmoja, imeongezeka asilimia 0.2 *from* 53. Hebu mtu yeyote anayejua hesabu aniambie, mwaka 2010 hatuwezi tukawa tumefikia asilimia 65, haiwezekani, *unless* watuambie ukweli hapa?

Tunaambiwa *by 2010* tutakuwa miji tumewapa maji kwa asilimia 90, lakini ukuaji tulioambiwa hapa ni wa asilimia moja. Hebu niambie hiyo *strategy* ya mwaka kesho,

ambayo tuta-*jump* kutoka kwenye asilimia moja angalau tufike asilimia kumi ili tuweze ku-*attain* hiyo asilimia 90 baada ya miaka mitano. *So* tunazo *strategy.* Hapa nilikuwa namsoma Waziri vizuri sana, kuna *strategy* mbili za maji lakini najiuliza, ili tuweze ku-*measure* kwamba tunakoenda ni kwenyewe, hebu tuulizane maswali tumefika wapi? Maana usitegemee kwamba, mwaka kesho utarudi, tunayo *National Water Supply,* ambayo ilianza mwaka 2002; *where are we now,* baada ya kutoka 2002 mpaka leo 2006? Tunayo *strategy* nyingine, *National* W*ater Sector Development Strategy,* imetufikisha wapi, *o*therwise tutakuwa tunatengeneza *strategy every time*? Ndio yale yale ambayo Mbunge mmoja alisema, tutakuwa kila siku tunaimba, tunatafuta maneno mapya ya kuonesha kwamba, tunakwenda. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nachotaka kuomba, kwangu mimi naona cha kwanza kabisa, tujue matatizo ya maji ni makubwa kiasi gani nchi nzima. Cha pili, tutengeneze *priority list* ya kutengeneza maji, ili pesa kidogo tulizonazo, tuzipeleke sehemu ambapo tukimaliza haturudi huko. Cha tatu, Waziri ame-*mention* hapa, kuanzia *National Water Fund, this is critical* na mimi nakubaliana na Waziri, ili tuweze kutatua tatizo la maji, lazima tufikirie namna ya kutafuta pesa na namna ambayo ninaona ni ya maana ni kutumia pesa za ndani. Hayupo mjomba atakaye tutatulia matatizo yetu, kwa sababu mtu ukimpelekea matatizo 50, anaweza akaamua mimi mwaka huu nahangaika na afya tu, sasa maji atakufanyia nani? Wewe una matatizo 100, mtu anakuambia nitakutatulia matatizo 10, yale mengine 90 atatatua nani? Tunayo matatizo mengi sana, kwa hiyo, lazima tufike sehemu tuseme hapana, angalau maji tumeanza, tunasema sasa na maji tuta-*invest* wenyewe, tutatue matatizo ya maji. *(Makofi)*

Lakini hata tukipata hizi pesa, tukaanzisha hii *fund* ikawa na pesa nyingi, staili ikawa ni hii hii ya kugawa kila sehemu kidogo kidogo, bado hatutofika. Ndugu zangu miaka 45 ya Uhuru, tafadhalini angalau tu baada ya miaka kumi ya Rais huyu, tatizo la maji tulisahau. Ni matarajio yangu, namfahamu Mheshimiwa Stephen Wasira, hii kazi anaiweza, basi aifanye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, narudia Kigoma hatuna maji, tunayo matatizo makubwa, tumeambiwa hapa kuna mipango ya maji, lakini ni historia. Mpango huu wa *Lake Tanganyika*, kwa sababu mpaka leo haujatekelezwa na *ADB*, wanasema tukifika *November, 2006,* hii *project* ina-*seize*, sasa sijui mnatuambiaje? Nasubiri kesho, naamini Waziri wa Mazingira anakuja na jawabu la hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo na mimi nawapongeza Wizara kwa kazi nzuri, wameandika *speech* nzuri sana, wamejitahidi kwa kweli kumridhisha kila mtu na kweli wanafanya kazi kubwa. Baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana kwa kunipatia fursa hii ya kuchangia katika hoja iliyo mbele yetu. Nianze kwa kumpongeza Waziri wa Maji, Mheshimiwa Stephen Wasira, Naibu Waziri, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, pamoja na Katibu Mkuu na watendaji wa Wizara hii, kwa kututayarishia hotuba nzuri, ambayo ina nia ya dhati kutatua kero namba moja kwa Tanzania, kero ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuipongeza Wizara kwa hotuba iliyoko mbele yetu, pamoja na mikakati mizuri ambayo inaonekana kwenye hotuba hii, nina mambo machache ya kuchangia.

La kwanza ninamwomba Mheshimiwa Waziri, wakati wa majumuisho atupe ufafanuzi, nitaanzia na jedwali namba moja, kiambatanisho namba moja, nichoelezea vigezo vilivyotumika. Nataka kujua vigezo vilivyotumika, kubaini idadi ya maeneo yaliyofanyiwa utafiti wa maji chini ya ardhi, kwa ajili ya kuchimba visima virefu kuanzia Julai, 2005 mpaka Juni, 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naangalia jedwali hili, sikuona jimbo la Sengerema ama Wilaya ya Sengerema. Kwa maoni yangu, nadhani hili ni kosa la kiutendaji, si kosa la Waheshimiwa Mawaziri. Nasema hivyo kwa sababu kumekuwa na taarifa ambazo si sahihi sana kutoka kwa watendaji wetu. Jimbo la Sengerema ama Wilaya ya Sengerema, pamoja na kwamba baadhi ya maeneo ya Wilaya hiyo hususan jimbo la Sengerema, limepakana na Ziwa Victoria, lakini kwa hakika, kuna maeneo ambayo ni makavu kuliko hata maeneo mengine ambayo tunayatambua kwamba ni makavu katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pale nina Tarafa ya Nacheche, kuna Kata ya Buyagu, Kata ya Igalula na Kata ya Tabaluka, haya ni maeneo makavu sana, yanakuwa na kipindi kirefu sana cha ukame. Inasikitisha sana inapofikia hatua hii, unaona hotuba nzuri ambayo tulidhani kwamba, itatupeleka mahali ambapo sasa tunaelekea kwenye neema, inaacha maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali isaidie kufafanua jambo hili. Narudia tena kusema kwamba, nadhani hili ni kosa la kiutendaji, watendaji hawana takwimu sahihi na nilikuwa naangalia ukurasa mmojawapo wa hotuba hii, Wizara ina vituo vingi sana vya kukusanya takwimu kuhusu suala la maji nchi hii, lakini kwa hakika inasikitisha sana inapojitokeza jambo kama hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, si hivyo tu, ukiangalia pia kiambatanisho namba mbili, kuhusu visima vilivyochimbwa na makampuni binafsi, tangu Julai, 2005 hadi Juni, 2006, utakiona kisima kimoja kwa Sengerema. Sasa kwa hali kama hii unashindwa kusema, nisisitize nirudie tu kwamba, tunaomba wakati wa majumuisho tusaidiwe, wananchi wafahamu kinachoendelea nini na pengine kama kuna mapungufu ya kiwango hiki, basi kutoka kwenye watendaji wetu, hatua kali zichukuliwe jamani kwa sababu tunaongelea kero namba moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, matarajio ni kwamba, *response* ya ku-*address* kwa sababu tunaisema hii ni kero namba moja, lazima iwe *proportional* na uzito wa jambo lenyewe. Kero namba moja, haiwezi kuwa *addressed* kilaini laini, ni tatizo kubwa hili. Nasisitiza tena, naiomba sana Serikali kupitia Wizara ya Maji na pengine nitoe mwaliko kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, karibuni Sengerema mjionee hasa katika maeneo ambayo nimeyataja, hasa Tarafa ya Naicheche, katika hizo Kata za Biyagu, Igalula, pamoja na Tabaruka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee suala la pili, naliunganisha na kitu ambacho nilikuwa nakisema sasa hivi. Wepesi wa kutatua kero zetu, tangu mwezi wa pili na wa tatu, kwa Wilaya ya Sengerema, tumekuwa tukifuatilia kupata mtambo wa kusukuma maji kutoka ziwani, kitaalam wanaita *floating pump*. Hapa nina vielelezo ambavyo nimekuwa navyo na nilisema hata wakati nachangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nikasema mambo mengine haya, hayahitaji fedha za kigeni, ni sisi wenyewe kuwa na nia ya dhati ya kutatua kero zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii ukiiangalia, imeelezea jinsi gani ambavyo wana mipango ya mawasiliano, kwa kushirikiana na Wizara nyingine ikiwemo TAMISEMI. Sisi pale mwezi wa kwanza, Katibu Mkuu wa Wizara hii, alimtuma *engineer* wake, nitamtaja kwa jina anaitwa Bwana Chusi. Baada ya malalamiko ya Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema, kwa tatizo la maji ambalo lilikuwa linaukumba Mji wa Sengerema na vijiji vilivyo karibu pale. Katibu Mkuu alimtuma mtu pale, *engineer* wake kuja kujionea mwenyewe, kufanya *assessment* ya tatizo la maji pale Sengerema. Mtaalam huyo alifika, aliporudi akatoa taarifa, akaiomba Ofisi ya TAMISEMI, akailekeza kwa taratibu zilizoko pale na hizi ni taratibu za kiutendaji tu. Akamwomba Katibu Mkuu Wizara ya TAMISEMI, aombe pesa kwa sababu Halmashauri iko chini ya Wizara ya TAMISEMI, tangu mwezi wa tatu.

Nilisema wakati nachangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, jambo hili sikupewa majibu wakati wa majumuisho ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Matarajio yangu ni kwamba, leo hatimaye kilio changu kitatolewa ufafanuzi, inatisha watu wamekuja, wakafanya *assessment,* wakaona tatizo limetokana na kushuka kwa kina cha maji Ziwa Victoria na uchakavu wa mitambo ya mashine ambayo imefungwa pale Kata ya Nyamaziwa kusukuma maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika kusema kwamba, pamoja na kwamba, nilisema nimekuwa nikifuatilia mwenye kwa nafasi yangu kama Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo hilo la Sengerema, lakini pia Halmashauri, kupitia kwa Mtendaji wa Halmashauri, imekuwa ikifuatilia na viongozi wengine Wizarani, mpaka leo hatujapewa jawabu, hivi haya mambo kweli tunaweza kwenda kwa staili hii kweli?

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha sana, namwomba Mheshimiwa Waziri, atupe majibu kama tutapata, sisi tulikuwa tumeomba shilingi milioni 49 na hiyo ilitokana na ushauri tulioupata kutoka kwa watalaam wa Serikali. Tatizo lilikuwa nini, mpaka sasa hivi tusipewe jibu, walau basi tuishi kwa matumini ya kuambiwa kwamba, jambo letu linashughulikiwa, lakini hata hilo halijafanyika.

Mazingira kama hayo unasemaje sasa, hatuwezi kusema tunamwachia Mwenyezi Mungu, nchi ni yetu, lazima tuelezane ukweli na tunaomba ufafanuzi. Narudia hii ni kero namba moja, tunatarajia *response* lazima iwe *proportional* na uhalisia wa tatizo lenyewe na sio vinginevyo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba tena nisisitize kwamba, suala la maombi yetu ya shilingi milioni 49 kwa ajili kufunga mtambo wa maji, yaani ile *floating*

*pump* pale Nyamazugo, tupewe leo na tujue kama hiyo pesa tutapata au hatupati, kieleweke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo lingine, haya mambo siyaelewi, kiutekelezaji yanakwendaje, kero namba moja hii bado nasisitiza kwamba inahitaji nguvu ya pekee ya kuishughulikia. Bajeti ya mwaka 2005 naamini hili sio tatizo la Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema peke yake, hapana. Katika bajeti zetu za Halmashauri, tumeomba utekelezaji wa Miradi kadhaa, mimi jimboni kwangu tulikuwa na Miradi kadhaa ya kutekeleza masuala ya maji. Fedha hiyo haijatoka, ina miradi kadhaa ambayo imekwama hadi hivi sasa. Bajeti ilipita, lakini tumekuwa tukifuatilia hili fungu na ni ruzuku maalum kutoka Serikali Kuu, hatujawahi kuipata, ile Miradi imesimama; tuna *move* namna gani ku-*address* hii kero namba moja?

Bajeti ya mwaka 2005/2006 na Mradi wa Maji wa Mwabaluhi pale ni shilingi milioni 17, hakuna kilichofanyika, ni kwa sababu hatujapata pesa. Lakini pia tuna Mradi wa Maji pale Busisi hatuna pesa, ni Serikali Kuu hapa ni shilingi milioni 18.5. Tuna Mradi wa Maji pale Kijiji cha Mwaliga, ni shilingi milioni tisa, Serikali Kuu, bajeti imepitishwa na Serikali, pesa haionekani! Nasema kwa maana ya kwamba, sungura wetu ni mdogon lakini nadhani kwa sababu tunafahamu hata katika kero zetu zinatofautianan kuna namba mojan namba ngapi, basi hii namba mojan tuipe kipaumbele hata wakati wa kutoa pesa jamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba ufafanuzi, hizi pesa zitatoka lini na kama niko *mis-informed*, basi wananisikia kule Sengerema sasa hivi, kama taarifa wanazozipata ni kwamba pesa imeshatolewa lakini mimi naambiwa haijatoka, basi tuelezwe. Kuna Mradi wa Maji wa visima vifupi, kuna Vijiji vya Nyatakubwa, Nyamaona, Nyakahako, Igumuki, Kome na vijiji vingine ambavyo siwezi kuvitaja kwa sababu ya ufinyu wa muda. Tunaomba tuelezwe hii pesa itatoka lini; na je, itatoka ama haitoki lakini? Mimi naamini kwamba, itatoka kwa sababu bajeti imeshapitishwa na mambo yamekuwa mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunadhani kwamba, ni jambo la msingi kero zetu tuzitatue kulingana na uzito ulivyo. Lingine ninalotaka kumalizia, ili niungane na wenzangu wengi, tumepigia kelele hapa suala la maji, tumeongelea kwa uchungu. Lakini kwa kweli namna ya kulichukulia jambo hili, nadhani tunahitaji kuweka vipaumbele na tuanze na mahali ambapo hii rasilimali ipo. Hatuwezi kutatua kero hii moja kwa *piece meal approach,* tunayofanya hapa. Tunagawa pesa, naishukuru Serikali sisi Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema mwaka huu, tumepewa shilingi milioni 103 si haba katika hali ya kawaida, kuna wengine wamepewa shilingi milioni kumi. Mheshimiwa Serukamba, alikuwa analalamika pale, Mheshimiwa Felix Kijiko kutoka Muhambwe, juzi alikuwa analalamika hapa, Mheshimiwa Simbachawene amelalamika hapa, Mheshimiwa Kilimbah kalalamika, Mheshimiwa Getrude Mongella kalalamika na Mheshimiwa Emmanuel Luhahula amelalamika, lakini tuna sehemu ambazo zina vyanzo vya uhakika.

Ukienda pale Mto Malagarasi, kwa wale ambao tunatoka Ziwa Victoria na sehemu nyingine ambazo zina vyanzo vya uhakika, hivi ni kweli leo uniambie mimi mtu

wa Kamanga pale Sengerema, ambaye *at a stone floor* anapata maji, anatumia maji ya kisima. Leo hatuwezi kuwa na mpango ambao ni endelevu, kuhakikisha kwamba, tunatatua haya matatizo ya miaka mingi, ili baada ya hapo tusonge mbele hatua kwa hatua. Ni kweli, ukienda pale Busisi, nenda kule Chifufu kule kwetu, tumezungukwa na ziwa, lakini hatuna maji ya bomba.

Ukerewe nina hakika, bahati mbaya kwa Mheshimiwa George Lubeleje, huko Mpwapwa hakuna ziwa, lakini kama lingekuwepo ningetoa hoja ile ile kwamba, hawa watu ambao wana vyanzo vya maji, tuweke mipango endelevu ya kuhakikisha kwamba, tuna tatizo limekwisha. Ukisha *solve* hili tatizo la hao ambao wako karibu na vyanzo vya uhakika, tunakuwa tumefanikiwa kwa kiasi kikubwa katika kutatua tatizo hili. Lakini eti tunapeleka kisima kidogo hapa tunashindwa, nadhani hii si *approach* sahihi sana, nadhani kwa mtazamo baadae tunaweza kuiangalia, tukaiboresha zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hilo, nashukuru tena kwa mara nyingine. Nasisitiza kusema kwamba, kero ya *floating pump* pale Sengerema, tanapenda Mheshimiwa Waziri, wakati anajumuisha, anipe jawabu imefikia wapi. Nadhani wanalienzi vizuri sana na Hazina, lakini pia na Ofisi ya Waziri Mkuu hasa TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, narudia kusema, naunga mkono hoja. Asante sana kwa kutumia nafasi hii. *(Makofi)*

**MHE. JOHN P. M. SHIBUDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii kwanza, kukushukuru kabisa kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika mwelekeo wa utendaji wa bajeti ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza kabisa, naomba kunena kwa dhati kabisa, nampongeza Mheshimiwa Stephen Wasira, Waziri wa Maji, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na watumishi na watalaam wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri ambazo wanafanya kwa maslahi ya nchi yetu, kwa nia njema kabisa ya kuhakikisha wanadhibiti kabisa tatizo la kero ya maji kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba kuipongeza Kamati ya Bunge, ambayo imeshiriki kwa dhati kabisa, kuhakikisha ya kwamba, wanatoa mawazo na michango mbalimbali ya kusaidia ufanisi wa maandalizi ya bajeti hii. Wahenga husema, kila punda huona mzigo wake ni mzito kuliko wa mwenzake, kwa uwongo wa macho. Naomba kurejea, kila punda huona mzigo wake ni mzito kuliko wa punda mwezake, kwa uwongo wa macho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimewasikia Wabunge wenzangu, sote tunalia, tatizo tulilonalo hapa ni mgao, lakini naomba nirejee nyuma kwamba, nitakuwa na maneno laini kwa sababu naelewa juzi juzi tulikuwa katika zahama ya njaa. Wizara ya Fedha, pamoja na Wizara ya Kilimo na Ofisi ya Waziri Mkuu, imefanya kazi kubwa sana kuhakikisha kwamba, Watanzania hatufi kwa njaa na kweli wananchi wetu tunaowawakilisha, nao wanajua ya kwamba, kila Mheshimiwa Mbunge wetu leo kasema

nini kuhusu tatizo letu la maji. Lakini usiache mbachao kwa msala upitao. Tukumbuke tulikotoka, ni kweli hivi sasa tunazungumzia matatizo ya mgao, hasa hiyo ndio kero kubwa na kwamba, kwa nini fulani kapata zaidi kuliko mimi. Lakini, naomba wananchi wa Maswa wanielewe na naomba wananchi wa Tanzania wenzangu vilevile wanielewe, hapa tatizo letu si maji bali madhila ya maji na umaskini. Sasa kilichopo, kuna *priority within priorities*, mimi niiombe Serikali Kuu na Mfuko Mkuu wa Serikali, kama pana akiba yoyote, waelewe kwamba, maji ndio hazina, ndio uhai, ndio msisitizo na ndio mwelekeo, ndio jibu na uamsho kwa maslahi ya ustawi wa maendeleo ya jamii. *(Makofi)*

Wizara ya Maji ni Wizara ya kifundi, kama hawana mashine za kutobolea ardhi tukapata maji tutawalaumu, maji hayaendi kwa falsafa za kisiasa. Sasa ninaomba Serikali Kuu, ielewe katika *priorities* za bajeti ijayo, leo tumetoa mchango wa mawazo wa kuelezea shida na dhiki mbalimbali, ambazo kila Mbunge anaelewa katika Jimbo lake, japo Wahenga husema kila mbuzi hula kwa urefu wa kamba yake. Sasa ninawaomba vile vile wale wenye dhamana, Katiba ya Chama cha Mapinduzi inasema, sitotumia madaraka yangu kwa maslahi binafsi. Sasa nakuombeni, binadamu hukumbukwa kwa yale mema aliyoifanyia jamii, hebu anzeni kusaidia Majimbo yetu na naomba muelewe kwamba, ukishakuwa Waziri, dhamana hiyo ni mtihani mkubwa. Nawapeni pole, kwa sababu kila jambo ambalo mgawo utakwenda kwa Mheshimiwa Waziri, utakuwa ni mtihani wa kusemana lakini hivi kweli si *charity starts at home*.

Huu ndio ukweli na siku zote ukweli huwa ni mwarobaini, lakini Mwenyezi Mungu, katujalia kila kinachosikika katika masikio, huamsha hisia. Sasa mimi naomba kusema, Mheshimiwa Waziri wa Maji, kuna maeneo ambayo kimazingira yanahitaji yapewe *priorities,* kwa sababu yameshaharibika kimazingira. Ni nani asiyetambua kuwa Mkoa wa Shinyanga ni jangwa nyemelezi hivi leo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo tulikata miti ili tupande zao la pamba, tunaambiwa tumeharibu mazingira, sio sisi. Leo kuna mahali binadamu anakunywa maji ya kushindana na mifugo, lakini kuna maeneo Mwenyezi Mungu, kawajalia katika nchi yetu, neno shida ya chakula kwao halipo. Nampongeza sana Mwenyezi Mungu, kwa sababu Mwenyezi Mungu, ndiye anayegawa riziki kila upande na kila hali. Sasa eneo ambalo linakutwa na jangwa nyemelezi, halina mazingira ya kwamba utachimba kisima kwa sululu upate maji, eneo hilo likipewa *priority* ni kumtimizia Mwenyezi Mungu, haki yake kwa waja wake. Kwa hiyo, nakuombeni wataalam, msiogope sana kauli za ukali, kwa sababu mtu unayempenda unamsemea kwa maneno ya ukali, kuamsha hisia za kumbukumbu na uamsho wa fikra endelevu. Nanena Kwa sababu isije kufikia mahali watalaam wakashindwa kukaa na hii ni kazi ya kiufundi hivyo, katika mipango wakasema tutalaumiwa, tutalaumiwa. Mimi nina imani kabisa Bunge hili linawatambua watalaam wetu, mnafanya kazi za kisiasa, kwa fikra za kisiasa, za kuhakikisha Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi inafaulu. *(Makofi)*

Nawakumbusha tu wataalam ya kwamba, pana *priorities within priorities* na mkienda kwa mtiririko huo, hakuna atakayewalaumu. Mkoa wa Shinyanga ni jangwa nyemelezi, lakini nasikia maji yakitoka Kahama, yanakwenda Nzega yanaelekea Igunga.

*Mashallah*, mpangaji Mwenyezi Mungu, lakini Mwenyezi Mungu pia ni mtihani kwa busara zetu na hekima. Hivi kweli Wilaya ya Kishapu, wale hata chakula cha mahindi kupanda ni nongwa, kwa sababu ya ukame, ukitoka pale unaingia Wilaya ya Maswa, Maswa ni hatari kubwa, jangwa nyemelezi. Mwenyezi Mungu, tumtendeeni haki yake. Maswa chakula shida, maji shida, elimu shida, kila jambo ni dhahama tupu, tunaishi kama wakati wa ujima na hamwishi kutucheka, Wasukuma wanalogana, wana vifo vya imani za uchawi, basi maji tuleteeni angalau tukabatizwe tuondokane na mitihani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba maji, Maswa maji ni dhahama. Mheshimiwa Waziri, namshukuru sana amefika ametazama mwenyewe. Maswa hali ya maji, sasa hivi wananchi wanakimbilia Rukwa, watu wa Rukwa wanasema hatutaki Wasukuma mje huku wafugaji, wakulima wafugaji, twende wapi? Hii ni nchi yetu sote, haijabinafsishwa, sasa wafugaji waende wapi? Nawaomba watu wa Wizara ya Maji, Mifugo na Mazingira, mkae mtazame jinsi gani ya ku-*solve problem* ya kuhamahama. Watu wanaondoka kwenye mitambiko yao na mizimu yao, sio kwamba wanapenda. Ingekuwa hakuna bahari Wasukuma sote tungekuwa tumejaa Zanzibar, Unguja na Pemba na mifugo yote ingekuwa kule, kilo ya nyama ingekuwa Sh.500 badala ya Sh.2,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naiomba Serikali, Maswa ni jangwa nyemelezi, tunachohitaji sisi watu wa Maswa ni msaada wa utaalam wa kuvuna maji ili wakati mvua inanyesha, angalau tuweze kuvuna na malambo makubwa ya maji ili tuweze kutenganisha malambo ya maji pamoja na mifugo. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, ni ngome kongwe, hata akipigwa radi haipasuka kwa uelewa wa masuala ya kisiasa, ni mwanasiasa kweli kweli, najua hata leo atatujibu kisiasa. Namjua Waziri wetu huyu si mfanyakazi za kisiasa bali ni mwanasiasa kwa damu, kama Nelson Mandela. Namtambua Naibu wake, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, ni hatari kweli kweli, ni nuru ya tumaini. *(Makofi/Kicheko)*

Namtambua Katibu Mkuu, mwana mapinduzi, mwana harakati pamoja na timu yake, sasa msivunjike moyo, endeleeni kuwashawishi wahisani mbalimbali ili waweze kusogeza misaada ya kutusaidia. Ninaomba Wizara na wataalam, waje Maswa. Mimi ninaahidi tutagharamia mahali pa kuishi ili waweze kuja kuona zahama iliyopo ili Mwenyezi Mungu ajaze baraka na hekima za kutuonea huruma, mtangulize kuiona *priority within priorities,* Maswa inahitaji maji.

Mwenyezi Mungu, atujalie sote, naunga mkono hoja ahsanteni. *(Makofi)*

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana, lakini kabla ya hapo, naomba radhi nilikuwa na udhuru kidogo, nikatoka nje ya Bunge, sasa nimerudi na nashukuru kwa kupewa nafasi hii. Naomba sana kutoa hongera nyingi hasa kwa Waziri, Naibu Waziri na wafanyakazi wa Wizara ya Maji. Hakika hotuba hii ni moja kati ya hotuba iliyowaridhisha watu wengi, kwa sababu kila mtu katajwa. Vijiji vyote vimetajwa na huyo huyo sungura mdogo amegawiwa kwa namna nzuri sana kwamba, tunaona wote fahari kumsifu Waziri na kuisifu Wizara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni maisha, maji ni uhai. Wizara hii ina kazi kubwa ya kutupatia maji binadamu, mifugo, umwagiliaji na viwanda haviendi bila maji na umeme haupatikani bila maji. Hoja iliyonifanya nisimame ya kwanza kabisa, ni kuiomba Serikali ikubali kwamba, Wizara hii haiwezi kwenda na ikatimiza majukumu yake, kwa kuipangia fedha kidogo kama hizi. Mahitaji ya maji sasa hivi ni makubwa. Shilingi bilioni 170 hazitoshi na shilingi bilioni 147.3 kwa ajili ya maendeleo hazitoshi kabisa. Sasa kwanza, Serikali ikubali kwamba, maji ni uhai, lazima tufanye mapinduzi katika maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama wale wanajua historia watakubali kwamba, Hayati Mwalimu Nyerere katika miaka ya mwanzo tu ya sabini, alitamka na kuamua kupeleka maji kila mahali. Ukienda leo vijiji vingi sana utakuta alama ya maji nchi nzima, kama mnabisha mtu aonyeshe kidole. Kwa hiyo, inawezekana kabisa nchi hii tukapeleka maji kila mahali kwa kufuata nyayo za Baba wa Taifa, ambaye aliamua katika miaka ya sabini kuapeleka maji kila mahali na kila mahali maji yalikuwepo.

Tatizo kubwa katika mpango ule lilikuwa, Watanzania walidhani ukipelekewa maji, basi Serikali itakuja tena chombo kikiharibika wakuletee spea, mtu kama anataka kuiba basi anajua hiyo ni mali ya Serikali. Mradi ule mkubwa ulisaidia wananchi wengi, lakini haukudumu, kwa sababu haukuwa endelevu kwa maana, wananchi hawakuelewa maana ya kupewa maji. Haikuwa kwamba, maji yakitolewa basi yatakuwa hivyo hivyo na yalitaka yawe endelevu. Ndio maana hata Sera ya Maji ikabadilishwa kutoka kuwapa maji tu ila sasa maji wapewe watu, yawe yao. Ndio maana sasa tuna Mifuko ya Maji vijijini, tunaendelea kusaidiana katika jambo hili. Lakini tulipofika sasa hivi, ninadhani turudi kule, *Cabinet* nzima ikubali, hakuna mtu atakayekaa katika ile *Cabinet* bila kunywa maji, watoto wao, mifugo yao, wakubali kabisa kurudi katika *chapter* ile ya Mwalimu Nyerere, tutoe maji kwa wananchi wote na mambo mengine yafuate. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa nazungumzia watumishi. Watumishi wa maji waangaliwe kwa sababu ni taaluma maalum na iwe endelevu. Kuwe na taratibu za kusomesha na kuwe na lengo kwamba, mwaka huu tunapeleka *engineers* kadhaa, baada ya miaka mitatu *engineers* kadhaa, kwa ajili ya maji. Nakumbuka Mheshimiwa Getrude Mongella, alizungumzia habari wakati fulani alipokuwa India, walikuwa wanapelekwa *engineers*. Wakati mmoja Maji ilipeleka *engineers* zaidi ya 200 kusomeshwa kwa ajili ya Mradi huu na wakarudi wengine wamezeeka na wengine tunao pale.

**NAIBU SPIKA:** Ni vizuri ukasema na wewe ulikuwa Katibu Mkuu huko. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Ahsante sana. Nilikuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji kwa miaka mitano, kazi yao nzuri na naiunga mkono saa yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *training* nataka tuihuishe, tuanze kuwa na *target* kwamba, kama nchi hii inataka *engineers* wa Wilaya kadhaa waliosomeshwa vizuri,

tunao *engineers* wangapi sasa hivi wenye umri wa kustaafu na wale wengine wenye bahati mbaya kushikwa na gonjwa balaa, yote haya yanatupunguzia *engineer,* wetu. Kwa hiyo, lazima kuwe na mpango maalum wa *replacement* ya *engineers* vijana, wapya na waliosomeshwa vizuri. Kwa hiyo, lazima liwepo fungu kubwa la kusomesha wafanyakazi wetu katika Wizara ya Maji. Hawa ukishawasomesha, lazima tuangalie na mafao yao. Mafao yanahitajika. Mimi nilikwenda, kama Katibu Mkuu, kuangalia kazi wanayofanya huko katika vyanzo vya maji, wanahitaji vitu vingi sana, acha kwamba, wawe na usafiri wa kutosha, lakini yako mambo mengine, hakika wapewe posho ya mazingira magumu, kila wanapokwenda katika sehemu ngumu wanayofanyia kazi. Usafiri ni muhimu, hawatakwenda kule kwenye vyanzo vya maji kwa baiskeli.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimetoka Rufiji, itakuwa dhambi kama sikutaja neno hili linaloitwa Rufiji, maana yake ni jito kubwa, linapeleka maji *Indian Ocean, billions of gallons*. Wazee wetu wamezaliwa wameuona ule mto, mimi nazeeka nauona tu ule mto, maji hayapungui, lakini nakuhakikishia, watu wa Rufiji wana matatizo ya maji ya kunywa kabisa, wanahitaji maji. Kata kama ya Mbwara, Nambunju, Kiwanga, Ndundu Tawa, Tawi, Kikobo, Ngarambe na Kingupira, hawana maji na ingawa tuko pale Rufiji. Sasa hii itanifanya nirudi huku katika mpango wa mradi wa maji vijijini na usafi wa mazingira. Mradi huu mzuri, ungetusaidia sana na baadhi ya watu tulio-*negotiate* Mradi huu pale Washington tupo. Lakini huu mpango wa kuchangia asilimia tano, vijiji vingi wanashindwa. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali iondoe hii asilimia tano ya wanavijiji wachangie ili wapate Mradi huu wa *World Bank.* Ni kweli watu wanahitaji mradi huu kila mahali, lakini wanashindwa kupata asilimia tano ya thamani ya Mradi. Kwa hiyo, naomba Wizara ikubali kufutilia mbali asilimia tano ya mradi huu. Pili, wanaopewa kazi hii kutekeleza, wanafanya kwa uchelewevu mkubwa sana yaani, afadhali yule jongoo anakwenda, hawa watumishi wanakwenda taratibu mno. Namwomba Mheshimiwa Waziri, ahakikishe ikiwezekana aanzishe kitengo cha ufuatiliaji tu kuangalia Mradi ukianzwa unamalizika lini? *(Makofi)*

Katika Mradi wa Maji Miji Midogo hapa nahusika kabisa. Utete, ni Mji Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, hauna maji. Hadithi hii kwamba pesa zitatoka Ufaransa watakuja kuchimba, yaani mimi nyumba yangu Utete inaangalia Mto Rufiji kama vile, yaani kama walivyo wale pale, lakini kuyatoa pale maji kutia katika nyumba haiwezekani. Naiomba Wizara itazame jambo hili na naomba mpango huu uanze Utete uende Kibiti na vile vile usiiache Ikwiriri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naomba tena kurudia kwamba, Serikali ikubali kuamua mapinduzi katika maji. Fedha wanazotoa hazitoshi. Mapinduzi yafuatane na *training* kama tulivyofanya miaka ya 1970. Halafu kuna watu wana chakula, wanakiona lakini hakiliki, Rufiji kuna mto mkubwa lakini maji hatuna. Tunaomba miradi iliyoandikwa kwa Rufiji ifanywe kwa haraka, lakini kwa kuwa natoka pale, naomba sana Mheshimiwa Waziri, usije ukanywa tope kule nyumbani, uje ulete mradi mapema uanze ili utakapokuja unywe maji safi na salama.

Baada ya kusema haya, napenda kushukuru sana kwa nafasi uliyonipa, lakini hakuna kubwa litakalofanyika kwa fedha finyu, Serikali lazima ikubali kutoa fedha nyingi kwa ajili ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. HEMED MOHAMED HEMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote sina budu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwa ni miongoni mwa wachangiaji katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia natoa pongezi zangu za dhati kwako wewe binafsi kwa umahiri wako wa kutuwezesha na kutufanya Wabunge wote kuwa ndugu.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani kwa Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa jitihada zake za kuwa mvushaji pale tunaposhindwa kuvuka. Mwenyezi Mungu amjaalie Mheshimiwa Edward Lowassa, nusra. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na Waziri wa Maji, hotuba yake ni nzuri sana ila mwanadamu hakosi kasoro. Pia namshukuru mtoa hotuba wa Upinzani kwa jithada yake kwa kuiomba Wizara iache mawazo ya dhana ifikapo. Maana mbio nyingi humfika yule anayejua nyuma yangu kuna adui.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukizungumzia maji ni kusema tunazungumzia maisha ya mwanadamu. Hii ni kusema Wizara hii inasimamia uhai wa mwanadamu kama vile Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inapaswa ikubali katika nchi yetu tatizo la maji ni sugu hasa huko vijijini. Kuna baadhi ya Wilaya katika nchi yetu wanakijiji wanatumia maji yasio na usalama kwa maisha ya Mtanzania. Kuna baadhi ya maeneo yetu mtu anapohitaji maji hulazimika aende maeneo ya mbali kuyachukua maji. Hali hii ni mpaka lini? Watanzania ambao wanaishi juu ya maji lakini hawawezi kuyatumia maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukitoka vijijini sasa kidogo tuiangalie hali huko Dar es Salaam. Serikali inapaswa itoe shukrani kwa watu binafsi ambao kwa makusudi wakaweza kuchimba visima ambavyo kwa kweli wameweza kuwasaidia wananchi suala la maji Dar es Salaam, kuna wafanyabiashara wa maji kwa mauzo ya kutembeza maji kwa kutumia magari na wengine huuza maji kwa ndoo, galoni na kadhalika. Pamoja na jitihada ya wafanyabiashara hawa, Wizara hadi leo imeshindwa kujua maji wanayotumia watu wetu yana usalama kiafya, je, maji yanavyouzwa chalingana na hali ya kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kila leo huzungumzia kilimo. Wizara yetu ya Maji inachukua hatua gani kuinusuru nchi yetu kutokana na ukame? Kukosekana kwa mvua ni balaa, mvua kuwa kubwa ni balaa. Wizara imejiandaje na kuepukana na mambo

kama haya? Ni vyema maji ya mvua yavunwe. Ma-*godown* ya mizigo tunaweza kuyajenga, kwa nini tushindwe kuyavuna maji? Wafugaji katika nchi yetu sijui wamekosa nini. Hadi leo wafugaji hawana sehemu za maji safi kwa wanyama wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenyezi Mungu ainusuru nchi yetu na ukame.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi cha miaka mitano Wilaya ya Sumbawanga Vijijini tumepitisha miradi ya maji katika Vijiji vya Matai, Mwazye, Mwimbi Kafukoka/Kasote chini ya mradi wa *World Bank* bado haijaanza utekelezaji wake, Wizara ione jinsi ya kusaidia katika miradi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TASAF* ilitoa fedha nyingi kuchimba visima vya maji katika Jimbo la Kalambo, lakini vingi havikuchimbwa kutokana na ukosefu wa magari ya kuchimbia visima, pia umbali toka vifaa hivi vilipo unaongeza gharama za uchimbaji wa visima katika Mkoa wetu. Gari lililopo ni kongwe na chakavu, je, Wizara haioni busara kwa Mkoa wa Rukwa kupata gari nyingine ili kuendeleza uchimbaji visima?

Mheshimiwa Naibu Spika, upo uwezekano wa kupeleka maji kwa vijiji vya Singiwe na Matai kwa kujenga bwawa kubwa la maji katika Mto Mzwalo. Maji haya yanaweza kutumika kwa binadamu, mifugo na pia umwagiliaji kwa ajili ya Vijiji nilivyotaja hapo juu (Matai na Singiwe). Je, Wizara watanisaidia vipi katika mradi kama huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ione jinsi ya kufufua mradi wa *NORAD* kwa ajili ya Vijiji vya Katuka (Jimbo la Kalambo) na Chelenganya, Kisumba, Mtanga, Mtimbwa Kasense na Kanondo vilivyoko katika Halmashauri ya Mji wa Sumbawanga lakini yakitoka Jimbo la Kalambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napongeza bajeti ya Wizara hii, sio tu kwa kuwa na mambo mengi ambayo yanatoa matumaini mapya lakini nimezingatia kuwa Jimboni kwangu miradi ya Kiwere, Kiponzelo na Kihanga imo katika mipango ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, hata hivyo naomba sana Wizara itazame uwezekano wa kuendeleza miradi miwili mingine kama ifuatavyo:-

Mradi wa maji ya kunywa wa Kiwere *(as opposed to Kiwele Irrigation)* ambao ulianza mwaka 1995-2000 na sasa umekwama baada ya wafadhili *(KKKT)* kushindwa. Vijiji vya Mgera, Kiwere, Mfyonye na Kitapilimwa vitafaidika. Kwa sasa maji yametoka mtoni (Malulumo) na kufika Mgera lakini vijiji vingine bado.

Mradi mwingine uko Magulilwa ulifanyiwa *feasibility study* miaka kama kumi hivi na ungefikisha maji ya kunywa katika vijiji visivyopungua 19 katika Jimbo la Kalenga na baadhi katika Jimbo la Kilolo na Isimani. Kuhusiana na miradi hii nitajitahidi kukuletea nakala za maandishi ya miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Wizara yako itusaidie kadri inavyowezekana. Kwa sasa nakutakia kila la kheri ili bajeti yako ipite bila matatizo wala usijali maneno ya waandishi uchwara wanaopiga vita wazee kama kwamba wao hawana wazee. *Keep it up! In fact you should run instead of walking so as to shame them.*

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wa Wizara kwa hotuba iliyoandaliwa kwa makini. Nawapongeza sana Wakala wa Uchimbaji wa Visima na Ujenzi wa Mabwawa kwa kazi nzuri wanayofanya ya kuchimba visima kama inavyojidhihirisha katika kiambatisho Na. 4 katika ukurasa wa 69 -85. Katika kipindi cha mwaka mmoja tu (miezi kumi na mbili) wamechimba jumla ya visima 437. Hongera sana *DDCA, keep it up.* Wingi wa visima vilivyochimbwa kwenye Wilaya inaonyesha ukubwa wa tatizo la maji kwenye eneo husika hasa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya Nyang'hanga na Kabila katika Jimbo la Magu imetengewa kiasi gani cha fedha? Miradi hii ni muhimu sana kwa kuwa maeneo husika yana matatizo makubwa sana ya maji. Miradi hii imekuwa ikipewa fedha kidogo kidogo sana, matokeo yake imechukua muda mrefu sana zaidi ya miaka mitano bila kufikia hata asilimia ishirini na tano. Naomba, chonde chonde miradi hii ikamilishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa fedha zilizotolewa kwa ajili ya kununua *floating intake* kwa ajili ya Mji wa Magu. Taarifa niliyopewa ni kwamba mashine tayari iko Magu lakini mfungaji ambaye ni *supplier* toka Afrika ya Kusini hajafika kuja kuifunga. Je, mashine hii itafungwa lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mabwawa, ni maoni yangu kwamba Wizara ichimbe mabwawa kila kijiji. Kama ilivyo kwa kila kijiji kuwa na shule ya msingi ingekuwa lazima kila kijiji kiwe na bwawa moja ambalo halikauki mwaka mzima. Kijiji changu cha Nyang'hanga Jimbo la Magu pia kingepata bwawa kama ilivyokuwa huko nyuma kulikuwa na bwawa lililojengwa na Mbunge wa Magu Marehemu Marco Mabawa, ambalo lilikuwa linahudumia vijiji vyote jirani. Naomba bwawa kila kijiji na mpango uandaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mji mdogo wa Kisesa katika Jimbo la Magu kuna tatizo gani hasa linalozuia wakazi wa Mji wa Kisesa kupata maji moja kwa moja toka Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Jiji la Mwanza? *Distance* toka mpaka wa Jiji la Mwanza na Mji wa Kisesa ni ndogo sana. Kwa nini Jiji wasilete maji Kisesa na wao watoze *bill?* Naomba ufafanuzi kwa nini hili lisifanyike ili kuwaondolea kero wananchi wa Kisesa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa mchango wa maandishi kama mchango wangu kwa Wizara ya Maji kama ifuatavyo:-

Nakiri kuwa Wilaya (Halmashauri ya Kibondo) imepangiwa shilingi milioni themanini kama fedha za kusimamia huduma za maji katika Halmashauri. Pamoja na kiasi hicho cha fedha bado ni kiasi kidogo mno ukilinganisha na matatizo yanayoikabili Wilaya hiyo. Matatizo ambayo yamekuwa sugu kwa zaidi ya miaka kumi iliyopita ni yafuatayo:-

Moja, bomba la maji linatoa maji kwenye *intake* ambayo iko umbali wa kilometa nne, ni nchi tatu kiasi kwamba bomba hilo halina uwezo wa kupitisha maji ya kutosheleza mahitaji ya wakazi 12,800 wanaoishi Kibondo Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuondoa tatizo hili ni kuwasaidia wananchi kwa Wizara hiyo ya maji kununua mabomba ya nchi sita ili wahandisi waweze kutandika mabomba hayo ambayo ndiyo yatawawezesha wananchi kupata maji bila matatizo. Mbali na hali hiyo Halmashauri pia imeshindwa kuwahudumia wananchi kwa kushindwa pia kutandika mabomba kwa wateja wa mji huo.

Pili, fedha za mafuta zinazotolewa kama *OC* ni ndogo mno kwa kuendesha mitambo inayosukuma maji kutoka kwenye *intake*. Ili maji yapatikane kila siku kwa mwezi Halmashauri inatakiwa kununua mafuta ya 17,600,000. Fedha inayopatikana ni chini ya kiwango kinachoweza kukidhi mahitaji. Ni vema sasa Serikali kwa kuitumia Wizara yenye dhamana kutuma wataalam Wilayani Kibondo kupata ufumbuzi wa matatizo hayo ambayo yamekuwa ni kero kubwa.

Tatu, kwa makusudi kabisa nashauri visima vichimbwe mashuleni kwa ajili ya huduma ya maji kwa wanafunzi.

Nne, kumekuwa kukijitokeza tatizo la watumishi wa Idara hiyo katika Wilaya ya Kibondo kutokufika kwa wananchi kunakotokana na Idara hiyo kutokuwa na gari. Nashauri lipatikane gari kwa ajili ya Idara hiyo nyeti katika Wilaya.

Tano, napendekeza pia lijengwe bwawa la kuhifadhi maji kwenye *intake* ili kuondoa tatizo la matope yanayosukumwa pindi mafuta ya kuendeshea mitambo yanapopatikana.

Sita, ombi la kununuliwa mashine kubwa ya kusukuma maji napenda kulitoa kwa Wizara yenye dhamana kununua mashine hiyo ya kusukuma maji. Mashine hiyo ni mbovu kila wakati na hali hiyo inasababisha wananchi wa Mji wa Kibondo kupata maji mara mbili kwa wiki. Hili lipewe kipaumbele.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia katika Wizara hii muhimu ya maji. Pia nimpongeze Waziri, Naibu wake, pamoja na wataalam wa Wizara yake kwa kuandaa bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tujuavyo maji ni kitu muhimu sana katika maisha ya binadamu, bila maji hatuwezi kufanya chochote kile kwa maendeleo ya wananchi na hatuwezi kufanya chochote kile kwa maendeleo ya wananchi na Taifa kwa

ujumla. Hivyo suala la maji ni jambo muhimu sana kwa maisha na Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, toka bajeti hii imesomwa kila Mbunge anayesimama na kuchangia anatoa kilio cha wananchi wake kuhusu tatizo la maji katika Jimbo analotoka. Napata wasiwasi kwamba zile asilimia 75 ambazo tumeambiwa maji yanapatikana katika nchi, sio sahihi nchi yetu, ingekuwa sahihi Wabunge wasingelalamika kama wavyofanya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimebahatika kutembea nchi nzima wakati wa kampeni, kwa kweli hali ya maji katika nchi yetu maji wanayotumia ni Mwenyezi Mungu tu ndiye anayewalinda na maradhi, vinginevyo Watanzania wengi wangepoteza maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, imefika wakati sasa kutekeleza ya leo yote mliyoahidi wakati wa kampeni kwamba wananchi watapata maji safi na salama, kura wametoa sasa kazi kwenu kutimiza yale yote mliyoahidi kwa wapiga kura wenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika tatizo hili la maji waathirika wakubwa ni akinamama hawa ndio wanateseka sana, hawana usiku wala mchana, wanashindwa hata kufanya kazi ndogo ndogo za kujitoa kwenye huu umaskini unaoikabili nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hayo maji ambayo yanapatikana hayafai kwa matumizi ya binadamu. Pia viko visima vingi vilivyochimbwa kwa gharama kubwa lakini havifanyi kazi, tunaomba Wizara hii husika iweze kufanya matengenezo katika visima hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la maji katika Jiji la Dar es Salaam ni kubwa sana, wakazi wa Jiji hilo wanapata shida sana hata huo mgao wenyewe uliosemwa haupo, misururu mingi ya ndoo tunayopishana nayo katika Jiji hilo inaondoa dhana nzima ya Jiji, naomba Wizara kwa kweli ifuatilie suala hili kama kweli tunataka kuondoa tatizo la ugonjwa wa kipindupindu katika Jiji letu, vinginevyo Watanzania wataendelea kufa kwa kukosa maji safi na salama. Mwisho nawatakia utekelezaji mzuri wa bajeti hii ambayo imewasilishwa katika Bunge letu hili. Naomba kuwasilisha.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naunga mkono hoja yako uliyoitoa hapo jana tarehe 10 Julai, 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuchangia Wizara hii upande wa mradi wa maji katika Mji mdogo. Katika mradi huu ambao unafadhiliwa na Ufaransa chini ya Shirika lake la *AFD.* Katika utekelezaji wa mradi huu uliohusisha Wilaya za Rufiji, Kilosa na Mpwapwa umeonyesha hali ya kusuasua kutokana na matatizo yafuatayo, moja, mkandarasi wa kuchimba visima hivyo alikuwa ni mmoja tu kwa Wilaya zote tatu. Hali hiyo ilisababisha utekelezaji wake kuchukua muda mrefu. Nashukuru visima hivyo vimechimbwa. Ushauri kwa hatua inayofuata ambayo ni ufungaji wa *pump* ni vizuri wakandarasi wakaongezwa ili utekelezaji wake uende kwa haraka.

Pili, kuhusu programu ya Taifa ya maji na usafi wa mazingira unaofadhiliwa na *World Bank* nao unasuasua. Visima vimechimbwa kwa muda mrefu lakini ufungaji wa *pump* umechelewa mno. Katika bajeti yake ameonyesha kuwa kwa mwaka huu wa fedha ukamilishaji wa visima hivyo virefu utatimia kwa kufunga *pump* katika vijiji vya Kimbuga, Mtawanya, Jaribu Mpakani, Ngarambe, Ruaruke na Muhoro. Ushauri, ni vizuri sana ufungaji wa *pump* hizo ukapewa wakandarasi wengi ili zoezi hilo likamilike kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ni vizuri sasa mabomba hayo yakaendelezwa katika vijiji vya jirani kwani visima vyote vina maji mengi. Vijiji kama Mchukwi, Miwaga, Ngulakula na Mjawa vinapatiwa maji kutokana na visima hivyo. Naunga mkono hoja.

**MHE. DR. MZERU O. NIBUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Napenda kuchangia Wizara hii muhimu kama ifuatavyo, katika Manipsaa ya Morogoro tunavyo vyanzo vya maji kutoka Mto wa Morogoro na Bwawa la Mindu. Matanki yaliyojengwa kwenye Mto wa Morogoro ilikuwa kwenye miaka ya 1960 ambapo idadi ya wakazi wa Morogoro walikuwa wachache sana chini ya 80,000 na katika bwawa la Mindu zipo hitilafu zilizojitokeza. Bwawa hilo hivi sasa limepoteza kina chake kutokana na kujaa tope na *filter* zilizopo hazina uwezo mkubwa wa kuchuja maji kwa ajili ya matumizi ya watu wetu, lakini pia mashine za kusaidia kusukuma maji kutoka kwenye matanki na kwenda Mjini kwa ajili ya matumizi.

Hivi sasa wakazi wa Manispaa ya Morogoro idadi yao imeongezeka kutoka chini ya 80,000 hadi zaidi ya 250,000. Hivyo basi, wananchi hawa karibu nusu ya idadi hiyo hawapati maji kabisa au hawapati maji ya kutosha. Hata hivyo, Shirika la Maji Safi na Maji Taka katika Manispaa hiyo bado inahitaji msaada zaidi kwani gharama za kuboresha huduma za maji ili watu wote waweze kupata maji safi, salama na ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, naomba Serikali (Wizara ya Maji) watusaidie kutuchimbia visima vya mdundiko kwani baadhi ya sehemu za Manispaa hazina maji kabisa na kusubiri maji ya bomba wanazidi kuumia hasa kwa kuzingatia maji ni uhai na pia tukitilia maanani kwamba Manispaa ya Morogoro ipo bondeni ikizungukwa na milima. Hivyo basi, milipuko ya magonjwa ya kuambukiza kama kipindupindu na *Typhoid.* Hivyo basi, naiomba Serikali itilie maanani kuwanusuru wananchi hawa wa Manispaa ya Morogoro ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani yetu ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi hawa hawataielewa Serikali yao kwa vile vyanzo vya maji vipo na vya kutosha ila uwezo wa Serikali kwa kuwasambazia maji wananchi haupo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba Wizara ya Maji itilie mkazo jambo hili sambamba na usambazaji wa maji ya bomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji kwa moyo wa dhati kwa kuchaguliwa bila kupingwa na wananchi wa Bunda na hatimaye kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri wa Maji. Mimi sikushangaa kwa hayo yote kwa kuwa najua uwezo wake wa uchapaji kazi pamoja na uzalendo wake. Hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyomwandikia Mheshimiwa Waziri wa Maji barua yangu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Rorya kwa kukubali kutusaidia kwa kutuwezesha kupata bwawa/lambo moja kwa mwaka wa fedha 2006/2007 na mwaka 2007/2008 bwawa la pili na baadaye mwaka 2008/2009 bwawa la tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeorodhesha mabwawa kwa majina katika barua yangu niliyomwandikia Mheshimiwa Waziri wa Maji kama alivyoagiza. Namshukuru sana Waziri wa Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani zangu, napenda kutoa ushauri kwa lengo la kuboresha hotuba ya Mheshimiwa Waziri iliyo nzuri yenye matumaini ya uhai kwa kuwa maji ni uhai kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 61 katika ukurasa wa 29. Naunga mkono mpango wa Wizara hii kuhusu kuwapatia wananchi wa vijijini huduma ya maji kwa ajili ya matumizi ya watu na mifugo kwa kujenga mabwawa na malambo. Kwa kipindi cha miaka 40 wananchi wa Jimbo la Rorya, Kata za Roche, Kitembe, Buhura na Ihoma walikuwa wanakwenda Kenya kufuata maji kwa ajili ya matumizi yao na mifugo. Walikuwa wananyanyaswa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia mwaka 2002 - 2005 wananchi kwa kushirikiana na Mbunge wao wameweza kuchimba mabwawa/malambo matatu, Wakenya sasa wanafuata maji Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu wananchi wa kijiji cha Ngape, Kata ya Roche wamechanga shilingi milioni mbili. Wizara hii imechangia shilingi milioni tano na Halmashauri ilitakiwa kuchangia shilingi milioni tatu hadi sasa hawajachangia. Tunashauri Wizara yako itoe shilingi milioni tatu na TAMISEMI ilipe Wizara ili kumaliza kero hii. Mabwawa 15 yamekwishapimwa na wataalam wa Wilaya na Mkoa, gharama ya kujenga ni kubwa na itachukua miaka mingi na tunaomba miradi ya mabwawa haya 15 yaingizwe katika Miradi ya Kitaifa itakayofadhiliwa na wafadhili kutoka nje. Baadhi ya mabwawa haya yataingizwa katika mpango wa MKUKUTA, hata hivyo fedha zilizotengwa ni ndogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa linalokabili na kurudisha nyuma jitihada za Serikali ya CCM katika kutoa huduma ya maji haraka ni ukosefu wa

Wahandisi wa Maji. Halmashauri ya Wilaya ya Tarime ndiyo iliyoathirika sana. Hakuna Mhandisi wa Maji aliyefuzu. Tunaomba Mhandisi wa Maji wa Wilaya na mafundi katika sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na barua yangu niliyokuandikia kuhusu jina la bwawa na pamoja na kuchagia hoja ya hotuba yako naendelea kukushukuru sana kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Rorya kwa kukubali kuwapatia bwawa moja katika bajeti ya mwaka 2006/07.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuletea jina la bwawa la Kanyisambo. Hata hivyo wananchi wa vijiji vinne wameomba bwawa sasa liwe bwawa la Kujunge. Nakutakia mafanikio mema.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri wa Maji kwa hotuba ya bajeti yenye kuleta matumaini na inayotekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tatizo la maji Mji wa Manyoni. Mji wa Manyoni una kero kubwa sana ya maji. Mahitaji ya maji kwa siku ni lita milioni moja lakini upatikanaji wa maji ni lita 150,000 tu kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Wizara kwa kumleta Naibu Waziri siku chache zilizopita kuja kuona tatizo hili. Tunashukuru pia kweli Mji huu sasa umekuwa chini ya Mradi wa Benki ya Dunia. Tunaiomba Wizara mambo mawili.

Moja, mwelekezi *(consultant)* aje haraka ili atupatie vyanzo vya maji ili mradi wa kuchimba maji usichelewe kwani wananchi wanateseka sana.

Pili, pamoja na kuchimba visima ambavyo wakati wa kiangazi kikali hukauka, tunaomba lichimbwe bwawa kama maji ya kianzio cha maji Mjini Manyoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kufufua mabwawa ya maji vijijini, huko nyuma vijiji vingi Wilayani Manyoni vilikuwa na mabwawa yaliyosaidia sana kupunguza tatizo la maji wakati huo. Mabwawa hayo yapo 25 takribani yote yamejifukia *(silting)*. Tunaomba Wizara iweke makatapila katika Kanda au Mkoani ili Wilaya ziyapate na kuweka dizeli na kuwalipa *operators* na kuchimbia mabwawa hayo yaliyojaa michanga. Mpango huu utaleta *impact* kubwa kwa muda mfupi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Miradi chini ya Benki Dunia. Tunashukuru sana Wizara kwa kubuni mradi huu wa Maji Vijijini na Usafi wa Mazingira. Wilaya ya Manyoni ilibahatika kuingia katika mradi huu tangu mwaka 2004/2005. Ni mradi muhimu sana. Tatizo ni utekelezaji wa mradi. Hivyo utekelezaji umechelewa mno. Tangu mwaka 2004/2005 katika Wilaya ya Manyoni hakuna mradi hata mmoja

uliokamilika. Lipo tatizo la wananchi kuchangia asilimia tano, lakini hata pale michango inapotolewa kwa kiwango cha kuridhisha bado ucheleweshaji upo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naishukuru tena Wizara hii kwa kazi nzuri inayoifanya katika kupambana na kero ya maji nchini na hivyo naunga mkono hoja hii.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la ushirikishaji na maelewano na sekta nyingine, kifungu cha 94 ukurasa 46 nashauri Wizara ya Maji ishirikiane na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kuhakikisha kuwa hakutakuwa na mgongano kati ya Sera ya Kuhifadhi Vyanzo vya Maji na Sera ya Umwagiliaji kwa kuzingatia utekelezaji wa tathmini ya athari za mazingira *(EIA)* ya miradi ya umwagiliaji na matokeo ya tathmini hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini za mazingira *(EIAS)* zinahitaji fedha na wataalam wa kufanya tathmini hizo. Bila shaka fedha hizo kwa ajili ya tathmini ya miradi hiyo zimepewa kipaumbele ingawa bajeti haionyeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila shaka suala la *EIA* na miradi yote ya maji na miradi ya umwagiliaji halitapuuzwa na kuendelea kutekeleza miradi ambayo haitakuwa endelevu kwa mabomba kutoa hewa baada ya muda na miradi ya umwagiliaji kwa kuitekeleza kwa kukosa maji au kuharibika kwa udongo.

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa mchango katika hoja hii ya maji. Mchango wangu mkubwa nauelekeza katika tatizo la ukosefu wa maji Kigoma Vijijini na hasa Jimbo la Kigoma Kusini. Karibu eneo lote la Jimbo ukiacha maeneo machache yaliyo na vyanzo vya maji vya uhakika. Vyanzo hivyo ni Mto Malagarasi ambao umetawanya maji eneo la ukanda wa Mashariki ya Jimbo ukipita Tarafa za Nguruka yenye Kata za Nguruka, Mganga, Mtego wa Noti na Uvinza. Mto huu unatosha kabisa kuwezesha vijiji karibuni vyote vya Kusini Mashariki kwa kila Jimbo kupata maji ya uhakika kama mipango ya uhakika itatiliwa mkazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo eneo la katikati ya Jimbo ambalo linaguswa na kupitiwa na mto Luiche, Ziwa Tanganyika na vijito vidogo ambavyo havikauki. Hili linahusisha Kata za Kandaga, Simbo na Ilagala.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatizo ni lile la Kigoma Kusini katika mwambao wa Ziwa Tanganyika ambalo lina Mto Malagarasi, Lugufu, Rongonya, Lagosa na mito mingine midogo na Ziwa Tanganyika. Maeneo yanayoguswa hapa ni Kata ya Sunuka, Sigungunga, Ilagala, Igalula, Buhingu na Kalya.

Ni vyema basi maji yaliyotawanyika kutokana na hali hiyo, hivi ni kweli tuna umakini katika Serikali tunapowahitaji vijiji wachangie asilimia tano katika kupatikana maji vijijini. Hivi ni kweli shilingi milioni 44 zinatosha kutoa huduma ya maji katika

Majimbo mawili ya Wilaya ya Kigoma Vijijini? Naomba ufuatiliaji wa hoja ya maji vijijini katika Jimbo hili.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza baada ya kumpongeza Rais wetu mpenzi Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi sana kuwa Mwenyekiti wa CCM pamoja na Sekretariati yake ikiongozwa na Mheshimiwa Yusuf Makamba Mbunge, naomba kutoa mchango wangu.

Pili, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Naibu Waziri pamoja na watumishi wote wa Wizara ya Maji kwa kazi nzuri sana. Ni hotuba iliyokidhi mahitaji na hisia ya Watanzania wengi , wembe ni ule ul maji *spirit*.

Tatu, kwa vile kazi ya kuwapatia maji wananchi wote nchi zima, maji kwa matumizi ya wanyama, maji kwa ajili ya umwagiliaji mashamba, haya ni majukumu makubwa sana. Ombi langu Serikali iongeze maradufu bajeti ya Wizara ya Maji ili kuboresha mafao ya watumishi wake wote na hususan wale wanaofanya kazi katika mazingira magumu. Serikali iongeze vyombo vya usafiri katika Wizara hii.

Nne, mradi wa maji vijijini na usafi wa mazingira ni mzuri sana, lakini vijiji vingi vinashindwa kuchangia ile asilimia tano. Kuna kucheleweshwa mno mpaka wananchi wanakata tamaa. Mwisho, tunashukuru kuwa kila Mkoa, Wilaya na Tarafa zimetajwa katika mradi huu.

Tano, Mradi wa Maji katika miji midogo, mradi huu ni mzuri sana. Vile vile Wizara imejitahidi sana kueneza mradi huu kila pembe ya Tanzania. Lakini utekelezaji wake unachelewa mno mpaka miji mingi midogo inakumbwa na magonjwa mengi hasa ya kipindupindu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ianze utekelezaji wa mradi huu, uanze na miji ya Utete, Kibiti na Ikwiriri kwani hali ya maji katika miji hiyo ni mbaya sana. Utete ni Makao Makuu ya Wilaya ya Rufiji, basi naiomba Wizara ianze na Mji wa Utete/Rufiji katika kuutekeleza mradi huu.

Mwisho, Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza tena Wizara ya Maji kwa kazi nzuri na bajeti safi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na nashukuru kwa kupokea mchango huu. Ahsante.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Naibu Waziri wa Maji kwa kazi nzuri wanazofanya za kufuatilia matatizo ya maji hapa nchini.

Kuhusu tatizo la maji Mkoani Dar es Salaam, mimi nadhani kungekuwepo na mipango ya muda mfupi na muda mrefu yenye utekelezaji wa uhakika na pia

uzingatie muda na utekelezaji wake. Mto Rufiji utumike kupunguza tatizo la maji Mkoani Dar es Salaam.

Kwa upande wa visima virefu vilivyopo Mkoani Dar es Salaam na kwa kuzingatia idadi kamili ya visima vilivyoko katika hotuba ya Waziri wa Maji, inaweza kusaidia kwa kiasi kikubwa matatizo ya maji, kwa maana ya kwamba mapato ambayo yanatokana na mauzo ya maji katika Kamati za Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati za Maji haziwajibiki ipasavyo, ingefaa Kamati hizi zitafutiwe muundo mpya au mfumo mpya katika kuboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingefaa Kamati za Maji ziwe na utaratibu wa kutoa taarifa za mapato na matumizi kila mwezi na ziende kwenye Kamati za Fedha na Uongozi za Halmashauri nchini kwa lengo la kudhibiti ubadhirifu. Hii itasaidia kuchimba visima vingi zaidi kuliko hali iliyoko sasa, Wenyeviti wa Mtaa wameshindwa kusimamia yaani wamezidiwa nguvu na wajanja walioko kwenye Kamati za Maji. Wengi wao si wazalendo na uaminifu ni mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Wilaya ya Ilala, Jimbo la Ukonga hali ya ukosefu wa maji ni mbaya na hasa katika maeneo yafuatavyo, ambazo ni Kata za Chanika, Msongola, Pugu, Segerea, Kinyerezi, Vingunguti, Buruguni, Kitunda na Tabata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Kata za Msongola na Chanika ni kame na maji hayapatikani kwa urahisi. Naomba Serikali ingalie maeneo haya korofi ya ukame kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante nawasilisha na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kupata nafasi ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Maji.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri. Pamoja na pongezi zangu ninaomba nichangie machache.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa na Wizara kuchimba visima virefu kwa lengo la kuwapatia wananchi maji, lakini jitihada hizi hazikufanikiwa kwa sababu maji hayapatikani, katika asilimia kubwa ya visima vinavyochimbwa hasa katika maeneo kame kama Dodoma, Singida na kadhalika. Kutokana na hali hii ni vyema sasa Wizara iangalie vyanzo vingine vya kuwapatia wananchi maji. Ushauri wangu ni kuwa tungeelekeza nguvu katika teknolojia ya kuvuna maji ya mvua, hususan uchimbaji wa mabwawa makubwa ikiwezekana tuchimbe bwawa moja katika kila Kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimkumbushe Mheshimiwa Waziri wa Maji kuhusu mradi mkubwa wa Ntomoko, Wilayani Kondoa. Nimefarijika kuona

kuwa *scheme* ya Ntomoko imewekwa katika bajeti ya mwaka 2006/2007. Naomba Wizara ifuatilie mradi huu uanze mapema iwezekanavyo kwa sababu wananchi wa maeneo hayo hawana chanzo kingine cha maji. Huko nyuma Serikali iliamua maji kwa ajili ya Mji wa Dodoma yatoke mto wa Bubu, Wilayani Kondoa. Utafiti uliofanyika ulibaini kuwa kama bwawa litajengwa katika Mto Bubu eneo la Kijiji cha Farkwa bwawa hili lingeweza kuwa chanzo cha maji kwa mji wa Dodoma. Maji hayo yangefika Dodoma kwa njia ya mtiririko *(gravity).*

Naomba nikumbushe Mheshimiwa Waziri kuwa Mji wa Dodoma unakua na utakua kwa kasi hasa pale Vyuo Vikuu viwili vitakapofunguliwa hivi karibuni. Vyanzo vya maji vinavyotegemewa hivi sasa katika Mji wa Dodoma ni visima virefu ambavyo vina ukomo maana maji yanazidi kupungua katika visima hivyo. Nashauri Wizara ianze maandalizi ya mradi wa maji ya Mto Bubu kwa ajili ya Mji wa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuchangia hayo machache, naomba kutamka kuwa naunga mkono hotuba ya Waziri wa Maji.

**MHE. MATHIAS M. M. CHIKAWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, jimbo la Nachingwea ni moja ya Wilaya ambazo zinakabiliwa na tatizo sugu la ukosefu wa maji safi na salama. Kwa kipindi cha zaidi ya miaka thelathini sasa juhudi za kuipatia maji Nachingwea zimegonga mwamba. Hatua zote ambazo zimechukuliwa hazijafanikiwa kumaliza tatizo la maji Nachingwea hata kwa asilimia 20% tu.

Wakati wa Kampeni za Uchaguzi za mwaka 2005, mgombea Urais wa CCM, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, aliwaahidi wakazi wa Nachingwea kuwa tatizo la maji Nachingwea litakwisha kwa Nachingwea kupatiwa maji kutoka chanzo cha Mbwinji. Imekwisha fahamika siku nyingi kuwa Mbwinji ina maji ya kutosha kwa miji ya Masasi na Nachingwe. Lakini tangu wakati huo hakuna hatua zozote za kuonekana ambazo zimechukuliwa na Serikali kutekeleza mradi huu wa Mbwinji.

Namuomba Waziri wa Maji wakati atakapowasilisha maelezo na majibu yake atoe maelezo kwa watu wa Wilaya ya Nachingwea kuhusu ni lini mradi wa kupeleka maji Nachingwea kutoka chanzo cha Mbwinji utaanza kutekelezwa. Kwa bahati mbaya, bajeti ya Wizara haionyeshi/haijatenga fedha zozote za kutekeleza mradi huu. Wananchi wa Nachingwea walipewa ahadi ya Maji ya Mbwinji na Rais wao kadhalika na Ubunge wao, yule aliyekaa miaka 30, aliyeondoka pamoja na mimi mwenyewe. Nashukuru sana kwa kunivumilia.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wa ngazi zote walioshiriki katika kuiandaa hotuba hii. Ni hotuba nzuri inayozingatia mahitaji ya wananchi kote nchini na uwezo halali wa Serikali kutoa huduma ya maji kwa mwaka huu wa fedha. Nawapongeza sana.

Namwomba sana Mheshimiwa Waziri wakati wa kuhitimisha hoja yake atoe maelezo japo kwa kifupi kuhusu haya yafuatayo:-

Kwanza, kwa mradi wa kupeleka maji Shinyanga na Kahama hususan ile sehemu inayopeleka maji Tarafa ya Mwamashimba, Kwimba. Ni lini mradi huo utakamilisha kwa kufikisha maji kwa Tanki la mradi wa zamani (Mhalo), ninaamini majukumu ya Halmashauri ya Wilaya katika mradi huo, wananchi katika mradi huu wana jukumu yapi na mara baada ya maji kufikishwa kwenye tanki la mradi wa zamani, lini maji yataanza kusambazwa katika tarafa ya Mwamashimba na usambazaji huo unatarajiwa kukamilishwa lini, na kwa utaratibu gani?

Kuhusu malambo kwa vile juhudi za uchimbaji wa visima virefu na vifupi Wilayani Kwimba hazijafanikiwa sana hususan Tarafa za Mwamashimba na Nyamilama, mfano *Hesawa* visima vingi havifanyi kazi. *UNICEF* mara kadhaa hawakufanikiwa kupata maji Chibuji, Mwamashimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Caritas* wameshindwa kabisa kupata maji katika visima 10 na pesa ikabakia kwa mfadhili *(Tanzania Japan Food Counterpart Fund).* Je, Wizara inaweza kuongeza juhudi zaidi kuhusu uchimbaji wa malambo na utaalamu wa uvunaji maji katika Jimbo na Wilaya ya Kwimba hususan katika taasisi kama shule za sekondari, shule za msingi, zahanati na vituo vya afya?

**MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Napenda sana nitolewe hofu ambayo sasa inanikosesha raha. Je, kuna *research* yoyote iliyofanyika juu ya kupungua kwa kina cha maji katika maziwa yetu. Sababu zake na nini kifanyike? Suala la kupungua kwa kina cha maji Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika kunaleta usumbufu mkubwa kwa waendeshaji wa vyombo vya usafiri (meli) katika maziwa hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, mradi huu wa maji yanayopelekwa Shinyanga na kwingineko hakutapunguza zaidi kina cha maji hasa ukitilia maanani yale yaliyofanywa na Uganda ya kujenga *dam* kubwa la kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Waziri je, uko tayari kufanya stadi ya kujua *prons & cons* za mradi huo na athari zake kwa vyombo vya usafiri katika maziwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kusogeza magati/chelezo katika kina kikubwa cha maji kwa vile itakuwa ni kujenga upya magati yote. Aidha, kuchimba na kuondoa mchanga ni gharama kubwa zaidi. Je, mradi wa maji ukianza itakuwaje? Suala hili linaikumba Burundi na Kongo kwa *Lake Nyanga,* tusaidieni, tushirikiane ili mradi ufanikiwe na sisi wengine tusiathirike.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hotuba ya Waziri wa Maji kwa asilimia mia moja na tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, namjua, najua uwezo wake, hana longolongo, ni mkweli, kama hakuna hasiti kusema haiwezekani.

Endelea kuwa muwazi na mkweli kama alivyokuwa Waziri aliyekutangulia Mheshimiwa Edward Lowassa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nafahamu uwezo alionao Naibu Waziri, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, tulikuwa tukikaa benchi moja Bunge lililopita, hivyo una msaidizi mzuri na niwapongeze akiwemo Katibu Mkuu wake, Wakurugenzi wote wakiwemo Wahandisi wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni uhai, bila maji hakuna uhai. Naipongeza Wizara kwa kuiweka katika mpango wa kukarabati miradi ya Maji vijijini hasa vijiji vya Sumve/Mantare, naomba na kusisitiza ombi langu la siku nyingi. Ninaamini chini ya Mkurugenzi wa Miradi wa Maji Vijijini, Bwana Sayi suala la Sumve/Mantare pesa zake zitatolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni mwanzo mzuri, naitakia kila la kheri na mafanikio makubwa Wizara yako. Naunga mkono hoja.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja hii asilimia moja kwa mia moja.

Kwanza nimpongeze Waziri wa Maji, Naibu Waziri kwa kutoa hotuba yenye mwelekeo wa kumaliza tatizo la maji mijini na vijijini. Vile vile niwapongeze watendaji kwa kuandaa hotuba hii.

Naishukuru Serikali kwa kutenga fedha za kujenga visima katika Wilaya zote za Mkoa wa Dodoma. Naishauri Serikali kwa kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge wa Majimbo na wa Viti Maalum tusaidiane kulimia na kukamilisha ujenzi wa visima hivyo.

Kwa sisi wa Mkoa wa Dodoma na kwa kuwa ni eneo lenye ukame mkali tunaomba Serikali ielekeze nguvu zake ikiwa ni pamoja na kufufua mabwawa ya kisima cha Ndege, Mwisanga kwa Madebe na mengine.

Naomba nisemee Bwawa la Mwisanga lililopo Wilaya ya Kondoa ambalo lilijengwa zaidi ya miaka 15 na liligharimu fedha nyingi za Serikali. Bwawa hili lilikuwa ni ukombozi wa vijiji vingi vilivyoko tambarare. Ningeomba Mheshimiwa Waziri mfike katika bwawa hilo muone jinsi lilivyo na umuhimu ili tusaidiane kuliwekea utaratibu wa kulifufua.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya naunga mkono hoja hii.

**MHE. PROF. MARK J. MWANDOSYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja ya Waziri wa Maji kwa asilimia mia moja. Hotuba imeandikwa kwa umakini, umahiri na ufundi wa hali ya juu. Sikutegemea vinginevyo kwani nilibahatika kufanya kazi na wengi wa watendaji, ikiwa ni pamoja na Katibu Mkuu Bwana Patrick Rutabanzibwa, miaka ya mwanzo wa 1990, nikiwa Katibu Mkuu wa iliyokuwa Wizara ya Maji, Nishati na Madini. Mheshimiwa Waziri Stephen Wasira ameiwasilisha hotuba yake kwa utulivu na kueleweka vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi iliyo mbele yetu ni kubwa. Matarajio ya wananchi ni makubwa na raslimali ni kidogo. Hata hivyo mipango iliyowasilishwa ni mizuri na inatekelezeka. Mwaka jana, kijana wangu akiwa Marekani, alipopitia *internet* akapata hotuba niliyoitoa Moshi, mwaka 1990, wakati wa ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa Wahandisi wa Maji na akaninukuu nikisema: "Serikali itahakikisha kwamba ifikapo mwaka 2000, kila Mtanzania atapata maji safi kwa umbali usiozidi mita 400." Akaniuliza vipi, mmefikia wapi? Nashukuru kwamba Wizara imepitia upya malengo hayo ili yawe yanayotekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo mchango wangu utahusu mradi tarajiwa *(proposed project)* ya *Lwangwa Water Supply Project*. Lwangwa ni mji mdogo ulio Wilaya ya Rungwe, jimbo la Rungwe Mashariki. Lwangwa ni Makao Makuu ya Tarafa ya Busokelo na vile vile Makao Makuu ya Jimbo la Rungwe Mashariki. Mradi wa maji wa Lwangwa ulibuniwa mwaka 1959 na ulitekelezwa mwaka 1970. Ulibuniwa kwa ajili ya kupeleka maji safi vijiji vya Ndembo, Mpanda/Kisangali na Lwanga/Ikama, wakati ule ulikuwa uhudumie watu 700 na sasa watu ni 10,000. Kutokana na uchakavu na ongezeko la watu na muda uliopita, kuna tatizo kubwa la maji. Lwangwa imekuwa kutoka kijiji kufikia mji mdogo wenye wakazi wengi na biashara kubwa. Utafiti wa awali umeonyesha kwamba vyanzo vile vile vya maji vya Sabilo na Mwandanji, vinaweza kukidhi mahitaji ya sasa na ya baadaye. Mradi unatakiwa usanifiwe na kujengwa upya. Makadirio ya awali ni kwamba mradi huu unaweza ukahitaji shilingi milioni 150, kwa gharama za mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sijaona mradi huu mkongwe katika mpango wa Wizara, naomba Mheshimiwa Waziri auzingatie na kuona nini kinawezakana katika mwaka huu wa fedha wa 2006/2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji kwa hotuba yake nzuri. Naahidi kutoa ushirikiano mkubwa katika suala la hifadhi ya mazingira ya vyanzo vya maji na usafi wa mazingira kwa ujumla. Naunga mkono hoja hii.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Stephen Wasira, Waziri wa Maji, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Maji.

Hotuba iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri ni nzuri, maelezo yake marefu na takwimu za kutosha inatoa matumaini kwamba ipo mipango ya mikakati ya dhati ya kukabiliana na tatizo sugu la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni uhai, hivyo kiasi cha maji yanayopatikana yanapaswa kutunzwa. Kinyume cha hili utashangaa kuona baadhi ya watu wakitoboa au kukata mabomba na kufanya yamwagike ovyo. Lakini pia maji mengi hupotea njiani kabla ya kumfikia mlaji/mtumiaji kutokana na mabomba yaliyochakaa. Wizara inayo kazi kubwa ya kudhibiti upoteaji wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi Wizara ina mpango gani wa kuvuna maji ya mvua zinaponyesha? Kama watu wote/wengi wangeshauriwa kuvuna maji ya mvua yangeweza kupuguza tatizo la maji. Kama wajenzi wangeshauriwa kuweka *gutters* za kukinga maji ya mvua kwenye majengo makubwa na kuyaelekeza kwenye visima vilivyojengwa kwa makusudi hayo, maji hayo yangeweza kutumika kwa matumizi mbalimbali ya kawaida lakini pia kumwagilia bustani za maua na mboga na hivyo kupunguza matumizi ya maji ya bomba yanayopatikana kwa gharama kubwa. Aidha, wananchi wa kawaida wahamasishwe kukinga maji ya mvua yanayopotea bure. Utakuta mvua inanyesha kwa wingi lakini baada ya kukatika mtu anasema hana maji. Suala la mabwawa katika maeneo kame ni muhimu sana kwa ajili ya matumizi ya binadamu na wanyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, namaliza kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa juhudi wanazofanya katika kutatua tatizo la maji.Naunga mkono hoja.

**MHE. MWANTUMU B. MAHIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia kuhusu tatizo la maji katika Wilaya mpya ya Mkinga iliyotokana na Wilaya mama Muheza. Miradi mingi sana ya maji imekufa Muheza tu. Napenda kuomba rasmi kuwa Wilaya ya Mkinga kama Wilaya mpya inafaa ikaandaliwa utaratibu maalum wa kuwapatia visima virefu ili wananchi wa Mkinga nao waweze kufaidika na huduma hiyo.

Napenda kushauri kuwa wataalamu waende sasa Mkinga kule Moa, Mayomboni, Duga Maforoni, Mtimbwani, Mkinga Mpirani, Chongoleani, Vyeru, Kwale Manza - Kilulu, Mbuyuni, wakapimiwe yaani *(survey)* ifanyike ili angalau kwa kuanzia wachimbiwe visima ambavyo vitapunguza kero na adha kubwa wapatayo wananchi hao.

Pili, naomba wataalamu waende Moa, kule kuna kisima cha muda mrefu (miaka mingi) ambacho kinatoa maji baridi yasiyo na chumvi. Ni imani yangu kuwa pale panao mwamba wenye maji mengi na mazuri. Kisima hiki nimekikuta na hadi leo kinatumika.Kwa heshima na taadhima, ninaomba Wizara ya Maji ipeleke wataalamu kule ili upembuzi yakinifu ufanyike. Hali ni mbaya sana kule hasa wakati wa kiangazi. Wananchi wa Mkinga wapo tayari kutoa ushirikiano ili wapatiwe maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Wabunge wenzangu katika kuwapongeza kwa kazi nzuri. Naunga mkono hoja.

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wasaidizi wao kwa kazi ngumu na nzuri wanayofanya ya kuhakikisha Watanzania wanapata maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara inisaidie katika Jimbo la Nkenge, Tarafa ya Missenyi na Kiziba kuboresha miundombinu ya maji. Naomba Wizara itambue kwamba tarafa hiyo ina rutuba lakini tatizo ni eneo kame. Naomba Wizara itoe

kipaumbele katika kuelekeza miradi ya maji katika Tarafa ya Missenyi, kama ambavyo hufanya katika maeneo mengine ya Tanzania yaliyo kwenye kundi la maeneo kame.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa Tarafa ya Kiziba, kuna miradi mingi ya maji iliyoanzishwa miaka ya 1970 ambayo kwa sasa haifanyi kazi. Naomba Wizara ishirikiane na Halmashauri ya Bukoba ili tuweze kukarabati miradi hiyo. Miradi ninayoomba kukarabatiwa iko katika kata za Gera, Ishozi, Ishunju, Kanyigo, Ruzinga, Bugandika na Kashenye.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi tajwa hapo juu ikikarabatiwa itasaidia sana kufikisha maji maeneo mengi ya Jimbo la Nkenge na kuwapatia wananchi maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba niwapongeze, Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kwa kuisimamia vema Wizara hii bila kuwasahau watendaji wakuu na watalaam wote katika Wizara hii. Hivyo ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Pili, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, kwa niaba ya wakazi wote wa Jiji la Mbeya, kwa ziara aliyofanya na kutatua matatizo yao bila kuchoka. Kwa kiasi kikubwa ametatua matatizo ya wananchi wangu kwa asilimia 90, hongera!

Tatu, naomba niwashukuru sana wafadhiri wa *EU* na Serikali ya *Germany* kwa utekelezaji wa mradi mkubwa wa maji ndani ya Jiji la Mbeya na pia niwashukuru Mamlaka ya Maji Taka na Maji Safi kwa usimamizi wao madhubuti wa mradi huu kabambe na kuhakikisha unakwisha kwa wakati.

Nne, naomba sasa nitoe ushauri wangu juu ya usambazaji wa maji safi ndani ya Jimbo langu la Uchaguzi la Mbeya Mjini.

Kwaanza, vioski kwa ajili ya watu wasio na uwezo wa kuvuta maji majumbani ziwepo katika kila mtaa na sera ya kuwapatia ndoo 8 kila siku kwa wasio na uwezo kabisa iwekwe wazi kila mtaa. Vioski vilivyofungwa vifunguliwe.

Pili, uongozi wa mamlaka ya maji safi na maji taka ndani ya jiji uachane sasa kuwatumia waliokuwa wajumbe wa bodi ya maji bonde la uyole, hawa kwa kiasi kikubwa hawafuati taratibu na sheria ila mabavu dhidi ya wananchi kusababisha kero zisizo za lazima. Sheria itumike zaidi kuliko ubabe na mabavu. Uongozi wa mamlaka ya maji taka na maji safi ujiamini na kutekeleza majukumu yao kadri miongozo iliyopo waachane na baadhi ya viongozi wa kisiasa ambao ushauri wao mwingi ni butu aidha, ni wa kimaslahi zaidi kuliko utendaji. Mfano tatizo la chanzo cha Mwatezi, Uyole, waliopewa jukumu hawakutekeleza kulimaliza mpaka alipofika Naibu Waziri na kuokoa jahazi.

Tatu, mamlaka ya maji safi na maji taka ya jiji la Mbeya izingatie makubaliano ya awali ya kuachia maji kwa ajili ya matumizi ya wakulima eneo la Nsalaga, eneo hili ni pale ambapo zimewekwa pampu kwenye *Nsalaga Springs,* ni vema maji yakaendelea kuwasaidia wananchi badala ya kuukausha mto wote. Ikumbukwe kuwa kama Mbunge nilifanya kazi ya ziada kuwaomba wananchi waridhie Mamlaka kuchukua maji hayo kwa ajili ya uboreshaji wa upatikanaji wa maji safi Uyole.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudie tena, mamlaka iachane kabisa na wajumbe wa bodi ya maji ya Bonde la Uyole kuwa sehemu ya watumishi wa mamlaka hawa ni kero. Watumishi wa umma watumike zaidi yaani wa mamlaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia hoja iliyopo mbele ya Bunge lako Tukufu hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ningependa kutoa pongezi zangu za dhati kwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Stephen Wasira Mbunge, Naibu Waziri, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Katibu Mkuu na watalaam wote wa Wizara kwa utendaji wao bora na hotuba nzuri yenye mwelekeo sahihi na kuleta matumaini kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005, sekta ya maji ina umuhimu mkubwa sana kwa maendeleo ya jamii na uchumi wetu kwa jumla. Zaidi ya mahitaji kwa ajili ya matumizi ya wananchi na mifugo yao, maji ni muhimu sana kwa sekta za uzalishaji kama vita kilimo, viwanda na nishati itokanayo na maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara hii kwa mipango, mikataba na hatua thabiti za kuhakikisha kupatikana maji ya kutosha, safi na salama kwa ajili ya matumizi ya wananchi, mifugo na shughuli nyingine za uzalishaji mali, kwa kupitia mipango mbalimbali, ikiwemo ya Benki ya Dunia na *TASAF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mpango wa maji chini ya Mradi wa Benki ya Dunia ningependekeza baada ya mpango huu kutoa fursa ya vijiji kumi kwa kila Wilaya. Nashauri Wilaya mpya kama vile Wilaya ya Mkinga ziongezewe vijiji vitano ili viwe na jumla ya vijiji 10 vitakavyofaidika kama ilivyo kwa Wilaya nyingine zote. Aidha, napendekeza Wilaya zilizozaa Wilaya mpya kama vile Wilaya ya Muheza, nazo ziongezewe vijiji vitano ili viwe na jumla ya vijiji 10 vitakavyofaidika kama ilivyo kwa Wilaya nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu na unyeti wa mahitaji ya maji unastahili ukaambatana na usimamizi madhubuti zaidi wa vianzio vya maji, mabonde mbalimbali na uvunaji wa mvua. Kero mbalimbali za upungufu wa maji zilizopo hivi sasa zitaweza kupunguzwa kwa kiasi kikubwa kutokana hatua zifuatazo:-

Kwanza, mamlaka ya mabonde ya maji kuwa na utaratibu mzuri wa ugawaji maji kwa ajili ya umwagiliaji na uendeshaji wa vinu vya umeme na pili, usanii wa vinu vya umeme ufanyike katika hali ambayo maji yataweza kurudishwa tena kwenye vinu *(recycle)*.

Tatu, kuvuna maji ya mvua kwa kiwango kikubwa zaidi kwa kutumia mabwawa na taratibu nyingine na nne, jitihada maalum kwa viwanda kama kile kiwanda cha bia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kugusia kwamba pamoja na milima mingi na mito mingi iliyopo Mkinga, Wilaya hiyo ya pembezoni bado inakabiliwa na kero kubwa sana ya maji. Nashauri Wizara itazame uwezekano wa kuondoa kero ya maji kwa jumla Wilayani Mkinga na hasa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji kwa kuanzisha sehemu mbalimbali za umwagiliaji katika mabonde ya zaidi ya mito tisa iliyomo Wilaya humo na hivyo kuongeza nafasi ya maendeleo ya uchumi ya Wilaya hiyo na taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja na ahsante sana.

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mchango wangu kwa hoja iliyotolewa na Waziri wa Maji. Nampongeza Waziri wa Maji na Katibu wake pamoja na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri wanayoifanya. Pia nawapongeza kwa hotuba nzuri iliyotolewa leo hapa Bungeni. Ninaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka miwili iliyopita niliuliza swali hapa Bungeni juu ya ukosefu mkubwa wa maji uliopo katika Wilaya ya Kasulu hususan katika Jimbo la Kasulu Magharibi hasa vijiji vya Hem Juu, Mganza, Mwanga na Muhunga (Tarafa ya Hem Juu) pamoja na vijiji vya Munanile, Kibwigwa, Mkatanga, Nyakimwe, Mwayaya, Kitumbaka, Nyaruboze na Rusaba (Tarafa ya Manyovu). Vijiji vyote hivi viko milimani na hatuna vyanzo vizuri vya maji vya kuvuta maji ya bomba. Ninachoomba vijiji vyote hivi vichimbiwe visima virefu vya maji.

Mwisho naomba Wizara itembelee sehemu hizo ili kueleza upana wa tatizo, wanawake hutembea mwendo mrefu kutafuta maji. Tafadhari Waziri liwekee maanani ombili hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kufikisha ujumbe wangu huu. Naunga mkono hoja.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Naibu Spika, raslimali maji ni muhimu kwa maendeleo na maisha ya binadamu na viumbe vingine kwa ujumla. Kwa msingi huo ipo haja nyenzo hii itunzwe ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo maji ya mvua yanapotea na mara tu mvua zinapokatika tunaanza kulalamika kuwa hatuna maji. Maji karibu yote yanatiririka baharini kwenye mito na maziwa. Ipo haja maji ya mvua sasa uundwe mpango na miundombinu inayostahili ili maji hayo yahifadhiwe kwa matumizi ya baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi kuzungumza upatikanaji wa maji bila ya kulinda mazingira. Kwa msingi huo ipo haja ya kuwa na mikakati ya pamoja katika kuendeleza shughuli zinazohusiana na Wizara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa katika maeneo ya miji hasa Dar es Salaam katika kukabili upungufu wa maji watu binafsi wameanzisha uchimbaji wa visima. Ninachoomba kwa afya wananchi maji hayo yafanyiwe uchunguzi kila baada ya muda maalumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila utalaam wa maji lengo la kuwapatia wananchi maji linaweza kuwa na ndoto kwa hivyo ipo haja ya kuimarisha vyuo vyetu vinavyohusiana na taaluma ya maji kuweko na vituo vya kupima ubora wa maji yetu. Matatizo yanayowakabili wasomi wa fani ya maji yaendelee. Ahsante.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana Wizara ya Maji kwa kazi nzito ya kuhakikisha tunafanikisha upatikanaji wa maji nchini. Ushauri wangu ni kuwa kasi ya utekelezaji wa mradi wa maji na usafi wa mazingira vijijini unaofadhiliwa na benki ya dunia. Tayari wananchi wanasubiri kwa muda mrefu. Nashauri Wizara isimamie kusukuma ili kasi iongezewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitengo cha uchimbaji wa visima na mabwawa ina mitambo ya kizamani sana. Nashauri Wizara ikiimarishe kwa kukipatia nyenzo mpya za kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba katika bajeti ya mwaka 2006/2007 kupatiwa visima kwa ajili ya vijiji vya Undomo, Nyagi, Idala na Ikonokelo ambako bomba la maji toka bwawa la Kilimi kwenda mijini Nzega limepita.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Maji, Mheshimiwa Stephen Wasira, Naibu Waziri, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Katibu Mkuu na watendaji wote walioshiriki katika kuandaa bajeti hii ambayo imetoa matumaini kwa Watanzania wengi ambayo imeonyesha kupunguza ardhi ya maji kwa kiasi kikubwa kwa maeneo mengi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitampongeza kipekee Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake kwa jinsi walivyoenda sambamba na kauli mbiu ya Mheshimiwa ya Rais ya ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya kwa kufanya ziara karibu nchi nzima na kuona matatizo ya maji na kujitahidi kuyatatua kadiri walivyoweza nawapongeza sana na Mungu awatangulie kutekeleza bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali kwa kutambua kwamba mabomba mengi ya maji yamechakaa na mengi na kuziba na kufanya wateja wengi kukosa maji, kwani imejitahidi kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa mabomba hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa njia nyingi za maji zimeziba na kuwafanya wateja wasipate maji naishauri Serikali ifuatilie kwa karibu ankara zinazotozwa kwa wateja kwani kuna wateja wanaotozwa bila kupata huduma ya maji hususan Mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kwani mara nyingi inakuwa na utaratibu wa kusimamia rasilimali za maji, mfano bodi za maji mikoani. Kwa kuwa nimefanya utafiti kwa bodi nyingi nchini, kati ya wajumbe kumi wa bodi wanawake ni mmoja ama wawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iongeze idadi ya wajumbe wanawake kwenye Bodi za Maji ili kuleta uwiano sawa katika vyombo vya maamuzi na kwenda sambamba na azma ya Mheshimiwa Rais ya kuongeza idadi ya wanawake katika vyombo vya maamuzi na nafasi za uongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kutafuta fedha za kuendeshea miradi ya maji ndani ya nje ya nchi. Naishauri Serikali kutekeleza miradi yake haraka iwezekanavyo na kupunguza muda wa utafiti mfano, miradi wa maji vijijini uliofadhiliwa na Benki ya Dunia, wananchi walichangia mapema kuonyesha nia lakini fedha za wahisani zimechelewa na ama kutokuletwa zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nimeona ni vema niishauri Serikali ifuatilie kwa karibu mgao wa maji unaotolewa kwa kila siku kwani hautendi haki na badala yake kuna baadhi ya maeneo hayapatikani maji yanapokuwa katika mgao. Mfano mzuri Naibu Waziri aliona mwenyewe katika Mji wa Manyoni alipotembelea wiki mbili zilizopita. Baada ya maelekezo yake sasa mgao unaridhisha kiasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri na Naibu wake wakati wa majumuisho, hoja zangu zijibiwe kwani nimetumwa na wapiga kura wangu na wanasubiri majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huu nimalizie kwa kuunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakupongeza wewe, Naibu wako na Wenyeviti wako wawili kwa kazi kubwa na nzuri ya kuliongoza Bunge hili. Nawashukuru wananchi wa Chambani kwa kunichagua kuja hapa Bungeni, naahidi nitafanyakazi nao kwa karibu sana. Nampongeza Waziri wa Maji kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni kitu muhimu kabisa katika maisha ya binadamu na ni moja katika vitu vyenye thamani kubwa. Lakini umuhimu wa maji anayeujua zaidi ni yule ambaye hana maji. Ni kwa umuhimu huu ndio maana Mwenyezi Mungu kayaweka maji angani (mawingu), ardhini na pia kufanya bahari. Tanzania ni nchi kubwa yenye kilometa za mraba 93,000,000 lakini ina maji mengi kama nchi kwani kiasi cha kilometa za mraba 5.5 milioni hukaliwa na maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo letu kubwa ni *distribution* ya maji tuliyonayo. Kuna Mikoa yenye maji mengi kama Morogoro, Tanga, Kigoma na kadhalika. Lakini kuna Mikoa haina maji kabisa kama Shinyanga, Manyara na kadhalika na kwa mfano huo maji huathiri maendeleo ya kiuchumi ya Mkoa husika kazi kubwa ya Wizara hii ni kufikisha maji katika maeneo ambayo hakunha maji. Najua hii ni kazi kubwa inayohitaji mitaji na nyenzo, lakini tunaweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maji mjini, Mkoa wa Dar es Salaam umekumbwa na matatizo makubwa ya maji, ushahidi ni pale tulipokuwa tukiona misururu mirefu ya maji ikisubiri maji saa 24. Pale wauza maji walipoanza kuwauzia wananchi maji yasiyopimwa tena kwa bei kubwa na pengine si safi wala si salama. Serikali ikaleta kampuni ya *City Water* lakini mambo yakawa mabaya zaidi. Sasa tuna *DAWASCO*. Mambo ni afadhali kidogo lakini bado matatizo yapo wananchi wamechimba visima vingi kukidhi haja lakini Serikali haijapima visima hivi kujua kuwa maji yanafikia viwango au la. Kituo cha maji Ruvu hakina uwezo wa kutosheleza Jiji la Dar es Salaam na vitongoji vyake kwa sababu mitambo yake imechakaa na mabomba pia ni mabovu. Kuna upotevu mkubwa wa maji njiani usiokubalika lakini hata hayo maji machache yanayofika Dar es Salaam yanakuwa siyo salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudi za Wizara na sasa za kuchimba bwawa la Kidunda kwa ajili ya kupeleka maji Dar es Salaam ni wa kutia moyo. Lakini hili likifanikiwa lazima usimamizi wa maji uwe wa kisasa na uwe *computarized* ili kuondoa matatizo yaliyopo sasa katika kusoma *meter* za wateja na kutengeneza ankara zao. Mamlaka ya Maji Tanga ni mfano mzuri wa jinsi utaalam wa kompyuta unavyoweza kuboresha huduma za maji, Jiji la Dar es Salaam linahitaji kuchota uzoefu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matatizo ya maji vijijini bado ni makubwa na sehemu nyingine ni ya kutisha. Vijiji vingi bado wanakunywa maji ya kuokota na hayo wanatembea kilometa nyingi kuyapata. Mbali ya hilo kuna hatari ya kupata magonjwa *(Waterborn diseases)* kama *cholera, dysentry*, magonjwa kama *bilharzia* au magonjwa ya ngozi haya yote yanamwandamana mwanakijiji ambaye hana kinga wala tiba hivyo uwezekano wa kupoteza maisha kwa maradhi ya mlipuko. Serikali kwa hivyo lazima ifanye kazi ya ziadi ili ifikapo mwaka 2010 zaidi ya 65% ya wanavijiji wanapata maji si zaidi ya dakika 30 ya wanamoishi kama ilviyo malengo ya MKUKUTA.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miradi ya maji vijijini ambayo inaanzishwa kwa pamoja kwa nguvu za wananchi na Serikali lakini baada ya kukamilika Halmashauri za vijiji ndiyo wasimamizi wakuu. Mfumo wa kuchangia huduma ya maji si mbaya lakini utaratibu wa kukusanya mapato si mzuri, katika baadhi ya vijiji hakuna utaratibu wa kuweka kumbukumbu kwa hivyo mapato mengi huenda kwa wajanja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vyanzo vya maji, matatizo ya maji yamesababisha na uharibifu wa vyanzo vya maji kwa watu kuachiwa kulima, kufuga au kukata miti katika maeneo hayo. Ni muhimu wananchi waishio karibu na maeneo hayo kushirikishwa katika kutunza vianzio hivyo. Lakini pia ni muhimu wanavijiji hao wawe wa mwanzo kufaidi maji hayo kabla ya kunufaisha wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa maji ni hazina kubwa kwa nini basi maji yasiyotumika kwa kunywa kutoka vianzio hivyo yasitumike kwa kilimo cha umwagiliaji badala ya kuachiwa yapotee bure?

Mheshimiwa Naibu Spika, bado naamini viko vianzio vingi vya maji nchini ambavyo Wizara haijavifichua. Ninao mfano mzuri wa mto Yovi, Kata ya Kisanga Wilaya ya Kilosa. Kuna maporomoko makubwa ya maji *(waterfalls)* katika kijiji cha Msowero ambayo yanapitiwa na mto huo havifaidiki na maji hayo. Kuna uwezekano mkubwa wa hata kuzalisha umeme kutoka maporomoko hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri wa Maji na watendaji wake watembelee kujionea wenyewe ili tuweze kutumia kila chembe ya raslimali tuliyoanyo kwa maendeleo ya nchi yetu na watu wake. Ahsante.

**MHE. GAUDENTIA M. KABAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimpongeze sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa ushindi wa kishindo kwenye uchaguzi Mkuu wa Desemba 14, 2005. Aidha, nimpongeze Waziri Mkuu kwa uteuzi na hatimaye kukubalika na Bunge hili kwa kishindo. Niwapongeze Mawaziri na Naibu Mawaziri wenzangu. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuniona na kuniteua katika wadhifa nilionao. Namshukuru sana na naahidi kutumia uwezo wangu wote alionipatia Mwenyezi Mungu katika kufanya kazi nilizopewa.

Mheshimiwa Naibu spika, nawashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Mara kwa kunichagua kwa kishindo kuwawakilisha hapa Bungeni, nawaahidi nitawatumikia kwa uaminifu mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Stephen Wasira, kwanza kwa uteuzi wake katika wadhifa wake lakini pia kwa kuonyesha nia thabiti ya kutaka kuwasaidia wananchi wa Tanzania ili wajikwamue katika adha kubwa ya ukosefu wa maji mijini hadi vijijini. Nampongeza sana Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, ameonyesha uwezo mkubwa katika kufuatilia kero za wananchi kuhusuana na adha ya maji. Hongereni sana, *it is a good team you are making.*

Katika kijitabu cha hotuba yako Waziri nimeona kuwa kuna mabwawa 20 yatachimbwa vijijini kwa mwaka 2006/2007. Aidha, kuna visima virefu vitachimbwa huko huko vijijini. *Concern* yangu nilikwishakuletea hapo awali kuhusu taabu kubwa waliyonayo wananchi wa Kata ya Buswahili mathalani kijiji cha Wegaro na Buswahili yenyewe.

Sasa sielewi kama kati ya mabwawa hayo, Wegero na Buswahili pia wamo? Kwa kweli hawa wananchi wamekunywa maji ya tope wanayoyapata mabondeni mbali kwa muda mrefu sana. Nilieleza katika maombi yangu hayo kuwa si binadamu tu bali hata wanyama huteseka wakati wa kiangazi wanaume huhama na mifugo yao kwenda karibu

na mto Mara na kuishi huko hadi mvua inyeshe hivyo kuathiri shughuli zote za kiuchumi, na pia hii siyo nzuri wa familia hizi anapoondoka baba na kuacha mama na watoto alimradi mifugo ipate maji.

Mheshimiwa Naibu Spika chonde chonde, lambo au bwawa moja hapo Wegero na utakumbukwa daima. Iwapo kuna uwezekano wa kisima kirefu pia itakuwa vema sana kwani bwawa moja halitafua dafu idadi ya mifugo ilipo Wegero na Buswahili.

Mheshimiwia Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono sana hoja hii ya ukombozi.

**MHE. DR. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote nawapongeza sana kwa bajeti nzuri. Wiliya ya Hanang ina matatizo makubwa ya maji katika Mkoa wetu wa Manyara. Nawashukuru kwa fedha mlizotuwekea katika bajeti. Ukiangalia idadi ya watu Hanang ni wengi hata eneo lake ni kubwa zaidi ya kuwa na matatizo makubwa. Sijui ni vigezo gani vilivyotumika kufikia ugawaji wa fedha katika kila Wilaya nchini na katika Mkoa wetu wa Manyara.

Kwa kuwa Wilaya ya Hanang ipo katika Bonde la Ufa hivyo upatikanaji wa maji ni wa matatizo, fedha nyingi zinahitajika katika kujenga mabwawa na kuchimba visima virefu.

Naomba wataalam na viongozi wa kisiasa washirikiane ili vyanzo vya maji vijulikane na miradi ya maji iweze kupewa fedha. Vile vile ningeomba mtembelee Wilaya ili muwe na *first hand information.* Nawapongeza tena na ninaunga hoja mkono.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa maoni yafuatayo:-

Kwanza Wizara iangalie uwezekano wa kufanya upembuzi yakinifu kutoa maji Ziwa Victoria kuja mji wa Dodoma, ili Mikoa ya Shinyanga, Tabora na Singida watumie maji ya Ziwa Victoria. Uandikwe mradi mpya na mkubwa kwa ajili hii.

Miradi ya *World Bank* inayoendelea sana iharakishwe ili tuweze kuwahimiza wananchi kuchangia kwa wingi. Vijiji vihimizwe kufanya miradi ya pamoja mikubwa zaidi badala ya kisima kimoja kila kijiji. Naunga mkono hoja.

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni tatizo kubwa ndani ya Tanzania yetu kwani ukosefu wa maji kwa maisha ya Watanzania, kwa wanadamu, wanyama hata miti na mimea ni ukosefu wa kuishi au uhaba wa maisha. Kwa hiyo, maji ni uhai, bila maji kilimo hakuna, bila maji viwanda havizalishi. Naomba Wizara ya Maji chini kusimamiwa na Serikali sasa litatuliwe hasa kuzingatia ahadi ya Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, aliliona wakati wa kampeni zake za nyuma kuahidi wananchi tatizo la maji, hilo litashughulikiwa haraka iwezekanavyo. Kwa hiyo, maji naomba haraka iwezekanavyo litatuliwe Tanzania nzima hadi katika Mikoa, Wilaya, vijiji, mitaa hadi kaya zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maji ndiyo mhusika wa mambo ya maji na kunafahamu Wizara wako macho kwa shughuli za Wizara kutembelea na kufuatilia ambapo Tanzania nzima tunahitaji maji na yasambazwe au yafike na tuyapate. Wizara ya Maji isimamie vyema wahisani au nchi ambazo zinatupa misaada kwa uchimbaji wa visima, kutoa maji kwenye chemichemi. Naomba tusiwe wezi wa fadhila tukaharibu, tukabaki na taabu Wizara iwe macho kupitia Serikali ya awamu ya nne. Wasihangaishwe akinamama wetu kutoa maji masafa marefu (mbali).

Naomba Mheshimiwa Waziri wa Maji awe mfano na kuridhia au kurithi mazuri kutoka kwa aliyekuwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Edward Lowassa, ambaye ni Waziri Mkuu na Mbunge wa Jimbo la Monduli.

**MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wataalam kwa kuandaa hotuba nzuri. Pamoja na pongezi hizo naomba kushauri ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mfano mzuri wa matumizi ya maji kutoka Ziwa Victoria, umefika wakati sasa Wizara itenge fedha za kutosha kufanya uchunguzi au utafiti wa namna maji ya Ziwa Nyasa yanavyoweza kutumika kwa usalama wa kunywa na umwagiliaji hasa kwa wananchi waishio kando kando mwa Ziwa Nyasa katika Mikoa ya Mbeya, Iringa na Rukwa. Usimamizi wa huduma za maji katika Halmashauri za Wilaya.

Ningependa kufahamu ni vigezo gani vimetumika katika kugawa fedha kwa uendeshaji wa shughuli za maji. Mkoa wa Mbeya pamoja na ukubwa wake umetengewa shilingi 349,000,000, ni kidogo sana. Kwa mfano, unapotoa shilingi milioni kumi kwa Mbeya Mjini au shilingi milioni 33 kwa Wilaya Rungwe (Wilaya yenye Majimbo mawili) hazitasaidia kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kutokana na uhaba wa fedha, Wizara itenge fedha kwa Wilaya chache kila mwaka ili kazi ionekane la sivyo fedha hiyo haina maana.

Kuhusu Bodi za Wakurugenzi Maji Mijini na maeneo mengine, kwa kuwa suala la maji na matatizo yake linagusa sana wanawake, nashauri Wizara ielekeze wahusika hasa Makatibu Tawala wa Mikoa kuzingatia uwakilishi kijinsia. Itapendeza iwapo idadi ya wanaume na wanawake inakuwa sawa na si vizuri wajumbe wanaume peke yake wachukue nafasi kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hoja hizo chache za ushauri, naunga mkono hoja hii asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. TATU M. NTIMIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza hotuba na kuunga mkono. Naomba majibu kwa yafuatayo:-

(i) Katika Jimbo la Igalula vijiji tayari wamekwishachanga fedha shilingi milioni mbili kila kijiji kwa ajili ya kuanzishwa mradi wa kuchimbiwa visima, utafiti tayari wananchi wanaulizana lini kazi hii itaanza?

Vijiji vingine pia karibu vimalize michango, sasa sijui lini vitaanza kufanyiwa utafiti ikiwa vile vilivyomaliza tu, kazi haijaanza. Pamoja na kutengewa Mkoa wa Tabora shilingi milioni 500, si ajabu yakajitokeza ya Majimbo ya Waziri yakapewa fedha na majimbo ya sisi Wabunge tutawekwa benchi wakati sisi sote tunawakilisha wapigakura wale wale waliotuletea ushindi wa uchaguzi. Ubaguzi wa huduma katika Majimbo mtatuletea taabu katika Ubunge wetu na kutugawa kimajimbo licha ya kimkoa.

(ii) Mradi wa kukarabati kisima na mashine ya siku nyingi iliyowekwa wakati wa Mwalimu Julius Nyerere katika kijiji cha mfano cha wakulima na tumbaku linaitwa Ipululu kata ya Igelula. Mashine hii tangu mwaka 2005 hadi leo bado hakijapatiwa ufumbuzi. Wananchi wanahangaika, tatizo ni kukichimbua na kubadili mashine. Nitashukuru suala hili likitatuliwa mwaka huu la sivyo itaniwia vigumu hata kwenda kushukuru kwa wapigakura. Naomba nipatiwe majibu.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba nzuri aliyoitoa wakati akifungua Bunge tarehe 30 Desemba, 2005 kwamba tatizo la maji ndicho kilio kikubwa cha Watanzania (maji ndiyo namba moja). Serikali ya Awamu ya Nne itakabiliana na tatizo hilo.

Aidha, nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi sana isipokuwa kwa kura moja kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze pia Mawaziri pamoja na wataalam wake na ile kamati iliyoshirikiana nao katika kuandaa Bajeti hii. Bajeti hii imewapa wananchi wetu matumaini makubwa sana. Hii imeonyesha jinsi Serikali yetu ya Awamu ya Nne inavyotekeleza mikakati ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Anthony Diallo, kwa kuweza kusimamia sekta hii ya maji katika Wizara hiyo. Huu ni ushahidi kwamba aliweza kufany kazi nzuri katika sekta hii muhimu sana kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Tunaamini kabisa kwamba aliteuliwa kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii kutokana na uchapaji kazi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze pia Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kwa umahiri wake na uchapaji kazi wake. Namwombea kwa Mungu azidi kumpa afya njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi zangu zote naomba sasa nichangie suala la maji katika Wizara hii. Ni wazi kwamba Serikali imejitahidi sana kuhakikisha kuwa Watanzania wengi watapata unafuu mkubwa kutokana na jitihada zilizopo katika

Mikoa, Wilaya, Kata na Vitongoji, kwa ujumla visima vimechimbwa na watu sasa wana matumaini makubwa sana ya kupata maji.

Mheshimwa Naibu Spika, mji wa Mererani, Mkoa wa Manyara ni mji uliosahaulika kwa kila kitu, maji, hospitali na barabara, la kushangaza hakuna mtu asiyeyafahamu ya Mererani. Viongozi wote Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Wabunge wote wanaifahamu Mererani vizuri sana. Wachimbaji wote walioko pale wametoka katika Mikoa yote ya Tanzania na si ajabu hata viongozi wengi wana ndugu zao, watoto wao na kadhalika, inakuaje mnathubutu kuwaachia watoto wenu wanakwenda kufanya kazi katika mazingira ya hatari namna hii? Hakuna maji, barabara na hospitali. Kweli ni aibu kubwa kwa mji maarufu kiasi hicho na unaojulikana dunia nzima kwa madini maarufu ya *Tanzanite.* Watu wanakufa kwa kipindupindu, wangine wanasema ni UKIMWI, si kweli, UKIMWI upo na kipindupindu kinamaliza watoto na watu wazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mererani ipo ndani ya Tanzania na si nje ya Tanzania madini yanayozalishwa pale ndiyo yaliyojenga mji wa Arusha na sehemu zingine. Kwa nini Serikali isitupie macho Mererani? Hiki kisiwa cha madini ya *Tanzanite* kinachoiletea Serikali mapato makubwa, kwa nini Wizara ya Maji isitembelee kule na kuona wananchi wanavyoteseka?

Mheshimiwa Naibu Spika, mbona mnawaleta wawekezaji hamuwaangalii wazawa? Boresheni afya za wananchi kwa kuwaletea maji salama. Hamuoni kwamba hata wageni wawekezaji wanatudharau na kuona kwamba hawa wananchi wa Mererani wamesahaulika hata Serikali yao haiwajali? Onyesheni upendo kwa wananchi wenu, msitutupe jamani, Mheshimiwa Waziri Mkuu ututetee Mererani tunaisha, barabara, maji hospitali na kadhalika. Wafanyabiashara wamefanya Mererani kuwa kitega uchumi chao. Ndoo ya maji ni shilingi 300, wananchi wasio na uwezo wa kununua maji wanakunywa maji ya visima ambayo si salama na ndiyo yanayopelekea watu kupata magonjwa ya mlipuko na kufariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali ituangalie wana Mererani. Wananchi wako tayari kusaidiana na Wizara ya Maji ili kuangalia uwezekano wa kupata maji ya Losaa ambayo yamekwishafika *Kilimanjaro Airport* ambako ni karibu sana na wananchi wako tayari kuchangia fedha kwa ajili ya hiyo ili waweze kupata maji safi na salama. Makampuni makubwa ya uchimbaji kama *Tanzania One, Tanzania Africa* na kadhalika, wachimbaji wadogo wadogo na wananchi wa Mererani na Naisanyai wako tayari kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena kuiomba Wizara itembelee Mererani na kuongea na wananchi, tatizo hili la maji Mererani linafikia wapi? Nakushukuru sana na naunga mkono hoja.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naipongeza Wizara kwa jitihada kubwa wanayoifanya ya kutatua kero ya maji kwa wananchi kwani maji ni uhai na bila maji hakuna maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la maji ni la msingi sana na ndilo linaloleta maendeleo kwa nchi yoyote ile. Cha ajabu nchi yetu yenye vyanzo kibao vya maji kama maziwa, mito na mabwawa makubwa imeshindwa kabisa kuwapatia wananchi wake maji salama na ya kutosha. Hii imesababisha wananchi hususan wanawake kutembea umbali mrefu kutafuta maji huku wakihitajika kufanya shughuli nyingine za uchumi kama kilimo na kulea watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti uliofanywa unaonyesha baadhi ya wananchi wakitumia hadi saa 6 kwa siku kutafuta maji. Sasa katika saa 12 ya siku kama mtu atatumia nusu siku kwa maji tu tena ndoo moja atafanya shughuli za ujenzi wa Taifa muda upi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ukosefu wa maji nchini watu wengi wamekuwa wakipata magonjwa *(water born diseases)* kama kipindupindu, kichocho kuhara damu na mengine mengi ambayo kimsingi yasingetokea kama maji yangekuwepo salama na ya uhakika. Ni jambo la kushangaza kuona kwamba Jiji la Dar es Salaam ambalo ndilo jicho/Ikulu ya nchi, wananchi wanabeba ndoo za maji kichwani. Hii ni aibu kwa nchi yenye vyanzo vya maji, ni kwa nini Serikali inaacha maji haya yanamwagika baharini badala ya kuyahifadhi katika mabwawa makubwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la kushangaza kuona wananchi wa maeneo yanayozunguka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kama Changanyikeni, Msewe na Makongo wakiwa na tatizo sugu la maji wakati Chuo Kikuu kilichokuwa na tatizo la maji sasa hivi ni historia. Pamoja na Chuo Kikuu kuwa kwenye mlima, Wasweden waliweza kuwaletea maji. Je, Serikali au Wizara inashindwa nini kusambaza maji katika maeneo hayo? Tatizo ni nini na ni lini Serikali itawapatia maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo la ankara za maji. Unakuta mtumiaji hana maji kwa kipindi kirefu lakini analetewa ankara. Je, mamlaka husika inafanyaje, inautaratibu gani? Tunaomba Wizara iliangalie kwa makini suala hili ili haki itendeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uchimbaji visima ni la msingi sana lakini cha ajabu bei yake ni kubwa mno. Wananchi wengi hasa wale wanaotoka sehemu ambazo *water table* iko juu wangependa sana kuchimbiwa visima lakini inasikitisha kuona bei ya kutambua tu kama kuna maji ni shilingi 150,000 na hii ni *non-refundable whether* maji yanapatikana au la.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninakotoka Moshi Vijijini, kulikwa na maji ya mabomba lakini tangu miaka ya 1990 mwanzoni maji yale yamekuwa historia. Katika vijiji vya Mbokomu na Kata ya Konni Kusini kuna tatizo kubwa sana hasa ukizingatia maeneo hayo yana wezee wengi hivyo kufanya tatizo liwe kubwa zaidi. Naiomba Waziri isaidie, nashukuru nimeona tayari upembuzi yakinifu umefanyika lakini baada ya upembuzi kunafuata nini? Tunaomba utekelezaji ufanyike haraka kwani mabomba yapo, upembuzi ni wa nini tena?

Mheshimiwa Naibu Spika, uwiano wa bajeti hii unasikitisha, nimeona kuna Wilaya bajeti yake inazidi ya Mikoa. Je, ni vigezo gani vimetumika?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niongelee suala la uangalizi wa vyanzo vya maji pamoja na kwamba Wizara ya Mazingira ndio mhusika mkuu lakini Wizara ya Maji ndiyo mdau namba moja. Hivyo ni jukumu la Waziri ya Maji kusimamia vyanzo vya maji ili wateja wake waondokane na kero ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi biashara ya maji imeshauri sana si tu katika miji na majiji bali hata vijijini. Ndoo ya maji inafikia shilingi 500 na lori moja shilingi 45,000. Hivi kwa mazingira ya pato la Mtanzania familia moja inayotumia lita 200 (ndoo 10) kwa siku ni shilingi 5,000 kwa siku, je, kwa mwezi ni shilingi ngapi? Mtanzania wa kawaida atamudu? Hii imefika watoto kushindwa hata kufua nguo zao, kuoga ndio hakuna au wanaishia kuogea kwenye mabwana, tumeshuhudia watoto wakioga kwenye madimbwi machafu na wanachangia na mifugo, ni vipi wasipate *water born diseases?*

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha maji cha Rwegarulila, kilikuwa kinatoa wataalam wa maji. Cha ajabu chuo hiki kilifungwa kwa muda mrefu. Je, nini kilichosababisha hali hiyo na ni sababu zipi zimepelekea kufunguliwa tena? Na Waziri imepata hasara kiasi gani jwa kufungwa kwa chuo hicho?

Mwisho na washauri Wizara itekeleze kwa kina hayo yote waliyoyaandika ili kutatua kero za wananchi wetu hasa ikizingatiwa maji ni uhai.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii ya awali nimpongeze Mheshimiwa Rais, kwanza kwa kukubali kuitenganisha Wizara ya Mifugo. Pia, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kumteua Mheshimiwa Stephen M. Wasira, kuwa Waziri wake wa Maji, Mheshimiwa Shamsa S. Mwangunga kuwa Naibu Waziri na Ndugu Patrick Rutabanzibwa kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa sababu Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wako *serious* katika kazi zao. Pili kwa kuwa sasa dira ya maendeleo ya maji imeanza kuonekana na tatu, kwa sababu hotuba imejaa mipango mizuri na nia ya kutaka kutekeleza kwa dhati.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri na watendaji wake kwa kunisaidia kujibu hoja zangu ambazo zilikuwa zinanikera ikiwa ni pamoja na kusuasua kwa kukamilisha *master plan* ya kukarabati miundombinu ya Mji wa Sumbawanga. Uchimbaji visima unakwenda vizuri hapo Mjini Sumbawanga na ununuzi wa mabomba nao unaendelea. Nashukuru sana kwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maombi yafuatayo kwenye Wizara hii:-

Moja, ahadi ya Wizara kukamilisha miundombinu ya maji mjini, pili ahadi ya kuongeza uchimbaji visima na kujenga *reserve tanks* nyingine ili kukidhi mahitaji

yanayoongezeka katika Manispaa, tatu, kukamilisha uanzishwaji wa Mfuko wa Maji Kitaifa na nne, kuendeklea kusimamia mpango wa *UN-HABITAT* kwa kulitaka Shirika hili la Kimataifa litekeleze azma ya kujenga Mfumo wa Maji kwa miji kumi iliyopangwa inayozunguka Ziwa Victoria. Waziri awatake watupatie maelezo kwa nini hawataki hata kuonyesha wamefikia wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalisema hilo kwa sababu kama tungefanikiwa na mradi huo, basi gharama kubwa zinazochukua asilimia 80 ya fedha zote za maji kutumika kutandika mabomba toka Mwanza, Shinyanga na baadaye Kahama. Bado tuna nafasi kubwa ya kuendelea kulishauri vizuri Shirika hilo litekeleze mipango yake. Tutumie nafasi ya *under Secretary General* wa *UN*, Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka, ambaye ni Mtanzania mwenzetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakutakieni kheri na fanaka na maendeleo mazuri kwa kazi nzuri ambayo mmeanza nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ningependa Wizara itupatie kwa kifupi ni nini hatma ya maji kupungua kwenye Mito, Maziwa na hata kwenye visima? Nini maisha ya binadamu bila maji? Naunga mkono hoja hii.

**MHE. JUMA J. AKUKWETI:** Mheshimiwa Naibu Spika,Wilaya ya Tunduru ni moja ya Wilaya zenye matatizo makubwa ya maji. Kuna vijiji ambavyo vina tatizo hili la maji kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikuarifu kwamba Wilaya ya Tunduru ilipata ahadi ya msaada kutoka Ujerumani kupitia taasisi moja ya dini ambayo iliahidi kutoa msaada mkubwa kama Serikali itachangia kiasi hicho hicho ambacho wao watatoa 50% kwa 50%. Taasisi hii ipo tayari kuchangia kiasi cha shilingi 200,000,000/= au zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara itenge pesa kwa ajili ya kuchangia mpango huu. Mimi nipo tayari kushirikiana na Wizara kuhusu mpango huu. Ahadi hii ilitolewa na wahusika wenyewe mbele ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati huo akiwa Waziri wa Maji alipokuja Tunduru.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote na mimi niungane na Wabunge wenzangu kumpongeza Waziri wa Maji, Mheshimiwa Stephen M. Wasira, Naibu Waziri Mheshimiwa Shamsa S. Mwangunga, Katibu Mkuu wa Wizara na watendaji wote wa Wizara walioshiriki katika kuandaa bajeti hii ya mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mambo yaliyo muhimu kwa matumizi ya binadamu, basi mojawapo ni maji, maji kwa matumizi ya binadamu ama maji kwa matumizi mbalimbali, ndio maana imekuwepo misemo kama vile maji ni uhai.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo yote ya kumgusa binadamu, maji yanachukua nafasi kubwa sana na ndio maana hata Mungu Muweza katika kuumba viumbe vyake aliviumba sambamba na upatikanaji wa maji katika maeneo mbalimbali vikiwemo vyanzo vya asili vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ni miongoni mwa nchi iliyo katika wimbi la kujikomboa na umaskini wa mambo kadha wa kadha ukiwemo huu umaskini wa mahitaji mbalimbali hasa wa ukosefu wa maji na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya ukosefu wa maji ni kero kubwa sana kwa wananchi wa Jimbo la Uchaguzi la Iramba Magharibi, hali hii imechangia kuzorotesha kwa shughuli zingine za kimaendeleo. Kwa kuwa wananchi hutumia muda mwingi katika maji, hasa kwa kuyafuata na upatikanaji wake ni wa matatizo makubwa sana. Pamoja na hayo baado usalama wa maji yenyewe siyo wa kuridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Iramba hatma ya kulinda maisha yao hasa kwa kutegemea maji safi na salama haipo kabisa kwani bado wanaendelea hadi hivi sasa kuchangia visima hivyo na mifugo na hata wanyama wa porini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na uhaba huo kwa binadamu pia hata wanyama, ng'ombe, mbuzi na kadhalika nao wana wakati mgumu sana. Kubwa zaidi bado ni tatizo la binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini sasa pamoja na mambo mengine Wizara kwa nini katika bajeti yake imeshindwa kutenga fedha kwa ajili ya kuendeleza vyanzo vya maji ambavyo kwa kiwango kikubwa viliweza kuzalisha maji muda wote hata nyakati za kiangazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya maji ya Benki ya Dunia *(WB),* iharakishe kufufuka kwa vijiji vyote ili wale wananchi ambao wapo tayari kuchangia wafanye hivyo kwa dhamira ya kupunguza tatizo la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mungu ampe imani na uadilifu mkubwa katika kuwatumikia Watanzania. Pia nimpongeze Mheshimiwa Spika na Naibu Spika, kwa kuchaguliwa kuliongoza Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji limekuwa ni tatizo sugu nchini mwetu, jambo ambalo ni la ajabu sana kwa sababu Tanzania Mungu ameibariki kuzungukwa na Maziwa kila pembe na Mito. Iweje leo Mtanzania alalamikie maji! Bila shaka ni kutokuwa na mipango mizuri kwa Serikali za awamu zilizopita. Hebu sasa Serikali ya Awamu ya Nne ijipange upya ili kukabiliana na tatizo hili la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tuelewe kwamba bila maji hatuwezi kuishi kwa sababu hatuwezi kufanya lolote la maendeleo. Maji ni tegemeo la kila kiumbe kilicho hai. Huwezi kuleta maendeleo bila maji na pia huwezi kumpunguzia umaskini Mtanzania ambaye anapoteza saa nyingi kwa ajili ya kutafuta maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanamke wa kijijini anategemea ajikomboe kutoka katika hali ya umaskini, lakini muda wake anaupoteza katika kutafuta maji, je, atafanya shughuli nyingine za kuondokana na umaskini wakati gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mtanzania anakunywa maji ambayo siyo salama ambayo hatma yake ni kupata maradhi ambayo ama yatamsababishia kifo ama kushindwa kufanya kazi ili kujiletea maendeleo. Kwa maana hiyo, bila maji hakuna uhai kwa sababu hakuna maendeleo na hakuna afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunataka kuendelea, basi kwanza tuweke mkakati katika sekta hii ya maji na tuachane na kuimba vitabuni tu. Ni lazima Serikali ilipe uzito suala hili. Tuyafumbie macho mambo mengine kwa muda mfupi ili fedha nyingi zielekezwe kwenye sekta hii ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wanaongezeka na mahitaji yao ya maji pia yanaongezeka. Lazima tutoe kipaumbele kwa sekta ya maji. Tukisubiri kesho, tutakuja tena hapa baada ya miaka mitano na takwimu itatuonyesha kamba tatizo limeongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kusaidia basi Serikali ingeweka umuhimu wa kuchimba visima virefu/vifupi ili visaidie katika kusubiri hayo maji ya bomba. Bila ya hivyo tutaendelea kuwa na umaskini, kwani kila kilichohai kinahitaji maji, huo ndio mzunguko wa maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa unyenyekevu kwamba wale wenzetu ambao wanakabiliwa na tatizo zaidi, basi waangaliwe kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na ahsante.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujua ile programu ya maji iliyokuwa itekelezwe kwa ushirikiano na Benki ya Dunia itaanza lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, jimboni kuna vijiji kama ifuatavyo vilichangishwa tangu mwaka 2005 mwanzoni:-

(i) Kijiji cha Chamndindi, Tarafa ya Ismani shilingi milioni tatu;

(ii) Kijiji cha Ikengeza, Tarafa ya Ismani shilingi milioni tatu;

(iii) Kijiji cha Mboliboli, Tarafa ya Pawaga shilingi milioni tatu;

(iv) Kijiji cha Malinzanga, Tarafa ya Idodi shilingi milioni tatu; na

(v) Kijiji cha Mahuninga, Tarafa ya Idodi shilingi milioni tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi hawa waliambiwa wachange 5% ya gharama za ujenzi na Serikali itakamilisha. Sasa, naomba kujua kwa uhakika, vijiji hivi miradi yake itatekelezwa lini? Naomba utekelezaji wa ratiba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la Ismani ni kame sana. Mwaka jana niliomba Bwawa Ismani, Wizara iliahidi na ilipeleka wataalam Ismani. Sasa Bwawa hilo litajengwa lini? Mheshimiwa Waziri ambaye sasa ni Waziri Mkuu na Katibu Mkuu waliagiza kazi hiyo ifanyike. Naomba sana sasa ifanyike. Lakini pia naomba mabwawa mengine katika maeneo yafuatayo ya Kata za Nduli, Kihorogota, Izazi, Malengamakali na Kata ya Mlowa maeneo hayo ni makame sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba majibu ya maombi yangu nipate kwa maandishi wakati wa kipindi hiki cha Bunge.

Mheshimwiwa Naibu Spika, nawapongezeni sana, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa kazi nzuri na bajeti nzuri. Ahsante.

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniruhusu kuchangia kimaandishi. Nianze kwa kumpongeza Waziri wa Maji, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii waliohusika na uandaaji wa bajeti hii ambayo imeandaliwa vizuri na inalenga kuleta maisha bora kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002 kama ilivyoainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ni kumwezesha Mtanzania, mkaaji wa mijini kwa asilimia 90 na vijijini kwa asilimia 60 kupata maji safi, salama na ya kutosha ifikapo mwaka 2010. Katika hotuba ya bajeti ya Wizara hii ukurasa wa 10 inaonyesha hadi sasa ukuaji wa upatikanaji wa maji kwa mwaka 2004/2005 ulikuwa kwa asilimia 0.2 vijijini na asilimia 1 mijini kwa ukuaji wenye kasi ndogo hivi, haiwezekani kufikia asilimia 90 na 65 mijini na vijijini kama ilivyolengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka ya nyuma, katika Mkoa wa Kagera, kulikuwa na vijiji vyenye maji, mifumo hiyo imechakaa hivyo kwa sasa hakuna maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza sambamba na ujenzi wa mifumo mipya ya maji ile mifumo iliyopo vijijini iliyoharibika ikarabatiwe. Ukarabati ukiwezekana na ukuaji wa utoaji wa huduma hii itawezekana kama Wizara hii nyeti itatengewa fedha nyingi na za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kagera una mvua nyingi, lakini wakati wa kiangazi baadhi ya mito hukauka na watu wengi hasa wanawake na watoto hulazimika

muda mwingi kwenda muda mrefu kwenda kutafuta maji. Wizara ya Maji itoe wataalam na vifaa vya kusaidia shule, hospitali na wanavijiji kuvuna maji ya mvua, ili wakati wa kiangazi wasihangaike vijana wetu wanaokaa vijiweni bila kufanya kazi, wanaweza kupewa utaalamu na mitaji ya kuanzia na kwa kutumia miradi hii wakajipatia ajira wakati huo huo wakiwezesha kuvuna maji ya mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukuru Wizara kwa kubuni mabonde tisa ya ya kuratibu na kusimamia utumiaji wa rasilimali maji. Kwa vile bonde moja linasimamia zaidi ya mkoa mmoja mfano ofisi ya bonde ya Ziwa Victoria inasimamia Mkoa wa Mara, Kagera, Mwanza na sehemu ya Shinyanga, basi inabidi *sub-offices* zilizo kwenye mikoa ziwezeshwe kwa kupewa wataalam husika na vitendea kazi kama magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa maji kila mtu anafahamu. Wahitaji na wawekezaji wengi wanalalamika kuwa utoaji wa vibali vya kutumia maji *(Water rights),* tangu wanapoomba inachukua hadi miezi saba au zaidi kabla hawajapata *water rights.* Tatizo hili linasababishwa na vikao vya Bodi ya Maji ya Bonde kukaa mara mbili tu kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza vikao vya Bodi viongezwe hadi vinne kwa mwaka ili watu waliiomba wapatiwe vibali kwa muda muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mito mingi imekauka, rasilimali maji imepungua sababu za watu kufanya shughuli za kibinadamu kando kando au karibu sana na miti au vyanzo vya maji ili kulinda vyanzo vya maji, Serikali ilisema kuwa maeneo haya yatapimwa, yatapewa hatimiliki. Lakini hadi sasa haijaeleweka hiyo hati miliki atapewa nani? Kijiji ambamo chanzo cha maji kipo, Halmashauri husika au atapewa yule aliyepewa water right ya kutumia maji hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, namuomba Waziri afafanue hili ili ijulikane muhusika ni nani, eneo liweze kutunzwa ipasavyo. Pili, sheria ya maji na sheria ya mazingira za utunzaji wa vyanzo vya maji zinakinzana. Sheria za maji zinakataza shughuli za kudumu za kibinadamu kufanyika ndani ya eneo la mita 200 kutoaka kwenye chanzo cha maji, wakati sheria ya mazingira hairuhusu shughuli hizo ndani ya mita 30 kuanzia kwenye chanzo. Je, hawa Halmashauri au Wilaya wanapotakiwa kuwaondoa wanaoharibu watumie sheria gani? Naomba sheria hizi ziainishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mji au jiji kuna Mamlaka ya Maji safi na maji taka. Lakini utakuta mifumo ya maji taka katika miji na hasa mji wa Bukoba hakuna watu binafsi, mahoteli, baa, magereza wakati wa usiku na wakati wa mvua wanatapisha vyoo. Uchafu wote unaelekezwa kwenye mifereji ya maji ya mvua. Uchafu huo unaenda moja kwa moja Ziwa Victoria. Vile vile wale wenye viwanda kama vya samaki wanatumia maji wanayarudisha Ziwani bila kuwa na viwango vya usafi unaokubalika. Viwanda vingi vina *oxidation ponds* ndogo na hawana wataalam wa kutosha wa kutunza mabwawa hayo. Hivyo, uchafu wote huo unaelekezwa kwenye Ziwa Victoria. Lakini, tutambue kuwa wapo watu wengi wanaotumia maji ya Ziwa Victoria kwa kupikia, kunywa, kufulia na kuogelea. Je, samaki tunaowavua kutoka humo wana usalama gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Sasa hivi samaki wamepungua sana, maji katika Ziwa yanepungua sana. Sababu mojawapo ni uchafu unaotupwa humo. Hivyo, Mheshimiwa Waziri ahakikishe kila mji una si mfumo wa maji safi tu bali na mfumo wa maji taka. Je, hii itatekelezwa lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. HASNAIN G. DEWJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niunge mkono hotuba ya Maji kwa asilimia mia moja. Hotuba hii ni nzuri, ina mpango mzuri sana kwa mwaka huu 2006/2007 kwa kuwa maji ni uhai na muhimu kwa kila mtu.

Mimi nikiwa Mbunge wa Kilwa Kusini nakerwa na hali ya uhaba wa maji huko Pande, Limario na vijiji vyake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina tatizo kubwa sana kwenye tarafa ya Pande. Tatizo kubwa wananchi wa Pande kwao maji ni kama ndoto. Naiomba Wizara ya Maji kuja Kilwa kushuhudia hali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mradi wa *Fin Water* ambao niliuliza swali langu Bungeni. Naomba Waziri sawa na ahadi yake hu mpango wa *Mpara Fin Water* uendelezwe. Maana mradi umebakia asilimia thelathini, mpango utafaidisha sana vijiji kama Mpara, Mtanga, Mkwanyule, Kisani na Kilwa Masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kilwa nimeona mwaka huu hakuna mpango wa utafiti, je, Wizara haina mpango wa utafiti katika Wilaya yetu? Naomba sana kuwe na utafiti ili visima vingine kwa kila kijiji vipatikane. Kuhusu fedha zilizotengwa kuendesha na kusimamia huduma za maji Kilwa imepewa shilingi 77,000,000/=, nashukuru kwa hilo. Lakini kwa kuwa Kilwa ni Wilaya kubwa ina majimbo mawili, hizi fedha ni kidogo hazikidhi mahitaji kwa Kilwa hii kubwa.

Mwisho nashukuru kwa nafasi hii na naunga mkono hotuba hii. Ahsante.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji pamoja na timu yake kwa maandalizi mazuri ya hotuba yake ambayo ameiwasilisha katika Bunge lako.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo linanishangaza ni namna gani suala la maji linavyoshughulikiwa na Serikali, wote kama tunavyofahamu maji ni uhai lakini wananchi wamekua wakipewa ahadi kila mara wakati wa uchaguzi wa kupata maji lakini mipango mingi imekua haitekelezeki na kuwaondolea shida ya maji wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, nchi nzima imeenea minara ya matanki ya maji hadi vijijini lakini hayatumiki na imekuwa viota vya ndege na popo. Mfumo wa mabomba unaoza, ardhini hakuna maji, fedha nyingi zilitumika katika miradi hiyo nchi

nzima, hivi Wizara inasema nini juu ya matumizi ya matanki hayo na Taifa linaridhia juu ya matumizi mabaya ya kodi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Serikali na Wizara ya Maji kuangalia namna ya k utumia kwa ufanisi miundombinu iliyopo kwa kutumia mashine ambazo zinaendeshwa kwa nguvu ya jua ili wananchi wapate maji kama ilivyokusudiwa katika miradi hiyo ambayo mingi imesimama kwa kushindwa kuendesha mashine zinazotumia dizeli.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la maji ni kubwa sana katika nchi hii mijini na vijijini pia hususan katika jiji la Dar es Salaam, Wizara pamoja na mikakati yake mizuri ya kuondoa au kupunguza kero hiyo Dar es Salaam lakini hofu yangu ni juu ya vyanzo vya maji Ruvu hata kule Wami kina cha maji hupungua wakati wa kiangazi naishauri Wizara kuangalia kama watapata maji mji wa Dar es Salaa kutoka Rufiji na maji ya Ruvu yanayotirika baharini yangehifadhiwa kwa kujenga mabwawa ya akiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpanda na Wilaya ya Mpanda kadhalika inayo matatizo makubwa ya maji. Mpanda Mjini wanao mfumo wa maji uliojengwa katika miaka ya 1950. Idadi ya watu imeongezeka na mji kupanuka na huduma za maji hazipo katika maeneo mengi katika Kata za Nsemlwa, Kawajense, Shanwe, Misunkumilo, Ilembo na Kashaulili katika maeneo machache.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tatizo la maji katika mji wa Mpanda liondoke, tunaiomba Wizara kuangalia namna ya kusaidia mradi wa maji Ikolongo ambao Mamlaka ya Maji Mpanda na Halmashauri hawawezi kuutekeleza kwa ukosefu wa fedha za kutosheleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vingi katika Wilaya ya Mpanda wana matatizo ya upatikanaji wa maji kama vile vijiji vya tarafa ya Inyonga hupata ukame na hawana visima vya kutosha pia Mpanda Mjini tuna upungufu wa visima virefu kwa ajili ya maji ya kunywa, maji ya bomba si salama. Wizara itatusaidia vipi ili kuweza kupunguza matatizo ya afya yanayosababishwa na maji.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, nakupongeza kwa hotuba nzuri pia nakupongeza wewe, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa kazi nzuri ambao mmeanza kuzitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nakumbushia ahadi iliyotolewa na Wizara yako mwaka 2004/2005 ambayo ulinipatia fedha za kununua mashine mbili za kupampu maji kwa ajili ya vijiji vya Kinyangiri na Tumuli, napongeza sana kwa hilo.

Mheshimiwa Waziri zilizofuatana na ahadi hizo ilikuwa mwaka unaofuata (2005/2006) ilikuwa ipewe fedha za kunua *windmill* moja kwa ajili ya kijiji cha Matongo na *pump* moja kwa ajili ya kijiji cha Marera. Gharama ya *wind mill* hadi kufunga ni shilingi 16,500,000/= na gharama ya *pump* ni shilingi 11,000,000/=. Mwaka jana sikupewa fedha hizo kwa ahadi kwamba zitatolewa mwaka huu. Hata hivyo nikiangalia

kwenye kitabu inaonyeshwa kwamba fedha hizi hazikutengwa au zimetengwa na kuweka kwenye fungu ambalo mimi sijalifahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sitaki malumbano na Wizara kwa sababu najua nitapata majibu mazuri bila kufika kwenye vifungu. Nakupongeza tena wewe Mheshimiwa Waziri na timu yako.

**MHE. ELIETTA N. SWITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa jitihada zake za kujaribu kupeleka maji kila panapowezekana nchini. Hata hivyo matatizo ya ukosefu wa maji hasa vijijini ni mkubwa mno. Aidha, upatikanaji wa maji safi na salama ni mbovu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu bajeti yetu ni finyu na kwa sababu hiyo Serikali imelazimika kukubali misaada kama ya *World Bank* katika kuwapatia wananchi wengi maji. Miradi kama hiyo huwahitaji wananchi kuchangia 5% ya mradi. Wananchi wengi kwa ajili ya uchumi duni mpaka leo wameshindwa kutimiza sharti hilo na hivyo kubaki bila maji mfano kijiji cha Mwimbi Sumbawanga Vijijini katika Jimbo la Kalambo ambako walitakiwa kuchangia zaidi ya shilingi milioni mbili. Mpaka mwezi Aprili, 2006 nilipokwenda kule kwa ziara walikuwa wamechangia kama shilingi 180,000/= tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini watu hawa watapata maji? Hata Zahanati ya Mwimbi haina maji. Siyo hao tu vijiji vingi vya mkoa wa Rukwa vina matatizo ya maji licha ya mkoa huo kuwa na mvua nyingi, lakini kwa sababu hakuna anayevuna maji hayo, yote hupotea na wananchi kubaki wanahangaika tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Bonde la Ziwa Rukwa wananchi huliona ziwa kwa mbali na mito ikiporomoka kutoka mlimani lakini upatikanaji wa maji hayo vijijini ni duni mfano kijiji cha Mwela katika Jimbo la Kwela watu hununua maji au kwenda safari ya saa nne hivi. Ndoo ya maji kwa mwaka 2005 ilikuwa shilingi 100/=, ni lini akinamama watakombolewa kutokana na adha hii? Ukienda Namanyere katika Wilaya ya Nkansi kilio ni kile kile maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iwaangalie watu wa Rukwa kwa jicho la huruma. Maji ni muhimu kwa afya ya wakazi wa Rukwa na kwa kilimo endelevu chenye kujenga uchumi na kuondoa umaskini wa kipato, MKUKUTA.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naunga mkono hoja ya Waziri wa Maji kwa asilimia mia moja.

Kuhusu maji mjini Namanyere, naomba Mheshimiwa Waziri atusaidie fedha kwa ajili ya mradi wa maji ya kutega kutoka chanzo cha maji cha Kantete, Kitongoji cha Nkata Kata ya Kate, Nkasi umbali wa kilometa 53 toka Wilayani mjini Namanyere.

Mradi huu utagharimu shilingi bilioni 3.4. Nilikwishaongea na Mheshimiwa Waziri juu ya tatizo kubwa sana la maji mjini Namanyere. Pili, naomba kuishauri Wizara iweke mipango kwa kila mkoa au Halmashauri kuchimba mabwawa/malambo makubwa

ya kuhifadhia maji kwa kumudu ukame wa maji unaojitokeza wakati wa kiangazi. Mfano Dodoma, Singida, Arusha, Rukwa na kadhalika. Mahali pale panapokuwa na shida ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ni uvunaji wa maji ya visimani kutokana na maji ya mvua. Hili ni muhimu vijiji vyote nchini viwekewe programu ya kufunza wananchi na kwa kutoa mfano Serikali ijenge visima katika shule au zahanati ama ghala la kijiji kama mfano. Hii itasaidia sana kuondoa kero ya maji kwa wananchi kwa kutumia teknolojia hii mpya. Naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani zangu kwa kupata nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Wabunge wenzangu kukupongeza wewe, Naibu Spika, pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri ya kuliongoza Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Maji, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kutokana na hotuba yao ambayo ikitekelezwa inaweza kusaidia tatizo gumu la maji nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni uhai na kukosekana kwake ni tatizo na adha kubwa si kwa binadamu tu bali hata kwa wanyama na mimea. Tumeona katika kipindi cha ukame jinsi wananchi hasa akinamama na wafugaji walivyokuwa wakikahangaika kutafuta maji kwa matumizi ya nyumbani pamoja na mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji safi na salama ni muhimu sana na ya lazima kwa wananchi wote waishio mijini na vijijini. Kwa bahati mbaya upatikanaji wa maji safi na salama katika nchi yetu limekuwa jambo la ajabu sana na la kukatisha tamaa kiasi kwamba baadhi ya wananchi wanatumia maji yasiyo safi na salama na yanayohatarisha afya zao na maisha yao kwa jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ilione suala la maji safi na salama kuwa la kufa na kupona. Kwa hiyo, Serikali iwe na mpango wa makusudi kabisa utakaohakikisha kwamba maji safi na salama yanapatikana kwa uhakika nchini kote, mijini na vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa kusambaza maji safi kwa nia ya mabomba utachukua muda mrefu sana kuwafikia wananchi wote ambao wanaendelea kutumia maji ambayo si safi na salama. Naiomba Serikali au Wizara itawanye wataalam wake wa maji mijini na vijijini kutoa taaluma na kuwasaidia waanchi katika uchimbaji wa visima virefu badala ya kusubiri maji ya mabomba peke yake. Uchimbaji wa visima utapunguza tatizo la maji kwa kiasi kikubwa na kuipa nafasi Serikali kuendelea na utaratibu wake wa kusambaza maji kwa njia ya mabomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, taaluma ya uvunaji wa maji ya mvua inafaa itolewe kwa wananchi wote ili waweze kuhifadhi maji kwa matumizi ya baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa malambo na mabwawa yatasaidia wafugaji kubakia katika maeneo yao ya ufugaji badala ya kuhama hama kama ilivyo hivi sasa.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kuwapongeza kwa hotuba nzuri yenye mafanikio na matumaini makubwa. Mheshimiwa Stephen Wasira, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, pamoja na wataalam wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, nichangie eneo la Tabora Mjini. Kuna sehemu ya maji baridi na chumvi kama ifuatavyo. Eneo la Kitete karibu na Hospitali ya Mkoa kuna Kisima ambacho kwa kweli ni cha miaka mingi, kilichimbwa na wakoloni na kuwahudumia wakazi wote wa mjini pale panapotokea upungufu wa maji toka Igomba na kutosheleza.

Ushauri/ombi, naomba visima hivi viboreshwe kwa kuwekwa mitambo ya kisasa na viwe chini ya Wizara ili viwe vinafanyiwa ukarabati wa mara kwa mara. Ingawa Mkurugenzi wa Maji Mkoani, Ndugu Ramadhani Kalingoji amejitahidi kuboresha, bado uwezo ni mdogo sana kiasi kwamba fedha hazitoshelezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za bajeti ya mijini iongezwe kutokana na ongezeko kubwa la mahitaji ya wakazi na ukizingatia kuna vyuo, sekondari nyingi, jeshi, viwanda, vyote vinahitaji gharama kubwa.

Kuhusu ukarabati wa Igombe, kutokana na sehemu hiyo kuharibiwa na wavamizi wa hifadhi hiyo na kuacha bwawa hilo kuna matope mengi, ningeomba Serikali isaidie jinsi ya kuondosha tope hilo kwa kuongeza wataalamu wa kutosha au vifaa vya kuondolea, ili wakati wa mvua kuwepo na kina kirefu tukihifadhi maji kwa wingi.

Mheshimiwa Naibu Spika kuhusu ukarabati wa bwawa la Kazima, ningeomba Serikali iangalie ili lifanyiwe ukarabati na kwanza kutumika katika maji safi na salama. Kwa kumalizia naomba niwapongeze, Waziri na Naibu Waziri kwa ziara zao hapa nchini, hususan walipofika Tabora. Naunga mkono hoja asilimia kwa mia moja.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia maeneo machache katika Wizara hii kama ifuatavyo:-

(i) Kurekebisha hati miliki zilizotolewa toka ukoloni hadi sasa. Mwaka 1997/1998 niliomba Wizara kupitia upya na kurekebisha hati miliki *(Water Rights)* zote zilizotolewa kwa mashamba ya mikataba Wilayani Karatu ambayo yako 45 (robo ya ardhi ya Wilaya ya Karatu). Wakati hatimiliki hizo zinatolewa wakazi/wananchi waliokuwa wanakaa *downstream* hawakufikiriwa kabisa na maji yote ya mto mzima yalitolewa kwa wenye mashamba ya mkataba badala ya utaratibu wa sasa wa *Lts/second or hour.* Hii imewafanya wenye mashamba ya kahawa kuchukua maji yote na wananchi kukosa maji kabisa. Athari hii ipo kwenye vijiji kama Endashangwet, Nangola Juu, Qurus na Bashay – japo Qurus na Bashay hatimaye wamepata mradi kutoka mbali zaidi na hivyo kuwa wa gharama kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2000 wataalam wa Wizara walitembelea maeneo yote ya mashamba ya mikataba Karatu na kuahidi kurekebisha hali hiyo kwa muda mfupi kwa kutumia sheria ya maji ya 1974 na kwa muda mrefu kurekebisha sheria ya maji ili iruhusu wananchi wa *downstream* kupata maji. Hadi sasa hakuna taarifa yeyote. Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu hitaji hilo ambalo ni muhimu kwa maisha ya wananchi? Ni lini sasa Sheria italetwa Bungeni ili *Water Rights* hizo zenye kutoa umiliki wa mto mzima kwa mtu binafsi urekebishwe? Napenda kupata maelezo ya kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi wa maji na usafi wa mazingira vijijini. Ni kweli huu ni mradi mkubwa na wa pekee kwa nchi yetu. Hata hivyo napenda kutoa tahadhari ifuatayo:-

(i) Umiliki wa mradi huu uwekwe moja kwa moja chini ya vijiji vyenyewe kwa uzoefu tuliopata kwa mpango wa *MMEM.* Tusipopata *ownership* ya wananchi wenyewe toka mwanzo programu hii haitakuwa tofauti na miradi mingi ya maji ambayo baada ya muda mfupi tu inaharibika na kwa vile haina mwenyewe inaachwa kuwa *White Elephant.*

(ii) Kama ilivyo kwa miradi mingi, fedha zielekezwe kwenye upatikanaji wa maji zaidi kuliko utawala kama inavyoonekana, kazi ya kuwapata wahandisi washauri mpaka sasa imechukua zaidi ya miezi saba. Ni vema *bureaucracy* ikafupishwa bila ku-*compromise quality.*

(iii) Je, Serikali inaweza kutangaza majina ya vijiji vyote vilivyoteuliwa kwani Halmashauri zilipendekeza na hadi sasa hatujapata mshindo nyuma *(feedback),* mathalani kwa Wilaya ya Karatu kama kwa nchi nzima itakuwa vigumu. Natanguliza shukrani.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Kilombero, Tarafa ya Mngeta, Kata ya Mchombe wananchi wa vijiji vya Lukongo, Mchombe na Mngeta wanategemea kupata maji ya mtiririko *(gravity water)* kutoka mto wa kudumu wa Mchombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakazi wa vijiji hivi ni zaidi ya watu elfu ishirini tukiwa na huduma za jamii zifuatazo, shule ya sekondari moja, shule za msingi sita, kituo cha afya na ni makao makuu ya Kata ya Mchombe na Tarafa ya Mngeta.

Mheshimiwa Naibu Spika, chanzo cha maji kimetengwa mahali ambapo ni chini ya makazi ya watu wa kijiji cha Msesele ili kuwawezesha wakazi hao kupata maji safi na salama, chanzo hicho kinabidi kihamishiwe juu ya mto ambako hamna maisha ya watu kwani ni hifadhi ya milima ya Udzungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa kuhamisha chanzo hiki ni mradi mkubwa kidogo ambao Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero haitamudu peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi, tunaomba Wizara itusaidie kuhamisha mradi huu ili wananchi wa vijiji vilivyotajwa wapate maji safi na salama.

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nichukue fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri wa Maji kwa hotuba yake nzuri yenye mchanganuo fasaha wa Makadirio ya Matumizi ya fedha ya Wizara ya Maji. Sambamba naye napenda kumpongeza Naibu Waziri wa Maji, Katibu Mkuu Wizara ya Maji na wakurugenzi wote wa Wizara hii kwa juhudi zao kubwa wanazozifanya katika kuhakikisha utendaji uliotukuka katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maji ina majukumu makubwa katika kuhakikisha upatikanaji wa maji nchini kuanzia utafiti wa maeneo yenye *reservoirs* asilia za maji, kuelekeza au kushauri matumizi bora ya maji, kuwapatia wananchi maji kwa ajili ya maendeleo yao. Ilani yetu ya CCM ya mwaka 2005 inaelezea vizuri sera ya maji kwa kuiagiza Serikali ya Awamu ya Nne kuhakikisha angalau asilimia 65 ya wananchi wa vijijini na asilimia 90 ya wale waishio mijini wanapata maji safi na salama. Pia inaelezea juu ya upatikanaji wa maji kwa ajili ya shughuli za kilimo cha umwagiliaji na ufugaji zinapewa kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini tunao watalaam wa miamba *(Geologists)* na wale wa maji *(Hydrologists)* waliobobea nchini. Serikali ihakikishe inawapa fursa ya kuchangia katika changamoto hii na mchakato mzima wa kuhakikisha upatikanaji wa maji nchini kwa kuwapatia nyenzo za kufanyia kazi. Wanahitaji vifaa maalumu vya utafitiwa maeneo mapya ya vyanzo vya maji na wingi wake, wanahitaji mitambo maalum ya kuchimbia maji. Vifaa vyote hivi ni ghali, Serikali inahitaji kuelekeza nguvu zake kwenye upatikanaji wa vifaa hivi ili kuweza kufanikisha lengo la Ilani yetu kwa muda muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka ya nyuma kidogo hususan wakati wa Serikali ya Awamu ya Kwanza juhudi kubwa sana ilifanywa kuhakikisha maji yanasambazwa katika vijiji mbalimbali ama kwa kuchimba visima au kuvuta maji kutoka mtoni na ziwani kwa pampu na kutandaza mabomba ya kugawa maji sehemu mbalimbali za vijiji. Katika maeneo mengi ziwani na matenki ya maji hayo yanabaki ni ishara tu ya kile kisicho kuwepo, kwani hakuna maji yanayotiririka. Pampu nyingi zimeharibika na kutokana na ukosefu wa vipuli ni kero tupu imetanda vijijini. Nashauri Serikali ifanye makusudi mazima ya kuwatuma sehemu mbalimbali za vijijini kufanya *inventory* ya pampu hizo na visima hivyo ili matengenezo yafanywe kwa manufaa ya wananchi hao.

Napenda nitoe shukrani nyingi sana kwa Serikali kwa mpango wake mpya wa hifadhi ya vyanzo vya maji na mazingira ambao unahusika pia uchimbaji wa visima vijijini kwa njia ya kuwahusisha wananchi katika kuchangia gharama kidogo. Ni matumaini yetu kuwa mpango huu utatengewa fedha zaidi ili mwezi kukidhi changamoto yetu ya kuwafikishia wananchi wetu maji kama ilivyobainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005 ya CCM.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upatikanaji wa maji safi na salama jimboni kwangu, naomba nielekeze hoja zangu kwenye maeneo mawili. Kwanza, ahadi ya Mheshimiwa Rais kuhusu tatizo sugu la ukosefu wa maji katika Mji wa Tunduma. Kwa

heshima na taadhima napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hapo tarehe 30 Agosti, 2005 wakati wa kampeni Mheshimiwa Rais alitamka kuwa anaelewa tatizo kubwa linaloukaribia mji ule na kwamba analifahamu fika toka akiwa Waziri wa Maji na pia wakati akiwa Waziri wa Fedha na kuahidi kuwa atahakikisha tatizo hilo linatakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya hata kutajwa mpango wa utekelezaji wake hautatajwa katika hotuba ya Wizara badala yake Wizara inaongelea juu ya ukarabati wa miradi. Kutokana na unyeti wa hali ya maji Tunduma na uzito wa kauli ya Mheshimiwa Rais naomba suala hili lichukuliwe kwa uzito wa pekee ili mji huo, sambamba na mji wa Mlowo jimbo la Mbozi Mashariki, utekelezaji wa upatiwaji maji uwekwe bayana. Suala ni kuleta maji Tunduma maana hakuna maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukosefu wa maji katika vijiji zaidi ya 75% ya vijiji 70 vya Jimbo la Mbozi Magharibi ni mkubwa sana. Katika maana ya ukanda wa juu *(plateau)* ambayo haina mito mingi, majira ya kiangazi wananchi huchota maji yao katika madimbwi ambayo pia hutumiwa na wanyama kama mbwa, nguruwe na ng'ombe na hivyo kusababisha magonjwa ya milipuko kama kipindupindu, homa ya matumbo na kuhara damu. Eneo hili linahitaji mpango kabambe wa kuwachimbia visima virefu. Maeneo mengi ya kuchimba visima hivyo yamekwishapimwa.

Katika uwanda wa Bonde la Ufa yenye mito isiyokauka kuna maeneo kadhaaa ambayo hapo nyuma yalikuwa yakipata maji ya bomba hivyo kinachohitajika ni kununua upya pampu za kusukumia maji na matengenezo ya mabomba ya kusambazia maji. Pia katika eneo hili kuna maeneo mengi ambayo kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa, mito inakuwa ikikauka kwa takribani miezi saba kwa mwaka na hivyo kuwafanya wananchi kufuata maji hadi umbali wa kilometa 20 toka vijijini kwao, naomba mpango wa makusudi wa kuvipatia vijiji hivyo maji upewe kipaumbele. Wananchi hawa wako tayari kuchangia mfuko wa maji bila ajizi. Pia maeneo ya kuchima visima katika ukanda huu yamekwishapimwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudie kuishukuru Wizara ya Maji kwa kufanya utafiti wa maji chini ya ardhi kwa maeneo 48 Wilayani Mbozi ina vijiji 175 ambavyo 70 viko Mbozi Magharibi. Ni matumaini yangu juhudi zaidi zitafanyiwa utafiti huo maeneo mengi zaidi ili wananchi wa Jimbo langu waweze kupatiwa huduma hiyo muhimu kabisa katika uhai wa viumbe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalamu wote wa Wizara hii kwa hotuba nzuri. Mimi ninaamini hotuba hii itatekelezwa kwa vitendo, suala zima la kero ya maji nchini itapungua kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitamke rasmi kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja hoja hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu nashauri na kuomba Wizara sasa ikamilishe miradi mikubwa ya maji ambayo ina uwezo wa kuwapatia maji wananchi wengi. Ipo miradi ambayo ni mikubwa kama vile wa *HTM*- Handeni, Korogwe, unaotoa maji kwenye chanzo cha Mto Luvu au Pangani na mradi wa mto Wami unaopeleka maji katika vijiji vya Chalinze, Mbwewe, Mkoita, Lugoba na kadhalika. Miradi ya aina hii ikiendelezwa itaweza kuokoa miradi ya aina hii ikiendelezwa itaweza kuokoa miradi midogo midogo ya maji ambayo haina uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tatizo la Maji Korogwe Mjini, toka nimeingia ndani ya Bunge mwaka 1995 nimekuwa nikieleza Wizara yako tatizo la maji katika Mji wa Korogwe na hasa ikifahamika kwamba mto Luvu/Pangani unapita katikati ya mji wa Korogwe na baya zaidi wananchi wanashindwa kutuelewa kwa sababu chanzo cha maji ya *HTM* kipo Korogwe kilometa sita hadi nane kutoka Korogwe Mjini lakini cha kushangaza Mji wa Korogwe unashida ya maji. Katika chanzo cha *HTM* kipo bomba lililotegeshwa kuwapatia maji Mji wa Korogwe na vitongoji vyake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nikiahidiwa kwa maneno tu bila vitendo kwamba tutaongeza chanzo cha *HTM* - Korogwe - Tabora ili Mji wa Korogwe nao upate maji hasa uzingatiwa kwamba Korogwe sasa ni Mji umepata hadhi ya *town council*. Mji huo unashida sana ya maji, Rais alipokuja Korogwe aliahidi wananchi kuondoa shida ya maji Korogwe, hivyo ni ahadi ya Rais naomba itekelezwe. Nataka nifahamu ni sababu zipi za msingi zinazofanya Korogwe isipate maji hayo ya kutoka *HTM* - Tabora ambapo ni kilometa sita hadi nane tu.

Mimi nafahamu idadi ya wakazi Korogwe mjini sasa ni watu 54,000 wanao uwezo wa kununua maji na mradi huo ukaishi kiuchumi bila tatizo na ukaweza kujiendesha, hivi kuna tatizo gani? Kama tatizo ni chanzo kidogo kwa nini chanzo hicho kisipambiwe ili kuweza kukidhi haja ya kutupatia maji Korogwe Mjini. Ni kinyume kabisa, maji na chanzo kitoke Korogwe, sisi Korogwe tukose maji na maji yaende Korogwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili limekuwa likipigwa dana dana muda mrefu. Safari hii wananchi wanataka majibu sasa ya kupata maji mji wa Korogwe toka *HTM* - Korogwe - Tabora. Naomba Wizara ifanye kila linalowezekana tupate maji hayo na wananchi wangu wapo tayari kuchimba mitaro toka Tabora hadi Korogwe na pia kuchangia.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza kwa jitihada kubwa mnayoonyesha, mnaweka bidii ya kila aina pamoja na shughuli kuwa ngumu. Tunatambua shughuli ya maji ni ngumu kila mmoja anahitaji maji na anayahitaji kila siku, mifugo pia inahitaji maji, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Karagwe (Kayanga), hii ni ahadi ya uchaguzi ya Mheshimiwa Rais si jimbo langu, lakini ni mji wa Wilaya yangu. Nilikuwepo kwenye mkutano wa kampeni, wananchi wa Wilaya ya Karagwe wanakumbushia mradi huu

mdogo wa maji ukarabatiwe, gharama itakuwa ni ndogo, ni mradi mdogo kwa kuwa kimji ni kidogo, huenda ni *pump* na kuongeza *reserve tank capacity* na kadhalika. Lakini nasisitiza kuwa hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais ya uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, visima na mabwawa ya kukusanya maji ya mvua katika jimbo la Kyerwa lina maeneo yenye tatizo kubwa la maji. Dawa yake ni kupata uwezeshaji wa kuchimba visima vya maji. Katika maeneo ambako visima haviwezekani, basi ni kuwawezesha wananchi kuwa na mabwawa ya kukusanyia maji yanayotiririka toka vilimani wakati wa mvua, yawekwe dawa kidogo na yawasaidie kipindi cha ukame. Wananchi wamejenga baadhi ya mabwawa lakini shida ni gharama, Serikali ingewasaidia kwa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jiji la Dar es Salaam labda huu mradi unaotekelezwa utasidia lakini kilio cha Masaki ni miaka zaidi ya 30. Tuna wasiwasi huenda wanaofaidika na kuuza maji ya *tankers* wasifurahishwe na Masaki kupata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kituo cha Kawe, utendaji wao si mzuri hata kidogo, wakazi wa Mikocheni B wanayo malalamiko mazito. Nia ya baadhi ya watendaji si kuwahudumia wananchi wanaijengea Wizara hii nzuri jina baya. Tafadhali fuatilia hili.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Stephen Wasira, Waziri wa Maji kwa kazi nzuri akisaidiwa na Naibu Waziri, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, tangu wamekabidhiwa Wizara hii ya Maji.

Maji ni uhai, maji yanapatikana kwa wingi na miradi iliyoanzishwa huko nyuma iliyokuwa inasimamiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu wa awamu ya nne, sasa inaendelea vizuri sana. Nawaombea kwa mola awape nguvu na moyo wa imani kubwa ili Watanzania wanywe, waoge na watakate kwa maji safi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni uhai Mradi wa Ziwa Victoria umewafurahisha sana wakazi wa Mkoa wa Mwanza na Mkoa wa Shinyanga, ilikuwa ndoto kwao maishani kupata maji mengi, watapata kutoka Ziwa Victoria nawashukuru sana Serikali na wafadhili wote wanaendelea kushiriki katika mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe ushauri baada ya kukamilika mradi huu wa Ziwa Victoria naomba Wizara isijitoe katika kulinda eneo palipopita mabomba wasiwaachie Halmashauri za Wilaya uzembe upo katika Halmashauri ya Wilaya. Aidha, Wizara iandae adhabu kali kwa Halmashauri ya Wilaya zitakazozembea kukuza vifaa ambazo vimepita katika maeneo yao ili uwe fundisho kwa maeneo mengine ambayo itaanzishwa miradi mikubwa kama huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mradi wa maji vijijini namshukuru sana Waziri kutoa maeneo kadhaa ya upanuzi wa visima virefu katika mkoa wa Mwanza, Wilaya ya Geita, Magu, Kwimba, Misungwi na maeneo menginie.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchimbaji wa visima virefu ndio mkombozi katika vijiji vingi, kulikuwa na miradi mingi katika Wilaya ya Geita kama Chakolongo, Kasamwa, Nyamtukunza, Nzera na Karumwa, visima hivi havifanyi kazi na vimeachwa kabisa. Naomba miradi hii ifufuliwe.

Nashukuru mifuko ya maji imeanzishwa lakini imeanzishwa baada ya miradi hii kufa. Nitashukuru kama Serikali itazingatia kuifuatilia hiyo miradi niliyoitaja hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri kwa hotuba yake ukurasa wa 24(51) kwa kuweka kijiji cha Malya kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya itapanua miradi ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kijiji cha Malya mitambo yote ilikarabatiwa vizuri sana ila naomba dawa iletwe sasa ili watumie maji safi na salama. Maji yaliyopo sasa yana rangi ya kijani toka katika lambo la Malya si safi, nitashukuru wakazi wa eneo hilo wapate maji safi na salama. Tatizo la Sinza maji hayatoki mchana wanaomba yatoke mchana si usiku.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali isisikilize mchezo wa kuigiza wa Wapinzani kubeza mafanikio ya CCM. Je, wao wameleta au wamechimba visima vingapi kama chama cha upinzani? Itabidi nao ruzuku zao ziwanufaishe Watanzania wote si kulaumu tu, naomba Waziri uwajibu hasa, tutashangilia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakia mema Waziri, Naibu na watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanazofanya. Naunga mkono hoja na wapewe fedha zote tunywe maji na tuoge.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kuchukua nafasi kukushukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watalaam wote kwa hotuba iliyoandaliwa vema na iliyoangalia kila kona ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa na Wizara, naomba nilete kero ya maji kwenye mji wa Sikonge. Naiomba Serikali iangalie mji wa Sikonge unaokuwa lakini miundombinu yake ya maji haitoshelezi mahitaji ya wananchi wa mji huo.

Aidha, tunayo tarafa ya Kiwere kata ya Kipiri yenye vijiji vyenye matatizo makubwa ya maji, naiomba Serikali ikishirikana na Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge itoe kipaumbele kwenye kata hiyo ya Kipiri na mji wa Sikonge. Mwisho naendelea kukushukuru Mheshimiwa Waziri na ninaunga mkono hoja.

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Maji kwa hotuba nzuri ambayo imegusa maeneo mengi ya nchi yetu, nampongeza Naibu Waziri, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, kwa kuweza kujituma kwa kusafiri sehemu mbalimbali ili kuona matatizo ya maji,

nampongeza Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri ambazo wamekuwa wakifanya kupunguza matatizo ya maji vijijini na mjini.

Naomba kuchangia kama ifuatavyo, kwanza nashukuru kwa kuutambua na kuona umuhimu wa kuundeleza mradi wa maji ulioko kata ya Madibiru, Mbarali, kata hii ina matatizo makubwa ya maji na kwa vile mradi ulianza kazi mwaka 2004/2005 naomba utiliwe kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Mbarali tulifanikiwa kuhamisha wananchi kwenye kila kijiji kuanzisha mifuko ya maji kwa ajili ya kuchimba visima vya maji na kufufua mabomba yaliyoharibika kwa muda mrefu na kusaidiwa na Halmashauri kwa kiasi kidogo. Tatizo limekuwa ni uchimbaji wa visima vya maji usio na mafanikio na kuacha tatizo la maji kubaki pale pale. Ombi langu ni kuwa utafiti wa njia za kuzipatia maji kata za Madibira, Mawimbi, Uboulal Utengule Usangu, Igunusi na Ruiwa kwa haraka zaidi kwani wananchi wamekwisha onyesha moyo wa kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna visima sita ambavyo vimechimbwa bila kutoa maji na gharama za kila kisima ni zaidi ya shilingi 6,000,000/= pesa ambazo zilichangwa na wananchi na kusaidiwa na Serikali Kuu katika kumalizia. Lakini sehemu hizo hazikutoa maji Wizara/Serikali itawasaidiaje wananchi hawa waliopoteza pesa zao bila mfanikio vijiji hivi viko kata ya Uburuku, Mawindi, Chimda na Utengule Usangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Mbarali haina watendaji wa Idara ya Maji. Tuna Mhandisi wa maji wa Wilaya ambaye ameonyesha kuwa hawezi kumudu matatizo ya maji katika Wilaya ya Mbarali bila msaada wa wasaidizi wengine ukizingatia ukubwa wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Wilaya Mbarali ni kame, matatizo ya maji yako katika kiwango kikubwa sana, wananchi walioko vijijini wanafuata maji kwa zaidi ya kilometa kumi. Lakini nimepitia katika hotuba hii na kuona kuwa imepangiwa shilingi 15,000,000/= na za kuendesha na kusimamia huduma za maji je, ni kigezo gani kimetumika katika ukurasa wa 65 wa hotuba. Lakini vile vile katika ukurasa 53 imetengewa visima sita tu katika Wilaya yenye ukubwa wa kilometa 16,600 na yenye vijiji vyenye umbali wa kilometa zaidi ya 20 kati ya kijiji na kijiji. Naomba utafiti ufanywe upya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi zangu za dhati kwa Wizara, Waziri, Naibu Waziri na watumishi wote wa Wizara hii, naomba nichangie kwa kifupi kama ifuatavyo:-

Pamoja na nia nzuri ya k utaka kuwapa *ownership* ya visima wale wananchi wanaopelekewa fedha kwa kuchimba visima, sharti la kuwataka watumishi mfuko wao wa maji kwa kiasi cha shilingi milioni mbili limekuwa ni kikwazo kikubwa kwa wananchi hawa maskini kufaidika na fedha hizo zitolewazo na Serikali/wafadhili. Je,

isingewezekana kubadilisha utaratibu wa namna ya hawa wananchi kuchangia? Kwa mfano, kwa nini miradi hiyo ya wananchi maskini, lakini watakiwe kulipia maji hapo ya visima virefu walau kwa shilingi 10/= hadi 150/= kwa ndoo hadi pale uwezo wa kuendesha visima hivyo utakapokuwa umejengwa? Hili suala bado linaweza kupewa tafakari mbalimbali ili mradi tu huduma hizi zisiendelee kuchelewa kwa wananchi hata pale ambapo fedha za kutosha kabisa zipo kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitembea katika nchi hii, hasa wakati wa misimu ya mvua utashangazwa na wingi wa maji yanayotiririka bila kukingwa na hivyo kuyapoteza wakati nchi yetu inasumbuliwa na shida kubwa ya maji kwa matumizi ya binadamu, wanyama/mifugo na hata kilimo cha kumwagilia. Kinachonisikitisha ni kwamba bado sijaona mpango wa maksudi kabisa wa muda mrefu wa kutaka kukinga maji haya yanayopotea bure tu. Kwa nini Halmashauri zetu zisisaidiwe kujenga uwezo wa mitambo, kama matingatinga ambayo pia yanaweza kutumika kwa matengenezo ya barabara zetu zilizo chini ya Halmashauri za Wilaya zetu. Kwa kuanzia, mitambo hiyo inaweza ikatafutwa kwa fedha za pamoja za Halmashauri kadhaa zilizo jirani ambazo pia zinaleta maana na urahisi wa matumizi ya mitambo yenyewe kwa ushirikiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu utafanikiwa pia kama utatekelezwa kwa ushirikiano kifedha na kitaalam kwa kushirikisha Wizara ya Maji, Wizara ya Miundombinu na Wizara ya TAMISEMI katika ofisi ya Waziri Mkuu. Utaona pia kuwa watalaam wa maji *(water engineers)* walio haba katika Halmashauri nyingi pia watatumika kwa Halmashauri za Wilaya kadhaa pia zinazoshirikiana huku pia wahandisi wa ujenzi wakisaidia pia kwa upande wa *damming* hata pale miradi ya barabara inapotekelezwa katika maeneo. Ushirikiano huo utaleta ufanisi mkubwa na kupandisha *utilization factor* ya vifaa/mitambo na watalaam wetu.

Mheshimiwa Spika, utaona kuwa hapa nasisitiza *holistic approach* katika kutatua matatizo ya maji kwa pamoja na yale ya barabara zetu huko katika Halmashauri za Wilaya zetu. *Packaging* au *integration* ya mipango ya maji, sambamba na ile ya ujenzi wa barabara zetu. Nadhani nimeeleweka hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la uhaba wa *qualified engineers* katika Halmashauri za Wilaya linalikumba hata hili eneo la wahandisi wa maji. Pengine tatizo hili halionekani hasa pale ambapo hata asiye na sifa stahili ya kuitwa mhandisi, basi utakuta anaitwa mhandisi wa maji kutokana tu na dhamira ya ile ofisi anayoshikilia. Je, si vyema sasa ikaandaliwa orodha ya Halmashauri za Wilaya zote na aina za wahandisi waliopo na wanaohitajika huku sifa za hao wenye dhamana hizo hivi sasa zikitambuliwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya haya machache, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. JOYCE N. MACHIMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwa maandishi kuhusu Wizara hii ya maji kwa manufaa ya wananchi wa Tanzania na hasa kwa maeneo yenye matatizo ya maji.

Naomba nizungumzie maji katika Mji wa Bariadi ambako kuna mradi unaoendelea Wilayani humo mimi binafsi, nina hoja hata kama haitawezekana kufanyiwa kazi Bajeti hii ya mwaka 2006/2007 naomba basi Mji mdogo wa Luguru katika Wilaya ya Bariadi ufanyiwe upembuzi ili maji yanayosambazwa mjini Bariadi yaweze kupelekwa pia katika mji mdogo wa Luguru ambao ni kilometa kidogo tu kutoka mjini Bariadi kwani wananchi wa mji huu wanayo dhiki kubwa ya maji hasa ukizingatia kuwa hata bwawa lililokuwepo pale limejaa udongo na kina kupoteza uhifadhi wa maji kufuatia ukame unaotukumba mara kwa mara sisi wakazi wa Mji wa Luguru.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi inaingia kiwango cha Halmashauri ya Mji ni vyema basi hata miji midogo iliyo karibu na Wilaya ikaboreshwa kwa miundombinu kama maji na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nilete hoja ya kuweza kuunganisha huduma ya maji kwa mji wa Mwamapalala ambao uko mpakani na Wilaya ya Maswa ambayo ina maji ya bomba hadi mpakani mwa Bariadi katika kijiji cha Malita. Hivyo itakuwa vyema kama na Mwamapalala itapata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. HALIMA JAMES MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wa Maji, pamoja na maelezo yangu ya mdomo kuna mambo kadhaa ambayo ningehitaji Wizara yenu iyatolee ufafanuzi wakati wa kujibu hoja.

Kwanza inahusiana na ripoti ya *REPOA* kuhusiana na MKUKUTA. Ripoti husika maelezo bayana kwamba MKUKUTA hautekelezeki na haufanikiwi kufikia mwaka 2010 isipokuwa Dar es Salaam ambapo baadhi ya malengo yatafanikiwa. Ningependa nijibiwe kwa kiasi gani Wizara yenu inaamini/kutoaamini utafiti huu?

Mheshimiwa Waziri vile vile ningependa nipate ufafanuzi ni vigezo gani ambavyo vilitumika hali iliyopelekea kupata takwimu kama zilivyoainishwa na kitabu cha MKUKUTA (kiambatisho ukurasa 21 kipengele 3.1.

Vile vile ningependa nipate ufafanuzi kuhusiana na mkakati uliopo kuhusiana na Mkoa wa Dar es Salaam ambao kwa sasa hali imezidi kuwa mbaya na biashara za maji zimeshamiri, hivi ni kweli 73% ya Mkoa wa Dar es Salaam (kama ripoti ya Mijini) inapata maji mpaka sasa mwaka 2006?

Vile vile tungependa/ningependa niambiwe ni kwa kiasi gani sera ya maji ya miaka ya 1990 ilishindwa kufanya kazi na kuna viashiria gani vinavyoonyesha kwamba MKUKUTA kwa mwaka 2009/2010 utafanikiwa kwa mfano 90% Mjini na 73% vijijini?

Mheshimiwa Spika, ni muhimu kuwa na kamati ambazo zinafuatilia miradi hii ili kuwa na takwimu sahihi. Poleni sana na kazi.

**MHE. KAIKA S. OLE-TELELE:** Mheshimiwa Naibu Spika,kwanza nampongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri ya Makadirio ya

Mapato na Matumizi ya fedha kwa Wizara yake ya Maji kwa mwaka 2006/2007. Pia nampongeza Naibu Waziri wa Maji Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, pamoja na timu nzima ya watalaam wa Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Waziri kwa heshima na unyenyekevu mkubwa naomba ukubali mwaliko wangu wa kutembelea Jimbo langu la Uchaguzi la Ngorongoro baada ya Bunge hili la Bajeti kwa siku na tarehe muafaka kwetu sisi Wabunge wawili majirani waliopita bila kupingwa wakati wa kinyang'anyiro cha kuwania safari hiyo ya utumishi wa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri akikubali mwaliko huu utaweka historia ya kuwa Waziri wa pili wa Serikali ya Awamu ya Nne kutembelea Wilaya ya Ngorongoro baada ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa bahati mbaya Mawaziri wengi hawafiki Loliondo, makao makuu ya Wilaya ya Hifadhi ya Ngorongoro na kubakiza zaidi ya kilometa 200 kufika Makao Makuu ya Wilaya yaani Loliondo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri kilio kikubwa cha wananchi wa Ngorongoro ni visima na mabwawa yajengwe katika maeneo ya Engusero, Sambu, Naan na mji wa Loliondo katika tarafa ya Sale ni Masusu, Oloirian, Magaiduru na Pinyinyi. Kwa tarafa ya Ngorongoro ni Bulati, Kakesio, Endulen, Olbalbal na Olpiro.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji yakipatikana katika maeneo hayo niliyotaja kwa kuchimba mabwawa na visima itanufaisha watu, mifugo na wanyamapori ambao ni wengi katika eneo langu la uwakilishi Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia mchango wangu kwa hotuba yako nzuri naomba nikukumbushe historia kidogo. Ndugu zangu Wamasai walipoondolewa na wakoloni huko Moru na Seronera ili kupisha uanzishwaji wa Hifadhi ya Serengeti mwaka 1959 wananchi hao walitakiwa waeleze nini wawekewe katika maskini yao mapya ya Nyanda za Juu za Ngorongoro, walitaja mabwawa na visima kwa sekta ya maji vituo vya afya ya mifugo *(Veriternary Centres)* dawa ya mifugo na majosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya rasilimali maji, vituo vya tiba ya mifugo, majosho, mabwawa na visima vimeharibika kwa uchakavu na kutokarabatiwa kwa zaidi ya miaka 40. Naomba bwawa la Bitin, Kakesio/Osiwoni na Ormekeke yaliyojengwa na wakoloni kwa madhumuni niliyoeleza hapo juu yafufuliwe ili kuzuia uhamaji wa wafugaji na kutunza/kuhifadhi mazingira katika uasili wake. Ahsante sana na karibu Ngorongoro. Naunga mkono hoja hii.

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii nimpongeze Waziri wa Maji kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa leo Bungeni ambayo imetoa mwelekeo wa Wizara ya Maji katika kukabiliana na maendeleo ya utoaji na upatikanaji wa maji nchini kwa mwaka wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niwapongeze Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara ya Maji, kwa kazi kubwa waliyoifanya katika uandaaji wa Bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, alipokuwa analihutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Desemba 30, 2005 Mjini Dodoma alisema hivi, ninaomba nimnukuu: "Tatizo la maji ndicho kilio kikubwa cha Watanzania mijini na vijijini. Ndiyo kero nambari wani. Serikali za awamu zote zimefanya jitihada kubwa kukabiliana na tatizo hili. Serikali ya Awamu ya Nne inakusudia kukabiliana na tatizo hili kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Nanyumbu ambayo imeundwa hivi karibuni, kero yake kubwa na nambari wani ni kero ya maji. Eneo kubwa la Wilaya hii ya Nanyumbu ni kame na halina vyanzo vya maji vya kudumu mwaka mzima. Sehemu kama Michiga, Likokona, Napacho, Nangomba, Chitowe, Chipuputa, Sengenya na Mkonona hali ni mbaya sana. Hivyo kwa kuwa, wananchi wa maeneo haya wanatumia muda mwingi kutafuta maji badala ya kufanya kazi nyingine za maendeleo kama vile kilimo na shughuli za pamoja za kimaendeleo. Naiomba Wizara ya Maji ichimbe visima virefu katika maeneo haya haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyotaja hapo juu, Wilaya ya Nanyumbu ni Wilaya mpya ambayo ujenzi wake wa Makao Makuu ya Wilaya karibu utaisha. Tunategemea uteuzi wa Mkuu wa Wilaya *(DC)* utafanyika hivi karibuni na watendaji wakuu wa Wilaya watakuwepo pale Makao Makuu ya Wilaya ambayo ni Mangaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, timu hii yote itakuwepo pale Mangaka wakati sehemu hiyo haina maji ya bomba. Serikali imejenga nyumba za kuishi na ofisi ambazo hazina huduma ya maji. Je, watendaji hawa wataishije bila kuwepo kwa huduma hii ya maji? Namwomba Waziri wa Maji atoe maelezo ya kina kuhusu upatikanaji wa huduma ya uhakika ya maji pale Makao Makuu ya Wilaya ya Nanyumbu yaani Mangaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Nanyumbu ina mto mkubwa Ruvuma ambao kama utapatiwa mradi mkubwa wa maji ungeweza kuondoa tatizo kubwa la maji Wilayani Nanyumbu na maeneo mengine ya Mkoa wa Mtwara. Hivyo ninamwomba Waziri wa Maji aeleze kama Wizara yake ina mpango wowote wa kuyatumia maji ya Mto Ruvuma kupeleka maji Wilayani Nanyumbu na Mkoa wa Mtwara kwa ujumla kama ilivyo kwa mradi wa maji wa Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda niseme kuwa nina imani kubwa kwa Wizara hii kuwa itatuondolea kero ya maji Wilayani Nanyumbu ili wananchi wapumzike na adha ya kuokota maji yasiyo salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja hii.

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza natoa pongezi zangu za dhati kwa Waziri wa Maji na Wizara kwa ujumla kwa mikakati ya kuboresha hali ya upatikanaji wa maji nchini ikiwemo Jimbo la Ukonga.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Ukonga, kero kubwa ya wananchi ukiacha barabara ni kero ya maji. Jimbo la Ukonga, lenye wakazi wanaokaribia 700,000 ni asilimia chini ya 20 wanaopata maji ya bomba toka Ruvu. Wananchi waliobaki zaidi ya 500,000 wanategemea maji ya visima. Hata ukarabati wa mabomba ya *DAWASCO* unaofanyika kwa sasa utawafaidisha wananchi wa Kata chache tu za Tabata na maeneo machache ya Kata za Segerea, Buguruni, Vingunguti na Kipawa. Asilimia 80 ya wakazi wa Jimbo la Ukonga kwa maana hiyo hawatafaidika na mabomba haya yanayokarabatiwa ya kutoka Ruvu, labda tutandaze mabomba mapya na njia mpya kabisa lakini kwa uwzo mdogo wa chanzo cha Ruvu Juu hilo haliwezekani mpaka chanzo kipya cha maji kipatikane.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na maelezo hayo na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Ukonga nina maombi mawili yafuatayo: -

(1) Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa chanzo kingine cha maji kutoka bwawa katika eneo la Kidunda, Morogoro au kupata maji toka Mto Rufiji, ambao bado uko kwenye utafiti wa awali, ukamilishwe haraka ili Jiji la Dar es Salaam na hususan Jimbo la Ukonga, tupate maji ya uhakika.

(2) Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mradi huo haujakamilika mradi wa Wizara wa kuchimba visima (Miradi ya maji safi na usafi wa mazingira) uweke kipaumbele katika Jimbo la Ukonga. Kwa sasa mradi huu umetenga fedha kidogo sana kwa jimbo la Ukonga kulinganisha na idadi ya watu. Kata zenye matatizo makubwa ni Ukonga, Pugu, Chanika, Kitunda, Kinyerezi, Kiwalani,Kipawa, Segerea na Msongola.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wote wa Wizara kwa jitihada zao katika kutoa huduma ya maji kwa wananchi. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ipatie kipaumbele Wilaya ya Muleba katika kutoa huduma ya maji safi na salama ili kuepusha uchafuzi wa Ziwa Victoria na upotevu wa maji ya mito kutokana na kutokuwepo mabwawa madogo madogo katika tarafa za Nshamba, Kimwani, Muleba na Kamachumu. Eneo hilo ni sehemu ya vyanzo vya mito mingi inayopeleka maji Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa hifadhi ya Ziwa Victoria unaweza kutoa fedha za kutosha kwa ajili hiyo kutokana na misaada ya wafadhili, kwa sasa wananchi wanachota maji mtoni na wakati wa kiangazi ni kero kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza tena Wizara kwa juhudi kubwa wanayofanya kueneza maji safi na salama nchi nzima hasa vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maombi ya wananchi wa Muleba yazingatiwe. Naunga mkono hoja.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumshukuru Waziri wa Maji, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa kazi waliyoianza katika awamu hii ya nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la maji Misungwi ni kubwa na Serikali inafahamu imekuwa inafanya juhudi za kumaliza tatizo hilo. Imefanya juhudi *ABD* haikufanikiwa, Serikali imeendelea, *AFD* wao wamefanya upembuzi yakinifu kwa kuchukua maji toka eneo la Nyakasanga Kijiji cha Ng'walogwabagole na kuainisha njia ya bomba litakapopita vijiji vitakavyo husika na huduma hiyo iwapo itatekelezwa ni Mwalo, Mwajombo, Nange, Mapilinga, Misungwi, Mwambola, Iteja, Lubuga na Mabuki.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hii ni ya kutia matumaini hasa baada ya jibu la lao hapa Bungeni 04 Aprili, 2006 kuwa shilingi bilioni 15.0 na utekelezaji ungeanza kwa awamu mbili, ya kwanza utayarishaji vitalu vya zabuni na ya pili mifumo mipya ya maji safi hiyo yote ni moja na Serikali iliahidi kutekeleza kutokana na shilingi 9.6 bilioni kwa miji mitatu yaani Bukoba, Musoma na Misungwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli hotuba ya Waziri kuitoa Misungwi kwenye hatua za kwanza ni kuwasononesha wananchi wa Misungwi, nashauri hatua ya kwanza ianze kama jibu la mwanzo la Serikali lilivyosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mradi wa Ziwa Victoria kupeleka Kahama na Shinyanga, vijiji vilivyosahaulika na viko ndani ya kilometa tano vihusishwe navyo ni Mahando kilometa 4.5, Mwagiligili (Mwamagili) kilometa 3.0 na Mwanazengo kilometa 4.0.

Mheshimiwa Naibu Spika, kijiji kingine ni Bulunda kilometa 5.5, Mwagimaji kilometa 6.0 umuhimu wa vijiji hivi ni vya kata ya Ilujamate hawa ndiyo walinzi wa mradi mzima tangu mwanzo wa ujenzi hadi leo wamepambana na wizi wa kila aina katika kata hiyo ni vyema wakafikiriwa kupewa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Misungwi kwa sasa vijiji vinavyofaidika ni sita tu, wakati ufumbuzi wa kudumu wa maji Misungwi huduma waliyokuwa wanapata kwa kusuasua ni kutoka Bwawa la Misungwi ambalo kama lingepata ukarabati wa hali ya juu ungesaidia sana naomba Serikali ilitenge fedha bwala hilo lisaidie wakati ujenzi unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa maji Misasi umekarabatiwa vizuri isipokuwa ombi ni kujengewa tanki kubwa linaloendana na ongezeko la watu katika mji huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ni imani yangu Serikali itatekeleza ahadi zilizotolewa na Mheshimiwa Rais hasa mradi wa maji Misungwi. Naomba kuunga mkono, ahsante.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuipongeza Wizara ya Maji kwa kazi nzuri inayofanya na hotuba nzuri ya bajeti ya mwaka 2006/2007.

Hata hivyo ningependa kufahamu bayana vigezo vilivyotumika katika kugawa fedha za maji katika Halmashauri mbalimbali, kwa mfano Wilaya ya Kilolo ambayo ni mpya kabisa na ina matatizo ya maji, inatengewa fedha kidogo sana shilingi milioni 33 ukilinganisha na Halmashauri nyingi kama ilivyoonyeshwa kwenye kitabu cha hotuba ukurasa wa 63 hadi 68.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitashukuru kama Wilaya hiyo yenye vijiji 84 na wakazi 230,000 itaongezewa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mipango ya kueneza maji ni mizuri sana. Tatizo ni utekelezaji, wataalam na watendaji hawapendi kuwashirikisha wananchi wa sehemu husika. Wanapofika kuchimba maji hawapendi ushauri kutoka kwa wananchi. Mfano mzuri ni kijiji cha Mwamageulee ambapo walichimba visima viwili bila mafanikio na wakaweka vioski vya maji mbali na mitaa wanayokaa wananchi.

Pili, Serikali bado haijatambua juhudi za wananchi kujitafutia maji wenyewe kwa kutumia utaalam wao wenyewe kama *water dousing*. Utaalam huu wa kugundua maji chini ya ardhi hautambuliwi ingawa ni wa uhakika, nashauri Wizara ilitazame hili na kuutambua utaalam huu.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mchango wangu niliochangia naomba niongeze yafuatayo:-

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa kampeni alifika Bukombe mji wa Masumbwe na Ushirombo, na kwa kuwa nilikuwa napambana na mgombea wa *CUF* aliyekuwa Mbunge kwa miaka 15 ndugu Emmanuel Mzalia Mnuke, Mheshimiwa Rais alisema namnukuu: “Huyu anayegombea *CUF* si mnamjua, amesahau nini Bungeni nichagueni mimi, nileteeni Luhahula, ninamjua ukereketwa wake, maji mtapata, umeme mtapata,” mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana suala hili lizingatiwe angalau kwa bajeti ya mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda kumwalika Waziri au Naibu Waziri wa Maji waje Bukombe waone hali halisi ilivyo na wananchi wa Bukombe wajue kwamba Serikali inawajali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, ahsante.

**MHE. MGANI J. KADIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia afya njema na kunijalia kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza wapiga kura wangu wa Wilaya ambao ndio walioniruhusu kuwa Mbunge. Pia sina budi kukupongeza wewe binafsi kwa kuweza kwako kutuongoza katika Bunge lako. Sasa naomba pongezi zangu zimfikie Mheshimiwa Lowassa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo sasa naomba niende katika mchango wangu, tukizungumzia suala la maji ni suala muhimu kwani maji uhai wa binadamu, wanyama pamoja na miti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza na binadamu, ni wakati tosha kuiuliza Wizara inafahamu hiyo? Pamoja na hotuba ya Waziri wa Maji inaonyesha kwamba bado nchi yetu haijaweza kuwaondolea shida watu wetu, Serikali inaitambua vyema nchi yetu kuwa kuna vijiji vyetu havina mategemeo ya kuondokana na matatizo ya maji. Wananchi wa nchi hii wanaonekana wazi kutumia maji yasiyo salama. Wizara ya Maji ipo lakini kubwa kuwafanya wananchi wetu kuishi kwa kubahatisha. Tujiulize mpaka lini watu wetu waishi kwa hali hiyo? Wizara imeshindwa haya maji wanayotumia watu wetu yako salama hata dawa ya maji Wizara haina.

Mheshimiwa Naibu Spika,katika nchi yetu hii hakuna sababu ya kukosa maji, kukosekana ni nia ya kuwapa maji safi watu wetu, penye nia pana njia. Watu binafsi wameamua kuchimba visima virefu na hivi sasa watu wanatumia maji kama biashara. Watu wamefanikiwa kwa hilo na linawasaidia wananchi, tujiulize Wizara ilishindwaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, maji pia humuhuisha mnyama, nchi yetu ina upana wa watu wake kuishi kwa kutegemea ufugaji, wafugaji wetu ambao wamejiajiri kwa mifugo yao Serikali imewadharau kabisa, wanyama hawana maeneo ya maji kukosenaka kwa maeneo ya maji ndiyo wafugaji hulazimika kuhama sehemu hii kwenda sehemu nyingine kunakopatikana hayo maji hawakutengewa maeneo ya kuosha dawa wanyama wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuondokane na ukame Wizara ya Maji yangehakikisha maji ni raslimali, Watanzania maisha yao ni kusema wako juu ya maji lakini hatuwezi kuogelea. Hii ndiyo sababu ya kuzama. Nchi yetu hupata balaa la njaa, kutokana na utaratibu wa kujua utaratibu wa kuyapata maji. Kilimo cha umwagiliaji maji upo uwezekano nchi yetu kukikuza kilimo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu hupata mvua. Tujiulize maji ya mvua yanaachwa kufunika ardhi na kusambaa katika mabonde ili yatoweke. Ni lini Wizara itaweza kuvuna maji ya mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi leo nchi yetu haina umeme wa uhakika kutokana na ukosefu wa maji. Tatizo la maji sio ukame tu, bali linadhoofisha nchi yetu na kuingiza nchi katika janga la njaa na hatimaye umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufanikishaji wa viwanda vyetu panahitaji Wizara itafute uvumbuzi wa maji. Kuwepo kwa maji kusukuma maendeleo ya viwanda jambo ambalo ndiyo pato la nchi yetu.

Mheshimiwa baada ya mchango wangu huo sasa niseme naitakia baraka njema Wizara ya Maji. Naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wale waliokuwa wameomba kuchangia Wizara hii wamemalizika isipokuwa mtu mmoja ambaye hatutampa nafasi kwa sababu hayupo humu ndani.

Kwa hiyo, mchana tutaingia na Wizara yenyewe kuanza kujibu. Kama kawaida ya Kanuni yetu atapewa nafasi ya muda wa saa moja, yeye Waziri watajua na Naibu wake wanagawa vipi *time* hiyo ili tuweze kuwa na muda wa kutosha kwenye Kamati ya Matumizi.

Sasa kama tulivyoeleza jana Kamati ya Matumizi leo tutaruhusu kwenye kifungu cha mshahara wa Waziri mambo yanayohusiana na utawala, mambo ambayo ni *technical* yako kwenye vifungu mbalimbali, naomba mkaangalie vizuri kusudi tuendeshe kikao chetu kwa kufuata Kanuni zaidi kuliko kusimama tu kila mtu anasema mshahara wa Waziri.

Kwa hiyo, muda mlio nao dakika 15 nyinginezo mkajipange vizuri, huo ndio utaratibu.

Sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 06.47 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyotangaza kabla ya kusitisha shughuli za Bunge mchana kwamba, wale waliokuwa wameomba kuchangia wote walipewa nafasi na sasa tunaanza moja kwa moja na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii adimu na ya pekee kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete na Makamu wa Rais Dr. Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa kwao kwa ushindi wa kishindo. Pia, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuniteua kuwa Naibu Waziri wa Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Edward Lowassa, Mbunge wa Monduli, kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini pia napenda kumshukuru kwa kazi kubwa aliyoifanya katika Wizara ya Maji ambapo sasa sisi tunaitekeleza. *(Makofi)*

Napenda pia kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote, Mawaziri, Manaibu Waziri kwa nafasi mbalimbali walizochaguliwa. *(Makofi)*

Napenda kutoa shukrani zangu kutoka moyoni kwa Umoja wa Wanawake Tanzania Mkoa wa Dar es Salaam kwa kunipitisha kwenye kura za maoni kwa kishindo na pia Wajumbe wa Baraza Kuu la Umoja wa Wanawake Tanzania ambao wamenichagua kwa kura nyingi kuwa mshindi na Mbunge wa Viti Maalum *NGOs*. Pia, napenda kumshukuru sana Waziri wa Maji Stephen Wasira, mkubwa wangu wa Kazi na Katibu Mkuu wangu, Patric Rutabanzibwa, kwa ushirikiano, ushauri na maelekezo wanayonipa katika kutekeleza kazi katika Wizara yetu ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwa kuanza niseme kwamba naunga mkono hoja hii ya Bajeti ya Wizara ya Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu hoja za Wabunge mbalimbali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ponsiano Nyami yeye alipenda kufahamu ujenzi wa maji wa mtiririko katika Mji wa Namanyere na pia kufahamu Namanyere kwa kutumia chanzo hicho cha maji ya kutoka katika chanzo kinachoitwa Kate.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa *program* ya maji ya usafi wa mazingira Vijijini unahusu Vijiji na Miji, hivyo Halmashauri za Wilaya zitoe kipaumbele kwenye maeneo hayo wakati wa kupendekeza miradi yao katika *program*. Namshauri Mheshimiwa Ponsiano Nyami ashirikiane na Halmashauri kutoa kipaumbele kuhakikisha kwamba Namanyere inapata maji haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Eustace Katagira, yeye aliuliza kuhusu kuimarisha huduma ya maji katika Mji wa Kayanga. Mji wa Kayanga umetengewa Shilingi milioni 50 kwa mwaka huu wa 2006/2007 kuanza kutekeleza shughuli za mradi wa maji kwa mwaka huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa George Lubeleje, yeye alitaka kufahamu kuhusu Serikali ilitumia vigezo gani katika kumpata Mkandarasi ambaye amepewa zabuni ya kuchimba miradi ya Miji midogo tisa. Wachimbaji hao, kazi ya uchimbaji wa visima kwenye Miji hiyo tisa iligawanywa katika makundi matatu na kutangazwa kwenye magazeti. Mkandarasi mmoja ndiye aliyeshinda kwenye makundi yote matatu, kwa hiyo ikambidi yeye apewe kwa sababu ndiye aliyekuwa na uwezo huo.

Pia, Mheshimiwa George Lubeleje alipenda kuomba kwamba dawa iwekwe kwenye maji Mjini Mpwapwa. Uwekaji wa dawa kwenye maji Mjini Mpwapwa unazingatiwa na tutahakikisha hiyo inafanyika.

Mheshimiwa Esther Nyawazwa aliulizia kuhusu ukarabati wa visima vya maji Wilayani Geita na kwamba vilisahauliwa kwa muda mrefu na sasa vimeachwa kabisa, vifanywe nini? Halmashauri ya Wilaya iviingize Vijiji hivi kwenye Awamu ya Pili ya

*Program* ya Taifa ya Maji na usafi wa mazingira na pia katika Vikao vya Halmashauri, ahakikishe kwamba hivyo vimepewa kipaumbele na pia aliomba kufahamu kwamba katika mradi mdogo wa Malya maji pia yatiwe dawa. Tunamjibu kwamba Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya itahakikisha kwamba maji ya mradi wa Malya yanawekwa dawa.

Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala yeye alipenda kufahamu uboreshaji wa miundombinu ya maji katika Tarafa za Misenyi na Kiziba. Vijiji vya Kashaba, Mwemage, Kenyana, Kideho na Bulembo vilivyoko katika Tarafa ya Misenye na Kijiji cha Ruzinga kilicho katika Tarafa ya Kiziba vimependekezwa kufanyiwa ukarabati wa miradi yake ya maji mwaka huu wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Dr. Luka Siyame alipendekeza kwamba Serikali iandae *inventory* ya pampu na visima vilivyoharibika vifanyiwe matengenezo. Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri itakusanya takwimu za miradi yote ya maji ikiwemo visima na pampu za maji ili vilivyoharibika viingizwe katika mpango wa matengenezo.

Pia Mheshimiwa Dr. Luka Siyame alipenda pia kufahamu kuhusu Serikali inasaidiaje upatikanaji wa maji ya kutosha katika Mji wa Tunduma pamoja Kijiji cha Mlowo na hivi ambavyo vilipewa ahadi na Rais. Katika mwaka huu wa fedha Wizara imetenga Shilingi milioni 20 kwa ajili ya Mji wa Tunduma kwa ajili ya kununua pampu ya kisima na mabomba yake. Pia, Halmashauri ya Mbozi inashauriwa kuingiza miradi hiyo kwenye *program* ya kitaifa ya maji na usafi wa mazingira Vijijini.

Mheshimiwa Dr. Festus Limbu aliuliza kuhusu ufungaji wa *float intake* katika mradi wa maji katika Mji wa Magu, ni lini wataalam wa maji watafunga *floating intake* hiyo? Mkandarasi anatarajiwa kufunga mashine hii mapema kabla ya mwisho wa mwezi huu wa Julai, 2006.

Mheshimiwa Michael Laizer, Mbunge wa Longido alipenda kufahamu kwamba mradi wa visima viwili vilivyochimbwa katika Vijiji vya Mundarara na Losingita unakamilishwa lini? Ukamilishwe. Kiasi cha Shilingi milioni 20 kilitumwa Wilayani kwa ajili ya Mradi wa Losingita mwaka 2005/2006 na zilipokelewa huko na pia kiasi cha Shilingi milioni 25 kimetengwa kwa mwaka huu 2006/2007 kwa ajili ya Mradi wa Mundarara.

Mheshimiwa Lazaro Nyalandu alitoa ushauri kwamba Wizara iangalie uwezekano wa kufanya upembuzi yakinifu kutoa maji Ziwa Victoria kuja Mji wa Dodoma na Mikoa ya Shinyanga, Tabora na Singida. Ushauri huo utafikiriwa na Wizara kwa kuzingatia kwamba Miji hiyo iko mbali na mradi huu, ni gharama kubwa, lakini ushauri umepokelewa lakini siyo ahadi kwamba itatekelezwa mpaka mambo mbalimbali yaangaliwe.

Mheshimiwa Ludovick Mwananzila aliulizia kuhusu Serikali ifufue miradi ya maji katika Vijiji vya Katuka, Chelengenya, Kisumba, Matanga, Mtimbwa, Kasense na Kanondo vilivyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga. Vijiji vya Katanga,

Mtimbwa, Kanondo na Mponda viko kwenye *program* ya maji safi ambayo inatekelezwa mwaka huu wa 2006/2007 na tunamshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba Vijiji ambavyo havikuwekwa mwaka huu ashirikiane na Halmashauri kuviwekea kipaumbele viingie kwenye awamu inayofuata.

Mheshimiwa Herbert Mntangi aliulizia kuhusu Serikali itatekeleza lini mradi wa Ubembe kwa Mhosi na pia Serikali itekeleze mradi wa Derema. Kiasi cha Shilingi milioni 80 kimetengwa mwaka huu 2006/2007 kwa ajili ya kuanzia Mradi wa Ubembe kwa Mhosi, lakini tunafahamu kwamba mradi huu gharama yake ni kubwa. Kwa hiyo, kila mwaka zitakuwa zinatengewa mpaka mradi utakapomalizika. Mradi wa Derema unaogharimu Shilingi bilioni 3.3 utatekelezwa fedha zitakapopatikana, kama tunavyofahamu sungura huyu ni mdogo.

Mheshimiwa Stephen Galinoma, alipendekeza kwamba uangaliwe uwezekano wa kujenga miradi ya Kiwere na Magulirwa, Halmashauri ya Wilaya inashauriwa kuingiza miradi hiyo miwili kwenye Program ya Taifa ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini.

Mheshimiwa Jacob Shibiliti aliulizia kuhusu wananchi wa Usagara kutoingizwa kwenye Bajeti ya mpango wa maji na usafi wa mazingira Vijijini. Ujenzi wa tangi la maji la Misasi utatekelezwa katika mpango wa maji na usafi wa mazingira Vijijini unaoanza mwaka huu 2006/2007 na pia mradi wa Usagara tayari umo kwenye *program* inayoanza mwaka huu 2006/2007 yote kwa ajili ya utekelezaji.

Mheshimiwa Felix Kijiko, anaelezea kuhusu hali mbaya ya maji katika Wilaya wa Kibondo. Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo inashauriwa kuingiza mradi wa maji ya Vijiji pamoja na Mji wa Kibondo katika mipango ya maendeleo, lakini pia hata hivyo na Wizara itachukua juhudi za kwenda kufanya utafiti ili kuweza kufahamu kina cha tatizo la maji ya Kibondo sawasawa ili tuongezee nguvu.

Mheshimiwa Bujiku Sakila ameongelea kuhusu uvunaji wa maji ya mvua kupitia mapaa ya nyumba, uendelezwaji katika Shule na Vituo vya Afya ili kuendeleza teknolojia hiyo kwa wananchi. Wizara kwa kushirikiana na wananchi, inaendelea kutoa mafunzo ya uvunaji wa maji ya mvua kwa mafundi binafsi katika ngazi ya Kata ili kuvuna maji ya mvua katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Eustace Katagira, aliomba Serikali ichimbe visima na kujenga mabwawa katika Jimbo la Kyerwa. Halmashauri inashauriwa kuweka kipaumbele katika kuweka mipango yake kwa kuingiza miradi mbalimbali ya Vijiji ikiwa ni pamoja na uchimbaji wa visima na ujenzi wa mabwawa. Hapo pia, napenda kuongezea kwamba, katika miradi hii ya Vijijini ndipo ambapo sisi Waheshimiwa Wabunge tuna nafasi kubwa ya kuweza kuhakikisha kwamba vipaumbele vya ahadi na kero zetu za maji zinapitia huko.

Kwa hiyo, ningependa kuwashauri Waheshimiwa Wabunge, kila mmoja wetu ahakikishe kwamba Vikao vya Halmashauri vinapokaa ndipo huko miradi hii inapendekezwa na kuletwa Wizarani na ni miradi ya aina zote mabwawa na visima.

Mheshimiwa Mwantumu Mahiza, alikuwa anaulizia kuhusu wataalam wa Wizara wakatembelee Wilaya ya Nkinga katika Vijiji mbalimbali ikiwa ni pamoja na Kijiji cha Moa. Ombi la kutembelewa na wataalam wa Wizara limepokelewa.

Mheshimiwa Danstan Mkapa, aliomba Serikali ichimbe visima virefu katika Wilaya ya Nanyumbu katika Vijiji vya Michinga, Likokona, Napacho na Nangomba. Tunamjibu kwamba, katika awamu ya kwanza ya *program* ya Maji Vijijini katika Wilaya ya Nanyumbu itahusisha Vijiji vya Chipuputa na Sengenye. Pia, Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na Halmashauri ya Wilaya katika kuchagua maeneo ya kipaumbele ili yaingizwe kwenye awamu ya pili kwa kufuatana na mahitaji aliyoyaelekeza hapa ikiwemo Vijiji vile ambavyo havijaingizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona muda unanipa mkono, lakini maswali yalikuwa ni mengi sana zaidi ya 80 na hata hivyo mengi tumeyajibu na mengine wakati Mheshimiwa Waziri atakapokuwa ana *wind-up* atayagusia mengine. Lakini kwa ujumla ni kwamba, maswali mbalimbali na ushauri mbalimbali tumeyapokea ukiwemo wa Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, ambaye aliomba visima virefu vichimbwe, tumeelekeza kwamba visima hivyo viingizwe.

Pia, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro yeye alikuwa anaomba kwamba Wilaya yake mpya ianze kujitegemea kwa kuchagua Vijiji vyake 10, lakini tumemshauri kwamba Wilaya mpya bado haina Watendaji. Kwa hali hiyo, ni kwamba, bado wataendelea kuhudumiwa na Wilaya Mama mpaka Watendaji watakapokamilika kwenye Wilaya yake, ndipo na wenyewe wataanza kushughulika moja kwa moja kwa kupendekeza na kuendeleza mambo ya kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, maswali yaliyobakia namwomba Mheshimiwa Waziri naye anisaidie kujibu. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Waziri, alishaunga mkono mwanzoni, alianza kusudi asisahau. Mheshimiwa Mtoa Hoja, Waziri wa Maji. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru sana tena kwa kunipa nafasi nyingine ya kuhitimisha hoja hii ambayo inaonekana ni hoja nyeti katika Bunge lako Tukufu na unyeti wake unatokana na wingi wa watu ambao wamechangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hii imechangiwa na watu 101, kati ya hao watu 27 wamechangia kwa kusema hoja zao na Waheshimiwa Wabunge kama 76 wamechangia kwa maandishi .

Kama alivyosema Naibu Waziri na ninamshukuru kwa kutoa majibu kwa baadhi ya hoja, ni kwamba, maandishi yote tuliyoyapokea tutaweka katika kumbukumbu ili tuwe tunayapitia na hata yale ambayo hatutayajibu hapa tutakuwa tunawasiliana na Wabunge wenye hoja hizo tunapokuwa tunahitaji maelezo zaidi. Hii maana yake ni kwamba

Wizara yangu uhusiano wake na Bunge hili unaendelea katika kusimamia utekelezaji. Kwa hiyo, hauwezi kuishia katika hoja tu, lakini tutaendelea kusoma majibu, kama kuna hoja ya kuuliza tutawasiliana na Mbunge aliyehoji, tutataka kupata maelezo zaidi ili tusaidiane naye katika kutafuta jibu la kudumu kwa tatizo la kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda kwanza niwatambue Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia. Mheshimiwa Idd Mohamed Azzan - Mbunge wa Kinondoni, kwa niaba ya Kamati ya Kilimo, Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe - Kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Capt. George Huruma Mkuchika - Mbunge wa Newala, Mheshimiwa Emmanuel Jumanne Luhahula - Mbunge wa Bukombe, Mheshimiwa George Malima Lubeleje – Mbunge wa Mpwapwa, Mheshimiwa Benedict Kiroya Losurutia - Mbunge wa Kiteto, Mheshimiwa Ernest Gakeya Mabina - Mbunge wa Geita, Mheshimiwa Fred Mpendazoe Tungu - Mbunge wa Kishapu, Mheshimiwa Herbert James Mntangi – Mbunge wa Muheza, Mheshimiwa Jacob Dalali Shibiliti – Mbunge wa Misungwi, Mheshimiwa Suleiman Omar Kumchaya - Mbunge wa Lulindi, Mheshimiwa Omar Shabani Kwaangw' - Mbunge wa Babati, Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto - Mbunge wa Kigoma Kaskazini, Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope – Mbunge wa Masasi, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer - Mbunge wa Longido na Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya - Mbunge wa Viti Maalum. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Balozi Hamis Suedi Kagasheki – Mbunge wa Bukoba Mjini, Mheshimiwa Felix Ntibenda Kijiko - Mbunge wa Muhambwe, Mheshimiwa Phares Kashemeza Kabuye – Mbunge wa Biharamulo Magharibi, Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Ibengwe Mongella – Mbunge wa Ukerewe, Mheshimiwa Halima James Mdee – Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Laus Omar Mhina – Mbunge wa Korogwe Vijijini na Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah - Mbunge wa Iramba Magharibi. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa George Boniface Simbachawene - Mbunge wa Kibakwe, Mheshimiwa Bujiku Philip Sakila – Mbunge wa Kwimba na Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi – Mbunge wa Mbozi Magharibi, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga - Mbunge wa Tabora Mjini, Mheshimiwa John Magale Shibuda - Mbunge wa Maswa na Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia - Mbunge wa Rufiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hao ndio waliochangia kwa kutoa maelezo hapa Bungeni, lakini vilevile tumepokea hoja na nitawaomba radhi kama katika hoja hizo nitashindwa kusoma jina lolote kwa sababu yalikuwa yanakuja kwa wingi mpaka ile *mail box* ilikuwa inapata matatizo katika kujua ni nani sasa ameleta na nani hajaleta.

Lakini ambazo tumezipokea ni kutoka kwa wafuatao: Tumepokea hoja za Mheshimiwa Balozi Abdi Hassan Mshangama, Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Eliatta Namdumpe Switi, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas Dewji, Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mheshimiwa Estherina Julio Kilasi, Mheshimiwa Dr. James Alex Msekela, Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele,

Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Prof. Peter Mahamudu Msolla, Mheshimiwa Jocob Dalali Shibiliti, Mheshimiwa Felix Ntibenda Kijiko, Mheshimiwa Grace Sindato Kiwelu, Mheshimiwa Abdul Jabiri Marombwa, Mheshimiwa Prof. Philemon Mikol Sarungi, Mheshimiwa Manju Salum Omar Msambya, Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia, Mheshimiwa Janeth Mourice Massaburi, Mheshimiwa Paschal Constantine Degera na Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki, Mheshimiwa Prof. Mark James Mwandosya, Mheshimiwa Elizabeth Nkunda Batenga, Mheshimiwa Dorah Herial Mushi, Mheshimiwa Tatu Musa Ntimizi, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, Mheshimiwa Bernadeta Kasabago Mushashu, Mheshimiwa Halima James Mdee na Mheshimiwa Joyce Nhamanilo Machimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengine nitawataja kabla sijafunga mjadala ili nipate muda wa kutosha kujibu hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika kujibu hoja itakuwa ni vigumu sana kumjibu kila Mbunge kwa sababu hoja hizi ni nyingi na zinahitaji muda wa kuzichambua na kuzitafutia majibu ya uhakika, lakini yapo mambo ya jumla ambayo ni lazima tuyaseme.

Moja ni hofu. Waheshimiwa Wabunge wamesema sana hoja hii na mimi nilikuwa najiuliza ni kwa nini Wabunge wengi wanaandika na ni kwa nini wengi wanasema, lakini baadaye nikakuta jibu lipo katika hotuba yangu katika ukurasa wa kwanza kabisa nilikuwa nimem-*quote* Rais katika hotuba yake aliyoitoa hapa Bungeni, ilisema, tatizo la maji ndicho kilio kikubwa cha Watanzania Mijini na Vijijini, ndiyo kero nambari *one*. Serikali za awamu zote zimefanya jitihada kubwa kukabiliana na tatizo hili. Serikali ya Awamu ya Nne inakusudia kulikabili tatizo hili kwa Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya. Nikagundua haya maneno Bunge hili kwa sababu linawawakilisha Watanzania, basi kilio cha Wabunge hapa ni kilio cha wananchi, nikaelewa kabisa kwamba hili ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hakuna Bajeti moja ya Wizara inaweza ku-*solve* matatizo yote. Haiwezekani kabisa, hata ahadi tulizozitoa katika Ilani, lazima zifanyiwe mchanganuo na ziwekwe katika *program* kwa muda wa miaka mitano inayokuja ili tujaribu kujibu hoja hizi na kilio hiki cha wananchi ambacho kinakuwa *reflected* katika Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Bajeti yetu ya mwaka huu wa 2006/2007 peke yake haiwezi na wapo Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia maeneo mengi sana, lakini nataka niseme kwamba Bajeti yetu ya fedha za ndani ambazo haziko *tied* kwa mradi maalum, maana zile za nje zinakuwa ziko *tied* kwa miradi maalum. Lakini hizi ambazo ndizo sungura tunayegawana ni Shilingi bilioni 77 na katika hizo Shilingi bilioni 77, Shilingi bilioni 52 tumezitoa kuendeleza ujenzi wa mradi wa Shinyanga kwenda

Kahama Mjini, kwa sababu tumerithi ule mradi kutoka Awamu ya Tatu na tuna *obligation* ya kuhakikisha tunaumaliza na tuna wakandarasi wako kazini ambao watamaliza mradi huu katika mwaka huu wa fedha. Tutakapomaliza tutakuwa bado wanatudai Shilingi bilioni 29 ili wakamilishe na tuagane nao mpaka kufika Shinyanga na Kamaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti hiyo maana yake nini? Maana yake ni kwamba ukiondoa Shilingi bilioni 52 utabaki na Shilingi bilioni 25 za kujibu matatizo yote yaliyoongelewa ndani ya Bunge lako Tukufu. Ni dhahiri kwamba isingewezekana kufanya. Hata hivyo, ukisoma hotuba yetu utaona tumejitahidi sana kufika kila mahali na *almost* kila Wilaya ya Tanzania, sasa kilio hiki tunaweza kukifanya namna gani? Kwa sababu kuna Waheshimiwa Wabunge wamehoji ikiwa ongezeko la *coverage* ya maji kwa mwaka 2005/2006 kwa Vijijini ni asilimia 0.2 na kwa Mjini ni asilimia moja, itawezekanaje tufikie asilimia 65 ifikapo mwaka 2010?

Hili ni swali zuri tu na mimi katika jibu langu nataka kuwatia moyo Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwamba kuanzia mwaka huu tunao mkakati ambao tukiusimamia vizuri, tutafika asilimia 65 ya maji Vijijini. Kwa sababu kwa kushirikiana na Benki ya Dunia, tunao mkopo wa gharama nafuu pamoja na Benki ya Maendeleo ya Afrika na Wahisani wengine kama Uholanzi na Ujerumani wapo tayari kuchangia ili tuweze kufikisha ile *program* tuliyoianza miaka miwili iliyopita Vijijini, ndio maana tumechukua Vijiji kumi kutoka kila Wilaya ya Tanzania. Ndio maana tunataka kutengeneza mpango huu kwa Vijiji 1100 kwa Tanzania nzima. Tukifanya hivyo mara tatu kabla ya uchaguzi wa mwaka 2010, tutakuwa tumevifikia Vijiji zaidi ya 3000 na nina hakika tutafika asilimia 65 na Chama kilichofanya hii jitihada kitashinda kwa kura nyingi ambayo haijapata kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka kuwaondoa wasiwasi kwa sababu tume-*program* lakini hiyo haitoshi. Nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba tumejidhatiti kusimamia jambo hili, sio kupanga tu, lakini hasa kusimamia. Wiki iliyopita Wizara yangu ilikuwa imekusudia kufanya Semina na Wabunge wote na nia yetu ilikuwa kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge juu ya *program* hii kubwa sana ambayo inafikisha huduma ya maji kwa mwananchi wa kawaida kabisa Kijijini. *Program* kubwa ambayo haijapata kufanyika kwa mara moja tangu tumepata uhuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme kwamba, Wizara yangu ipo tayari kushirikiana na Wabunge na Bunge hili kuona kwamba hakuna mtu atakayesimama mbele kuzuia *program* hii isifanikiwe. Tunayo mipango, tumewapa watu wanaitwa *consultants* ambao ndio wanaanza kazi ile ya kufanya *feasibility study* na kufanya *design* kabla hatujaweka *contractors* wa kusimamia kazi hiyo na mimi wiki ijayo nitakutana na wale *consultants* Dar es Salaam kuwaambia kwamba, ambaye yuko tayari kuufanya mpango huu ufanikiwe anaendelea, ambaye atakuwa kazi yake ni kuuchelewesha anatoka. Hilo jambo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, tumewaambia wataalam na ninasema wananisikiliza, tunatengeneza *action plan* ya kusimamia utekelezaji wa kazi hii

kuhakikisha kwamba kila baada ya miezi mitatu kuna jambo linafanyika mpaka kufika mwisho wa *financial year*. Tunajua kwamba *World Bank* ina *bureaucracy,* tunajua inaweza kutupa fedha hizi baada ya Septemba, lakini pamoja na hiyo, tutakuwa na *action plan* ambayo tutaeleza lini tunafanya nini chini ya mpango huo ili kuhakikisha kwamba kweli tunapata matokeo na matokeo ni wananchi kupata maji ya kunywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Waheshimiwa Wabunge walikuwa wamesema, tutajuaje asilimia ngapi kwa mwaka huu na asilimia ngapi kwa mwaka kesho? Tutakuja Bungeni hapa kueleza asilimia kila mwaka. Bajeti ikifika tutawaeleza kama tumekwenda mbele zaidi kuliko mwaka jana, kwa sababu hatukuwa na *investment* na huwezi kupata asilimia kubwa bila ku-*invest.* Lazima u-*invest*! Sasa mwaka huu tuna-*invest* kwa fedha hizo za *World Bank.* Kwa hiyo, tuna matumaini ya kwamba *output* itakuwa kubwa zaidi kuliko huko tulikotoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo ndilo jambo la kwanza kabisa ambalo nilitaka kuliweka wazi ili ku-*boost morale* kwa sababu hakuna kupigana vita bila *morale* na mimi nadhani hayo maneno yatasaidia ku-*boost morale* ili sisi wote tuwe jeshi, tupambane, tuhakikishe watu wetu wanapata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, ningependa sasa kutumia nafasi hii kuishukuru Kamati ya Kilimo na Ardhi ambayo imetushauri vizuri sana. Nataka kuwahakikishia kwamba ushauri wao waliotupa tutauzingatia na tutaufanyia kazi. Wametuambia juu ya uhaba wa wataalam Wilayani, tunautafutia ufumbuzi kupata wataalam maana huwezi kufanikiwa bila kuwa na wataalam na tutashirikiana na TAMISEMI kuona kuwa wametueleza juu ya ankara katika maji ya Mjini, tunaagiza mamlaka zile na zimeanza kuchukua hatua za kuwa na *system* ya *computer* ambayo inatoa zile ankara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumeamua kwamba, tutaleta sheria Bungeni kuanzia Mfuko wa Maji maana hii ni kazi kubwa kabisa. Lazima tuwe na Mfuko wa Maji unaochangiwa na kila mtu anayetaka kutusaidia ili tuweze kushinda vita ya kuwapa wananchi maji na kupambana na kero namba moja kama ilivyokuwa katika maelezo ya Rais. Tunasimamia kwa nguvu kabisa uharibifu wa vyanzo vya maji kwa sababu bila kufanya hivyo hatutafanikiwa, maana maji yatakuwa yanapungua kila siku. Kwa hiyo, tutasimamia na usimamizi huu unahusisha Mikoa yote, Wilaya zote, Wizara ya Maji, wenzetu wa Maliasili na kila mtu ambaye anaipenda Tanzania atasimamia kuhakikisha kwamba uharibifu wa mazingira unadhibitiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninayo mambo machache ya kujibu na hasa yaliyotoka kwa rafiki zangu wa Kambi ya Upinzani. Mimi naheshimu sana mawazo tofauti kwa sababu kweli usipoyaheshimu utakuwa wewe unataka mawazo yako tu. Kwa hiyo, naheshimu mawazo tofauti, lakini ni vizuri mawazo tofauti yenyewe yawe ya msingi na sio ya kukoleza Baraza. Maana kukoleza Baraza tu haiwezi kutusaidia sana. Sasa yapo mambo yaliyozungumzwa na Msemaji wa Upinzani, namheshimu sana, tena ni Mbunge kutoka Mkoani kwangu, naheshimiana naye sana ingawa huwa namsaidia sana kueleza tofauti ya Chama kinachotawala na cha Upinzani, tena huwa namsaidia kwa

sababu nina uzoefu wa vyote. Nimewahi kuwa Mbunge wa Chama cha Upinzani, kwa hiyo, namsaidia kuelewa tofauti kati ya Chama cha Upinzani na Serikali. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi Mheshimiwa Mbunge alisema MKUKUTA ni sera ya Chama gani? Mimi nikashangaa, ehee! MKUKUTA ni neno lililofupishwa, maana yake ni Mpango wa Kufufua Uchumi na Kuondoa Umaskini. Ukisoma sera zote za CCM, kuna kuinua uchumi na kuondoa umaskini. Kwa hiyo, ni sera ya CCM. Lakini haizuiliki kwa Upinzani kuunga mkono sera ya CCM, ni sawa. Kwa sababu Upinzani sio shari, unapinga kinachowezekana kupingwa na unaunga mkono kinachoungwa mkono. Ndio maana wanasema *the royal opposition and royal government*, tumeitoa kule kwa wakubwa wa Uingereza, zote ni *royal* maana ni nchi yetu wote.

Kwa hiyo, unatoa mawazo, unapinga pale unapoona kweli kupinga kunasaidia nchi hii. Ukiona hakusaidii unaunga mkono. Ndio Upinzani huo wa kiungwana. Lakini sasa huu wa kugombagomba, tunazungumzia maji, wewe unazungumza mauaji Tarime, mimi sielewi. Unazungumzia mauaji Tarime wakati tunajadili maji, hiyo ni *confusion*! Huo sio Upinzani mzuri. Unazungumza mauaji Tarime wakati unajadili Usalama wa Raia. Sisi tunaongelea maji, halafu tukujibu tena masuala ya mauaji, kwani mauaji yale yametokana na mafuriko? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Msemaji wa Upinzani amehoji juu ya *City Water*. Sasa nataka nimwambie, kwanza *City Water* hatukuwa tume-*privatize,* tulikodisha. Miundombinu ya maji ya Dar es Salaam na nia ilikuwa njema tu kwamba, tunahitaji Menejimenti inayoweza kukodi halafu i-*perform*. Sasa ukikodisha na mwenye kukodi akakataa kukulipa pango utafanyaje? Unaendelea naye tu mpaka ufariki! Itabidi umwondoe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Msemaji wa Upinzani anahoji kwamba kwa kumwondoa, tumevuruga huduma. Sio kweli! Huyu alifeli, *he failed completely* na nitawapa *figure*. Alisema atakuwa *expert* wa kukusanya fedha na katika hizo fedha ambazo alikuwa akusanye alikuwa ailipe *DAWASA* ambayo ndio *owners* wa *infrastructure* kwa niaba ya Serikali. Alikuwa anakusanya Shilingi milion 950. Hawa *DAWASCO* sasa wanakusanya Shilingi bilioni moja na nusu kwa mwezi na maneno mengine. Kwa hiyo, alishindwa kulipa *rent*. Kwa hiyo, mtu akipanga nyumba yako na akashindwa kulipa *rent,* tena siku hizi *National Housing* wanawatoa bila huruma. Ni mpangaji mbaya huyo! Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu amesema kuna mikopo iliyokuwa ya *City Water.* Sio kweli. Mikopo tuliyonayo inatoka *World Bank,* inatoka *European Investment Bank* na *African Development Bank* na mikopo hiyo ndiyo inayokarabati huduma za Jiji la Dar es Salaam kwa sasa, *infrastructure* na mabomba yale yote mnayoona tunaweka pale ni mkopo huo. Kwa hiyo, wala hatukukopeshwa na *City Water*, sisi tumekopa kwenye vyombo vya fedha. Kwa hiyo, nilitaka rafiki yangu ajue kwamba haya ni mambo ya kujifunza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Msemaji Mkuu wa Upinzani aliendelea kusema, mambo mengine pengine nitamsamehe sana. Baadaye aligeuka, badala ya kuwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani akaamua kuwa Mbunge wa Tarime, akaacha kabisa mambo ya Upinzani, akasema ananipongeza kwa kwenda Tarime. Lakini hakunipongeza kwa kwenda Arusha au Newala. Sasa huu Upinzani ni wa Tarime tu? Maana nimekwenda kila mahali, Mikoa kama kumi na moja. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu anasema Tarime katika Wilaya nzima hakuna Kijiji chenye maji. Mimi namwambia haya ni mambo ya kukoleza Baraza. Hadi mwezi Desemba, 2005, huduma ya maji katika Wilaya ya Tarime ilikuwa asilimia 42.93 kutokana na miradi iliyopo. Wilaya ya Tarime ina miradi ya maji mikubwa 16 na kati ya hiyo, mitano ndio inayofanya kazi ambayo ni Nyanduga, Nyasoko, Ingiri Juu, Shirati na Kasangura Nyamwaga. Aidha, vipo visima vya asili 78 ambavyo vimetengenezwa na kuboreshwa ambavyo vinatoa huduma kwa wananchi wa Tarime. Sasa anasema hata Kijiji kimoja hakuna! Hiyo ni kukoleza Baraza. Sasa tuwe *serious,* huwezi kusema maneno tu ambayo hayana *figures*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani alizungumzia sana mambo ya Wilaya za Sikonge, Mkuranga na Igunga. Lakini alitumia taarifa fulani hapo ambayo ilikuwa inafanya kazi wakati wa sensa ya mwaka 2002. Lakini watu wote ambao wamesoma Shule wanajua kwamba *sample* ikiwa ndogo unapata *results* tofauti, ukifanya *sample* kubwa unapata *results* tofauti. Kwa hiyo, nadhani *sample* ilikuwa *wrong* na kwa sababu nadhani yalikuwa ni mambo ya sensa, wanahoji watu wachache tu, sio watu wengi sana. Halafu vile vile sisi tunajua kwamba huko Tabora kuna matatizo makubwa ya maji, tunafahamu wala hatuna haja ya kubishabisha juu ya hilo na matatizo makubwa ya Tabora yanatokana na uhaba wa vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekwenda Tabora, hata pale Mjini kuna bwawa moja tu linaitwa Igombe ambalo ndilo linatoa huduma ya maji na halitoshi. Nami nimewaambia tuna mpango wa Swiss pale wa kusaidia kuboresha huduma ya maji Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumewaambia watumie hiyo fedha watafute chanzo kingine cha maji ambayo ni pamoja na maji chini ya ardhi kwa sababu Dodoma walisema haina maji. Lakini sasa hivi Dodoma yote inahudumiwa na maji ya chini ya ardhi. Kwa hiyo, kinachotakiwa ni kufanya utafiti zaidi. Lakini ni kweli kuna *problem* Igunga, tumechimba visima hamsini ambavyo haviko kwenye ripoti ya yule Bwana. Kati ya hivyo, 45 tumepata maji, vitano vimekosa kwa sababu inategemea unachimba wapi.

Kwa hiyo, tuna *problem* Tabora ya kupata *source,* ndio maana tunatumia zaidi mabwawa. Hata pale Nzega tunatumia zaidi bwawa kuliko maji ya chini kwa sababu ni *problem.* Lakini nataka kuwahakikishia wananchi wa Tabora kwamba tunafanya kila linalowezekana kuinua kiwango cha maji katika Mkoa wa Tabora na nawaomba wananchi wa Tabora matatizo yao yasitumiwe kisiasa kutafuta umaarufu katika Bunge. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua mambo yakiuma, lazima utasikitika! Mambo yakiwa makali sana lazima utasikitika! Maana safari moja mzee Nyerere alituambia: "Wazungu hawa ni watu, maana wakipigwa wanalia." *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la watumiaji wa maji kule Karatu na hili limeongelewa vile vile na Mheshimiwa Mbunge wa Karatu. Mimi nataka kumhakikishia kwamba tuko *serious* na *serious issues*. Sasa Bodi ya Maji ya Karatu tuivunje, imekosa nini? Iendelee na kazi yake! Sisi hatuna *problem* na hiyo Bodi, imekuwa *registered,* ni ya wananchi wa Karatu na waendelee kuwapa wananchi wa Karatu huduma ya maji. Kwa hiyo, wala siitolei maelezo mengi kwa sababu mimi sioni kama ni *serious problem* hapa, maana angalau wamefurahi maana mapigo yalikuwa makali kidogo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa ningependa kuzungumzia suala la maji Dar es Salaam. Wapo Waheshimiwa Wabunge wametuuliza juu ya suala la maji Dar es Salaam, wengine kwa maandishi, wengine kwa kusema. Dar es Salaam bado tuna *problem* ya maji, lakini hatua tunazochukua zinatuelekeza katika kutafuta jibu na huwezi kulipata hilo jibu kwa muda mfupi sana. Sasa hivi tunashughulika na ukarabati kwa sababu miundombinu ya Dar es Salaam ilikuwa imeharibika sana. Kwa hiyo, hata kama uki-*pump* maji zaidi, lazima yaingie katika bomba ambalo inayakubali, ambalo haliwezi kupasuka. Kwa hiyo, tunaimarisha mabomba yanayotoka Ruvu Chini kuja Dar es Salaam. Tunaimarisha mabomba yanayotoka Ruvu Juu kuja Dar es Salaam, tunaimarisha miundombinu ya Dar es Salaam ili maji yaweze kuwafikia wanywaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefanya kazi moja, tumeimarisha usukumaji wa maji kutoka Ruvu Juu kama hatua ya muda mfupi ya kupunguza *problem*, imetusaidia sana kwa sababu wananchi wa Ubungo, Tabata na wa njia hiyo inayotoka Ruvu Juu kuja Dar es Salaam walikuwa hawapati maji kabisa. Sasa bado hayatoshi kwa sababu *capacity* yetu bado ni *eighteen millions gallons,* lakini sasa angalau tuna *constant supply* na tunatoa kwa mgao lakini wanajua nasaha na siku ambayo maji yatafika, ndio maana huoni vile vibuyu vya Dar es Salaam, yale madumu hayaonekani kwa sababu tumefanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajaribu ku-*manage* na unajua bidhaa inapokuwa kidogo na mahitaji ni makubwa, siku zote kunakuwa na matatizo ya *supply* kwa sababu una-*supply a bigger demand* kuliko *supply* yako. Kwa hiyo, tunajitahidi kuboresha huduma za Mji wa Dar es Salaam ili tuhakikishe kwamba tunapata maji na wakati ule ule tunatafuta *source* nyingine ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi Wizara yangu iliwatuma wataalam kufanya utafiti juu ya uwezekano wa kufanya Ruvu Chini iweze kuingiza maji mengi zaidi Dar es Salaam kuliko inavyofanya sasa. Sasa hivi tunaingiza galoni milioni arobaini kwa siku. Hata hivyo, tulijiuliza, hivi haiwezekani kufanya marekebisho kidogo halafu tukaweza ku-*pump* galoni milioni sitini? Tumefanya utafiti, umekuja sahihi kwamba, tunahitaji kurekebisha mfumo wetu wa maji Ruvu Chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji kuweka bomba jipya kilomita 15 ili kupunguza ile nguvu inayotokana na *pumping* ya lita nyingi zaidi za maji kuliko ilivyo hivi sasa. Halafu maji yale yanaweza ku-*serve* eneo lile lote la Tegeta na maeneo yale na kiasi kikubwa cha maji yakafika kwenye matenki ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambayo ndio yanahudumia Mji wa Dar es Salaam kinachotupa matatizo. Ni *bill* ya kufanya kazi hiyo maana maji ni ghali tunaambiwa *thirty million dollars*. Sasa tupo katika kuzitafuta maana lazima watu wanywe maji. Tutatafuta popote pale panapowezekana kuzipata tukizipata itatuchukua *fifteen months* kuongeza *capacity* ya maji yanayoingia Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ndio mambo tunayoyafanya. Tunajaribu kuchimba visima vikubwa sana vitatu ili maji yakipatikana tuyaingize katika *system* ya Dar es Salaam ili tuongeze kiwango cha maji yanayoingia Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafikiria kuchimba bwawa kule Morogoro ili tuwe na *constant supply* kwa sababu unapotokea wakati wa ukame Dar es Salaam inakuwa na matatizo makubwa sana ya maji. Kwa hiyo, tunafanya hivyo kama njia moja ya kuhakikisha kwamba maji yanapatikana. Baada ya yote hayo, tutakuja kuona kama kuna umuhimu tena wa kwenda Rufiji na ikionekana umuhimu upo, hiyo itakuwa ni hatua yetu ya siku za mbele, lakini kwanza sasa hivi lazima tutibu matatizo ya upungufu wa maji katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wa Kishapu na rafiki yangu Shibiliti, Mbunge wa Misungwi, walizungumzia juu ya Vijiji ambavyo vimeachwa kupewa maji katika ule mradi wa njia kuu inayotoka Luhelele kuja Shinyanga. Tumeagiza wataalam waende watazame vile Vijiji ambavyo vipo karibu. Makubaliano ya awali ni kwamba visizidi kilomita tano kutoka kwenye bomba. Kwa hiyo, kama kuna Vijiji ambavyo vipo karibu *within five kilometres,* basi hivyo vifanyiwe upembuzi yakinifu ili tuone namna tutakavyoweza kuviingiza kwa sababu shabaha ya mpango wenyewe ni ku-*solve problem* ya maji. Kwa hiyo, kama *problem* inaweza kuwa *solved* na hiyo *system* tunaitumia ku-*solve problem,* kwa hiyo, tumesikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo hoja nyingine kali kidogo ambazo lazima tuzieleze kidogo. Rafiki yangu Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti amekuwa mkali kidogo juu ya Misungwi, nami namwelewa kabisa kwa sababu Misungwi ni *problem* kweli! Hakuna maji pale! Mimi nimewahi kupita hapo, Mkutano ukakutanika ghafla tu baada ya kusikia Waziri wa Maji anakuja. Ni *problem!* Wanafikiri labda mimi natembea nayo. Kwa hiyo, pale ni *problem!* Tuna bwawa na linakauka, lakini tulipeleka Wafaransa kwenda kufanya utafiti, wamefanya utafiti ule halafu wamekuja na *bill* ya *Euro* tisini na tano milioni, lakini wanatuambia wao watatupa milioni 7.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa *bill* ya Misungwi peke yake ni kumi na tano na hakuna miundombinu. Kwa hiyo, hata ungeziweka zote, Misungwi usingepata *output* na mipango ilikuwa imefanywa, walikuwa wame-*study* Bukoba na Musoma pamoja, ndio ilikuwa *bill,* siyo ya Misungwi peke yake. Ni ya Miji yote mitatu. Sasa kwa sababu Musoma na Misungwi na Bukoba kuna matatizo vile vile ya kurekebisha miundombinu, ikaonekana zile fedha zinaweza kufanya kazi ya kurekebisha miundombinu tu na sio

kufanya kazi ya maana. Lakini tukabaki na deni la kutafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza mradi wa Misungwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunazungumza na Wahisani, wala mimi sijasema tumepata pesa, lakini tumezungumza na *Millennia Challenge Population* ya Marekani wala sio siri, maana tumezungumza nao na wameonyesha *interest*. Tena kusema kweli wametuambia miradi ya maji wanaipa umuhimu mkubwa kwa sababu tuliwaeleza, kwa nini maji ni muhimu kwa kuondoa umaskini na mimi nilikwenda Washington, nikawaeleza vizuri waelewe, maana umaskini kama hujaujua sana, utaujua ukielezwa vizuri na mtu anayeujua. Nikawaeleza, Wazungu wale walielewa kabisa, ndio maana wanashabikia sana miradi. Lakini walitupa *conditions*, walituambia ni lazima tuwe na miradi ambayo imefanyiwa *feasibility study* ili waweze ku-*consider*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumewapa miradi ambayo imefanyiwa *feasibility study* na mmoja ni wa Misungwi ambao *feasibility study* yake ilifanywa na Wafaransa. Sasa rafiki yangu Mheshimiwa Mbunge pale alikuwa anasema hawa Mawaziri wanakuja hapa, kila mtu anasema *Millennia Challenge*, sasa *Millennia Challenge* si *donors* kama *donor* mwingine yeyote! Kama tumezungumza naye, si tumezungumza naye na *donors* hawa si wanazungumza na Serikali! Sasa kama Mheshimiwa Zitto anapatapata habari hivi sasa, labda anaweza kuongezea habari na hizi ninazompa kwamba tunazungumza nao na wameonyesha kwamba wana *interest* ya kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani itakuwa vigumu sana kuweza kujibu kila hoja. Lakini ningependa kutumia nafasi hii kueleza kidogo juu ya *problem* ya mradi wa Geita na Mbwinji – Masasi, kuna *problem* ya maji tena inakuwa kubwa zaidi kutokana na watu wengi kuhamia pale kwa sababu ya uchimbaji wa madini. Lakini ili tuweze kuchimba maji Geita, tunahitaji Shilingi bilioni 18. Kwa hiyo, tunao Mradi wa Geita na tunautafutia fedha kama ilivyo Misungwi. Tukizipata tutatekeleza mradi ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa Mbwinji, ule wa rafiki yangu, Mheshimiwa Mrope kule Masasi, Mheshimiwa Rais ametusaidia sana kuzungumza na Benki ya Kiarabu ya Maendeleo kwa Afrika *(BADEA)* na nataka kuwahakikishia kwamba *BADEA* wameichukua hii, mimi nimeongea nao na wameichukua *seriously,* wanaipa *priority* na hiyo ni pamoja na mradi katika eneo la Same, Same ile ya tambarare. Wiki hii baada ya Bajeti, tunatuma wataalam kwenda Same kufanya utafiti wa awali ili tupate habari za kuwapelekea *BADEA* watusaidie kupata fedha za kujibu *problem* ya Same ambayo wote mnajua ni mahali *dry* kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nimesema, kuna watu wengine waliniandikia *rough*, nikawa sikuwataja. Nataka kuongeza Mheshimiwa William Ngeleja, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mheshimiwa Mgana Msindai na Mheshimiwa Dr. Maua Daftari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, rafiki yangu Msindai alikuwa amezungumzia mambo ya *windmill,* sijui yupo au ametoka! Nataka kumhakikishia *windmill* atapata, tumezi-*incorporate* kwenye mradi ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka kuwaambia Waheshimiwa Wabunge kwamba hata wale ambao maelezo yao sikuyajibu ni kwa sababu ya muda, tunaweza wakati wowote tukawasiliana juu ya matatizo hayo kwa sababu Wizara hii ni sehemu ya Bunge hili katika kutekeleza kazi ambayo tumepewa. Kwa hiyo, hakuna kusema huyu anafanyaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nimalizie tu kwa kusema kwamba, kulikuwa na hoja imetolewa hapa kwamba katika kitabu hiki, jedwali la tatu kuna fedha pale ambazo hazijulikani imekuwaje. Sasa mimi nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba, fedha hizo mnazoziuliza Shilingi bilioni 9.6 hazipiti katika fungu la 49 la Wizara ya Maji. Ile ni ruzuku ya Serikali ambayo inakwenda kwenye Halmashauri za Wilaya na fedha zile zilikwishakuwa *voted* wakati wa Wizara ya TAMISEMI, Bunge limekwishaziidhinisha. Sisi Wizara ya Maji kwa sababu zinatuhusu ni za maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliandika hili ili tuwaonyeshe Waheshimiwa Wabunge kwamba, kuna fedha zimekwenda kule ili mzifuatilie. Hata za Bunda sikuzijua na mimi nimezikuta humu. Wala Wizara yangu haikuhusika hata kidogo kufanya *allocation.* Ni Halmashauri za Wilaya zinaomba Hazina na zinakwenda na kesi zake. Nimewauliza Hazina *how did it come*? Kwa sababu mimi ni Mtanzania na nchi yetu ni moja. Lazima tutoe huduma kwa Watanzania na wala mimi siwezi kutumia nafasi yangu ya Uwaziri kuwapa Bunda zaidi kuliko wanavyostahili Watanzania wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *record* yangu ni *very clean* na Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru ni shahidi wangu, ndio nimewahi kuwa Waziri wa CCM huko nyuma sijawahi kuwa na tabia ya namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka wajue ni kwamba wananchi wa Bunda nao wana haki, lakini maana msije mkawanyonga kwa sababu Mbunge wao ni Waziri wa Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**FUNGU 49 – WIZARA YA MAJI**

**NAIBU SPIKA:** Kama tulivyokubaliana, wale watakaokuwa na hoja wawe na uhakika na vifungu vinavyohusika.

Kifungu cha 1001 – *Administration and*

*General* ... ... ... ... ... ... Sh. 3,666,751,500/=

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuzungumzia *programme 10, Sub-Vote 1001 Administration and General.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Ningependa kuzungumzia machache kuhusiana na majibu ya Mheshimiwa Waziri ambayo kwa ujumla yamesikika. Lakini nilitaka kuzungumzia jinsi ambavyo amesema kwamba mimi nilizungumzia mauaji badala ya maji.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, Spika ame-*rule out* kwa sababu tuna kesi nayo. Endelea kwa mambo mengine. Tuna kesi nalo hilo. Mheshimiwa Mbunge naomba ukae chini. Nasema hili tunayo kesi yake tarehe 17 Julai, 2006, utaleta uthibitisho. Sasa hakuna sababu ya kumjibu Mheshimiwa Waziri, ameisemea kama wewe unavyosema, lakini wewe una kesi. Kwa hiyo, naomba tuendelee kwa suala lingine. *(Makofi)*

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *record* imewekwa sawa, ila ningependa vilevile kuzungumza kwamba sija-*focus* kwa Jimbo la Tarime peke yake. Nimezungumza katika hotuba yangu, kama Mheshimiwa Waziri aliisoma vizuri, nimeongelea Tanzania nzima na kuonyesha *water resources* ambazo zipo katika Tanzania na *failure* ya Serikali kuweza kuwa na mkakati wa jumla ambao ungeweza kutuwezesha kupata maji. Hilo nimelizungumzia. Nadhani hao wanaojaribu kuzungumza wanavunja vifungu hapa, maana yake nimeruhusiwa. Unaweza uka-*challenge* baadaye ukitaka.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chacha Wangwe naomba ukae.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia kifungu namba 55(1), ulitoa maelezo kabla kwamba Mbunge yeyote anayetaka kutoa hoja yake aelekee katika ile hoja ambayo inahusika. Sasa naomba kupata maelezo, Mheshimiwa Mbunge ni jambo gani ambalo anazuia katika kifungu hiki cha 1001? Naona anazungumzia mambo ya maji na kwenye kifungu hiki hakuna mambo ya maji. Naomba mwongozo wako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, hoja yako ni ya kweli kwa sababu tunapofikia wakati wa Kamati ya Bunge Zima ikishughulikia *Finance,* tunasema ni kifungu cha 81(2)(a): "Katika Kamati ya Matumizi Mwenyekiti atawahoji Wabunge kuhusu kifungu kimoja kimoja cha Makadirio ya Matumizi ya mwaka na kila kifungu cha Makadirio ya Matumizi kitaafikiwa peke yake isipokuwa kwa Makadirio ya Mikoa na Makadirio mengineyo." Sasa, kwa maana hiyo, mimi nahoji vifungu. Sasa tukianza kuzungumza Waziri alisema na alichosema, nafikiri hatuendi sawasawa. Kwa sababu sasa tunapitisha fedha, hatupitishi maneno yaliyotokea wakati mwingine. Mheshimiwa Chacha Wangwe.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sikubaliani na nazuia Shilingi ya Waziri kwa sababu hiki kifungu kinazungumzia mambo ya *Administration and General,* wala siyo sera. Kwa hiyo, kuna njama ya kujaribu kuni-*harass* hapa ili nisiweze kuzungumza. Lakini haya tumeyazoea na tutaendelea nayo hivyo hivyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, toa Shilingi na eleza hoja yako sisi tukusikilize, halafu tufanye uamuzi, ndivyo tunavyofanya. Unatoa hoja, sisi wote tutakusikiliza. Halafu nitawahoji Wabunge wote. Mheshimiwa Chacha Wangwe naomba ukae.

Mheshimiwa Chacha Wangwe, ni hivi , unapotoa Shilingi, inakupa nafasi wewe ya uhuru kabisa kueleza hoja ambayo sisi wote sasa tumeacha mengine yote tunakusikiliza wewe tu na hatuendi kokote mpaka nitakapohoji Wabunge kuhusu kifungu ulichochukua Shilingi. Kama Wabunge wanashinda kwa kukukubaliana nawe, basi tena, tutakwambia tutakuwa tunakwenda bila Shilingi moja. Kama Wabunge watakupinga, basi tunaendelea na biashara. Sasa umetoa Shilingi, endelea na toa hoja siyo maneno tu. Toa hoja. *(Makofi)*

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba Serikali itueleze kwa niaba ya wananchi kwamba fedha ambazo imekuwa ikizitumia kwa ajili ya kuwaletea Watanzania maji tangu mwaka 1961, Chama hicho hicho kikiwa madarakani, ni ngapi na zilitumikaje na kwa nini wananchi wa Tanzania hawana maji mpaka leo? Nadhani hiyo ni hoja ya msingi, kwa sababu Chama hicho kiko madarakani, Serikali hiyo hiyo na watu wale wale. Mpaka dakika hii hata hii Bajeti ya sasa haijatupa mpango unaotuonyesha jinsi kila Mtanzania atakavyopata maji.

Kwa hiyo, ningependa kujua kwamba ni kiwango gani cha fedha ambacho kimetumika na kimetumika vipi hadi wananchi wakakosa maji kwa miaka hiyo yote 45? Sasa hayo madeni ambayo yametokana na fedha hizo hizo ambazo wamekuwa wakitumia na mpaka sasa yapo yanatarajiwa kulipwa na Watanzania, yatalipwaje? Hiyo ndiyo hoja yangu ya msingi ya kutoa Shilingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, ahsante. Mheshimiwa Waziri, maelezo. Mkumbuke hii hatu-*debate,* akishajibu tunaendelea na kazi. Kifungu cha 82(3).

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama hapa kujibu hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Chacha Wangwe. Kwanza, labda nianze kwa kusema kwamba, maendeleo sio lelemama. Maendeleo ni kazi na sio kitu ambacho unaweza ukasema unaweza ukafanya mambo kwa mara moja yakawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu tumejitawala mwaka 1961, jamii ya Watanzania ilikuwa milioni tisa. Leo Watanzania ni milioni 36. Kwa hiyo, hata ungelikuwa unataka kuwapa maji wote, bado wangezaliwa wengine wakayadai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiondoa hilo, hivi sasa asilimia 53.7 ya Watanzania wanapata maji na asilimia 74 ya Watanzania wanaoishi Mijini wanapata maji, tena hiyo ni *average*. Ukienda Arusha ni asilimia 90, ukienda Moshi Mjini ni asilimia 95, ukienda Tanga inakaribia asilimia 100 na Dodoma hapa maji ni mengi kuliko mahitaji. Bado kuna *invest* kubwa katika Miji mikubwa kama Mwanza, kama Mbeya ukiondoa mradi wa bilioni 193 wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda Shinyanga na Kahama. Maendeleo sio lelemama. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge kwa sababu tunaanza, nitawasomea kifungu cha 81(2)(c), kinasema: "Hali kadhalika Mbunge yeyote aweza kutoa hoja isiyokuwa na mjadala ya kupunguza Shilingi moja katika kifungu chochote cha fungu hilo. Madhumuni halisi ya hoja ya aina hiyo ni kumwezesha Mbunge aliyetoa, aweze kueleza kutoridhika kwake na utekelezaji wa jambo fulani mahsusi ambalo dhahiri linahusika na kifungu hicho. Hoja hiyo itaamuliwa bila mjadala wowote. Lakini Waziri anayehusika atapewa nafasi ya kutoa majibu yake kwa hoja hiyo na endapo hoja itakubaliwa, basi kifungu kinachohusika kitakuwa kimepitishwa kikiwa na upungufu huo wa Shilingi moja."

Waheshimiwa Wabunge, sasa nawahoji, wanaoafiki kupunguzwa kwa Shilingi moja aliyosema Mheshimiwa Chacha Wangwe.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Hoja ya kupunguza Shilingi kwenye Makadirio ya Wizara ya Maji ilikataliwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi niko katika kifungu hicho hicho, *Administration and General* katika *Policy*. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, ukurasa wa 24 kuna programu ya Taifa ya Maji na Usafi wa Mazingira ambayo sasa imetapakaa katika nchi nzima.

Baada ya majaribio ya Wilaya ambapo Kiteto ilikuwemo, lakini katika mradi huu kulikuwa na *component* ya kupeleka maji katika Miji midogo ambayo ni Igunga, Kiomboi, Kondoa, Kongwa na Kibaya ilikuwepo na ushahidi ni aliyekuwa Waziri wa Maji wakati huo ambaye ni Waziri Mkuu sasa hivi. Halafu ushahidi mwingine ni *Engineer* Mwaka, Lwakabare ambao ni wataalam katika Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachouliza, hapa kulikuwepo na migongano ya sera, wakati huo Mji wa Kibaya ulikuwa unafanyiwa *feasibility studies* na *SIDA* Sweden. Sasa hawapo *SIDA* Sweden wala hawapo Benki ya Dunia. Mji wa Kibaya sielewi sasa umesimama wapi kwa sababu ya migongano ya Sera. Naomba Mheshimiwa Waziri atuhakikishie kwamba Mji wa Kibaya unashughulikiwa vipi sasa na *SIDA* Sweden? Maana yake sioni kama Benki ya Dunia ipo katika hotuba yake!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo ilikuwa tu hoja yangu, nijibiwe kwamba tuko wapi? Ndiyo maana nimekuwa katika kifungu hiki kwa sababu siyo *rural* wala siyo *urban*. Imekuwa mchanganyiko, *in general* na ni Shilingi ya Waziri.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Benedict Losurutia kwa kuuliza, alikuwa ametuandikia kuhusu hoja hii. Tulikuwa na majibu, lakini muda haukutosha kumjibu. Lakini nataka kumhakikishia kwamba iko Miji midogo 12 ambayo itafanyiwa upembuzi yakinifu na Benki ya Dunia kuanzia mwaka huu wa fedha na Mji wa Kibaya ni mmojawapo. Na Mji wa Kibaya pamoja na ile Miji 12 baada ya upembuzi yakinifu kumalizika, Benki ya Dunia imeonyesha *interest* ya kutoa fedha za kutekeleza miradi katika Miji hiyo 12.

Kwa hiyo, nataka kumhakikisha Mheshimiwa Benedict Losurutia kwamba mambo yanakwenda vizuri na huduma ya maji katika Mji wa Kibaya itapatikana chini ya Mpango huu. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *Programme* 10 *Sub-vote* 1001 *Administration and General* na kifungu 250100 Mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo ambayo tumeyahoji hapa. Tumehoji maswali kadhaa kuhusu *City Water*. Waziri ameweka blaa blaa hajajibu swali hata moja. Tumehoji na tumesema katika hotuba yetu kwamba nchi imekopa *dolla*r milioni 145 na tumetaja maeneo gani ambayo nchi imekopa na kama Waziri alivyosema mwenyewe kwamba alikuwa Mbunge wa Upinzani. Kama alikuwa katika Wabunge wa Upinzani ambao hawafanyi utafiti ni kipindi hicho. Tumeingia Wabunge wa Upinzani ambao tupo makini na tunafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Waziri, Mheshimiwa Stephen Wasira, nakuheshimu sana tujibu. Fedha za mikopo ambazo tumekopa tunazilipa namna gani? Kwa sababu moja ya sharti la kukopa *World Bank* ilikuwa ni kukodisha *City Water* na kukodisha ni sehemu ya *Privatization*. Siyo kwamba kukodisha siyo *Privatization*, kukodisha ni sehemu ya *Privatization.* Kwa hiyo, tunataka Waziri utueleze, hivi fedha hizi hatima yake ni nini? Ni fedha za wananchi, tunalipa sisi, inawezekana wewe sasa hivi ni alasiri, sisi bado ni vijana wadogo tutaendelea kulipa kodi ya nchi hii kulipa hizi fedha. Tunahitaji maelezo kuhusiana na suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumehoji ni lini Bunge lilikaa likapitisha Sheria ya Kuunda *DAWASCO? When*? Kama tulitumia *option* ya *Cap 1(2)* ya Msajili ya Makampuni, ni nani *subscribers* wa Kampuni ya *DAWASCO? We want to know* na Watanzania wanataka kujua, hatutaki ubabaishaji. *We have to know and you have to tell this House*! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumemhoji Mheshimiwa Waziri wa Maji, Sheria ya kuanzisha *DAWASCO* inazungumzia nini kuhusu Mtendaji Mkuu wa *DAWASCO* tuweze

kujua anateuliwaje?! Aliteuliwa na Mheshimiwa Rais kwa taratibu zipi na Rais alitangaza lini? Haya mambo ni muhimu tuweze kuyajua na tunapohoji, ni kwa sababu tunaipenda nchi yetu, hatuhoji tu kwa sababu ni Wapinzani.

*We love this country and we want to serve this country.* Hakuna Chama ambacho kina hatimiliki ya hii nchi na sisi kesho tupo huko. *I am telling you* na baadhi yenu mtakuwa katika uhai wenu mtakapoona tunakaa katika Kiti alichokaa Mheshimiwa Edward Lowassa hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, MKUKUTA *we know,* ndiyo maana nikasema kwamba sasa hivi ni Bunge la watu wanaofanya utafiti. MKUKUTA umeanza kabla ya Ilani za Vyama. Katika MKUKUTA, watu wameshiriki kuandaa, ni *plagiarism* kusema kwamba Ilani ya CCM inasema hivi na MKUKUTA unasema hivi, *is just a plagiarism.* MKUKUTA *is a National Document, is not party's document.* Kwa hiyo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri wa Maji aeleze kuhusu hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa, Mheshimiwa Waziri anasema kwamba, sensa ndiyo ilitumika kuangalia na kusema kwamba Sikonge, Mkuranga na Igunga ni Wilaya za mwisho kwa maji, *is not true* na ndiyo maana hata Msemaji Mkuu wa Upinzani alisema kwamba labda Mawaziri hamsomi. *Report* ya Serikali *Poverty and Human Development Report* ya mwaka 2005 ambayo Mheshimiwa Zakia Meghji aliizindua mwezi Mei, 2006 kabla hatujaja kwenye Bajeti, ndiyo amesema hivyo, ni ripoti ya Serikali. Sasa mawili, aidha, mserereko au m-*produce report*s za namna hii kwa sababu vinginevyo tunatumia *document* hizi kutaka mtupe maelezo mnanyenyesha mambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwomba Mheshimiwa Waziri kabla sijatumia kifungu ninachotumia upande wa (c) Waziri anipe maelezo ya *DAWASCO*, mikopo yetu, fedha ambazo nchi italipa, Waziri anieleze kuhusiana na suala zima; afafanue vizuri suala la MKUKUTA na kama hawezi tutamsaidia kufafanua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, mwisho kabisa aweze kueleza kuhusiana na suala ambalo nimelizungumza hapo mwanzoni la mpango mzima wa *City Water DAWASCO* ilivyoundwa na mambo kama hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata maelezo kutoka kwa Waziri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na ninamshukuru Mheshimiwa Kabwe Zitto kwa maelezo yake. Katika kujibu hizi hoja, nitarudia yale ambayo nilikwishayasema. Mkopo ni wa *dollar* za Kimarekani milioni 164, umetolewa na Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika na Benki ya Maendeleo ya Ulaya kwa ajili ya kutekeleza miundombinu na kurekebisha miundombinu ya maji katika Jiji la Dar es Salaam. Ni kweli kulikuwa na hoja ya *City Water or Privatization is a condition.* Lakini *City Water* haiku-*perform* na sisi Serikali kwa niaba ya Watanzania ndiyo tuliokopa. Tumerudi *World Bank* na kwa wakopeshaji kuwaeleza

*what happened* na wamekubali ndiyo maana fedha zile zinatumika Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu haikuwa kwamba *City Water* ndiyo watalipa. Ile ilikuwa *one condition,* lakini kama haiku-*work* ni mkopo wetu. Sasa sisi tunasema, kwa niaba ya *City Water* au kwa niaba ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuwe *specific.* Tunasema kwa niaba ya nani? Maana mkopo upo, fedha tumesaini na kazi ya kuwasaidia watu wa Dar es Salaam kupata maji inaendelea kwa mkopo huo. Nimeeleza vizuri jambo hili kwamba *City Water* walishindwa kutekeleza masharti. Sasa huwezi ukasema kwa sababu *City Water* wameshindwa kutekeleza masharti, Watanzania wote wawe *penalized,* sio *fair.* Tumewaeleza *World Bank*, *African Development Bank*, *European Investment Bank,* wameelewa, wamekubali, wanaendelea kutoa fedha na tunatekeleza ule Mpango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *DAWASCO* baada ya kuwa *City Water* ime-*fail* na wakati ule matatizo ya wananchi wa Dar es Salaam na Watanzania, kwa maana hiyo Kibaha na Bagamoyo kuondoka kwa *City Water* kungeacha *vacuum* ambayo ingewafanya wakose maji. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tatu, alitumia mamlaka yake chini ya Sheria inayomwezesha kuanzisha vyombo kama *DAWASCO* akaunda *DAWASCO as a temporary measure* kwa ajili ya kuendeleza huduma wakati tunazungumzia vile vyombo namna ya kuendesha. Walikuwa wametupa mambo matatu ya kufanya. Moja, walitaka tuunde kitu kinaitwa *EWURA* ili kiwe kinasimamia bei za maji, tumeunda *EWURA* na imeanza kazi.

Walikuwa wametupa *conditions* za kusema kwamba tuhakikishe kwamba *DAWASCO* ina-*perform* na tunawaonyesha kwamba *DAWASCO* ina-*perform* na sisi siyo nchi pekee yake katika Afrika Mashariki ambayo ina chombo kinafanana na *DAWASCO*. Uganda wanacho chombo kinafanana na hicho. Hata ukitaka kuki-*privatize,* bado unaweza ukatafuta *investors* wa hapa Tanzania, wakakifanya *private* kama inavyowezekana. Maana kuwa *private* siyo lazima iwe *foreign,* siyo lazima wawe Wazungu ndiyo wawe *private*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mamlaka ya Mheshimiwa Rais yalitumika kuunda hicho chombo na chombo hicho kinafanya kazi yake vizuri. Sasa mimi sijui tatizo letu hasa ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, juu ya MKUKUTA maana MKUKUTA huu unaweza ukawa biashara ya ajabu kidogo. Lakini *issue* siyo Ilani ya Chama. Kabla ya Ilani, CCM ina sera. Sera ya CCM ya miaka 2000 - 2010 mwelekeo wa Sera za CCM na inaeleza juu ya kupambana na umaskini na kuondoa umaskini na kukuza uchumi.

Kwa hiyo, hata kama MKUKUTA ilikuwa ni Sera ya Taifa, lakini mawazo yalitoka CCM. Maana Taifa haliko hewani, Taifa sio watu Mheshimiwa Kabwe Zitto na mawazo sio lazima yatoke mahali. Sasa kumbe itakuwaje? *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, angalau sasa Mheshimiwa Waziri amejibu na ndiyo maana ya kuwa na *opposition bench* kwamba yale ambayo yanafunikwa funikwa, leo tumeyafahamu na namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *DAWASCO* iliundwa na Mheshimiwa Rais kwa mujibu wa mamlaka ambayo Mheshimiwa Rais amepewa. Sasa kigugumizi alichokuwa anakipata Mheshimiwa Waziri wa Maji kujibu mwanzo ilikuwa ni nini? Kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Maji kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia namshukuru sana Waziri wa Maji kwa kukubali kwamba MKUKUTA ni wa Taifa. Mawazo yanatoka wapi is *something else*, lakini kwamba MKUKUTA ni wa nini? Ni wa Taifa. Hilo namshukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie tu la mwisho, kwamba hizi gharama za hii kesi ambayo *City Water* wametufungulia, tunalipaje na ni kiasi gani? Wakili wetu na ni gharama kiasi gani? Naomba anisaidie hili basi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, katika hoja zako za mwanzo, gharama za ulipaji wa kesi hazikuwepo, kwa sababu wewe hatukupi nafasi ya kuendeleza maswali. Tulitaka uridhike kwa yale aliyojibu Mheshimiwa Waziri, ndiyo maana tumekupa nafasi ya pili. Tunaendelea na Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu, kwa bahati mbaya sikusimama.

**MWENYEKITI:** *Okay*, basi tulikuona vibaya.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 1002 - *Finance and Accounts*... ...Sh. 770,905,300/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 1003 - *Policy and Planning*... ... Sh.994,173,500/=

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kile kidogo cha 310700 - *Feasibility Studies, Project Preparation and Design*. Ni kitu kidogo tu nataka kujua kwamba, hii miradi ya maji mikubwa na midogo inaweza kuwa na athari kubwa sana kwenye mazingira. Sasa kwa vile katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri hakutaja kabisa suala la tathmini ya mazingira, nilitaka tu kujua kama katika *sub-vote* hii ndiko kuna fedha za kufanyia *EIA* kwa ajili ya miradi ya maji hii. Ahsante sana.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, namshukuru Mheshimiwa Mwalyosi katika swali lake. Ni kweli kila mradi tunaofanya kwa wakati huu tunazingatia mazingira. Kwa hiyo, sehemu ya fedha hii ya *Feasibility Study* itakuwa inashughulika na *assessment* na mazingira kwa miradi yote ya maji. Ahsante sana. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 2001 - *Water Resource Assessment and Exploration... ... ...* Sh. 3,265,382,100/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 2002 - *Central Stores... … ...* Sh. 565,415,800/=

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *sub-vote* ile ile, nilichotaka kujua,....

**MWENYEKITI:** Ile ile ngapi bwana?!

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Kifungu cha 310700. Kuna fedha zimetengwa pale Sh. 99,273,000 na zaidi kwenye *Central Stores,* kuna vitu gani ambavyo vinafanyika, vinavyohusu *Feasibility Studies* na *Project Preparation and Design* katika kifungu cha *Central Stores?* Ahsante.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Prof. Mwalyosi. Hapa tumeweka fedha kidogo za *Feasibility Studies* kwa ajili ya *Government Stores* kwa sababu kuna vi-*project* ambavyo vinaambatana na *Government Stores* ambavyo huwezi kuvitekeleza mpaka kwanza ume-*study.* Kwa hiyo, hiyo fedha imewekwa kwa ajili hiyo na sio fedha nyingi, lakini lazima ufanye *Feasibility Study* kabla hujafanya kitu chochote kwa ajili ya *Government Stores.* Lakini kwa maelezo zaidi, kama Mheshimiwa Mwalyosi anataka, tutaweza tukamweleza zaidi, lakini hiyo fedha inafanya kazi hiyo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 2003 - *Water Laboratory… … …*Sh. 751,243,600/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 3001 - *Urban Water Supply and Sewerage... ... ... ... ... ...* Sh. 6,891,729,300/=

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, programu ya 30, kifungu cha 3001, kifungu kidogo cha 250100 - *Urban Water Supply Basic Salaries.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia kanuni ya 81, kanuni ndogo ya 2 (b) kupata ufafanuzi zaidi kuhusu mambo yafuatayo:-

La kwanza ni katika majibu yake. Mheshimiwa Waziri katika suala la *City Water* amesema haiku-*perform*. Sasa nilitaka kujua hatari moja ninayoiona na tamko la namna hii la Waziri ni kwamba, mtu yeyote asipotekeleza kitu fulani, sheria haifuatwi. Tunakamata sheria mkononi na ndicho anachohalalisha Waziri ndani ya Bunge hili.

Napenda kupata ufafanuzi kama Waziri anahalalisha *City Water* iliyoingia nchi hii kwa utaratibu iliyokuwa na Mkataba na Serikali yetu ambao ni wa Kisheria, haikutekeleza majukumu yake, ni kwa nini haikupelekwa Mahakamani badala yake inaondelewa na Waziri anasema haiku-*perform?* Kwa hiyo, inaondolewa kwa utaratibu ulioondolewa!

Hatari ya pili, tumepiga kelele ndani ya Bunge hili kila siku kwamba Watanzania wamejichukulia sheria mikononi, wanachoma watu, wanaua, tumewaomba wasichukue Sheria mikononi. Je, ni halali kwa Serikali kuchukua sheria mikononi mwake bila kufuata utaratibu? Maswali mawili. *(Makofi)*

La tatu, ningependa kujua sasa kuhusu kesi iliyoko kwa jinsi Waziri alivyojibu na tunauliza masuala haya kwa sababu tuna nia njema na nchi yetu. Hatupendi majibu ambayo ni ya kisiasa ndani ya Bunge hili. Waziri amejibu kisiasa akijaribu kukandia Upinzani. Anasahau kwamba Upinzani ni sauti ya Watanzania vile vile, anasahau na sisi Wapinzani tunatoka kwenye Majimbo, tuna haki ya kuuliza kwa niaba ya wananchi wetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nenda kwenye hoja Mheshimiwa Mbunge. Nenda kwenye hoja

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Ninaruhusiwa Mheshimiwa Mwenyekiti, kuzungumza kwa dakika tano najenga hoja yangu.

**MWENYEKITI:** Ahaa! Sawa, lakini hamruhusiwi kumhutubia Spika kipindi hiki. Kwa hiyo, nenda kwenye hoja, mimi niweze kupitisha Shilingi basi.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Nakubaliana, lakini ufafanuzi hauwezi kupatikana kama hoja haikujengwa. Sasa kama kifungu hiki unasema tusifuate, ni sahihi, lakini kifungu kinasema unaomba ufafanuzi. Sasa mimi naomba ufafanuzi kutokana na yaliyosemwa.

Sasa najaribu kuendelea na kifungu kinatamka kabisa kwamba unaombwa ufafanuzi wa kitu. Sasa mimi naomba ufafanuzi. Ningependa kujua kuhusu kesi hiyo iko wapi? Mawakili ni akina nani na inagharimu kiasi gani? Haya ni masuala ambayo Watanzania tunatakiwa kujua. *IPTL* tuligharamia sana na kesi haijakwisha mpaka leo. Tumelipa sisi Watanzania kwa kodi ya Watanzania na hii tutalipa kwa kodi ya Watanzania. Tuna haki ya kujua kesi iko wapi? Mawakili ni nani na itagharimu kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapenda kupata majibu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja tatu. Moja kuvunja mkataba. Sasa mimi nataka kusema *City Water* ilikuwa na Mkataba na *DAWASA* kwa niaba ya Serikali, walitiliana saini. Wakakubaliana mambo ambayo *City Water* inatakiwa kutekeleza. Ndani ya Mkataba mle kulikuwa na *provision* ambayo inaitaka moja ya *signatory* wa ule Mkataba kutoa *notice* anapokuwa hakuridhika.

*City Water* ilipewa *notice* kwa mujibu wa Mkataba ule. *City Water* ikawa inang'ang'ania kwamba itaendelea kuendesha, wakati imeambiwa haina haki ya kuendesha kwa sababu Mkataba ule umevunjika kwa sababu *part* moja haikubaliani tena na vitendo vya *City Water*. Kwa hiyo, hakuna sheria yoyote iliyochukuliwa mkononi kwa sababu *City Water* ilipewa *notice* ya kisheria kwa mujibu wa Mkataba wenyewe. Sasa mimi nilidhani tumetekeleza na Utawala Bora ni pamoja na kufuata sheria na sheria ilifuatwa. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Slaa ajue kwamba hivyo ndivyo ilivyotokea na hakuna tatizo lolote.

Sasa juu ya kesi, unajua kesi unafungua hata kama wewe ndio umekosa, hiyo ni kawaida. Kwa sababu ukikosa ukawa *penalised,* lakini hukuridhika unakwenda kufungua kesi. Halafu anayeitwa kotini hakatai kwenda. Unaitwa na kwenda kuna gharama. Lakini ile kesi inafanyika Paris. Sisi tuna haki tumeweka *counter claim* ili wakishindwa na wao watulipe. Tunao ushahidi wa makosa yao. Kwa hiyo, kwa sababu linasubiri maamuzi na liko Mahakamani na Kanuni zetu zinazuia kuzungumza mambo ambayo yako Mahakamani basi.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninadhani Mheshimiwa Waziri amejaribu kueleza pamoja na kwamba ameambiwa achia hapo. Naomba nitumie *Parliamentary Privileges and Immunities Act.* "Mbunge yoyote wakati wowote anaruhusiwa kuomba hati yoyote toka Serikalini." Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari, kwa kuwa na mimi niko chini ya kiapo, kunipatia Mkataba huo wa *City Water* na *DAWASA*? Kwa sababu mgogoro uliokuwepo kati ya *City Water* pamoja na *City Water* na mimi nimeuona na majadiliano yaliyoendelea niliyaona.

**MHE. ANNA M. ABDALLLAH:** Kuhusu utaratibu. Ibara ya 50 fasili ya 8(b): "Ni marufuku kwa Mbunge kutumia haki yake ya kusema kwa madhumuni ya kutaka kuchelewesha shughuli za Bunge." Kwa kweli Mheshimiwa anaomba apewe Mkataba ambao yeye mwenyewe anasema ameuona. Sasa kama ameuona anautakia apewe wa nini? *(Makofi)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kama ni kuchelewesha Bunge ndiyo hiyo.

**MWENYEKITI:** Bwana endelea, acha habari ya kujibu mambo yasiyohusiana na hoja ya msingi.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Kama kuuliza swali linalohusu watu, anachelewesha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Slaa, mimi ndiyo naongoza Kikao. Nimesema endelea na hoja uliyokuwa nayo.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa maelezo hayo na mimi nashukuru kwamba ujumbe, umefika.

Nimesema, nimeuona Mkataba. Kabla sijamaliza, nilikatizwa. Nilisema kwamba nimeuona na kuna mgogoro na ninajua kwamba hilo suala kwa sasa liko *arbitration,* haliko Mahakamani. Katiba yetu haizungumzii tusiongee masuala yaliyoko *arbitration.* Yanazuiliwa masuala ambayo yako Mahakamani. Sasa Serikali ituambie kama iko Mahakamani, iko Mahakama ipi? Kwa sababu hatuwezi tukaambiwa tu tukakubali. Mimi nataka kujua kama liko Mahakamani tuambiwe liko Mahakamani, kesi namba fulani, Paris. Lakini mimi najua iko *arbitration.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa suala linalokuwa *arbitration* halikatazwi kuzungumziwa ndani ya Bunge, *unless* leo mnatuambia kwa mara ya kwanza kwamba inakatazwa.

Kwa hiyo, tuna haki ya kupata taarifa na mimi nimeomba kwa kutumia *Parlimentary Privileges and Immunities Act* kama Mbunge, kwa kutumia sheria ya Bunge iliyotungwa na Bunge hili kujua masuala hayo, tupate hiyo ili niweze kulinganisha na kile nilichonacho ili niweze kujua kwa niaba ya wananchi, inasimamia wapi?

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napata taabu kidogo kuelewa wananchi anaowawakilisha Mheshimiwa Slaa katika jambo hili ni wa wapi? Maana *City Water visas* ni *United Republic*. Wewe unasimama kwa nani? Kwa wananchi au kwa *City Water*? Hilo la kwanza. *(Makofi)*

*It is City Water visas the United Republic.* Wewe unataka kusimama, unamwakilisha nani hapa? Hilo la kwanza. La pili, ule Mkataba umesema umeuona. Kwa hiyo unao. Nikupe wa nini? Utakuwa nayo miwili bure! Utumie ule ulionao. *(Makofi)*

La tatu, *arbitration* ninakwenda kwa kanuni zile zile za Mahakama. Kwa hiyo, hatuwezi kusema mambo ambayo yako kwenye *arbitration.*

**MWENYEKITI:** Tunasimama mara mbili Mheshimiwa Slaa. Kifungu gani unatumia?

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Natumia kifungu cha 81, kifungu kidogo cha 2(c). Nilitumia (b) sasa natumia ( c) - kuondoa Shilingi kueleza kwamba sijaridhika na maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ya Serikali hayaridhishi kwa sababu Waziri ana wajibu wa kujibu Watanzania. Ananiuliza, wewe unawawakilisha nani? Ninawawakilisha Watanzania wanaotaka *principle.* Kuna tofauti kati ya *principle* na kati ya mtu aliyehujumu! Mimi sikusema *City Water* hawajakosea. Nimesema tunataka *principles* zifuatwe na Serikali ifuate *principle*. Sasa *principle* ni lazima ijibiwe ndani ya Bunge.

Ya pili, ni kwamba mimi nimeona zile *documents,* ninataka *authentic document* toka Serikalini ndiyo maana nimetumia *Parliamentary Privileges and Immunities Acts.* Kama kifungu hicho hakipo sheria ile ifutwe**.**

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 4001 - *Rural Water Supply* ... ... Sh. 5,197,462,100/=

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *program* 40 - *Rural Water Supply sub vote* 4001 – 250100 - *Basic Salary.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimechangia sana leo kuhusu Wizara ya Maji na nilizungumza sana kuhusu matatizo tuliyonayo ya maji katika Wilaya ya Mbozi. Nimesema tunalima sana kahawa, lakini tunaoshea maji machafu. Nikasema Serikali ituambie na kwa sababu Mbozi hatuna hata mradi mmoja mkubwa wa maji, nikasema hilo naomba litolewe maelezo. Waziri au Naibu Waziri hakuna aliyetoa maelezo.

Lakini pili, nikasema, Mheshimiwa Rais alipopita kwa ajili ya Kampeni tarehe 31 Agosti, 2005 aliahidi kupatia maji Miji ya Mloo na Tunduma. Mimi nikasema ninaomba sasa Wizara itambue ahadi hiyo ya Rais na kwamba sasa iwe kwenye orodha ya zile ahadi za Mheshimiwa Rais. Sijajibiwa chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mbozi wanajua ahadi ya Mheshimiwa Rais, sasa kama haionekani popote, tutawaambia nini watakapohoji? Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atolee maelezo hoja yangu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Zambi ni sahihi. Alikwishaniandikia kuulizia juu ya hoja ya ahadi ya Rais. Sisi majibu yetu ambayo tulikusudia kumpa kwa maandishi ni kwamba tunaheshimu na kutambua ahadi zote za Rais na kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi ilikwishatuandikia kutueleza kwamba Rais aliahidi na sisi tutaiweka Mbozi na maeneo

yale aliyoahidi Rais katika programu ya utekelezaji katika kipindi cha miaka mitano. Tutapeleka wataalamu Tunduma pamoja na Kijiji kingine kinaitwa Mloo kwenda kufanya upenguzi yakinifu ili tuingize Mloo na Tunduma katika programu ya utekelezaji ya kuwapatia wananchi wale maji.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 5001 - *Water Resource Institute*... Sh.718,373,400/=
Kifungu cha 6001 - *Drilling*… … ... ... ... ... Sh. 140,727,400/=

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**FUNGU 49 - WIZARA YA MAJI**

Kifungu cha 1003 - *Policy and Planning*… Sh. 5,390,956,000/=

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa naomba tu nipate ufafanuzi, sina tatizo la msingi, lakini ningependa katika suala la *sub-vote* 1003 *design and studies*. Nilichangia katika hoja yangu na nimeeleza kwamba kutoka mwaka 1997/1998 nilipeleka hoja ya kwamba katika mito mingi, sheria iliyokuwa inatumika ilikuwa inatoa hatimiliki ya mto mzima kwa mtu mmoja. Ile *Water Right* ilikuwa inakabidhiwa kwa *owner* mmoja au mtu mmoja hasa kwenye maeneo ya *estates* kubwa kubwa. Nikaomba kazi hiyo ifanyike na nikatumia mfano wa Karatu na leo nimetumia pia mfano wa Karatu maeneo ya mashamba ya Mkataba ambapo mto mzima unamilikiwa na mtu mmoja na wananchi walio wengi chini ya mto hawapati maji.

Tulivyoendelea, sasa hali imezidi kuwa mbaya na mwaka 2000 Wizara ya Maji ilikuja Karatu ikatathmini, lakini mpaka leo hatujaambiwa chochote. Hapa, kwa kutumia sheria ya mwaka 1973 ambayo inaeleza wakati wa ukame, mashamba yanaondolewa matumizi ya maji, *priority* ya kwanza inapelekwa kwa mwananchi, ya pili inapelekwa kwa wanyama na ya tatu ndiyo inakwenda kwenye kilimo. Tumepita kwenye hali ngumu sana mwaka huu wa 2006 hasa kwa ajili ya ukame, hakuna kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kujua marekebisho hayo ambayo ni ya nchi nzima yatafanyika lini na ninajua kwamba yanahusu sheria na kwa hiyo, inatakiwa sheria ile iwasilishwe Bungeni. Nilitaka kupata uhakika tu hiyo sheria inayofanya marekebisho hayo italetwa Bungeni lini?

Pili katika maeneo ambapo hali ni mbaya kama Karatu ambapo ukame unakuwa mkali na watu wachache wanamiliki maji, ni lini sheria ile itatumika kwa sababu mwenye mamlaka ni *Principle Water Officer* peke yake, anaweza kufanya *modification.* Lini *modification* hizo zitafanyika ili wananchi walio wengi waweze kupata maji kuliko mtu mmoja mwenye uwezo ambaye anatumia maji kwa *irrigation?*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Dr. Slaa kwa hoja yake. Katika hotuba yangu nimeeleza kwamba Wizara yangu inakusudia kuwasilisha sheria mbili katika Bunge lako Tukufu wakati wowote kuanzia sasa kufikia labda mwezi Novemba kama kazi itakuwa imekamilika. Moja ya sheria hiyo itahusu umiliki na uhifadhi ya vyanzo vya maji. Kwa hiyo, sheria hiyo ndiyo ita-*govern* na Wabunge mtapata nafasi pamoja na Mheshimiwa Dr. Slaa kuijadili na kuona inaweza kuwa sheria ya namna gani itakayokuwa badala ya hiyo sheria anayoiongelea.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kifungu kidogo cha 3436, suala la *Coordination Monitoring of Water and Sanitation.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kwamba kwa kuanzisha miradi mingi sana ya maji sasa hivi nchi nzima na kwenye Miji mingi sana, suala la kufuatilia au kufanya *monitoring* na hata *coordination* itakuwa ni *very crucial*. Sasa nikiangalia mwaka uliopita kipindi kilichopita tulikuwa na fedha nyingi za kigeni. Mwaka huu fedha za kigeni zimepungua. Mwaka wa fedha uliopita ukilinganisha na fedha zetu, zimeongezeka kwa Shilingi milioni tano tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni kwamba, kwa vile tutakuwa na majukumu makubwa zaidi kutokana na miradi mingi sana itakayoanza kutekelezwa hapa nchini kwenye *Rural* na *Urban areas* ambayo itahitaji *monitoring* na *coordination,* naona kama fedha iliyotengwa ni kidogo ukilinganisha na kipindi cha fedha kilichopita. Je, tutafanikiwa kweli ku-*coordinate*, ku-*monitor* miradi yote kwa fedha hizi? Ahsante.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa hoja ya Mheshimiwa Prof. Mwalyosi. Ni kweli tunaanzisha miradi mingi ya Vijijini na Mijini. Lakini vile vile tunao utaratibu wa kupeleka madaraka katika Halmashauri za Wilaya. Kwa hiyo, *monitoring* inakuwa inafanywa katika ngazi mbalimbali. Kwa upande mmoja kutakuwa na *monitoring* inayofanywa katika ngazi ya Wilaya yenyewe ndiyo maana tumesema tunapeleka wataalamu.

Lakini vile vile tutakuwa na wataalamu katika ngazi ya Mkoa watakaokuwa wanasaidia kufanya *monitoring* katika ngazi ya Wilaya ili kusaidia Wizara. Ukiondoa hiyo, Wizara itakuwa na *unit* ambayo itakuwa ina-*supervise* na kutembea na kuhakikisha kwamba utekelezaji wa miradi hii unafanyika. Kwa hiyo, kutakuwa na l*evels* za *monitoring*. Zile za Wilaya zitakuwa zinatumia *vote* za Wilaya na hizi za Wizara zitatumia *vote* ya Wizara. Kwa hiyo, tunadhani kwamba *monitoring* itawezekana katika mazingira hayo.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Mwenyekiti, *sub-vote* 1003 - *Policy and Planning,* kifungu kidogo cha 2325 - *design and studies.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia, nilijaribu kueleza kwamba ziko sehemu ambazo zinafanyiwa utafiti na zimepimwa. Lakini nikasema Wizara ya Maji isije ikaingia kwenye matatizo ya migogoro ya ardhi kwa sababu ya kulipa fidia kwa

wananchi ambao wako kwenye eneo hilo ambalo limepimwa. Nikasema vile vile, wananchi wengi wanaonesha kwamba pengine eneo lililopimwa ni kubwa, kwamba pengine sehemu yote haina maji.

Sasa sikusikia Waziri akijibu pengine ni kwa sababu ya muda, lakini nilisema jambo hili lisichukue muda mrefu kwa sababu wananchi kwa sehemu kubwa watakuwa wamezuiwa wasifanye jambo lolote kwenye maeneo haya. Sasa inaweza ikachukua miaka miwili, mitatu, minne wananchi watakuwa tena hawafanyi shughuli pale. Nilieleza kwamba, bonde hilo ndilo bonde ambalo wananchi wamekuwa wakilima mazao kwa muda mrefu. Kwa hiyo, ni mategemeo yao. Kama ni fidia, basi Serikali iingie. Nikasema kama fidia ni kubwa, basi Serikali ikae na wale watu na iweze kuzungumza nao na kuona kwamba wanaweza wakaishi vipi kwenye hayo maeneo jirani na maeneo hayo ambako Wizara inaona pengine yanaweza yakapatikana maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilitaka tu maelezo kwamba Waziri atalishughulikia vipi suala hili?

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Kwaangw' kwa hoja yake. Tumeitazama ile hoja yake ila hatukuwa na muda wa kutosha kujibu hoja zote. Lakini eneo lile ambalo linazungumziwa, nadhani la Maisaka tumesema utafiti uanze mapema ili tufanye uamuzi kama lile eneo halitakuwa chanzo cha maji, basi tutumie vyanzo vya maji vingine pamoja na Ziwa Babati.

Kwa hiyo, tunachukua hatua na hatutachukua muda mrefu sana mpaka kuwaweka wale wananchi. Tutachukua hatua ili tuhakikishe kwamba kama hatuwagusi wale, basi wataendelea kuishi katika mazingira yao kwa sababu ni watu wengi na fidia inawezekana ikawa kubwa zaidi. Inawezekana tukalipa fidia ikiwa ndiyo chanzo peke yake cha kuwapa maji wananchi wa Babati.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 2001 - *Water Resource Assessment & Exploration* ... ... ... ... ... ... Sh. 1,000,000/=
Kifungu cha 2003 - *Water Laboratory*… … ... ...Sh. 95,000,000/=
Kifungu cha 3001 - *Urban Water Supply and Sewerage* … ... ... Sh. 92,607,185,800/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 4001 - *Rural Water Supply*… Sh. 46,286,686,100/=

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho *sub-vote 4001 - Rural Water Supply.* Ninaomba tu Waziri sasa atoe kauli rasmi kwamba katika

mchango wangu nilimshauri kwamba Watendaji wa Wizara ya Maji wazisaidie Halmashauri fedha kutoka *EU Water Facility.*

*N*aamini kabisa kwamba ushauri wangu atakuwa amekubaliana nao, lakini naomba autoe rasmi ndani ya Bunge ili uwe *recorded* kwamba amekubali ushauri huo kwamba Watendaji wa Wizara ya Maji watasaidia Halmashauri kwa ajili ya *EU Water Facility.*

Pili, ninamwomba Mheshimiwa Waziri anitamkie rasmi kwamba sasa anakubaliana na ushauri wangu kwamba pia Vijiji vya Mwandiga na Nyalubanda viingie katika mpango ule wa Maji Vijijini kama nilivyoshauri badala ya Kijiji cha Mahembe na Kamala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Zitto, ametushauri juu ya suala la kuomba fedha kutoka *EU Water Facility*, tunalifahamu, tumewahi kuomba na tumewahi kupata, sio geni. Lakini nasema ya kwamba *EU Water Facility* ina masharti, ukiomba fedha kule wanataka lazima uwe na *counterpart financing*.

Kwa hiyo, sio kuomba tu na kupata. Mpaka uombe na uonyeshe kwamba una uwezo wa kupata *financer* mwingine wa kushirikiana na *EU Water Facility.*

Kwa hiyo, wataalam wangu watawasaidia watu wanaotaka kusaidia, lakini na wewe Mheshimiwa Zitto utusaidie kupata *counterpart fund* kama unazo, halafu tutawapa. Hilo sio *problem* hata kidogo, kwa sababu ni fedha itakayokuja ku-*solve problem* ya wananchi, wala hatuna sababu ya kukataa. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

La pili, vile Vijiji vyako viwili shirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma kwa sababu huko ndiko *source.* Sisi hatuwezi kusema hapa Bungeni kwamba tunakubali viingie, halafu Halmashauri ikasema hivyo siyo vyenyewe na wewe ni Diwani wa Kigoma kule, nenda useme na wenzako Madiwani halafu utuletee. *( Makofi)*

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti , nami ninataka tu maelezo, *sub-vote 4001* kifungu kidogo cha 3223 - *Bore hole Drilling and Dams Construction.* Nilizungumza kwenye maelezo yangu kwamba kuna Kijiji cha Lesing'ieta ambacho akina mama wanachota maji kilomita 20 na katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri alisema ametoa milioni 20 kwa mwaka 2005. Ni kweli hizo fedha zimetolewa, lakini zimenunua mashine tu na pampu.

Kwa hiyo, hizo fedha hazikutosha na bado wananchi wanaendelea kupata matatizo. Kisima kingine kilichochimbwa ni cha Mundayara, amesema ametoa milioni 25, nashukuru.

Lakini kwa vile wananchi hawa wameteseka kwa muda mrefu na inawezekana zikiongezwa hizi fedha zinaweza zikakamilisha visima vyote viwili. Je, Waziri hawezi kuona huruma kwa kukamilisha hivi visima viwili ili wananchi wa Lesing'eita na Mundayira wapate maji ili wasiende masafa marefu?

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Laizer alikuwa ameliongelea jambo hili na majibu tumetoa kwamba kiasi cha Shilingi milioni 20 zilipelekwa na mwaka huu wa 2006, tumetenga Shilingi milioni 25 kwa ajili ya Kijiji cha Mundayira. Sasa kama Shilingi milioni 20 hazikutosha na sisi shida yetu ni kuona watu wa pale wanapata maji, namwomba Mheshimiwa Laizer aje tuongee namna ya ku-*solve* hilo tatizo. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 5001 - *Water Resource Institute* ... Sh. 460,300,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 6001- *Drilling* … ... ... … ... Sh. 1,500,000,000/=

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia hoja hii kwa maandishi, nilizungumzia kuhusu visima ambavyo vilichimbwa na wakala wa wachimba visima. Kuna visima kama sita vilichimbwa kwa kubahatisha, lakini bila ya mafanikio ya kupata maji, vyenye thamani ya zaidi ya Shilingi milioni nane, yaani kila kisima ni Shilingi milioni sita na wananchi hawakubahatika kupata maji kwa sababu vimechimbwa kwa kubahatisha. Sasa katika kifungu hiki nimeona kuna Bajeti ya Shilingi milioni 600. Sasa nataka nipate maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri; Je, hiki kiwango kitasaidia kweli kuhakikisha kwamba wanapata vifaa vya kupimia sehemu za kuchimba visima badala ya kubahatisha na pili kuwa na mashine za kuchimbia visima nyingi zaidi ya mbili kuliko moja kuzunguka nchi nzima?

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii kazi ya ku-*drill* visima inafanywa na *agency* inaitwa *DDCA*. Hii *DDCA* ina vifaa vya ku-*drill* maji na siyo viwili tu, tunaagiza viwili vipya. Lakini viko vingine ambavyo bado viko katika hali nzuri na sehemu ya fedha hizi itatengeneza vile ambavyo vimeharibika ili viweze kuwa katika hali nzuri ili kuongeza kasi ya kuchimba visima. Kwa hiyo, hili suala analolisema Mheshimiwa Mbunge kwamba walijaribu ku-*drill* kwa kubahatisha, sijui walibahatishaje na hayakupatikana. Lakini kwa kawaida tunao watu wa *water resources* ambao huwa wanakwenda kufanya *survey* katika maeneo hayo. Lakini tunaelewa hali ya Wilaya ya Mbarali, matatizo yake ni makubwa hasa ya maji chini ya ardhi, lakini ikiwa kuna haja ya kujaribu tena kufanya ku-*drill* na kufanya utafiti, basi inabidi tufanye utafiti ili tuone jinsi tunavyoweza kutumia fedha hizi kufanya kazi ambayo Mheshimiwa Kilasi anaisema. Lakini kwa sasa, tunaomba hizi fedha ili *agency* hii iweze kufanya kazi yake vizuri. Ahsante.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2006/2007 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa liyakubali makisio hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, napenda kuridhika kwamba tumeanza vizuri.

Pia, napenda kufafanua kwamba kile kifungu cha kutoa Shilingi mkisoma vizuri kinazungumzia kazi ya vifungu. Ndiyo maana nilikuwa nawakatalia ndugu zangu kuleta habari sijui za kwao, sijui za Wapinzani, hapa hakuna. Tukiingia kwenye Kamati ya Matumizi hakuna Wapinzani wala hakuna Chama Tawala, ni Bunge.

Kwa hiyo, ndiyo sababu nilikukatalieni kwamba sikubali hiyo na maelezo yako *very clear*. Ukitaka ufafanuzi zaidi kuhusu utekelezaji wa mambo hayo, inasema, fungu hilo madhumuni halisi ya hoja ya aina hiyo ni kumwezesha Mbunge aliyeitoa hoja hiyo aweze kueleza kutoridhika kwake na utekelezaji wa jambo fulani mahususi.

Waheshimiwa Wabunge, utekelezaji wa jambo fulani sio siasa wala Chama chochote, wala mahala fulani, ama maelewano yenu ya huko nyuma, hiyo hairuhusuwi. Ndiyo maana nikaawaambia hiyo sivyo, nadhani tumeanza vizuri na tuweze kuendelea namna hii, tuweze kuendesha Bunge letu kwa utaratibu zaidi. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, naahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 01.09 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano, Tarehe 12 Julai, 2006 Saa Tatu Asubuhi)*